Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MBILI

**Kikao cha Thelathini na Moja – Tarehe 24 Julai, 2008**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**HATI ZIFUATAZO ZILIWASILISHWA MEZANI:-**

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009.

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI):** Taarifa ya Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji, kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa Mwaka wa Fedha uliopita pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2008/2009.

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA (MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI WA WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI):** Taarifa ya Kambi ya Upinzani, kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa Mwaka wa Fedha uliopita pamoja na maoni ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2008/2009.

## MASWALI KWA WAZIRI MKUU

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako, napenda kuuliza swali kwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, mwaka 2003, wafanyakazi wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Serikali iliahidi kwamba wangemaliza matatizo yao ya malipo na wakati ule Serikali kwa kupitia Bunge hili, iliahidi wafanyakazi hao kwamba katika kipindi cha mwaka 2003/2004 wangeweza kupatiwa malipo yao. Leo, Watanzania wote wanashuhudia wafanyakazi hawa wakiendelea kulalamika, kunung'unika na hata kufikia hadi kulala Ikulu, wakiendelea kudai haki zao. Serikali yetu inasema kwamba inafuata kanuni za utawala bora, je, ni kwa nini Serikali hadi leo imeshindwa kumaliza tatizo la wafanyakazi wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba nimjibu Mheshimiwa Hamad Rashid, swali lake kuhusiana na wafanyakazi wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki kama ifuatayo:-

Mheshimiwa Spika, naweza nikasema, kwa sehemu kubwa, tatizo hili Serikali imelishughulikia kikamilifu kabisa na wakati mwingine hata mimi ninapowaona wananchi wanakuja Ikulu pale, nashindwa kujua hasa kuna nini katika jambo hili.

Sasa, nimemwambia Waziri wa Fedha kwamba pengine namna moja ya kujaribu kupunguza jambo hili, tutoe kwenye gazeti taarifa inayoonyesha watumishi ambao *so far* tumekwisha walipa, tuonyeshe vile vile hundi ambazo zilitolewa zaidi ya 6,000, zimekaa mpaka zikaharibika, zikarudishwa tena Hazina. Tuonyeshe vile vile hundi ambazo zipo, lakini wenyewe hawajaonekana.

Mheshimiwa Spika, nadhani hili linaweza likasadia pengine kuliambia Taifa kiwango ambacho Serikali tumejitahidi kushughulikia jambo hili, kwa sababu picha ninayoiona sasa kwa sababu nimejaliwa na mimi kulifuatilia sana, kwa upande mmoja jambo hili limegeuzwa kama sehemu tu ambapo tunaweza tukanufaika kwa kiwango fulani, maana kuna watu wanachangiwa fedha ili wawe ndio wasemaji wakuu kwenye jambo hili, kitu ambacho mimi nadhani si sahihi hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nadhani Mheshimiwa Hamad, tukishafanya lile zoezi, litawasaidieni Wabunge wote na nchi nzima kwa ujumla kujua kiwango ambacho tumeshughulikia jambo hili. Kama kutakuwa bado maeneo mengine ambayo bado hatujayashughulikia, tutakuwa radhi kuyashughulikia. *(Makofi)*

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, swali hili lilikuwa na pande mbili. Upande wa kwanza, ni suala la malipo yao halali ambayo waliahidiwa na aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tatu ambayo ilikuwa kama ni Sh.*400 billion*, hilo ni tatizo la kwanza la msingi. Lakini la pili katika hili hili, ni kwamba, hata Serikali iliposema wale ambao wana ithibati walipwe, hawalipwi!

Mheshimiwa Spika, nina mfano halisi wa bwana mmoja anaitwa Abdallah Issa Khamis. Nimechukua *document* zake, nimezipeleka mpaka Wizarani na mpaka leo ninavyokwambia, hajalipwa. Kwa hiyo, siyo kweli kwamba watu wakipeleka *document*

zao, wanalipwa. Bado tatizo hili ni la msingi. Je, Mheshimiwa Waziri Mkuu, haoni sasa ni vizuri, tuka-*form committee* ya Wabunge, tukasaidia hili jambo likaweza kupata ufumbuzi? *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, analolisema Mheshimiwa Hamad, inawezekana kabisa lipo na ndio maana mara ya mwisho, Naibu Waziri wa Fedha, alidiriki hata kusema kama yuko mtu ambaye bado *genuinely* anaidai Serikali, aende kumuona. Hili mimi nililichukulia kama ni changamoto nzuri kwamba endapo mtu atakwenda kumuona Naibu Waziri huyu, halafu bado mambo yake yasifanikiwe, tuweze kumbana sasa Naibu Waziri kwa *commitment* aliyoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini, la pili kwamba tuunde pengine Kamati ya Pamoja ya Wabunge labda na Serikali katika kujaribu kulishughulikia jambo hili, mimi niko radhi kwa sababu halinipi tatizo hata kidogo. Lakini, naomba tufanye hiyo kazi baada ya kuwa hii hatua niliyoliarifu Bunge kuwa imekamilika ili tuweze kuona ni maeneo gani sasa hata kama tunapeleka hiyo Kamati ya Pamoja, tuweze kutumia muda wetu mwingi kupata ukweli juu ya tatizo hilo. *(Makofi)*

**MHE. HABIB MOHAMED MNYAA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru.

Ninapenda niulize swali moja dogo na kwa kifupi sana. Kwa kuwa una uzoefu wa kutosha wa Ikulu; na kwa kuwa wewe pia ni Mwanasheria, unaweza ukaliambia Bunge lako hili Tukufu, nini kilicho juu kisheria baina ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Makubaliano ya Muungano *(Article of Union)?*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mnyaa hanitakii mema kwa upande mmoja, maana leo kwenye magazeti nimeona wanasema kwamba Serikali ya Mapinduzi Zanzibar wamejitahidi, wamezima maandamano dhidi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa sababu ya suala hili hili, sasa naona Mheshimiwa Mnyaa, ananirejesha kule kule. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, sikutaka sana kuliendeleza jambo hili kwa sababu nilifikiri tumefika mahali pazuri ili tuweze kulimaliza kiutu uzima. Sasa ili nisiendeleze na mimi malumbano maana kwa kadri nitakavyokujibu nitazidi kuchochea fikra ambazo pengine sasa hivi zipo, nikuombe sana Mheshimiwa Mnyaa, nilitoa kauli hapa kwamba acha tuzungumze, *Attorney General* wetu na Mwanasheria Mkuu wa upande wa Zanzibar, ili tuone ni wapi hasa kuna tatizo.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa upande mwingine, mimi naamini kwa dhati kabisa kwamba kwa mwelekeo wa jambo hili linavyokwenda sasa, ni muhimu jambo hili Chama cha Mapinduzi sasa ilichukue na ilitolee kauli kwa sababu sisi ndio tunaotawala kwa maana ya kuwa na Serikali. Hatuwezi kulinyamazia hivi, litaendelea kuzaa matatizo na matatizo na matatizo. Kwa hiyo, nadhani na Chama nao watalizungumza, maana Chama

kile kinahusisha pande zote mbili, wako Wazanzibari na tuko Watanzania Bara. Nadhani baada ya pale, tunaweza tukapa jibu ambalo ni sahihi zaidi. *(Makofi)*

*(Hapa Mheshimiwa Habib Mohamed Mnyaa alisimama)*

**SPIKA:** Nachelea kama unajaribu kuliongezea hilo itakuwa kama ni fujo tu kwa kweli kwa sababu kama limekwishakabidhiwa Wanasheria Wakuu wa pande zote mbili na pia kuna mwendelezo kwenye ngazi ya Chama Tawala, tusubiri! Tunaendelea!

**MHE. DR. ALI TARAB ALI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Muungano wa Tanzania ni Muungano wa wananchi wa Tanzania Bara na Zanzibar, kwa hiyo suala hili kwa kweli lisiwe tu ni Chama Tawala, lisiwe ni upande mmoja, liwe ni la wananchi. Kwa nini haturuhusu mjadala wa Kitaifa ili *at the end of the day* tuwe...

**SPIKA:** Mheshimiwa Dr. Ali Tarab Ali, Kanuni ya 53(8), jambo likishakuwa limeamuliwa na tangazo limetoka, Bunge haliwezi kuendelea tu kulizungumzia.

Sasa Kanuni 53(8) inasema wazi wazi kabisa kwamba:-
*"Mbunge yeyote hataruhusiwa kufufua jambo lolote ambalo Bunge lilikwisha kuliamua ama katika Mkutano huo uliopo..."*

Sasa, Waziri Mkuu alikwishalijibu swali hili siku ya Alhamisi iliyopita na akaelekeza kwamba Wanasheria Wakuu wakutane. Wabunge mlipiga makofi kuashiria kwamba hilo mmelikubali. Kwa hiyo, *ruling* yangu ni kwamba suala hili hatuliendelezi tena! *(Makofi)*

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kumuuliza swali Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Sheria ya Serikali za Mitaa ya mwaka 1982 na nyongeza zake zilizofuata, zimetoa viwango mbalimbali vya makato ambayo wakulima na wenye viwanda, hutakiwa kulipa kwenye Halmashauri zetu za Miji. Wakulima hulipa kati ya asilimia 0 - 5 ya mazao yao kama kodi ya mazao au *cess*, wakati wenye viwanda hulipa asilimia 0.3. Je, Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa tofauti hiyo kubwa, hatuoni kwamba huyu mkulima anabebeshwa mzigo mkubwa zaidi wa kodi kuliko hawa wenye viwanda ambao tungefikiri kwamba wana uwezo?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba nimjibu ndugu yangu Zambi, kwanza, nataka niliweke vizuri, sheria ile inasema:-

*"Mazao ambayo yanauzwa na mkulima yatatozwa si zaidi ya 5% ya bei ya zao hilo katika kituo ambacho linauziwa"*.

Mheshimiwa Spika, si hiyo tu, anayelipa ushuru ule si mkulima, anayelipa ushuru ule ni yule mfanyabiashara anayekwenda kununua zao hilo kwa mkulima. Kwa maneno

mengine, mkulima anabakia na fedha ile ambayo tulitaka apate, anayekwenda kugharamia atakuwa ni huyo mnunuzi, ile sheria ndivyo inavyosema.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa maana ya swali lake, ndiyo maana nimesema isizidi aslimia 5, sasa hii inategemea kati ya bidhaa moja na bidhaa nyingine. Kwa hiyo, inawezekana kabisa upande mmoja ikaonekana kama vile pengine tunafanya uonevu, lakini itategemea mazingira ya aina ya bidhaa ambayo tunaizungumzia.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nimshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kulifafanua vizuri. Kwa kuwa, sheria pia inasema kama alivyosema yeye mwenyewe, itakatwa kule ambako ndio chanzo, lakini Halmashauri nyingine zimeenda kukata pia kodi hiyo kwenye mnada kule Moshi. Sasa ni ipi tafsiri halisi unaposema kwenye chanzo au kwenye mnada kule Moshi, maana hili pia linaleta mkanganyiko wa kisheria miongoni mwa wazalishaji hapa nchini?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba nijaribu tena kutoa ufafanuzi juu ya jambo hili.

Mheshimiwa Spika, ameuliza jambo zuri na sidhani kwamba ni kwa kahawa tu, hapana, hata mazao mengine. Kwa mfano; chukua hata mazao ya mahindi tu, ukishatozwa ushuru wa asilimia tano pale kwenye kituo cha ununuzi, ukachukua mahindi haya ukayapeleka kwenye Soko la Kariakoo, pale utatozwa ushuru mwingine, unaitwa ushuru wa soko. Sasa hii haina maana kwamba ni viwango viwili vinatozwa bila sababu. Kwa hiyo, mimi naamini (sijafanya utafiti kwa kile unachoita tozo upande wa Moshi mnapokwenda kuuza kahawa) lakini, nina hakika utakuwa ni ushuru wa jambo fulani ambalo inaonekana kisheria nao ni vizuri ukawepo.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, swali langu linawezekana kuonekana kuwa kama la Mheshimiwa Dr. Tarab, lakini ni tofauti kidogo, kwa hiyo, naomba mnisikilize.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wabunge wa Tanzania Bara na Wabunge wa Tanzania Zanzibar, wanapopiga kura katika yale mambo nane yaliyomo kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika Ibara ya 98(1)(b), huwa kila upande unahitaji kuungwa mkono na theluthi mbili ya Wabunge wake, ni kwa vipi mambo haya yanakuwa?

**SPIKA:** Sijakuelewa! Inabidi Spika naye aelewe swali! *(Kicheko)*

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, ni kwa vipi Wabunge wa Tanzania Bara na Wabunge wa Tanzania Zanzibar, wanapopiga kura katika yale mambo nane yaliyomo kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 98(1)(b), huwa kila upande unahitaji theluthi mbili ya maamuzi kwa Wabunge wake, ni kwa vipi mambo haya yanafanywa?

**SPIKA:** Hilo ni jambo zuri tu!

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ni jambo zuri na mimi nakubaliana na wewe.

Mheshimiwa Khamis, tulipokuwa tunapitisha ile Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, yako mambo kwa uzito wake ambayo ilionekana ni vizuri tukapata ridhaa kwa mfumo uliueleza, ndiyo maana kuna theluthi mbili zinahitajika kwa Wabunge wa upande mmoja na theluthi mbili kwa upande wa Wabunge wa upande wa pili kwa sababu ni jambo ambalo ni vizuri pande zote mbili zikaridhia kwa kiwango cha kuridhisha. Kama ni jambo kubwa, ni vizuri mfumo huo ukaendelea.

*(Hapa Mheshimiwa Salim Hemed Khamis alisimama)*

**SPIKA:** Mheshimiwa, unaliendeleza hilo?

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Hata! Mheshimiwa Spika, nashukuru...

**SPIKA:** Huwezi kuuliza lingine sasa! Unaendeleza hilo ama?

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Hilo hilo! Mheshimiwa Spika, kwa kuwa katika mwaka 1994, wakati wa kubadilisha nafasi ya Makamu wa Rais katika nchi hii, Bunge lilipiga kura kwa theluthi mbili ya Wabunge wote waliokuwemo Bungeni; Je, Mheshimiwa Waziri Mkuu, haoni kwamba kwa utaratibu huo, Bunge lilikiuka kipengele cha Sheria, hicho ambacho sasa hivi amekizungumza cha theluthi mbili za kila upande na kwamba Makamu wa Rais yupo kinyume na Katiba tokea mwaka 1995?

**SPIKA:** Hilo ni swali la kukisia tu kwa sababu mimi nilikuwa ndiye Waziri wa Katiba na Sheria na halikufanyika hivyo anavyosema. Kwa hiyo, tunaendelea! *(Kicheko)*

**WAZIRI MKUU:** Haya, ahsante! *(Kicheko)*

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, swali langu linahusu mikataba ya ulinzi wa wawekezaji kutoka nchi ya Canada. Kwa mujibu wa taarifa iliyochapishwa katika Tovuti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Biashara ya Canada ambayo mimi nimeisoma kwa msaada wa Tovuti ya Jamii *Forum*, hivi sasa Serikali ya Tanzania inafanya majadiliano na Serikali ya Canada kwa ajili ya kulinda wawekezaji wa Canada waliopo hapa nchini na hasa wawekezaji katika Sekta ya Madini; na kwa kuwa tayari hivi sasa ripoti ya Jaji Bomani imekuwa ni mali ya Bunge na imepangiwa muda kwa ajili ya kujadiliwa, Mheshimiwa Waziri Mkuu huoni kitendo cha Serikali yako kujadiliana na Serikali ya nchi ya kigeni kuhusu suala ambalo lipo ndani ya Bunge, tunaingilia mamlaka ya Bunge? *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ni kwa bahati mbaya tu kwamba Mheshimiwa Kabwe hakuniambia tovuti hiyo inazungumzia majadiliano hayo ya wakati

gani! Kwa hiyo, kama ni majadiliano ambayo yalikuwa yameanza wakati taarifa imewasilishwa Bungeni, hakutakuwa na mgongano wa namna yoyote kwa maana tu ya taratibu zilivyo.

Mheshimiwa Spika, lakini, labda nikiri tu kwamba nitakuwa simtendei haki kama nikijidai kulijibu swali hili, kwa sababu yeye amepata *access* ya taarifa hiyo kwenye tovuti. Mimi sijaiona na sijapata nafasi pengine ya kuzungumza na Mheshimiwa Waziri Membe. Kwa hiyo, labda nitende haki kwa kusema hebu nipe muda basi na mimi nilitazame, nione kama kweli lina mgongano na pengine tuweze kufanya kitu ambacho ni kizuri zaidi. *(Mkaofi)*

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nina swali moja kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Kwa kuwa sasa hivi dunia nzima ikiwemo Tanzania tunakabiliwa na changamoto kubwa ya ongezeko la bei ya chakula na bei ya mafuta ambapo kwa nchi yetu bei ya mafuta inaonekana ndiyo imeathiri sana na maisha ya wananchi yamekuwa magumu. Ukiangalia bei za usafiri na usafirishaji zimesababisha bidhaa kuendelea kupanda na maisha kuwa magumu, je, Serikali ina mkakati gani katika kukabiliana na changamoto hiyo?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba nimjibu dada yangu Ruwanya kwamba nakubali kabisa kwamba si Tanzania tu, ni tatizo sasa karibu la Dunia nzima, nchi zote sasa tumeathirika sana na kupanda kwa bei za mafuta duniani, lakini vile vile hata kupanda kwa bei za vyakula duniani. Sasa tunafanya nini kwa upande wa mafuta? Naweza nisiwe na jibu zuri sana kwenye eneo hili lakini ninachoweza kusema ni kwamba hili jambo ni letu wote. Tunajaribu sana kuwaomba wenzetu, Mamlaka inayodhibiti Bei za Mafuta, kujaribu kufuatilia jambo hili kwa karibu ili kusiwe na ongezeko ambalo siyo la lazima sana, na ndio maana unaona taratibu zinafanywa kila wakati kubana mabasi, kujaribu kudhibiti hiyo hali isipande sana. Lakini, mimi nadhani mwisho wa yote, ni lazima turudi tuwekeze katika mambo ambayo yatatuondoa katika matumizi haya ya mafuta na hapa nawaza vitu viwili. Moja ni uwezekano wa matumizi ya gesi ambao Serikali inalifanyia kazi. Tunaweza tukafika mahali, tukapata nafuu sana kama magari mengi zaidi yanaweza kutumia mfumo wa gesi badala ya mafuta. *(Makofi)*

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa kivutio kimojawapo cha nchi yetu kwa wawekezaji ni kuwaondolea kodi na katika hotuba ya Kamati ya Fedha na Uchumi na pia katika hotuba ya upinzani, imeonyesha hiyo hali ya misamaha, kwa upande wa Zanzibar imeonyesha ilikusanywa bilioni 20 na ikasamehewa bilioni 19, nafikiri na pointi moja, hicho ni kiasi kikubwa sana, je, Serikali haioni kwamba tunao uwezo wa kudhibiti au kurekebisha sera zetu lakini hatuna uwezo wa kudhibiti bei ya mafuta Duniani? Je, Serikali haioni kwamba kuna haja ya kurekebisha sera zetu hasa za kodi kwa kuondoa hiyo misamaha ili pesa hiyo iweze kutumika kama ruzuku kwenye mafuta au kutoa kodi kabisa kwenye mafuta

kwa sababu tutakuwa na makusanyo mengine tumeyapata kutokana na kuondoa misamaha ya kodi ili kupunguza ugumu na ukali wa maisha kwa Watanzania?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, wazo lake zuri na nafikiri ni kitu kinazungumzika. Lakini niseme, katika hatua ambazo tayari tumeishafikia sasa, bajeti ya Wizara ya Fedha imeishapita, tumeishaanza kuitekeleza, tunachoweza kusema ni kwamba sawa wacha tumkabidhi Waziri wa Fedha jambo hilo, tuone kama kweli tuna uwezo wa kuchukua hatua hizo kwa lengo la kupunguza makali yanayotokana na kupanda kwa bei za mafuta. Lakini kama tukishindwa, tutarudi na kusema imeshindikana na tutaeleza kwa nini.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuuliza kuhusu maj, kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi, inasema tunapofika mwaka 2010, tutakuwa tumepeleka maji kwa asilimia 90 mijini, tutakuwa tumepeleka maji kwa asilimia 65 vijijini lakini ukiangalia kwenye bajeti ya mwaka huu ya Wizara ya Maji, ni bajeti ambayo imepunguzwa karibia kwa bilioni 84. Mheshimiwa Waziri Mkuu, bado unaamini lengo hilo litafikiwa?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, najua tatizo la maji ni kubwa kama anavyosema Mheshimiwa Serukamba. Hiyo si siri, wote tunajua tatizo ni kubwa sana. Lakini, mimi sijakata tamaa kama ambavyo Mheshimiwa Serukamba anataka kuonyesha. Nadhani bado tujipe matumaini, mnayo bado bajeti ya mwaka kesho na ya mwaka keshokutwa. Nina hakika Waziri wa Maji atakapowasilisha bajeti yake, atatueleza vile vile mipango ambayo iko ndani ya Serikali katika kujaribu kukidhi au kufikia kiwango kinachohitajika. Mimi bado ninaamini hata kama hatutafikia kiwango chote Mheshimiwa anachokisema, lakini tunaweza kuwa karibu sana na lengo tulilojiwekea. Kwa hiyo, nafikiri tuvute subira, tuone litakalotokea.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Spika, kujitegemea ni jambo la msingi sana. Ukiangalia kwenye bajeti hii, imepungua kwa sababu ya mradi ule wa Kahama ambao sasa unakwisha. Mimi nilidhani kwa sababu ule mradi ulianzishwa kwa nia njema na kwa kweli walioamua jambo lile walifanya jambo kubwa sana, kwa nini tusingeamua sasa zile pesa zilizokuwa zinaenda Kahama ziendeleze sasa miji yetu kama miji ya Kigoma, Mpanda, Urambo na Tabora?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, Serukamba anatumbukiza na Mpanda pale, lakini kwa kweli lengo lake zaidi ni Kigoma, ndiyo anataka hasa tu. (*Kicheko)*

Lakini kwa upande wa Kigoma bahati nzuri, suala la maji liko katika mradi mwingine ambao juzi tulitoa maelezo kidogo hapa. Kwa hiyo, nadhani utakapokuwa mradi ule ume-*takeoff*, inawezekana tatizo la Manispaa ya Kigoma Ujiji likapungua kabisa.

Mheshimiwa Spika, lakini niseme tu kwamba, kwa upande wa mradi ule wa kupeleka maji Shinyanga na maeneo mengine, ni kweli tulikuwa na *component local*, lakini vile vile tulikuwa na *component* nyingine ambayo ilikuwa ni kutoka nje. Sasa

kupanga ni kuchagua. Wazo analolisema Mheshimiwa Peter Serukamba ilikuwa ni sahihi kabisa, lakini nadhani wote mnajua tukifika wakati wa bajeti tunavyohangaika kuipanga, kwa hiyo, kwa mwaka huu, tuliona tufanye hivyo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, lakini nataka nikuhakikishie Mheshimiwa Serukamba kwamba kwa bajeti ya mwaka kesho, kwa mtazamo tulionao ndani ya Serikali, ni dhahiri kabisa lazima tutatoa nafasi kubwa sana kwenye Wizara ya Maji na ndio maana nasema tujipe matumaini.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, imekuwa kama desturi na desturi ni kama sheria kwamba inapotokea Halmashauri zetu za Wilaya kupata Hati Chafu na wakati mwingine kukosa watumishi wa kukaimu, hunyimwa miradi ambayo Serikali Kuu inatoa. Sasa kosa hili ni la watendaji, wanaopewa adhabu, ni wananchi na Madiwani ambao wanakuwa na nafasi ndogo sana katika kudhibiti hali hiyo isitokee? Je, Serikali inaweza kutoa kauli gani kuwapa matumaini wananchi? *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, anachokisema Mheshimiwa Selelii, kwa kiwango Fulani, ni kweli kwa maana kwamba tumekuwa na uhaba wa wataalamu hasa upande wa ile Idara ya Fedha. Lakini, wote ni mashahidi kwamba kupitia Wizara ya Fedha, tumejitahidi sana kurekebisha hiyo kasoro na sasa hivi naweza nikasema kila Halmashauri sasa hivi inao wataalamu wa fedha na inao wataalamu kutoka Idara ya Ukaguzi wa Ndani. Kwa hiyo, tunaamini jambo hili litakuwa sasa si tatizo kama lilivyokuwa hapo awali.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa upande mwingine unapoona umepata Hati Chafu, si suala la kigezo kimoja kinachosababisha wewe kupata Hati Chafu. Kwa kawaida ni mambo mengi pamoja yakiunganishwa ndiyo yanapelekea uamuzi huo kufikiwa.

Kwa hiyo, kwa upande huo Mheshimiwa Selelii, nataka tu nikutoe wasi wasi kwamba kigezo si hicho tu cha utumishi ambacho kingeweza kikarejesha lawama kwa Serikali, ni pamoja na na upungufu mwingine ambao unakuta hauna uhusiano na wa moja kwa moja na Idara nyeti kama ya Fedha.

**SPIKA**: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Waheshimiwa Wabunge, huo ndiyo mwisho wa maswali kwa Waziri Mkuu. Tunaendelea kumshukuru na kumtakia afya njema, hii nusu saa siyo nyepesi hata kidogo. (*Makofi*)

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa maswali ya kawaida, ni zamu ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji.

Na. 277

**Mradi wa Umwagiliaji Maji wa Naming'ongo**

**MHE. DR. LUKA J. SIYAME** aliuliza:-

Kwa kuwa, tarehe 24/12/2006, siku tano tu kabla mkandarasi hajaikabidhi Serikali mradi wa umwagiliaji wa Bonde ka Naming'ong'o (*Navigation Irrigation Scheme*) ulio kata ya Chitete, Tarafa ya Msongano-Mbozi Magharibi, mradi huo ulibomolewa na kusombwa na maji ya Mto Nkana kutokana na ujenzi mbovu.

Baada ya tukio hilo, Serikali ilifanya tathmini ya gharama za uharibifu huo na kuwaahidi wananchi kuwa ingeukarabati, je, ni nini kinachoendelea kwa sasa?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Luka Jelas Siyame Mbunge wa Jimbo la Mbozi Magharibi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mradi wa umwagiliaji wa Naming'ong'o, uliharibiwa na mafuriko yaliyoikumba sehemu kubwa ya nchi yetu katika msimu wa mvua wa 2006/07 na kuleta uharibifu mkubwa wa miundombinu katika maeneo mbalimbali nchini. Serikali imekamilisha tathmini ya uharibifu wa banio hilo na kufanya usanifu wa banio litakalojengwa kwenye mradi huo. Napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali imepanga kuukarabati mradi wa Naming'ong'o katika mwaka wa 2008/2009

Mheshimiwa Spika, suala la uharibifi wa mazingira katika (*catchments area*) ya mradi wa umwagiliaji wa Naming'ong'o, ni tatizo kubwa sana linalosababisha mafuriko na magogo makubwa yanayokatwa na wananchi na kusababisha uharibifu wa miundombinu ya umwagiliaji na mengine. Wizara ya Maliasili na Utalii na Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi inafanya jitihada kupata ufumbuzi wa kudumu wa tatizo la uharibifu wa mazingira katika eneo la Naming'ong'o ili kupunguza gharama za ujenzi wa miundombinu zinazosababishwa na mafuriko.

**MHE. DR. LUKA J. SIYAME:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba kuuliza maswali mawili madogo.

Kwa kuwa sambamba na ujenzi wa mradi huu, pia kulikuwa na mradi wa ujenzi wa miradi ya umwagiliaji miwili katika Kata za Kapele na Miunga katika vijiji vya Iendwe na Chilangu lakini mara baada ya kufariki Afisa Kilimo Umwagiliaji wa Mbozi mwaka jana miradi hii imesimama:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani juu ya ujenzi wa hiyo miradi miwili?

(b) Kwa kuwa magogo yanayosemekana kuharibu mazingira katika bonde la umwagiliaji la Naming'ong'o yanatoka kwenye hifadhi za misitu ya Taifa ambapo kuna walinzi ama *forest guards* wa Serikali kitu ambapo kilibainishwa mara baada ya wataalamu wa umwagiliaji na wananchi wa Kata za Bonde hilo, je, mpaka sasa kwa sababu ni toka mwaka jana ulipofanyika uchunguzi huo Serikali imefanya nini?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu miradi ile ambayo ilikuwa imepangwa kwamba ingetekelezwa na hatimaye mtaalam akafariki, napenda nimjibu kwamba kufariki kwa mtaalamu, hakutazuia miradi kuendelezwa. Isipokuwa, naomba awe na subira, siwezi kusema sasa hivi kwamba miradi ile tumeichukua katika mwaka huu, kwa sababu hotuba itasomwa jioni hii lakini pia nimpe matumaini kwamba kama miradi hiyo imefuata taratibu za uibuaji wa miradi kutoka ngazi ya Wilaya mpaka kufika katika ngazi inayotakiwa basi miradi hiyo mimi namhakikishia kwamba Serikali itaitizama na kumsaidia kuitekeleza.

Mheshimiwa Spika, kuhusu magogo, kama nilivyosema katika majibu yangu ya msingi, ni kweli kabisa tatizo la mazingira katika *catchments area* ile ni kubwa. Kama alivyosema mwenyewe kwamba magogo haya yanatoka katika sehemu ya hifadhi, tunachofanya hivi sasa kama nilivyosema hapa labda sikutaja tu kwamba Mamlaka ya Hifadhi nayo tunaishirikisha lakini yapo mambo mengi yanayotakiwa katika kushirikisha wananchi ili wasiharibu mazingira. Naomba awe na subira kidogo na mipango ambayo imepangwa au utaratibu ambao umefanywa kwa kushirikisha taasisi zote, utatolewa kwa sababu ndiyo mpango endelevu tunaoutaka isiwe wa Wizara moja tu.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, namshukuru Naibu Waziri kwa majibu mazuri kama lilivyo swali la msingi kwamba mradi huu uliharibika siku tano kabla ya *liability period* haijaisha na Waziri ametueleza kwamba mradi huu utakarabatiwa pia katika mwaka wa fedha huu, je, utakarabatiwa kwa fedha za nani, za mkandarasi au za Serikali?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, katika taratibu za ujenzi na taratibu za mikataba, zipo Kanuni zinazotawala taratibu hizo. Napenda nimweleze suala moja tu kwamba inapotokea tatizo ambalo halikutarajiwa, Kanuni tunayoiangalia ni kwamba je, mradi huo umetokea kwa uzembe wa mkandarasi au ni bahati mbaya. Kipo kipengele kinaitwa kitaalam *force majeure* katika mradi huu wa Naming'ong'o. Kilichotokea ni hicho cha *force majeure* kwa maana kwamba mafuriko yameharibu kwa hivyo fedha zitakazotumika ni fedha za Serikali.

Na. 278

**Walimu kwenye Sekondari za Kata**

**MHE. FELISTER A. BURA** aliuliza:-

Kwa kuwa wananchi wa Mkoa wa Dodoma wameitikia wito wa kujenga shule za sekondari kila Kata; na kwa kuwa Serikali kwenye bajeti ya 2007/2008 iliahidi kuajiri Walimu elfu sita kwa lengo la kupunguza upungufu wa Walimu kwenye shule:-

(a) Je, katika mwaka 2007/2008, Serikali imeajiri Walimu wangapi nchini?

(b) Je, ni Walimu wangapi waliopangiwa kufundisha Mkoa wa Dodoma ambao wameripoti na kuendelea na kazi kwenye vituo walivyopangiwa?

**MHE. GAUDENTIA M. KABAKA (NAIBU WAZIRIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Felister Bura, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007/08, Serikali imeajiri jumla ya Walimu 3861 na kati ya hao 3460 ni wa kiwango cha Stashahada na 401 ni wa kiwango cha Shahada.

(b) Mheshimiwa Spika, mahitaji ya Walimu wa elimu ya sekondari katika Mkoa wa Dodoma ni 2489. Walimu waliopo ni 1445 na upungufu ni 1044. Kwa mwaka 2007/08, Walimu waliopangwa Mkoa wa Dodoma ni 156, kati ya hawa waliopangwa ba kuendelea na kazi ni 98.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu itaendelea kuajiri na kuwapanga Walimu Mkoani Dodoma na Mikoa mingine nchini katika utaratibu wa kawaida ili kukabiliana na upungufu huo wa Walimu. Mwaka huu Julai, 2008 jumla ya Walimu 12,692 watahitimu katika Vyuo vya Ualimu na Vyuo Vikuu hapa nchini.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

(a) Kwa kuwa upungufu wa Walimu Mkoani Dodoma ni zaidi ya asilimia 50 kwa sababu wanaohitajika ni 2469 na upungufu ni 1044; na kwa kuwa bajeti ya Wizara hii imeshapitishwa na Bunge lako Tukufu, je, Wizara inawapa matumaini gani wananchi wa Mkoa wa Dodoma?

(b) Kwa kuwa Walimu waliopangwa Mkoani Dodoma ni 156 kwa mwaka 2007/08 na walioripoti ni Walimu 98 na kwa kuwa baadhi ya shule Mkoani Dodoma, hakuna Walimu wenye Stashahada wala Walimu wenye Shahada, je, Serikali inaipa kipaumbele gani Mkoa wa Dodoma katika kuwapa Walimu wenye Stashahada na Shahada kwa mwaka 2008/09?

**MHE. GAUDENTIA M. KABAKA (NAIBU WAZIRIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI):** Kwa kweli sasa hivi hatupeleki Walimu wasio na Shahada kwa shule za sekondari. Mimi hilo naona kama siyo sahihi kwamba shule za Dodoma hazina Walimu wa Stashahada na Shahada, angalau tuna Walimu wa Stashahada katika shule zetu za sekondari. Naomba tupatiwe taarifa ya shule za Mkoa wa Dodoma ambazo zina Walimu ambao siyo wa Stashahada kwa shule za sekondari.

Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza naomba nimpe matumaini Mheshimiwa Bura kwamba kama nilivyosema tunaajiri Walimu zaidi ya elfu kumi na mbili mwaka huu na katika hao, Mkoa wa Dodoma pamoja na mikoa mingine nchini itapata.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba niulize swali moja la nyongeza ikiwa ni pamoja na kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri.

Kwa kuwa, Walimu hawa wachache ambao wanapangiwa katika Mkoa wa Dodoma na baadhi yao wanapangwa katika Wilaya ya Kongwa, wamekuwa wakianza kufanya kazi kwa matatizo makubwa sana ya mishahara; na kwa kuwa baadhi yao hadi leo hawajapata mishahara ya mwezi wa saba, nane na tisa ya mwaka 2006 kwa shule nyingi za Wilaya ya Kongwa, je, Wizara inasema nini kuhusu unyanyasaji huu mkubwa hadi leomtu hajapata mshahara wa mwaka 2006?

**MHE. GAUDENTIA M. KABAKA (NAIBU WAZIRIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI):** Mheshimiwa Spika, tatizo la kutopata mishahara mapema, naomba niseme kwamba mara nyingine linatokana na Walimu wenyewe, kwanza hawaripoti kwa wakati wanapopangwa na mara nyingine wanaripoti katika shule ambazo hawakupangiwa. Wizara ina taarifa kwamba Mwalimu yupo shule fulani Mkoa fulani, kumbe Mwalimu ameenda katika Mkoa usiohusika, hilo ni tatizo moja.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo la pili, inawezekana pia taarifa kutoka kwa Wakuu wa Shule hazifiki Wizarani mapema. Lakini kama kuna tatizo ambalo ni nje ya hayo niliyoyataja na mengine ambayo hayakutengezwa na Walimu, tunaomba tupate taarifa za Walimu ambao hawajapata mishahara hususani kama kuna Mwalimu ambaye hajapata mshahara kuanzia mwaka 2006, kwa sababu sasa hivi tunatanguliza mishahara kabla ya Walimu hawajaripoti.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja la nyongeza.

Je, Waziri wa Elimu anafahamu tatizo la ukosefu wa Walimu katika Mikoa ya Dodoma, Kigoma, Tabora, Shinyanga na Rukwa kuwa inatokana na baadhi ya Watendaji Wizarani kuwabadilisha Walimu Mikoa waliyopangwa na kuwapeleka katika Mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro na Arusha?

**MHE. GAUDENTIA M. KABAKA (NAIBU WAZIRIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI):** Mheshimiwa Spika, kwa kweli tatizo hilo hatunalo kwamba Maafisa wa Wizara wanabadilisha Walimu bila ridhaa yao siyo utaratibu, lakini kama una taarifa yoyote ya Afisa yeyote aliyehusika katika kitendo kama hicho, tunaomba tuarifiwe.

Na. 279

**Ufanisi wa Ubalozi wetu Nchi za Scandinavia**

**MHE. MKIWA A. KIMWAGA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Mabalozi wanaoiwakilisha nchi yetu nchi za nje, wanatakiwa kutumia nafasi zao kukuza mahusiano ya kijamii na kiuchumi na nchi hizo kwa manufaa ya Watanzania; na kwa kuwa Ubalozi wetu uliopo nchi za Scandinavia na Baltic unahudumia takribani nchi nne, jambo linalopunguza ufanisi wa kazi:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa ni mzigo mkubwa kwa Balozi wetu aliyeko huko?

(b) Je, Serikali iko tayari kupeleka Mabalozi wa ziada katika nchi hizo ili kuongeza ufanisi wa kazi?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Ubalozi wetu nchini Sweden ndio unaoisimamia nchi nyingine za Scandinavia na Baltik. Ni kweli kwamba shughuli za mahusiano baina ya Tanzania na Nchi hizi ni nyinhgi na zenye manufaa kwetu. Kwa hivyo ni mzigo kwa Balozi aliyeko Sweden kuhudumia nchi nyingine katika kanda hiyo, lakini kutokana na ufinyu wa bajeti Serikali imelazimika kufanya hivyo. Serikali imelazimika kufanya hivyo pia kwa Balozi mbalimbali zinazoiwakilisha Tanzania nje ya nchi kama vile Ujerumani inayohudumia nchi za Poland, Czech, Slovakia, Hungary, Bulgaria na Romania. Urusi inahudumia Belarus, Georgia, Ukraine na nchi nyingine zilizokuwa kwenye muungano wa *Soviet*. Nyingine ni Belgium inahudumia Luxermberg, Netherlands na Jumuiya ya Ulaya. Italia inahudumia Uturuki, Ugiriki, Slovenia na Crotia, hali hii hata sisi hatuipendi.

(b) Mheshimiwa Spika, hali ya kifedha itakapokuwa nzuri, Wizara itawasilisha mapendekezo ya kufungua angalau Ubalozi mmoja zaidi katika nchi za Scandinavia na sehemu nyingine zenye mapungufu kama hayo ili kuzipunguzia mzigo Balozi.

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, swali la kwanza, je, Serikali hutumia sifa au vigezo gani katika mchakato wa kuwateua mabalozi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa, Mabalozi wa jinsia ya kike katika nchi za nje ni wachache; na kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba pesa itakapopatikana, wataweka mapendekezo ya kufungua ubalozi mwingine katika nchi za Scandnavia; je, Serikali haioni umuhimu wa kumteua Balozi wa kike wakati huo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Spika, suala la uteuzi wa Mabalozi, haliko chini ya Wizara yangu, mamlaka inayohusika ndiyo inayoteua Mabalozi kwa kuzingatia vigezo ambavyo mamlaka hiyo itaridhika navyo. Kwa hiyo, ukifika wakati huo, Balozi wa kike kama Idara inayohusika itaridhika na vigezo alivyonavyo mwanamke yeyote yule, basi atateuliwa.

**MHE. SUSAN A.J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi. Kwa kuwa swali la msingi lilikuwa linahusu uhaba wa Mabalozi na swali hili kwa kweli linashabihiana sana na Ubalozi wetu kule India ambao umekuwa ukipokea wagonjwa wetu, tunajua wagonjwa wengi wanapelekwa India, je, Serikali haioni kwamba kuna umuhimu sasa wa kuwa na kitengo maalumu kwa ajili ya kupokea wagonjwa ili Balozi wetu aweze kufanya kazi zingine za Ubalozi? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli Balozi wetu New Delhi, ana kazi nyingi na ni kweli kwa sasa ndiyo kituo cha kupokea wagonjwa pale.

Mheshimiwa Spika, tumeshaanza kufanya utaratibu pale kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, kupeleka mtu maalum pale wa kushughulikia masuala ya wagonjwa ili kupunguza kazi anazokabiliana nazo Balozi wetu.

**WAZIRI WA KAZI AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia ukubwa wa tatizo ambalo linaikabili Ubalozi wetu wa India, Hospitali ya Apollo imeshaanza mazungumzo na Serikali hasa kwa kushirikiana na Shirika lake la NSSF kuona jinsi ambavyo wanaweza wakafungua tawi hapa hapa Tanzania ili kuweza kuwahudumia wagonjwa wengi zaidi.

Na. 280

**Vurugu za Kisiasa Barani Afrika**

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS** aliuliza:-

Kwa kuwa chanzo kikubwa cha vurugu katika nchi za Kiafrika ni viongozi watawala kukiuka maadili ya kidemokrasia ya uchaguzi kwa kukataa matokeo:

Je, nini kifanyike ili Afrika iondokane na aibu hii?

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba utulivu, kuna wengine wanapiga kelele na upande wa Uhandisi, kuna malalamiko kwamba kuna baridi sana upande wa koshoto, sijui ni kweli au, Waheshimiwa Wabunge wawili wamelalamika.

**WABUNGE FULANI:** Ni kweli.

**SPIKA**: Kwa hiyo, ukumbi mzima ni baridi sana? Hapana.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO WA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Salim Hemed, Mbunge wa Chambani kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba kutoheshimu miiko na maadili ya demokrasia hususani kutokubali matokeo ya uchaguzi, ni chanzo kimojawapo cha vurugu na migogoro Barani Afrika. Hata hivyo, hiki si chanzo kikuu cha migogoro Barani Afrika. Migogoro mingi inatokana pia na sababu zifuatazo:

(i) Matatizo ya mipaka iliyowekwa na Wakoloni na ambayo imezigawa baadhi ya jamii za Kiafrika;

(ii) Migogoro inayotokana na matatizo ya kikabila;

(iii) Kugombea rasilimali za nchi kama vile madini, mafuta, maji na misitu;

(iv) Uchochezi wa Mataifa makubwa yanayotafuta rasilimali za Bara la Afrika;

(v) Ukandamizaji, utawala wa kimabavu na uvunjaji wa haki za binadamu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu nini kifanyike ili Bara la Afrika liondokane na tatizo hilo, Serikali ya Muungano wa Tanzania, inaamini kuwa inafaa kwa kuanzia, kujenga utamaduni wa kuheshimu dhana ya utawala bora na kukuza demokrasia, kwa kuboresha taasisi za kusimamia uchaguzi pamoja na kuweka mifumo inayohakikisha uwazi katika usimamizi wa uchaguzi katika nchi mbalimbali.

Wizara yangu inaamini kuwa mpango wa Nchi za Afrika wa kujithamini *(African Peer Review Mechanism-APRM*), ambao hivi sasa unaendelea katika nchi kadhaa Barani

Afrika ikiwemo Tanzania, ni njia muafaka ya kuimarisha demokrasia na utawala Bora. Kupitia mpango huu, nchi mbalimbali za Kiafrika zitaweza kujifunza na kuingia mifumo bora ya uendeshaji nchi pamoja na kusimamia uchaguzi Barani Afrika.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi kuuliza maswali ya nyongeza:-

(a) Kwa nini vyombo vikuu vinavyotarajiwa kusimamia demokrasia kwa mfano Umoja wa Mataifa na Umoja wa Afrika, vinasubiri mpaka watu waanze kuuana ndiyo vinachukua hatua za usuluhishi?

(b) Kwa kuwa vyombo hivi vikubwa vinavyotarajiwa kusimamia demokrasia duniani, vinaelewa wazi kwamba Rais wa sasa wa Zimbambwe na Rais wa sasa wa Kenya, hawakushinda katika chaguzi zao walizofanya hivi karibuni, Kwa nini vyombo hivi vyenye demokrasia kubwa zinazoaminika zinakubali kupinga demokrasia kwa kuwafanya wale walioshindwa washirikiane na wale walioshinda ili kufanya Serikali ya pamoja?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO WA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Spika, sikubaliani kwamba Nchi au Vyombo Vikuu vya Umoja wa Mataifa na AU, unangojea mpaka vurugu zimeanza ndipo ziingile kati, kwa sababu hata Umoja wa Mataifa na *African Union* haipendelei migogoro katika Afrika.

Mheshimiwa Spika, vile vile hatutegemei kwamba kuna nchi ambazo haziwezi kuheshimu demokrasia na utawala bora katika nchi zao, inatokea kwa bahati mbaya kama ilivyotokea Zimbabwe, Kenya ndipo nchi za AU na wasuluhishi wengine walipojitokeza kusaidia.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, haitegemewi kwamba uchaguzi unapofanyika nchi fulani kwamba zitokee vurugu kwa sababu tunaamini nchi hiyo inaamini utawala bora na inaheshimu demokrasia.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Zimbabwe, kama nilivyojibu awali, pia haikutegemewa Zimbabwe kufanya hivyo ingawa dalili zilionesha na ndiyo maana *AU* haikumtambua Rais Mugabe kama Rais halali, kwa sababu vigezo vyote huru na halali havikufuatwa ikiwa ni pamoja na wagombea kupewa haki ya kufanya kampeni, kupewa haki ya kutumia vyombo vya habari na pia wagombea kutokamatwa wakati wakiendeleza shughuli zao kampeni na ndiyo maana hata *AU* haikuridhia uchaguzi wa Zimbabwe.

Mheshimiwa Spika, *AU* ilijaribu kushawishi kwamba uchaguzi wa Zimbabwe ule wa pili usifanyike mpaka hali itakapokuwa muafaka, hata hivyo bahati mbaya, wito huo

haukusikilizwa na ndiyo maana mpaka sasa hali ya Zimbabwe iko hivyo na kwamba Rais wa Zimbabwe hatambuliki na nchi nyingine za *AU*.

Mheshimiwa Spika, hakuna hata nchi moja ilimpongeza Rais Mugabe kwa kujua kwamba uchaguzi ule haukuwa huru na wa haki na haukutimiza vigezo vyote vya uchaguzi.

Na. 281

**Matumizi ya Lugha ya Kiswahili**

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA** aliuliza:-

Kwa kuwa chimbuko la lugha ya Kiswahili ni Tanzania na kwamba nchi nyingi hivi sasa zinatafuta namna ya kufundisha katika shule na Vyuo vikuu vyao na kwa kuwa matarajio yao ni kupata Walimu wazuri wa lugha hii kutoka Tanzania:-

(a) Je, Serikali imetumia fursa hii ya kukua kwa Kiswahili Duniani na kuwapatia vijana ajira kwenye nchi jirani na za ng’ambo?

(b) Je, kwa kuwa Kongo, Nigeria na Libya ziliwahi kuomba Walimu wa kufundisha Kiswahili na zaidi ya vijana 1000 walitakiwa, je, nchi yetu ilitumia fursa hiyo vipi?

(c) Je, Serikali inajisikiaje kuona Kiswahili cha mitaani toka Kenya, kikifundishwa kwenye vyuo vya nchi za nje kama ndiyo Kiswahili fasaha?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ludovick John Mwananzila, Mbunge wa Kalambo, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali imetumia na inaendelea kutumia fursa ya kukua kwa lugha ya Kiswahili duniani. Mfano kwa kutumia mikataba ya ushirikiano wa elimu na utamaduni, watalaam binafsi wa lugha ya Kiswahili wamekwenda katika nchi mbalimbali na kujipatia ajira kama vile Burundi, Rwanda, Libya, Nigeria, Botswana, Marekani n.k.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kufuata taratibu za Kiserikali bado hawajapelekwa rasmi Walimu wa Lugha ya Kiswahili katika nchi za Kongo, Nigeria na Libya kwa sababu hadi sasa juhudi za Serikali za kuziomba nchi hizo kuleta mchanganuo wa mahitaji yao na masharti ya ajira zao hazijafanikiwa. Hata hivyo, Wizara yangu ilitoa tangazo magazetini kuwataka Walimu wa Kiswahili wenye sifa na raghba ya kufundisha Kiswahili nje ya nchi waombe kuorodheshwa kwenye *data* maalum, ili pindi nafasi thabiti za kazi zitakapopatikana waweze kupatiwa ajira hizo.

(c) Mheshimiwa Spika, Kiswahili kama ilivyo kwa lugha nyingine duniani, mtu ambaye sio mzawa wa lugha husika ni vigumu kuzungumza au kutamka kwa ufasaha kama inavyotakiwa. Aidha, kulingana na uelewa mdogo alionao anaweza pia kuwa Mwalimu wa lugha hiyo kwa wale ambao hawafahamu kabisa. Lakini kwa kufanya hivyo, ndivyo anavyojifunza lugha hiyo na kuelewa.

Mheshimiwa Spika, Serikali inajisikia vibaya pale inapoona Lugha ya Kiswahili ambayo ndiyo lugha yetu ya Taifa haizungumzwi kwa ufasaha kama vile mfano alioutuoa Mheshimiwa Mbunge wa ndugu zetu wa nchi jirani ya Kenya na hata nchi nyingine za kigeni.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ukweli huu wa matumizi mabaya ya lugha yetu ya Kiswahili yanayofanywa na wageni, pia upo ukweli wa Watanzania wenyewe kushindwa kutumia lugha hiyo kwa ufasaha. Mfano, neno mashirikiano badala ya ushirikiano, washika dau badala ya wadau, masaa badala ya saa, mauaji ya kimbali ikiwa na maana ya mauaji ya halaiki na mifano mingi tu. Kwa hali hiyo, ni vizuri sisi wenyewe tukaonyesha mfano mzuri wa matumizi ya lugha yetu ya Kiswahili kwa ufasaha zaidi ndani na nje ya nchi.

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sasa ni kipindi kama cha miaka minne tangu aliyekuwa Rais wa Nigeria, Olusegun Obasanjo, kuiomba Serikali ya Tanzania Walimu 250 kwenda kufundisha katika shule zake yeye binafsi lakini hadi leo hii Serikali haijaweza kumpa majibu ya kupatikana kwa Walimu hao:-

(a) Hivi kweli nchi hii tunajipenda kutafutia wananchi wetu kazi za nje ili tuweze kupata fedha kigeni? (*Makofi*)

(b) Serikali hii itakubaliana nami kuwa tabia hii ya Wizara na taasisi za Serikali kutojibu barua ndivyo hivyo hivyo inavyowakosesha vijana na wananchi wa nchi hii nafasi ya kufanya kazi katika mashirika kama *UN* na *AU* kwa sababu tabia ya Makatibu Wakuu kutojibu barua ndiyo kunawakosesha Watanzania kufanya kazi katika vyombo hivi na kuwatafutia Watanzania ajira katika nchi za nje? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, suala hili la Rais Obasanjo kwa Walimu 250 kwamba Serikali imeshindwa, nimeeleza katika jibu langu la msingi kwamba Serikali imewaandikia kuwaomba watuelezee kwamba utaratibu wa ajira utakuaje ili tuweze kuwapeleka na tumeshatoa matangazo kwenye magazeti ili tupate Walimu wenye sifa. Hatuwezi tu kupeleka Walimu ambao hawana sifa nchi kama vile Nigeria. Kwa hiyo, Serikali inachofanya ni kutafuta Walimu ambao wana sifa zinazokidhi ili tuweze kuwapeleka. Suala hili tunalifahamu na liko kwenye mchakato kama ambavyo nimejibu mwanzoni. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Mbunge, avute subira tu tutajitahidi na tunataka tupate ajira nyingi inavyowezekana. Wala siyo Walimu hao 250 tunatakiwa tupate Walimu

wengi tu ili waweze kwenda kule kwanza tujitosheleze sisi wenyewe ili tuweze kupeleka huko.

Mheshimiwa Spika, labda niwe muwazi kabisa sasa hivi Walimu hasa wa Kiswahili *perse,* ni kitu ambacho ndiyo tumeaanza. Chuo Kikuu cha Dodoma kinaanza kutoa Shahada ya Kiswahili. Chuo Kikuu Huria kinaanza kutoa Shahada ya Kiswahili ili tupeleke Walimu wenye sifa na Tanzania ipate sifa, siyo kupeleka makanjanja ambao wanakwenda kutia aibu kule. (*Makofi*)

Suala la pili, tabia ya Makatibu Wakuu kutokujibu barua, nataka nimwombe Mheshimiwa Mwananzila, kama anazo barua ambazo hakujibiwa baada ya kipindi hiki anipatie ili tuweze kushughulikia.

Mheshimiwa Spika, lakini mimi naamini kabisa Makatibu wetu Wakuu wanajitahidi kujibu barua na wale ambao hawajibu basi natoa wito kwamba wajibu ili isije ikaleta matatizo katika Serikali yetu kwa watu ambao hawajibiwi, si kitu kizuri, inatakiwa mtu anapoandika barua basi ajibiwe. Naomba nitoe wito kwa Makatibu Wakuu wote nchi nzima kama hawajibu barua basi ni kipindi hiki sasa wajirekebishe waweze kujibu barua hizi ili Serikali yetu iweze kuwa na utaratibu mzuri wa mawasiliano na wananchi. (*Makofi*)

**MHE. DR. CHARLES O. MLINGWA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa matumizi ya Kiswahili yakichanganywa na Kingereza, yanashika kasi sana hadi kusababisha lugha inayoitwa *Kiswanglish* je, Serikali inachukua hatua gani ya kuendeleza matumizi fasaha ya Kiswahili badala ya *Kiswanglish*? (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, napenda kukubaliana naye kwamba nchi yetu *Kiswanglish* kwa kweli kimezidi mno na kinatumika sana. Hapa niseme tu ni kubadilisha *altitude of mind*. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, na mimi nimechomekea hapo *Kiswanglish*. Ni kubadilisha mtazamo wa kuelewa hasa kutokana na kwamba tunatakiwa tuzungumze Kiswahili fasaha.

Mheshimiwa Spika, bahati mbaya, Watanzania wengi wana lugha tatu, wana lugha ya kuzaliwa, lugha ya Kiswahili na Kingereza, sasa tumeathirika. Lakini nitoe wito kwamba tukitendee haki Kiswahili, Kiswahili ni lugha ambayo sasa hivi ndiyo lugha yetu ya Taifa. Kwa hiyo, tuachane na kuzungumza *Kiswanglish*. Ukizungumza Kingereza zungumza Kingereza kabisa, ukizungumza Kiswahili, zungumzwa Kiswahili moja kwa moja. Tunapata matatizo hayo kutokana na kuathirika kwa kutumia Kiswahili na Kingereza. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari, maswali yamekwisha na muda wa maswali umepita.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. CHRISTOPHER K. CHIZA**: Mheshimiwa Spika, nawapongeza Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika , Naibu Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, Katibu Mkuu na wataalamu wote kwa kuandaa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba kuchangia kuhusu matrekta. Tanzania ina eneo la hekta milion 44 zinazofaa kwa asilimia 25 tu. Aidha, eneo linalofaa sana kwa kilimo cha umwagiliaji ni hekta milioni 23. Maeneo haya hayawezi kulimwa kwa kutumia nguvu kazi *(family labour)* ya familia. Kwa kuwa jambo hili ni la muda mrefu, Wizara inachukua hatua gani za makusudi kuongeza upatikanaji wa matrekta na zana nyingine za kilimo hasa kwa wakulima wadogo?

Mimi nashauri, pamoja na kutumia *SACCOS* kuwepo na mkakati maalum wa kuzishawishi Halmashauri za Wilaya kuwadhamini wakulima ili wakope zana za kilimo. Utaratibu unaoendelea hivi sasa hauwapi nafasi wakulima wadogo kukopa zana za kilimo kwa wingi.

Kuhusu mfuko wa pembejeo, pamoja na mfuko huo kuwa na fedha kidogo, mimi nimesikia malalamiko kutoka kwa wakopaji wakidai kwamba mkopo ukitolewa, mfuko hautoi *grace period* ya kuanza kulipa. Ingefaa *grace period* izingatie msimu wa mavuno na siyo kukopa mwezi mmoja na kuanza kulipa mwezi unaofuata. Kama hivyo ndivyo nadhani kuna haja ya kurekebisha.

**MHE. PROF. PHILEMON M. SARUNGI**: Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumpongeza Mheshimiwa Stephen Wasira, kwa hotuba yake inayotoa dira, mikakati na mwelekeo wa nchi yetu kujitosheleza kwa chakula, kuongeza mazao ya biashara na kupanua, masoko. Nampongeza kwa mipango mkakati kwa kufufua na kuimarisha vyama vya ushirika kama chombo cha ukombozi cha wakulima na pia uti wa mgongo wa uchumi wa Taifa letu. Nampongeza Naibu Waziri, Katibu Mkuu na maafisa wote na wataalamu wa Wizara kwa kazi nzuri wanayofanya.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia hotuba hii kama ifuatavyo, kuimarisha kanda za kilimo cha mazao ya chakula na mazao ya biashara katika Wilaya ya Rorya katika lengo la kuboresha kilimo endelevu na lenye tija katika Wilaya ya Rorya.

Katika Wilaya ya Rorya kuna kanda mbili za kilimo ambazo ni Kanda ya Nyanda za Chini – Tarafa za Nyamicho, Luo-Imbo na Suba. Wastani wa mvua ni 500mm kwa mwaka. Mazao ya chakula ni mihogo, mtama na viazi vitamu.

Mheshimiwa Spika, ombi langu kwanza ni kuhusu kilimo cha pamba, kimefanyiwa majaribio katika kata za Wamuge (Suba) Roche na Goribe (Birango) na kuonyesha kuwa pamba inastawi katika Nyanda za Chini Wilaya ya Rorya. Wananchi wanaomba wapatiwe mafunzo, mbegu za kutosha na wataalamu wa kutosha ili wakulima

katika Nyanda za Chini katika tarafa za Nyamcho, Suba, Luo-Imbo na sehemu ya tarafa ya Girango waweze kulima pamba kama zao la biashara. Kwa sasa hawana zao la biashara na kwa kuwa Mheshimiwa Waziri wewe kama Mbunge wa Bunda umefanya kazi nzuri sana kuhusu kilimo cha pamba katika Wilaya ya Bunda ambayo inaongoza kuhusu kilimo cha pamba mkoa wa Mara na hata Kanda ya Ziwa. Nakuomba kama mtaalamu wa zao la pamba kwa niaba ya wananchi wa Rorya uwasaidie kama wananchi wako.

Kuhusu kilimo cha Kahawa. Zao hili linalimwa kama zao la biashara katika Kanda ya Nyanda za Juu katika kati zao Ikoma, Goribe na Koryo tarafa ya Girango, mvua za maeneo haya wastani kati ya 700mm hadi 900mm kwa mwaka. Mazao ya biashara ni pamba, kahawa, alizeti na katani. Ombi, wananchi wawezeshwe kuongeza uzalishaji wa kilimo cha kahawa kwa kila hekta kwa mwaka. Kuwawesha wakulima kupata mafunzo na teknolojia ya kilimo cha zao la kahawa kwa lengo la kuongeza tija, mavuno, pato la wakulima na kupiga vita umaskini.

Mheshimiwa Spika, kilimo cha Alizeti. Kilimo cha zao la alizeti limeanza kulimwa katika kata ya Koryo, Mirare, Bukwe, Kitembe (Tarafa ya Girango), Komuge (Suba), Rabour (Tarafa ya Luo-imba). Majaribio ya kilimo cha alizeti kama zao la biashara yameonyesha mafanikio makubwa. Ombi, kilimo cha zao la alizeti, kiendelezwe na Wizara katika tarafa zote za Wilaya ya Rorya kama zao la biashara.

Kuhusu kilimo cha mkonge unalimwa katika kata za Koryo Nyathorogo na Goribe, Wizara isaidie kwa utaalamu kuendeleza kilimo cha katani kama zao la biashara.

Mheshimiwa Spika, Wilaya mpya ya Roya wananchi wake hawana zao la biashara. Wananchi wametambua umuhimu wa kutumia ardhi kubwa ambayo hadi sasa haijapata msukumo wa kutosha kuhusu kilimo ili waweze kujitosheleza kwa chakula na kuuza mazao ya biashara. Mpango wa kuanza kilimo cha mazao mapya lenye soko la hakika yataanza kulimwa, mazao hayo ni mananasi, vitunguu, pilipili, ufuta na artemizia. Wanaomba Wizara iingize mpango wa kilimo cha mazao ya biashara Wilaya ya Rorya katika mpango wa Kitaifa. Naomba, tena naomba msaada.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DR. JAMES A. MSEKELA**: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu wake na timu nzima ya wataalamu wakiongozwa na Katibu Mkuu, Bwana Peniel Lyimo, kwa kazi nzuri ambapo Wizara inaendelea kuifanya.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Wizara hii ni nyeti katika nchi yetu hasa kwa kuwa wananchi wapatao 85% ya Watanzania wote wanaishi kwa kutegemea kilimo cha mazao ya chakula na biashara na kilimo chao hawa ni kile kinachoendelea kutegemea zana duni, hususan jembe la mkono na pembejeo chache, aghali na zinazochelewa kuwafikia katika msimu husika. Kwa maana hiyo basi, tutaendelea kuiomba Wizara na Serikali kwa ujumla, kumsaidia mkulima huyu mdogo ili aweze kuwa na kwanza nyenzo

na zana mwafaka na pili, mbegu bora na pembejeo zingine muhimu ambavyo atavipata kwa bei nzuri ikiwezekana, hata kwa ruzuku ya Serikali, na tatu, masoko ya uhakika na bei nzuri. Kila mkulima nchini anastahili kusaidiwa kuyapata yote haya bila kubaguliwa.

Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Serikali kwa kuendelea kufanya hivyo kupitia programu mbalimbali zinazotekelezwa chini ya *ASDP* na mipango mingine. Hata hivyo, bado kuna mahitaji makubwa sana ambayo yanaipa Serikali yetu changamoto kubwa na kuitaka kuendelea kujielekeza kwa karibu na kwa upana zaidi katika kumhudhumia huyu mkulima mdogo. Hapa ningependa kushauri Wizara iongeze ugatuaji wa shughuli zake kwenda katika Halmashauri zetu za Wilaya. Zoezi hili lihusishe upelekaji wa wataalamu na fedha huko katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, lakini pia kumeendelea kuwa na haja ya bodi za mazao mbalimbali kujikita zaidi katika kumsaidia mkulima huyu mdogo, zaidi ya wanavyoonekana kufanya hivi sasa. Wakulima wengi hupata hisia kuwa wanaachwa kujitetea wenyewe mbele ya sekta binafsi ya wenye fedha (makampuni), ingawa utaratibu wa stakabadhi ya maghala unabadilisha picha hiyo. Ndiyo maana namwomba Mheshimiwa Waziri na timu yake kuweka nguvu ya kueneza hilo mithili ya alivyofanya kwa mkoa wa Mtwara na Lindi katika zao la korosho.

Mheshimiwa Spika, swali la kujiuliza ni kwa namna gani na lini Wizara itaanzisha utaratibu wa sheria ya stakabadhi ya maghala katika zao la tumbaku?

Mheshimiwa Spika, pia ningependa kumuuliza Mheshimiwa Waziri kuhusu mpango wa Wizara katika upelekaji wa pembejeo ya ruzuku mwaka huu wa 2008/2009 katika mkoa wa Tabora kwa wakulima wa tumbaku kuna mpango gani?

Mheshimiwa Spika, pia, msimu huu wa mauzo ya tumbaku, sarafu ya Kimarekani yaani dola imeendelea kutumika lakini hadi kufikia sasa malalamiko yamekuwa mengi sana kutoka kwa wakulima kwamba sarafu hii ya kigeni inawachanganya, hasa kutokana na kubadilika kwa thamani ya sarafu hiyo dhidi ya shilingi yetu ya Tanzania kiasi kwamba wakulima wamenituma kusema kwamba hawataki tena kuuza tumbaku yao kwa dola za Kimarekani na kwamba wanataka sarafu yetu ya Tanzania itumike. Katika kufanya hivyo, wametaka uwepo umakini zaidi katika kupanga bei kwa shilingi huku ikizingatiwa bei ya wastani ya dunia. Je, Mheshimiwa Waziri atatoa tamko gani?

Mheshimiwa Spika, kumeendelea kuwepo madaraja mengi sana ya tumbaku kitu ambacho kinaendelea kuwasumbua wakulima katika kupanga tumbaku zao katika madaraja hayo mengi kwa usahihi, huku kukiwa na hisia kwamba wanunuzi hutambua tumbaku zao kuwa za madaraja hafifu na hivyo kutoa malipo duni kwa wakulima, kitu kinachowafanya wabakie katika lindi la umaskini bila matumaini ya kujikwamua kupitia zao hili ambalo linaendelea kuwasumbua wakulima katika kupanga tumbaku zao katika madaraja hayo mengi kwa usahihi, huku kukiwa na hisia kwamba wanunuzi hutambua tumbuka zao kuwa za madaraja hafifu na hivyo kutoa malipo duni kwa wakulima, kitu kinachowafanya wabakie katika lindi la umaskini bila matumaini ya kujikwamua kupitia

zao hili.  Je, Serikali sasa itaona madaraja haya yakipunguzwa ili yawe machache kama ilivyo katika zao la pamba?

Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Serikali kwa namna inavyoendelea kuwashirikisha wakulima kuibua miradi ya *DADPs*, ikiwepo ujenzi wa majengo ya soko katika maeneo ya vijijini.  Rai ninayopenda kuitoa hapa ni kuwa na ramani ya majengo haya ikilenga kuwa na eneo la kuuzia mazao mchanganyiko ya wakulima hawa. Majengo haya yawe tofauti na masoko ya mjini ambako lengo ni kuuzia mazao mchanganyiko ya wateja kwa rejareja.

Mheshimiwa Spika, masoko ya wakulima hawa yanatarajiwa kuwa ni mahali ambapo wakulima watauza mazao yao kwa wingi (madebe/magunia).  Hii itawarahisishia wakulima hawa kuuza mazao yao mchanganyiko kama vile mahindi, ufuta, maharagwe, karanga, alizeti na kadhalika.  Utaratibu uweze kuwekwa kwamba siku ya Jumatatu kwa mfano, yaweza kuwa ni siku ya kuuza karanga tu ili kwamba wakulima wenye zao hilo walifikishe sokoni siku hiyo ili kuwawezesha wanunuzi wakubwa kufika huko vijijini na kufanya ununuzi kwa gharama ndogo, huku wakulima pia wakiwa wamepunguziwa usumbufu wa kutafuta walanguzi wa kila mmoja madebe yake mawili, matatu hivi tu ama kiasi kingine kidogo.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu pia ni kwamba masoko haya ya *DADPS*, yajengwe karibu na maghala yaliyopo katika vijiji husika kwa kadri inavyowezekana. Hii itakuwa pia njia ya upanuzi wa fursa za kufanikiwa katika matumizi ya sheria mpya ya stakabadhi ya maghala, mfumo ambao pia utasaidia sana wakulima kupata *bridging finance* wakati wanasubiri bei nzuri kwa mazao yao.

Mheshimiwa Spika, napenda nimalizie mchango wangu kwa kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika.

**MHE. AZIZA SLEYUM ALLY:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri na Naibu wake kwa kazi nzuri wanayofanya.  Pia watendaji wote.

Mheshimiwa Spika,  naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, suala la ununuzi wa tumbaku kwa dola sasa linaonekana kama ni tatizo, yote haya yanatokana na wananchi hasa wakulima kuwa hawana mwamko wa kutumia dola.  Je, Serikali inasema nini kuhusu kero hii na kuwafahamisha wananchi hapa bungeni?

Mheshimiwa Spika, napenda kufahamu hivi hizi pembejeo zina kuwaje ni ghali zaidi kwa wakulima na tunasema kilimo kishike hatamu wakati pembejeo hazipatikani ni sawa na kufuga nywele na kitana huna.

Mheshimiwa Spika, nina mashaka sana na muundo wa Wizara.  Wizara haina muundo mpaka chini watendaji wanao wajibika katika Wizara hiyo.  Ilivyo sasa watendaji hao huwajibika TAMISEMI, kama kweli tunahitaji kubadilika tufanye

kinachokuwa na muundo ambao watendaji hawa wawajibike Wizarani na kwa Wakuu wa Wilaya na Mkoa wawe ni wasimamizi wa shughuli hiyo bila ya hivyo tutatimba bila ya kucheza.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kanuni bora za kilimo kwa wakulima, kanuni hizo hufanyika au kutofanyika maana hata viwanda tulivyosema vijengwe kutokana na mazao ya hapa nchini hayana pa kwenda mengine huoza.

Pia Wizara iweze kuangalia wakulima wanaoamua kulima alizeti na karanga na kuamua kuachana na kilimo cha mazao mengine ambayo wanaona hayana tija tena kwao waangalie sana wasije kuacha kilimo cha chakula na kuanza kulima mazao ya biashara kama hayo niliyoyataja.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimwia Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wasaidizi wake, wakurugenzi na watumishi wote na idara zilizoko chini ya Wizara yake na watumishi wote hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, mpaka leo bado usemi wa kilimo ni uti wa mgongo hapa kwetu, lakini mimi naona usemi huo si sahihi kwa sababu kilimo hapa kwetu kimekuwa umiza migongo ya wakulima, kwa sababu Serikali haiwajali wakulima kwa kuwapatia pembejeo mbalimbali kama vile mbolea, mbegu bora, zana za kilimo na kadhalika. Hata mikopo wanayopewa ina masharti magumu mpaka wanashindwa kurudisha pia mikopo ni muda mfupi kiasi kwamba wanakuwa haiwezi kufanya kazi ya kilimo kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa wataalamu wa ugani bado hawatoshi kwa hiyo, kuna umuhimu sana wa kuongeza jitihada ya kutenga fedha za kutosha ili kutoa mafunzo kwa vijana wetu wengi na hatimaye waajiriwe na kufanya kazi za ugani vijijini pia hata wataalamu wa utafiti hawatoshi kwa hiyo waongezwe na kupewa vitendea kazi.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa mikoa ya Singida, Dodoma, Manyara, Shinyanga, Tabora, Kigoma na Iringa na mikoa mingine ni wakulima wazuri sana wa mazao ya biashara kama vile alizeti, karanga, ufuta, mawese na kadhalika kwa nini mpaka sasa mazao haya hayaundiwi bodi? Kwa nini Serikali haiwatafutii wakulima wanunuzi wa kudumu na mpaka leo kwa nini Muswada hauletwi hapa Bungeni. Kuna nini kinafichwa kwenye Muswada huo na kwa nini mpaka leo Serikali haijarudisha asilimia kumi ya kodi ya mafuta yanayotoka nje mafuta ambayo hatujui ubora wake na yakiingia hapa nchini yanafanya bei ya mbegu za mafuta yetukushuka thamani.

Mheshimiwa Spika, kuonyesha ya kwamba mazao ya mbegu yanayolimwa na wakulima wetu hayathaminiwi kwa sababu mpaka leo toka sheria ya stakabadhi ya mazao ghalani mpaka leo haifanyi kazi. Mwanya huu unawafanya wakulima wetu waendelee kulanguliwa na walanguzi.

Mheshimiwa Spika, tunazungumzia kuondoa umaskini kwa wakulima wetu huo umaskini utaondokaje? Kama hatuwajali na kuwahudumia ipasavyo wakulima wetu

wataendelea kutumia jembe la mkono mpaka lini? Lini wakulima wetu watapata pembejeo zinazotakiwa, masoko mazuri na kadhalika?

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Singida umeanza kulima pamba, wananchi wengi wa Iramba Mashariki maeneo ya Lyelambo, Yulanzoni, Msingi, Kidi na kadhalika ambao huko nyuma waliacha kulima pamba wakaanza kulima alizeti na mazao mengine lakini baada ya ushawishi kutoka bodi ya pamba wamenza kulima tena na msimu wa mwaka huu ulizinduliwa Lyelembo Iramba Masharika bei ya shilingi 400 kwa kilo, hivi bei hii inatosha kweli kurudisha gharama zilizotumika na mkulima apate faida? Baadhi ya wakulima wanasema bei hizi zikiendelea wataacha na kurudi kulima alizeti ambayo ukulima wake ni rahisi hauhitaji dawa na palizi ni mara moja tu.

Mheshimiwa Spika, wakulima wetu wanalima mazao kwa ajili ya chakula chao lakini mpaka leo dawa za kuhifadhia mazao hazipatikani na zinazopatikana vijijini haziui wadudu.

Mheshimiwa Spika, Madiwani wa Wilaya ya Iramba tumeamua kuleta mapinduzi ya kilimo tunaomba wataalam wa kutosha waletwe, tupewe fedha za kujenga maghala ya kuhifadhi mazao yetu, maafisa ushirika waletwe ili kutoa elimu ya ushirika na pia kudumisha na kuongeza *SACCOS* kila kata.

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Spika, utabiri wa hali ya hewa, taasisi ya hali ya hewa nchini *(TMA)* wana uwezo sasa hivi kutoa utabiri wa hali ya hewa kwa muda wa miezi mitatu mbele (msimu).

Taarifa zao za utafiti huzisambaza kwa Ma-*RC,* Ma-*DC* na ofisi/idara zingine.

Matatizo/mapungufu yaliyopo ni pamoja na taarifa hizi mara nyingi huchelewa kufika Wilayani kwa mfano taarifa za Novemba/Desemba zinafika Wilayani Juni/Julai mwaka ufuatao, taarifa hizi zinapofika zimechelewa huwekwa kwenye mafaili na ndio mwisho wake zinabaki kuwa kumbukumbu.

Athari zake ni kuwa wakulima wanaendelea kupanda mazao kwa kubahatisha. Mfano, msimu uliopita wa kilimo mkoa wa Mwanza na sehemu ya mkoa wa Shinyanga ulikuwa na ukame (mvua haba). Matokeo yake wakulima kwenye mabonde na mbuga *(black cotton soil)* waliopanda mpunga hawakuvuna, wakati wangepanda mahindi au pamba wangevuna.

Ushauri, wadau wakuu wa tabiri za hali ya hewa ni Serikali za Mitaa kwa maana ya Halmashauri, kwa hiyo Halmashauri zielekezwe kuwajibika kupata tabiri za hali ya hewa kabla ya msimu kwa mfano Kanda ya Ziwa kuna misimu miwili kwanza mvua za vuli na pili, mvua za masika. Halmashauri zipeleke taarifa hizi kijijini na Madiwani, Wenyeviti wa vijiji na vitongoji wafanye mikutano ya kuwaelewesha wananchi juu ya taarifa hizi na ni mazao gani ya kupanda. Ma-*Veo* wabandike kwenye mbao za

matangazo taarifa hizi ambazo zitakuwa na ushauri wa kitaalam wapande mazao gani msimu husika.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, chakula ni uhai na hivyo kilimo ni lazima kipewe kipaumbele hasa ikizingatiwa kuwa zaidi ya 80% ya Watanzania ni *peasants*. Pamoja na kwamba bado kilimo chetu si cha kisasa na kwamba Serikali imeshindwa kwa kiasi kikubwa kuboresha kilimo hicho ikiwa ni pamoja na kutoa pembejeo kwa mikopo nafuu na dawa na mbolea. Lakini pamoja na nchi yetu kuwa karibu na *equator* na hivyo kukosa mvua za kutosha na nyakati nyingine kukosa mvua kabisa, bado Serikali imeshindwa kabisa kuwa na kilimo cha umwagiliaji ambacho ndio kingekuwa jibu sahihi kwa kupata mavuno ya uhakika kila mwaka na hata kuvuna mara mbili. Tanzania imejaaliwa mabonde mengi yenye rutuba na pia tuna vyanzo vingi vya maji kama maziwa, mito na mabwawa, hivyo kama kweli Serikali ikiamua kuwekeza katika kilimo cha umwagiliaji wananchi wangeweza kupata chakula cha kutosha na cha ziada.

Kuhusu bei za vyakula, bei huwa zinasaidia sana ama kuboresha kilimo au kutelekeza kilimo. Kwa bahati mbaya sana bei za bidhaa mbalimbali za vyakula zimekuwa ndogo na haziendani kabisa na mfumuko wa fedha yetu. Kibaya zaidi miundombinu yetu ni mibovu sana hasa katika mikoa ile inayotoa mazao kwa wingi *big four* hivyo kufanya bei za mazao kuwa chini sana na kuvunja ari na moyo kwa wakulima hao. Kwa mfano, bei ya gunia moja la mahindi Sumbawanga ni shilingi 5,000/= wakati gunia hilo likifika Dar es Salaam linakuwa shilingi 50,000/=. Hii inafanya wafanyabiashara wapate faida kubwa sana huku mkulima aliyeumia sana na kilimo hicho akiambulia patupu. Kwa hili kuna haja kubwa sana kwa Serikali kununua bidhaa hizi kwa wakulima au vyama vya ushirika ili kusaidia wakulima. Gharama za usafirishaji zimekuwa zikipanda kila mwaka na hakuna siku zitapungua. Je, Serikali basi haioni ni busara sasa Serikali kuingilia kati ili kuwasaidia wakulima hawa maskini.

Kuhusu kuuza mazao nje ya nchi, imekuwa ni kawaida kwa wakulima kuzuiwa kuuza nje ya nchi mazao yao. Kimsingi ni jambo zuri kwani ilikuwa tabu kama mazao yatauzwa halafu tulie njaa. Lakini lazima Serikali iwe makini kwani kutokana na uwepo wa soko huria na kwa kuwa bei za nje zinaweza kuwa kubwa zaidi ni vyema Serikali iruhusu kwa kiwango kinachowezekana kwani inawezekana mkulima akawa na tani zaidi ya 20 kwa vyovyote vile ni lazima aziuze. Serikali kwa kushirikiana na Halmashauri wanaweza kutambua wakulima wenye mazao mengi na hivyo kuuza popote watakapo ili mradi hawavunji sheria.

Kuhusu wataalamu wa kilimo, kwa kuwa kilimo ni msingi wa maendeleo ya nchi kwani bila chakula hatuwezi kuishi na tumbo lenye njaa kamwe halitaweza kufanya kazi yoyote ile ya uzalishaji. Kutokana na kilimo cha kisasa kuna umuhimu mkubwa sana kwa sasa kuwa na wataalamu wa kilimo ili kilimo chetu kiboreke na kiwe cha kisasa zaidi. Ni jambo la kusikitisha kuona hadi leo bado tuna upungufu mkubwa sana wa wataalamu na hadi leo tuna wagani 309 tu kati ya 2,500. Hii ni sawa na 13% tu. Kwa mwendo huu ni dhahiri kwamba bado kilimo chetu kitakuwa ni cha asili na sio cha

kisasa. Tuliomba wale wanaosomea shahada za kilimo wapewe udhamini *(grants)* ili wasome kwa wingi na bila matatizo ya kufukuzwa kwa kukosa fedha za ada.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mazao ya mafuta *(Biofuel),* pamoja na kupanda kwa bei za mafuta duniani bado wazo la Serikali la kuwekeza katika *biofuel crops* si la msingi, kwani bado hatujajitegemea kwa chakula. Mazao ya *biofuel* sio tu yataua yale ya kilimo cha chakula lakini pia yatafanya wakulima wengi kuhama katika kilimo cha *biofuel* hasa ikizingatiwa bei zake zitakuwa za juu kuliko chakula. Hii ni hatari.

Mwisho naomba Serikali iache huu wimbo wa *green revolution* kwani kila mwaka unaimbwa lakini mapinduzi hayo hayaonekani zaidi ya kuzidi kuomba chakula nje ya nchi kila mwaka na maeneo mengi ya kilimo kuonekana kame na hivyo suala zima la kijani kutokuwepo.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri yenye ufafanuzi wa kina kuhusu Wizara yake.

Pili, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Pamoja na kuunga mkono hoja hii napenda kuchangia maeneo yafuatayo:-

Kwanza ni kuhusu sekta ya ushirika (Maendeleo ya Ushirika). Kwa kuwa mkoa wa Dodoma hauna chama kikuu cha ushirika; na kwa kuwa wananchi wa mkoa wa Dodoma wanapata shida mahali pa kuuza mazao yao; na kwa kuwa mkoa wa Dodoma ikiwemo Wilaya ya Mpwapwa kila kata wameunda *SACCOS.* Je, Serikali haioni umuhimu wa kuunda chama kikuu cha ushirika mkoa wa Dodoma? Je, vigezo gani vinavyotumika kuunda chama kikuu cha ushirika? Je mkoa wa Dodoma kuna *SACCOS* ngapi zimeundwa na ngapi zimepata mikopo ya kuongeza mitaji yao? Je, vyama vikuu vya ushirika vingapi vina matatizo na madeni makubwa na Serikali imeweka mikakati gani kusaidia vyama hivyo ili wananchi waendelee kuuza mazao yao bila matatizo.

Kuhusu huduma za ugani, kwa kuwa huduma za ugani ni muhimu sana katika sekta ya kilimo; na kwa kuwa maafisa ugani ni wachache sana. Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka afisa ugani kila kijiji ili aweze kutoa ushauri kwa wakulima na hii itasaidia sana kuboresha hali ya kilimo katika nchi yetu. Je, Serikali ina mpango gani wa kupunguza bei ya pembejeo, mbolea, matrekta, majembe ya kukokota na mifugo, dawa za mazao na kadhalika? Hii itasaidia wananchi kupata pembejeo kwa wingi na kwa bei nafuu na kuboresha hali ya kilimo katika nchi yetu.

Kwa kuwa vyuo vya kilimo ni vichache na ili kupata wataalam wengi wa kilimo ipo haja ya kujenga chuo cha kilimo kila mkoa ukianzia mkoa wa Dodoma ambapo kuna vituo vya utafiti wa kilimo, Hombolo na Makutupora, majengo yapanuliwe ili viwe vyuo vya kilimo. Kwa kuwa Serikali ilikuwa na mpango wa kuunda bodi ya mazao mchanganyiko na hadi sasa bodi hiyo haijaundwa, je, kuna sababu gani za kutokuunda bodi ya mazao mchanganyiko?

Kwa kuwa watumishi wa Wizara ya Kilimo wanafanyakazi katika mazingira magumu ya kukosa vitendea kazi kama vile magari, pikipiki na maslahi duni, je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia vitendea kazi kama magari, pikipiki kwa ajili ya huduma ya ugani na hasa vijijini ambako ndipo wakulima wengi wapo pia maslahi yaboreshwe ili maafisa ugani wa kata na vijiji kuboresha utendaji katika maeneo yao ya kazi.

Kwa kuwa Wilaya ya Mpwapwa na mkoa wa Dodoma kwa ujumla mazao ya chakula katika msimu huu hayatakuwa mazuri, je, Serikali imeweka akiba ya chakula ngapi ili kuhudumia familia zitakazokuwa na upungufu wa chakula katika Wilaya ya Mpwapwa na Mkoa wa Dodoma kwa ujumla?

**MHE. JUMA A. NJWAYO**: Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumpongeza Mheshimiwa Stephen Masato Wasira, Naiba Waziri Mheshimiwa Dr. David Mathayo David na watendaji wa Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa jitihada na hatua wanazochukua kukabiliana na changamoto mbalimbali zinazojitokeza kwenye Wizara yao.

Mheshimiwa Spika, ufuatao ni mchango wangu kwa Wizara hii, mosi napenda kuipongeza Wizara hasa Mheshimiwa Stephen Wasira, kwa kusimamia vizuri sheria ya stakabadhi ghalani kwenye zao la korosho. Msimamo wake, ukaribu wake wa mapenzi makubwa kwa nchi yake imesaidia sana kuboresha mapato ya wakulima wa korosho pia kuvijengea uwezo vyama vya ushirika vya msingi. Hivi sasa baadhi ya vyama vya msingi Mambamba na Mahuta ambayo viko jimboni kwangu Tandahimba viko kwenye hatua ya mwisho ili kukopa magari (malori). Jambo hili linawezekana sasa kwa msimamo na uimara wa Waziri Mheshimiwa Stephen Wasira na Serikali yote, hongera.

Mheshimiwa Spika, pili, napenda kushauri kuwa Wizara iache mara moja kupeleka fedha za *export levy* kwa bodi ya korosho. Fedha hizo zipelekwe moja kwa moja kwa halmsahauri husika kwani kupitishia bodi ya korosho ni kwenda kinyume na sheria ya *Finance Act, 2006/2007* kwani sheria hiyo haitaji bodi kupokea fedha hizo.

Mheshimiwa Spika, tatu, napendekeza pia mabadiliko madogo ya namna ya kugawa fedha za *export levy*. Kwa maoni yangu bado ipo haja ya bodi ya korosho kupewa 1%, Ari Naliendele 1% na inayobaki ipelekwe kwa halmashauri. Hii itasaidia sana kwenye uendeshaji wa shughuli zinazohusu korosho kwa bodi na pia ufanisi wa utafiti mbalimbali. Hali ya sasa Wizara kutoa fedha za Bajeti yake kwa vyombo hivyo hazitoshi kuendeleza zao hili.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa uzalishaji wa chakula ni mdogo nchini jambo linalochangia kupanda kwa bidhaa za chakula, ushauri wangu sasa tuanze kilimo cha lazima cha angalau hekta moja kwa kila kaya nchi nzima kwa mazao ya chakula (nafaka). Tukifanikiwa tutaboresha hali ya chakula nchini.

Tano, ili kuongeza thamani ya zao la korosho kwa kutumia vikundi vinavyobangua korosho vikakopeshwa na mfuko wa pembejeo mashine ya kubangulia korosho ili kusaidia thamani ya korosho kuongezeka na kuongeza ajira kwa wananchi.

Sita, ni vyema ili kuongeza tija na utaalamu katika kilimo na chakula wanafunzi wanaomaliza kozi mbalimbali za kilimo wakapata ajira moja kwa moja kama ilivyo kwa walimu badala ya kuhangaika kuomba ajira hizo. Naunga mkono hoja.

**MHE. KILONTSI M. MPOROGOMYI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuipongeza Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa kazi nzuri na mipango waliyonayo kuhusu kilimo nchini. Nampongeza sana Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika Mheshimiwa Stephen Wasira, Naibu Waziri Mheshimiwa Davidi Mathayo David, Katibu Mkuu, Peniel Lyimo na wataalamu wote katika Wizara hiyo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Yapo maeneo machache ambayo ningependa kupata ufafanuzi wakati wa kufunga hoja ya Wizara hii. Kuhusu *COASCO* kama chombo kinachotakiwa kuboresha tija ya ushirika hivi sasa kina migogoro mingi ambayo inahitaji kutatuliwa. Katika kipindi cha zaidi ya miaka miwili iliyopita *COASCO* imegubikwa na kesi na migogoro mingi. Matumizi ya fedha nyingi za chombo hiki badala ya kushughulikia ushirika zimekuwa zikitumika kuendesha kesi (zaidi ya shilingi milioni150 zimetumika).

Mheshimiwa Spika, aliyekuwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika Mheshimiwa Profesa Peter Msolla alipotembelea Shirika hili mwezi Aprili, 2008, alitoa maagizo ya kuhakikisha kesi zinarudishwa mezani kwa majadiliano. Mkurugenzi Mkuu wa *COASCO* alipuuza agizo hilo na kesi zimeendelea kufunguliwa na mfuatiliaji wa kesi hizi ni Mkurugenzi Mkuu mwenyewe na haijulikani kazi zingine za uzalishaji na ukaguzi anazifanya wakati gani. Kutoka Juni, 2007 *COASCO* haina bodi kwa nini? Makisio ya bajeti ya *COASCO* yaliyoletwa Wizarani na hatimaye Bungeni, hayakupitishwa na bodi kama sheria ya *COASCO* inavyotaka (kifungu Na.15 (13). Nani ahidhinishe bajeti hiyo? Je, Mkurugenzi Mkuu, aliomba msaada wowote toka Wizarani?

Kwa kuwa kilimo cha kahawa katika vijiji vya Muhinde, Nyamboze na Mabunga tarafa ya Manyovu vimepanuka na kwa kuwa wananchi wa kijiji cha Muhinde wangependa kuwa na chama chao cha ushirika, Je, Serikali inasemaje juu ya jambo hili?

Napendekeza waruhusiwe kwa sababu wanazalisha kahawa nyingi zaidi kuliko vijiji vya jirani kama vile Nyamboze ambao wana chama chao cha ushirika, kijiji cha Mwayaya ambao pia wana chama chao cha ushirika.

Kuhusu pembejeo, kwa kuwa pembejeo ya ruzuku haiwafikii wakulima wengi katika tarafa ya Manyovu na Kalinzi Wilayani Kigoma na Kasulu ambo ni wazalishaji wakubwa wa kahawa yenye ubora mkubwa nchini, je, Serikali iko tayari kuchukua mahitaji ya wakulima hawa na kisha mbolea hiyo itengwe kwa ajili yao na isichukuliwe na mtu yeyote?

Mheshimiwa Spika, tafadhali naomba ufafanuzi na naunga hoja mkono.

**MHE. MWADINI ABBAS JECHA:** Mheshimiwa Spika, nadharia ya kwamba kilimo ni uti wa mgongo wa uchumi wa Taifa letu ni dhana ya muda mrefu. Kwa kuona umuhimu huo viongozi mbalimbali na hasa wa awamu ya kwanza walibuni programu kadhaa za kukuza na kuendeleza kilimo nchini. Siasa ni kilimo na kilimo cha kufa na kupona ni miongoni mwa programu hizo. Aidha, kwa kutambua umuhimu wa kuendeleza sekta ya kilimo nchi za *SADC* walikubaliana kwamba nchi wanachama kutenga asilimia kumi ya Bajeti ya Serikali, lengo hili bado halijafikiwa na kwa bahati mbaya hata Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005 inazungumzia suala/lengo hili. Ishara inaonyesha wazi kuwa lengo hili limekuwa gumu kutekelezeka.

Mheshimiwa Spika, ni vyema basi Serikali kwa ujumla wake kama ina nia ya dhati ya kuleta mapinduzi ya kilimo nchini hapana budi pia kuzingatia azma na makubaliano ya kuongeza Bajeti ya kilimo kufikia 10% ya Bajeti ya Serikali ili wakulima wapatiwe mbolea ya kutosha na ya bei nafuu, dawa, kuimarisha masoko ya mazao mbalimbali, utaalamu na kadhalika. Aidha, kile kinachopatikana katika Bajeti ya Serikali ni lazima kutumika ipasavyo na kwa uadilifu wa hali ya juu ili kukuza kilimo hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, hali ya hewa ulimwenguni imekumbwa na mabadiliko ya mara kwa mara yanayosababisha mfumo wa uzalishaji wa mazao ya kilimo. Aidha, ongezeko na mfumko wa wadudu na viatilifu na ukosefu wa mvua za kutosha imekuwa ni mzigo mkubwa kwa wakulima wetu. Kwa bahati mbaya wakulima wetu takriban 90% wanategemea mvua kuzalisha mazao. Hii ni hali ya hatari hasa katika karne hii ambapo uharibifu wa mazingira umesababisha kwa kiasi kikubwa kuathiri mienendo ya upatikanaji wa mvua nchini.

Bungeni kupitia hotuba yake ya Bajeti ya mwaka 2006/2007 kwamba inategemea kuendeleza hekta milioni moja kwa shughuli za umwagiliaji katika kipindi cha miaka mitano. Ni jambo la kusikitisha kwamba mpaka hivi sasa ni 27.5% tu sawa na hekta 275,388 ndio eneo lililoendelezwa kwa umwagiliaji. Tukumbuke kwamba miaka mitatu imeshapita na imebakia miaka miwili. Serikali inapaswa kutueleza watatumia mbinu na mikakati gani waliyoiandaa kuhakikisha kwamba lengo lililokusudiwa linafikiwa ili kuleta ukombozi katika kilimo.

Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa matunda nchini umeongezeka kwa kiasi kikubwa. Lakini kama ilivyo kawaida matunda mengi yanazalishwa kwa misimu maalum. Hali hii husababisha matunda mengi kukosa soko au soko kuwa duni na hivyo kuwa ni hasara kwa mkulima. Ukombozi pekee unaoweza kuwakomboa wakulima wa matunda ni kuwajengea viwanda mbalimbali vya kusindika matunda hayo. Viwanda hivi ni vyema vikajengwa karibu na maeneo ya wakulima ili kuwapunguzia usumbufu wa usafirishaji. Bila shaka matunda yaliyosindikwa yanaongezeka thamani na hivyo kuleta faida kwa mkulima.

Mheshimiwa Spika, namuomba Mheshimiwa Waziri atueleze ni mipango gani Wizara imejipangia itayopelekea viwanda vya kusindika matunda vitajengwa kwa wingi na katika maeneo ambayo matunda yanazalishwa kwa wingi. Naomba maelezo.

Mheshimiwa Spika, maendeleo ya kilimo hayaji tu kwa kuwa na pembejeo za kutosha, bali matumizi bora ya pembejeo hizo ni jambo la msingi sana. Mbegu bora, utunzaji, uvunaji na ushindikaji ni miongoni mwa mambo ambayo kama hayakupewa mtazamo mpana basi mkulima siku zote atazalisha katika viwango vidogo sana.

Kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa duniani ni dhahiri kwamba *production process* kwa mkulima ni lazima ibadilike na ili jambo hili liwe na faida kwa mkulima ni lazima suala la utafiti wa mazao, udongo, utunzaji, uvunaji na usindikaji ni jambo la muhimu sana. Jambo la kushangaza na bila shaka la kusikitisha ni kuwa taasisi za utafiti wa kilimo zimekuwa hazipewi fedha za kutosha kuendeleza shughuli za utafiti. Pamoja na juhudi za watafiti mmoja mmoja kujituma lakini bado wanavunjwa moyo na kiasi kidogo cha fedha ambazo zinatengwa kwa shughuli za utafiti. Serikali itueleze ni namna gani tunaweza kupiga hatua za uzalishaji katika kilimo pasi na kuipa umuhimu ipasavyo suala la utafiti.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, nawapongeza kwa kazi ngumu na nzito.

Mheshimiwa Spika, inatakiwa Serikali iwape Bajeti yenye kulingana na umuhimu wa Wizara na jinsi inavyoajiri wakulima wengi. Mipango ya *ASDP* bado haijawa na msukumo wa kutosha hasa kwa wananchi kuibua miradi. Katika kuimarisha zao la tumbaku Serikali ichukue madeni wanayodaiwa wakulima kama ilivyofanya *SHIRECU* na *NYANZA.*

Mheshimiwa Spika, iundwe bodi kwa ajili ya mazao mchanganyiko. Kutokana na mabadiliko ya mara kwa mara ya hali ya hewa ni lazima kuweka mkazo kwenye kilimo cha umwagiliaji kwa sasa hizo skimu bado zinatumika kama kuna mvua.

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa jimbo langu la Siha, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, Mheshimiwa Stephen Masato Wasira, kwa hotuba yake nzuri na yenye kuleta matumaini kwa Taifa letu hasa wakulima ambayo imetolewa asubuhi hii. Nimefurahishwa sana na utaratibu wa hati punguzo ambao naamini utatuondolea matatizo makubwa tuliyonayo katika upatikanaji wa mbolea. Naunga mkono hoja hii.

Kipekee naipongeza *TACRI* chini ya uongozi wa Profesa Terry, kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kufufua zao la kahawa. Wilaya yangu ya Siha imeanza kunufaika na huduma nzuri ambayo inatolewa na taasisi hii ambayo inajishughullisha na masuala ya utafiti na upatikanaji wa miche mipya ya kahawa ambayo inastahimili magonjwa mbalimbali ikiwepo *CDB.* Tayari mashamba darasa yameanzishwa katika baadhi ya maeneo ya Wilaya ya Siha jambo ambalo linawapa wananchi fursa kupitia vikundi

mbalimbali ya kujifunza namna ya kubadili kilimo cha kahawa pamoja na migomba na hivyo kuweza kujiongezea kipato.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo kwa maoni yangu ipo haja ya kuona uwezekano wa kuiongezea *TACRI* Bajeti yake ili iweze kutekeleza majukumu yake makubwa ipasavyo. Tatizo kubwa ambalo linaikabili *TACRI* ni lile la mahitaji makubwa ya miche ya kahawa ambalo halilingani na uwezo wake wa kutoa miche hiyo. Pamoja na mawazo mazuri ya kuwataka wananchi washiriki kikamilifu katika kukuza miche yao wao wenyewe, bado kuna tatizo kubwa la upatikanaji wa miche ya kawaha. Ndio maana nashauri *TACRI* iongezewe uwezo ili iweze kufanya utafiti zaidi na kuzalisha miche mipya ambayo *sofar* imeonyesha mafanikio makubwa. Natoa pongezi kwa *TACRI* kwa kazi nzuri.

Mwishoni, kuna haja kubwa ya kutilia mkazo kilimo cha umwagiliaji. Miche mipya ya kahawa na migomba haiwezi kustahimili hali ya ukame. Kwa hiyo, kuna haja ya kujizatiti kikamilifu katika kilimo cha umwagiliaji Wilaya ya Siha ni Wilaya ambayo kama Wizara ya kilimo na ile ya maji na umwagiliaji zitashirikiana vizuri katika kufufua mifereji ya asili mapinduzi ya hali ya juu ya kilimo yatapatikana.

Kwa mara nyingine narudia tena kumpongeza Mheshimiwa Stephen Wasira pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Dr. David Mathayo David, kwa kazi nzuri ambayo inafanyika katika Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika. Naunga mkono hoja hii.

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Spika, naomba kushauri Wizara kama ifuatavyo na nikihakikishiwe kuwa maoni yangu yatazingatiwa nitakuwa tayari kuunga mkono hoja.

Suala la kilimo nchini ni jambo ambalo linategemewa sana na idadi kubwa ya wananchi lakini kadri siku zinavyoendelea kilimo kinabaki pale pale. Tunatarajia mapinduzi ya kilimo, hata mbegu ni vema zikapatikana mbegu za muda mfupi kuliko mbegu za sasa mfano Mkoa wa Iringa ndani ya mwaka mmoja wanalima na kuvuna mara moja tu. Morogoro mahindi mara mbili, hivyo ni muhimu sana ikapatikana mbegu ya kisasa na sio mbegu tu hata vitendea kazi kama matrekta ya kisasa.

Mheshimiwa Spika, katika nchi inayoendelea soko huria katika mazao ni lazima liangaliwe sana. Wakati mwingine wafanyabiashara hujipangia bei zao ambazo zinamlalia mkulima. Hivyo ni muhimu Serikali isaidie kuratibu bei kama ilivyofanya katika korosho.

Mheshimiwa Spika, suala la mbolea katika sekta ya kilimo limekuwa ni kikwazo kikubwa sana, mahitaji ya mbolea ni mengi na makubwa kuliko upatikanaji wake. Aidha, bei ya mbolea ni kubwa mno wakati wa kilimo bei huwa inafika hadi laki moja.

Mheshimiwa Spika, kilimo cha umwagiliaji ni muhimu kipewe kipaumbele na kuongeza maeneo lya umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, aidha, viwanda vya usindikaji bidhaa za mazao ni muhimu ikawa ni jukumu la msingi la Wizara ya Kilimo maana ni *guarantee* ya soko. Mkoa wa Iringa Wilaya ya Njombe tunaomba kiwanda cha viazi.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Iringa ungependa kujua hatma ya *National Milling Corporation (NMC)* iliyopo Iringa. Ushauri ni kwamba Wizara ibinafsishe na huduma *(service)* itakayotolewa pale iendelee kuwa kama iliyokuwepo mwanzo ya kununua mahindi na kuuza yaani kuboresha kilimo.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri Mheshimiwa Stephen Wasira, kwa hotuba nzuri lakini pia kwa kuteuliwa tena na Mheshimiwa Rais kuwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika. Nampongeza pia Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wengine.

Mheshimiwa Spika, kuhusu fedha za kuboresha kilimo kupitia *ASDP* zinapelekwa mikoani zinatukika zaidi kwa masuala ya utawala ikiwa ni pamoja na posho za uhamisho, badala ya fedha hizo kuinua na kuboresha kilimo hili ni tatizo na sio makusudio ya kuwa na mpango wa *ASDP*. Nashauri Wizara iliangalie hili kuhakikisha kuwa fedha za *ASDP* zinatumika kuendeleza kilimo sio mambo ya utawala. Bado maofisa ugani ni wachache hasa kwenye kata na katika vijiji vyetu. Hivyo wananchi hawawezi kufaidika na utaalam wanaouhitaji.

Nashauri Serikali iongeze wataalam wa ugani na kuwapeleka vijijini hasa maeneo yaliyo mbali na makao makuu ya Wilaya. Wapo maofisa ugani ambao hawapendi kukaa katika vituo vyao badala yake wanapendelea kukaa mijini au makao. Hili ni tatizo sugu naomba Serikali/Wizara ilipatie ufumbuzi. Maofisa ugani husika wachukuliwe hatua kali za nidhamu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *SGR*, nashauri Serikali inunue chakula cha *SGR* sasa badala ya kungojea bei zinapopanda sana. Matokeo yake bei ya *SGR* kwa wananchi nayo inakuwa kubwa na hivyo wananchi wanashindwa kununua chakula cha *SGR* kwani bei yake inakuwa haina tofauti na ya wafanyabiashari. Hili litazamwe.

Suala la kulima mibono (jetropha) kwa ajili ya mafuta ni zuri lakini ni hatari kwani tukishindwa kulima mazao ya chakula na hivyo kushindwa kujilisha inadai na kilimo cha Mibono kinahitaji eneo kubwa na hivyo kupunguza eneo la kilimo la chakula.

Mheshimiwa Spika, Wilaya yangu ina maofisa ushirika wawili tu. Hivyo hanamudu kuunda *SACCOS* ambazo ni muhimu hasa kwa ajili ya mikopo JK. Naunga mkono hoja.

**MHE. HEMED MOHAMED HEMED:** Mheshimiwa Spika, ni vyema nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyeniwezesha kuwepo hapa hali nikiwa mzima. Pia nimpongeze Mheshimiwa Stephen Masato Wasira kwa hotuba yake iliyojaa nuru njema kwa wakulima wetu nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa kuanzia napenda kusema kubaki kwenye karatasi na kutenda huleta maendeleo. Maneno mengi yemeshasemwa na bado ukweli unabaki pale pale katika makaratasi.

Mheshimiwa Spika, tukiangalia kilimo chetu hapa nchini utaona bado Serikali haijawa tayari kukuza kilimo. Haiwezekani jembe la mkono ambalo hadi leo ndio linalotegemewa kwa kilimo likaweza kikidhi mahitaji kwa nchi nzima sio sahihi. Pili, kilimo cha kubahatisha kwa kutegemea mvua za vuli na kadhalika sio sahihi. Kama kweli Serikali ina nia njema juu ya kilimo ni lazima tuondokana na kilimo cha jembe la mkono pia umwagiliaji maji uboreshwe ili tuepukana na kilimo cha miongo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia maeneo, kuinua kipato cha wananchi walio wengi na kufikia azma ya maisha bora kwa kila Mtanzania. Hili litabaki kuwa ndoto katika nchi yetu kama Serikali haikuwa tayari kuleta mapinduzi ya kilimo. Suala hili limekuwa kama kauli mbiu ya kudumu hapa nchini. Kutokuwepo kwa bei nzuri pia soko la uhakika kwa mazao ya wakulima hakutompa mkulima maisha bora. Ili mkulima awe na nguvu ya kazi yake ni lazima Serikali imuandae mkulima huyu kwa kumuondolea mkulima jembe la mkono na kumpatia bei nzuri soko la ndani na nje na pembejeo kama vile mbolea na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kukosekana kwa benki ya kilimo, kunachangia sana kukosekana dhana ya kukua kwa kilimo. Wakulima wetu wengi ni wale wadogo wadogo. Serikali inapaswa kuwapatia benki yao wakulima wetu ili waweze kupata mikopo ambayo itawawezesha kukuza kilimo na kuliondolea tatizo la chakula nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Watanzania ni maskini ndani ya nchi yao kubwa, kwao ni kunyimwa uhuru wa kuuza bidhaa zao pale inapoonekana wana soko lenye maslahi nalo. Kwa nini Serikali iwalazimishe wakulima wauze mazao yao ndani ya nchi hata kama bei mbaya?

Mheshimiwa Spika, baada ya ya maelezo hayo nasema ahsante.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Waziri na Naibu wake pamoja na wataalam wao kwa kuandaa hotuba hii na kuwasilisha vizuri. Hata hivyo napenda kuchangia katika maeneo machache kama ifuatavyo:-

Kwanza kushukuru kwa uzalishaji wa zao la Kahawa. Kahawa ni moja ya mazao makuu ya biashara yanayolingizia Taifa fedha nyingi za kigeni. Hata hivyo uzalishaji wake umekuwa hauna maendeleo mazuri sana. Pamoja na kwamba Waziri kwenye hotuba yake ya Bajeti ukurasa wa 26, anasema kwamba; "upungufu huo umetokana na tabia ya zao la kahawa kupunguza tija katika msimu unaofuatia misimu ambayo uzalishaji ulikuwa mkubwa."

Mheshimiwa Spika, sababu zilizotolewa na Waziri hazina ukweli sana. Sababu za msingi za kushuka kwa uzalishaji wa zao hilo ni pamoja na hizi zifuatazo:-

Moja, bei kubwa ya mbolea hasa *CAN* ambayo hutumika zaidi kurutubisha zao hilo. Kibaya zaidi mbolea hiyo *CAN* haipo kwenye mbolea za ruzuku. Swali la kujiuliza hivi ni wakulima wangapi watumudu bei kubwa ya mbolea hiyo, shilingi 25,000/= hadi 40,000/=? Na hizo ni bei ya Dar es Salaam; inapofika Mbozi bei hufika hadi shilingi 100,000/=! Hii ni sababu kubwa sana ya kushuka kwa uzalishaji wa zao hilo.

Pili, bei kubwa ya dawa kwa ajili ya kukabiliana na magonjwa ya kahawa. Kwa mfano kilo moja ya kopa huuzwa kwa wastani wa shilingi 15,000/= hadi shilingi 20,000/=. Wakulima wangapi wataweza bei hizo? Tatu, upungufu mkubwa wa maafisa ushauri wa kitaalam na baadhi ya maafisa ugani wanaopelekwa vijijini hawana utaalam wa zao la kahawa. Nne, kushuka kwa bei ya zao la kahawa, kulisababisha wakuliwa wengi kuyatelekeza mashamba yao.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali iweke ruzuku kwenye mbolea ya *CAN*, kwenye dawa za kilimo kwa mfano kopa na kuendelea kupeleka watalam (wagani) wa zao la kahawa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu bei kubwa ya mbolea. Nchi hii imejaliwa sana kuwa na ardhi nzuri sana. Sehemu kubwa ya ardhi hiyo inafaa sana kwa kilimo, aidha, wananchi wetu wana bidii kubwa sana ya uzalishaji wa mazao ya biashara na chakula. Tatizo kubwa la Serikali ni kushindwa kuwapatia wananchi wetu (wakulima) pembejeo za kilimo na hususan mbolea kwa bei wanazoweza kumudu na kwa muda muafaka.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa bei za mbolea na kama alivyokiri Waziri ni kubwa sana kuanzia shilingi 25,000/= hadi shilingi 100,000/=; narudia tena kujiuliza tena hivi ni Watanzania wangapi, tena wakulima wa vijijini, watamudu bei hizo? Matokeo yake ni wakulima wengi kama kununua mfuko mmoja wa kilo 50 na kuamua kupanda mazao hivyo hivyo. Matokeo yake ni uzalishaji duni na baadae njaa.

Mheshimiwa Spika, haya ni ya kujitakia, kwa mfano Mkoa wa Mbeya, moja ya mikoa mikubwa sana ya uzalishaji wa mazao ya biashara na chakula hapa nchini hupewa chini ya 30% ya mahitaji ya mbolea. *Are we really serious? I doubt!*

Mheshimiwa Spika, mwaka jana (tarehe 3/10/2007) Mheshimiwa Stephen Wasira, Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, akiwa kwenye msafara wa aliyekuwa Katibu wa Mwenezi na Itikadi wa CCM Taifa Ndugu Aggrey Mwanri na kwenye mkutano wa hadhara uliofanyika kwenye viwanja vya shule ya msingi Ilomba, Jijini Mbeya aliwaambia wana Mbeya kwamba kuanzia mwaka wa 2008/2009 mbolea itakuwa nyingi sana. Aidha, Mheshimiwa Wasira alisema mbolea itapatikana vijijini kama soda ya *coca cola* inavyopatikana. Waziri pia alisema Serikali itahakikisha kwamba mifumo miwili ya mbolea, yaani mbolea ya bei ya soKo na mbolea ya ruzuku inaondoka. Waziri alisema azma ni kubaki na mfumo mmoja tu wa mbolea.

Mheshimiwa Spika, sasa nataka Waziri anihakikishie mimi na wana Mbeya, je, utekelezaji wa ahadi zake hizo nzuri na zenye kutia matumaini zinatekelezwa kwa kiasi gani?

Mheshimiwa Spika, kushuka kwa Bajeti ya kilimo, mimi najiuliza hivi mapinduzi ya kilimo *(green revolution)* ni ya kweli au ya kufikirika tu? Kama ni ya kweli; kwa nini Bajeti ya Wizara ambayo ndiyo inasimamia kilimo inaendelea kushuka? Aidha, sehemu ya tatu (sura ya tatu) ya Ilani ya uchaguzi ya CCM, kigungu cha 31(i) kilimo kinasema; "Kilimo kitengewe si chini ya 10% ya Bajeti ya Taifa." Lakini leo kilimo kinatengewa 6.4% tu, je, tutafika? Waziri atueleze tutafikaje huko kwa mwendo huo? Ahsante sana.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, naanza kwa kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, kilimo ndio pekee mkombozi wa Watanzania na zaidi ya 80% ya Watanzania ni wakulima. Na ili tuwapatie ukombozi wa kudumu ni lazima tulete ukombozi wa kudumu kwa kuboresha kilimo kwa vitendo.

Mheshimiwa Spika, nchi za Malaysia, Indonesia, Thailand na hata India katika miaka ya 1960 takwimu zinaonyesha walikuwa na tatizo kichakula sawa sawa au hata kuliko nchi za Afrika ikiwepo Tanzania. Leo hii nchi zote hizi nilizozitaja zimepiga hatua kubwa sana katika kilimo na wanauza nje kwa kiwango kikubwa sana. Sababu ni zipi?

Mheshimiwa Spika sababu ya kwanza ni mbegu bora kulingana na ardhi, pili, kuhakikisha matumizi ya mbolea bora, tatu, kuunganisha kilimo na viwanda ili kusindika mazo yenye hadhi ya kusindikika na nne, kutumia teknolojia za kisasa katika kilimo na mengi mengineyo ili tubadilike katika kilimo na kuondoa umaskini kwa asilimia kubwa ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, sasa nihamie jimboni kwangu. Asilimia kubwa zaidi ya 60 ya wananchi wangu wanaishi milimani. Zao lao kuu la biashara ni tangawizi.

Mheshimiwa Spika, wananchi wangu wanatumia saa 16 kwa siku kufanya kazi hii ya kilimo cha tangawizi kwani tangawizi inahitaji kunyweshwa maji mengi na zoezi hili mara nyingi linafanyika usiku.

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa linaloatlhiri wananchi wangu ni bei ya tangawizi mbichi ambayo ni bei ya kilanguzi shilingi 150/= mpaka shilingi 200/= kwa kilo. Bei hii inawaumiza wananchi wangu sana na badala ya kuwakomboa inawazidishia umaskini na kuwazeesha kwa kuchoka mno kwa kazi ngumu.

Mheshimiwa Spika, nimelalamika mno ndani ya Bunge hili Tukufu. Nimelalamikia bei hii kupitia Baraza la Madiwani.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kumpongeza kwa dhati Mkurugenzi wa Wilalya ya Same kwa kuchukua *serious* kilio cha wananchi wangu na kukitafutia utatuzi. Mkurugenzi alishirikiana na mkuu wangu wa Wilalya Ibrahimu Marwa, Mkuu wangu wa Mkoa Mohammed Babu na kufikia hatua kupitia *AMSDP* na Akilimali kuona kwamba utatuzi wa tatizo hilo la bei ya tangawizi ni kujenga kiwanda cha kusindika tangawizi katika *form* ya *powder* na *chips.* Akilimali kupitia *AMSDP* walifanya utafiti wa kitaalam na wa kina na kutoa andiko la ujenzi wa kiwanda chenye hadhi ya kutoa tangawizi *powder* na tangawizi *chips* zenye kufungashwa Kimataifa na kuweza kuhimili soko la nje la ushindani.

Mheshimiwa Spika, wananchi waliunda chama cha ushirika kilichoandikishwa kisheria na kuunda vikundi 21 vyenye wanachama 2000 waanzilishi. Tulinunua eneo sisi wenyewe. Kata ya Miamba. Ujenzi umeanza ambao unazingatia maelekezo ya *AMSDP* na Akilimali na usimamizi wa halmashauri. Wananchi kwa nguvu zao wenyewe wamekusanya mawe, kokoto, mchanga, wamefyatua matofali na kuyachoma ya kutosha jengo zima wameanza sasa ngazi ya msingi.

Michango yao ya mali ni shilingi 15,500/= kila kichwa na Mbunge nimechangia shilingi milioni mbili, mifuko 200 ya cement, mabati 300 ya geji 28 na kofia 100. Japo ili tuweze kupata mitambo kwani jengo lote tutajenga wenyewe lenye thamani ya kati ya shilingi milioni 38 au 40 tunaiomba Serikali kupitia Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika ituchangie shilingi milioni 300 kwani mtaji wa kuendesha (mzunguko) wa biashara kwa miezi mitatu tutahitaji shilingi bilioni 1.3. Natanguliza shukrani.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hoja hii kama ifuatavyo, kwa kuwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati wa kampeni na baadaye katika ziara yake aliahidi mambo kadhaa kwa ajili ya tarafa ya Eyasi, na kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika Mheshimiwa Chiza amefuatilia kwa karibu sana utekelezaji wa ahadi hiyo ya Rais ikiwa pamoja na kutembelea eneo hilo mara kadhaa, sasa je, mpango wa uimarishaji wa mbegu bora ya vitunguu kwa lengo la kuzalisha vitunguu bora vinavyoweza kuuzwa katika soko la nje umefikia hatua gani?

Mheshimiwa Spika, iwapo mpango huo upo je, ni utaratibu gani unafanyika kuwawezesha wakulima hao wawezea kufikia masoko ya nje ya nchi? Je, Serikali iko tayari kushirikiana na *Tanzania Chamber of Commerce* katika kujenga mtandao mzuri wa wakulima ili waweze kupata manufaa ya kilimo chao?

Ahadi hiyo ilikuwa ni pamoja na kuimarisha barabara ya Njia Panda – Matala, angalau kufanya ipitike wakati wote wa mwaka kuinusuru malori ambayo wakati wa mvua hutumia muda mrefu sana njiani kwa ajili ya ubovu wa barabara na hivyo kufanya vitunguu viharibike.

Kwa vile bei ya mbolea ambayo ni muhimu sana kwa kilimo cha vitunguu katika bonde la Eyasi, tarafa ya Eyasi Wilayani Karatu; na kwa kuwa mbolea hasa ya ruzuku inapatikana kwa shida na inapopatikana mfuko wa kilo 25 ni sawa na shilingi 50,000 jambo ambalo wakuliwa wengi wanashindwa na hata wale wenye uwezo bei hiyo haina tija kwani gharama ya uzalishaji inakuwa kubwa kuliko bei ya vitunguu katika soko.

Kwa kuwa pembejeo na hasa zana zinazotolewa na mfuko wa pembejeo zimekuwa na manung'uniko mengi, Serikali iko tayari kutoa taarifa kamili ya wakulima waliokopeshwa na mfuko huo; kila mmoja alipewa kiasi gani na kwa ajili ya kasi gani. Hii ni kwa sababu kuwa tuhuma na taarifa kuwa kati ya watu waliopewa mikopo hiyo, wala hawakutumia fedha hizo kukarabati trekta hizo na au hata trekta za kukarabatiwa hazikuwepo.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi taarifa kamili ya walionufaika na mikopo hiyo itasaidia Mbunge kufuatilia matumizi ya fedha hizi katika eneo lako. Naamini taarifa hizi ziko kwenye *computer* na hivyo si kazi kupatikana. Naomba taarifa ya kina.

Mheshimiwa Spika, natanguliza shukrani za dhati.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba kumpongeza sana Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, Mheshimiwa Stephen Wasira, Naibu wake Mheshimiwa Dr. David Mathayo David, Katibu Mkuu, Peniel Lyimo na viongozi wengine wa Wizara hii kwa mikakati mizuri ya kuimarisha kilimo waliyoionyesha kupitia Bajeti ambayo Mheshimiwa Waziri kaiwasilisha leo.

Katika kuunga mkono Bajeti hii, napendekeza mambo yafutayo yapewe kipaumbele, kwanza ni kuhusu bei ya pamba. Wakulima wa pamba mwaka huu wamepewa adhabu wasiyostahili na benki ya *CRDB* ambayo imeweka bei ya kununulia pamba kwa wateja wake. Kitendo cha *CRDB* kuweka bei ya shilingi 400/= kwa kilo mwaka huu, chini ya hata ile ya mwaka jana iliyofikia shilingi 600/= eti ili wafanyabiashara wapate faida kubwa, ili walipe limbikizo la riba la mwaka jana na mwaka huu ni unyonyaji wa kutisha.

Naomba Wizara iingilie kati haraka sana. Hali hii ni pigo kubwa kwa juhudi za Serikali kuongeza uzalishaji wa pamba nchini na hivyo kupunguza umaskini. Kwa haraka kabisa, naomba Wizara isaidie uanzishaji wa mfumo wa stakabadhi ya mazao ghalani kwa ajili ya wakulima wa pamba. Ni vizuri Wizara ikafanya mawasiliano na benki zingine zitoe mikopo kwenye kilimo.

Mheshimiwa Spika, pili, ni deni la wakulima wa pamba wa Kahama wanaiodai *KACU* toka msimu wa mwaka 2004 ambalo ni kama shilingi milioni 130. Kwa kuwa Serikali lilishaamua kulipa madeni ya wakulima, naomba iwalipe wakulima hawa wa Kahama haraka.

Mheshimiwa Spika, tatu, kuhusu mbolea, naishauri Wizara, iweke utaratibu wa kuwezesha kuanzishwa mashamba makubwa *(Spiceial incentive scheme for investors in agriculture).* Haya ndiyo yapewe ruzuku, halafu Serikali inunue mazao yao kwa bei itakayokubaliwa mapema. Mtindo wa sasa wa kutoa ruzuku ya mbolea kwa mikoa michache haina tija, maana wakulima wa mikoa hiyo wanakuja kuuza mazao yao kwa bei ya soko, hivyo mkulima wa mkoa kama Shinyanga hanufaiki na ruzuku hiyo. Ni bora basi, walau, Serikali ipanue *SGR* ili inunue mazao mengi na kuyauza kwenye mikoa yenye upungufu kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Spika, miradi ya *DADIPS* haina usimamizi wala haieleweki kwa wananchi. Naishauri Wizara iweke utaratibu wa kutangaza miradi yote ya *DADIPS* kwenye Wilaya ili wananchi wajue fedha zinazotumika.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. SIJAPA F. NKAYAMBA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nimshukuru Waziri pamoja na Naibu wake kwa hotuba yao nzuri.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa Mkoa wa Kigoma hauna njaa kama ilivyo mikoa mingine, kwa kuwa mbolea huwa inakawia kufika mkoa wa Kigoma na wananchi wanakosa mbolea hiyo Serikali inasemaje? Na kwa kuwa wakulima wa kahawa walioko Manyovu na Kehazi malalamiko yao ni mbolea kwa nini Serikali isilete mbolea hiyo mwaka mzima? Na kwa kuwa wananchi wa Kigoma vijijini hasa kijiji cha Basanza kuna wananchi ambao ni wanakikundi wanaojitolea kuleta mbolea kutoka Kigoma Mjini wanapokuwa wamenunua mbolea hiyo wanajaribu kuomba gari la halmashauri, lakini hawapati gari hilo kwa ajili ya kuwabebea mbolea na kama watakodi gari shilingi 300,000/= nao wanapenda waiuze zaidi ya shilingi 24,000/= wakati ni mbolea ya ruzuku, je, Serikali inasemaje kuhusu halmashauri ya Wilaya ya Kigoma vijijini kuwapatia gari la kuweza kubebea mbolea hiyo ya ruzuku, je, Serikali inasemaje?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja asilimia mia kwa mia.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri Mheshimiwa Stephen Masato Wasira, Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. David Mathayo David, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri ya maandalizi ya Bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kuwapongeza wakulima wote wa jimbo la Iramba Magharibi hasa kwa kujitoa kwa hali na mali katika kuhakikisha wanalima vya kutosha mazao yale ya chakula na biashara ikiwa ni hatua ya kujiondolea umasikini.

Mheshimiwa Spika, wananchi (wakulima) wa jimbo langu kwa juhudi zao binafsi na pengine bila kupata ushauri wa kitaalam wamefanya kazi kubwa na hivyo kuliondolea jimbo langu aibu ya njaa kwa kipindi cha mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, kauli mbiu ya Tanzania ni kwamba kilimo ni uti wa mgongo na kutokana na ukweli huo kwa idadi ya takribani 80% ya wananchi wa nchi yetu ni wakulima, lakini ukulima wenyewe ni ule unaowagawa Watanzania tabaka la wakulima wadogo wadogo ndilo linaloongoza. Nchi yetu kwa ujumla inatawaliwa na wakulima hawa wadogo wadogo kama wapo wakulima wa kati na wa juu basi ni kwa idadi ndogo sana.

Mheshimiwa Spika, wakulima wadogo wadogo bado wanatumia zana duni za kilimo, hawatumii mbolea, hawalimi kufuata utaalam. Ninao ushauri ufuatao katika Bajeti ya mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri atambue kwamba hivi sasa nchi yetu lazima iondokane na ukulima wa kubahatisha ukulima usiofuata kanuni na taratibu ili kuondokana na hali hiyo ni lazima kwako na wataalamu wa kilimo wenye hadhi ya vyuo vya kilimo vilivyotambulika, katika maeneo ya kata hadi vijijini.

Kwa kuwa kilimo cha kupata mazao bora na mengi ni lazima utaalamu uwepo lakini pia suala la mvua za kubahatisha kuzitegemea inabidi tuondokane nao katika hali hiyo lazima sasa kilimo cha umwagiliaji kukitilia mkazo. Eneo kubwa la Tanzania yapo wazi yapo, maeneo ya mabonde yenye ardhi nzuri na rutuba nzuri ambayo tukiitumia vizuri yatatukomboa na kundokana na tabia ya kuomba omba hasa kwa masuala ya chakula. Yale maeneo yalisemwa juu ya ukanda wa kijani, maeneo hayo muhimu yenye kuhifadhi maji kwa kipindi kirefu yangetumika.

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti mbili zilizopita, ya mwaka 2006/2007 na mwaka 2007/2008 ipo mikakati mingi na mizuri iliyofafanuliwa ambayo ni hatua za kufanya mapinduzi ya kilimo. Mipango hiyo ni mizuri sana lakini bado haijatumika ipasavyo katika kufanya mapinduzi ya kweli, hivyo ni wajibu wa Wizara katika kutumia Bajeti hii ndogo inayotengwa katika sekta hii ya kilimo.

Kuhusu matumizi ya mbolea, kwa kuwa mapinduzi yanahusu nchi yetu sote kwa ujumla hivyo Serikali iepukane na ile hali ya kufanya upendeleo kwa baadhi ya mikoa kuipatia mbolea ya ruzuku na ruzuku ya pembejeo. Jimbo la Iramba Magharibi tunalima sana zao la biashara la alizeti. Namwomba Waziri na watendaji wa Wizara kutoa ushirikiano wa karibu ili wananchi hawa wawezeshwe kitaalamu na kinyenzo waweze kuzalisha alizeti kwa wingi.

Mheshimiwa Spika, umwagiliaji umehamishiwa Wizara ya Maji kwa kuwa shughuli ya umwagiliaji inaendana na kilimo basi ni muhimu sasa Wizara kufanya kazi kwa ukaribu sana na Wizara hii, kwa maana kuwa na maafisa kilimo wa kutosha Wilayani na pia kuishauri Wizara ya Maji kuwa na maafisa umwagiliaji Wilayani na hivyo kufanya kazi sambamba.

Mheshimiwa Spika, bado utumiaji wa matrekta ni mdogo sana kwa maeneo yote, pamoja na sekta binafsi ya biashara, wamejitahidi kuleta matrekta mengi kuzingatia sasa haulingani na hali ya kilimo kwani trekta nyingi zimekufa kwa mwaka wa kwanza.

Kuhusu mfuko wa pembejeo, mikopo kwa wananchi wa kada ya chini bado mfuko huu kuwasaidia wengi walio mijini na hasa Dar es Salaam, hivyo mfuko huu upanue wigo uwafikie wananchi vijijini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mpango wa *ASDP*, mpango huu haujapata mafanikio ya kutosha mbali na fedha nyingi za umma kuishia kwenye mikono ya watu wachache. Utaratibu wa stakabadhi ghalani uendelee kwani ndio pekee unaompa fursa mkulima kupata uwezo wa kujiwezesha. Naunga mkono.

**MHE. RAYNALD A. MROPE**: Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri, Mheshimiwa Stephen Wasira, Mheshimiwa David Mathayo David, Naibu Waziri na Katibu Mkuu Ndugu Peniel Lyimo, kuleta hoja hii mbele ya Bunge Tukufu.

Mheshimiwa Spika, la kwanza kabisa bado sijaridhika na sera ya Wizara kuhusu umwagiliaji. Nasikitika kusema kuwa vyanzo vya maji nchini ni vingi mno lakini suala la umwagiliaji nchini bado ni dogo mno, kwa nini? Eneo la Kusini kuanzia mto Rufiji, Matandu, Mbwenkuru, Lukuledi na Ruvuma, mito yote hii mikubwa hakuna mpango wa maana wa kutumia maji ya mito hii ili kumwagilia maji ya mito mikubwa hii yanapata bure kwenda baharini. Seikali inatumia fedha nyingi kuwa na mipango ya umwagiliaji kutoka katika vijito vidogo vidogo na hasa zaidi wakati wa masika katika kilimo cha mpunga badala ya kutumia raslimali fedha kwa miradi mikubwa ambayo ingeleta maji nyakati zote kwa mwaka. Utekelezaji wa sera ya umwagiliaji upo wapi kama hatuhusishi mito hii mikubwa niliyoitaja.

Mheshimiwa Spika, nimekuwapo Bungeni toka mwaka 2000, sijaona utekelezaji dhahiri wa mpango wa umwagiliaji kutumia vyanzo vikubwa sasa mambo haya yataendelea mpaka lini?

Mheshimiwa Spika, zao la korosho kweli limeongezeka kutokana na utaratibu mzuri na stakabadhi za mazao ghalani ambao kwa mara ya kwanza bei kwa wakulima ilikuwa nzuri. Wakulima wengi wamefurahia utaratibu huu na ni mategemeo yangu kuwa Wizara itaendelea miaka ijayo na mpango huu. Mwaka huu kwa bahati mbaya ruzuku ya mbolea imekawia sana kiasi kwamba wakulima hawakuwahi kupata salfa ya kutosha. Kulikuwa na ugomvi hasa baina yao kugombania salfa na *biofidan* ya ruzuku.

Mheshimiwa Waziri kukosekana kwa salfa ya kutosha kunaweza kuathiri sana upatikanaji wa korosho msimu ujao. Kwa nini mwaka huu maandalizi hayakuwa mazuri na je, ile 6.5% ambayo halmashuri zetu ilipasa ipate moja kwa moja toka *TRA* imetolewa? Kama fedha hizi zingepatikana, halmashauri zingewahi kununua salfa na kuwapelekea wananchi mapema.

Mheshimiwa Spika, suala la ugani katika Wilaya yangu ya Masasi bado ni la wasiwasi. Hatuna maafisa ugani wa kutosha katika kata na vijiji kiasi kwamba wakulima mpaka leo hawafuati kanuni za kilimo bora na kadhalika. Suala hili kila nikiuliza naambiwa ni la Kitaifa sasa tutaendela vipi kama hakuna mabadiliko ya upesi. Tuelezwe kwa nini mpaka leo kata zetu zinakosa mabwana shamba.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja, hata hivyo maoni yangu machache yaangaliwe na Wizara.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Spika, naunga hoja. Nimeona nchi zilizopata mafanikio ya kilimo, wamewawezesha wakulima kwa kupata mikopo. Mabenki duniani hutoa mikopo kwa wakulima kwa masharti ya shamba kuwa ni bima, *formular* inayotumika Bima – Shamba – *Loan.* Tujaribu hapa kwetu.

**MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, napongeza Wizara hii kwa kuwasilisha hoja hii mbele ya Bunge hili Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mchango wangu wa kwanza kwa Wizara hii ni kulifuatilia suala muhimu sana kwa kuanzishwa benki ya mikopo kwa wakulima wadogo wadogo ili ile 70% ya wakulima waweze kukopa na hatimaye walime kwa kujitosheleza na hatimaye kuchangia katika Pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jambo ambalo Watanzania tunapaswa kujivunia ni majaliwa tuliyopewa na uwezo wa Mungu juu ya ardhi tuliyobarikiwa, zaidi lazima tujivunie wataalam wetu waliosoma vizuri tena katika nyanja zote zikiwemo za kilimo, tatizo kubwa tulilonalo ni kupanga jinsi gani ya kulima kwa kuuza na kujipatia chakula. Lazima hivi sasa Serikali ikope fedha nyingi kwa kushirikiana na *WFP* kwa ajili ya kilimo cha chakula ambacho hivi sasa ni tatizo kubwa duniani.

Mheshimiwa Spika, upo mpango hivi sasa uliobuniwa na wakulima wakubwa duniani, wao kazi yao ni kugharamia kila kitu hivyo kuja kugana mazao, huu nadhani ni mpango mzuri mradi tu ardhi inatumika vizuri hasa katika utumiaji wa mbolea jambo ambalo linapaswa kusimamiwa vizuri ili kulinda ardhi yetu.

Mheshimiwa Spika, nakumbuka zamani palikuwepo kampuni ya *Lohnro* ambayo ilikuwa inamiliki mashamba makubwa hivyo waliweza kuzalisha chakula na huku wakitoa ajira kwa wazawa, binafsi nashauri Serikali lazima itafute makampuni kama hayo ambayo yapo duniani kwa ushirikiano wa pamoja.

Mheshimiwa Spika, kilimo ni utafiti hivyo nashauri vituo vya utafiti viongezewe fedha ili utafiti hasa wa mbegu ufanyike vyema. Lakini kubwa zaidi wataalam wa kilimo wapewe uzito wa mishahara na iwe sekta hii ya kilimo iwe kimbilio la wasomi badala ya kuikwepa na kuiona ni Wizara isiyo na tija.

Mheshimiwa Spika, mimi leo nakumbuka Balozi wa Japan Bwana Sato alisema Watanzania mtapata shida ya angalizo ya uchumi wenu msipotilia mkazo kilimo chenye tija, maneno haya aliyasema Morogoro katika *Pilot Project* ya mpunga wa umwagiliaji ambapo ilivutia watu wengi kwa sehemu ndogo lakini mavuno makubwa.

Mheshimiwa Spika, hakuna kitu muhimu kama kujaribu, hasa katka msemo maarufu wa mapinduzi ya kijani. Mimi naiomba Wizara hii hebu kwa siku za mbele ijaribu kwa kuwapatia Wabunge wote kila Mbunge apatiwe ekari 500 na kukopeshwa trekta kama *pilot project* hivyo Wizara itakuwa imezalisha chakula pia na kazi kwa vijana na kulipwa fedha za pembejeo zote kwa uhakika.

Mheshimiwa Spika, mwisho tungeelezwa na Wizara hii mpango ambo ulipewa changamoto na Rais Mheshimiwa Jakaya Kikwete juu ya mkoa wa Morogoro kuwa ghala la Taifa. Lakini zipo tetesi kwamba wananchi wa mkoa huo hawakushirikishwa vyema. Zaidi ni kuzingatia mbegu zinazoingizwa nchini kiholela ni hatari.

**MHE. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Spika, halmashauri ya Wilaya ya Ludewa imejikita katika kilimo cha umwagiliaji kiasi cha hekta 1000 zimefanyiwa upembuzi yakinifu eneo la Manda kwenye bonde la mto Ruhuhu. Matarajio yetu ni kuanza utekelezaji wa mradi huu mwaka 2008/2009 katika kifungu 121 ukurasa wa 74, Serikali inatarajia kutoa mafunzo kwa wataalam wanafunzi 200 kuhusu matumizi ya zana bora za kilimo na kuhamasisha ulimaji wa mashamba katika eneo moja, *block farming.* Je, Serikali inaweza kunihakikishia kuwa Ludewa tunapata fursa katika mafunzo hayo na kuhakikisha kuwa *block farming* katika mradi wa Ludewa inakuwa *practiced.*

Mheshimiwa Spika, kutokana na mipango kabambe ya uanzishwaji wa migodi ya chuma na makaa ya mawe na viwanda mama vitakavyoanza hivi karibuni Wilayani Ludewa, je, Serikali itakuwa tayari kutusaidia kutenga ardhi kwa ajili ya kilimo, ufugaji na wakazi katika maeneo yanayozunguka Liganga na Mchuchuma kama inavyoelekeza katika kifungu 128 ukurasa wa 78.

Kutokana na wananchi wa Ludewa kuhamasika kulima chai na kahawa mpya kwa kuanzisha vitalu vingi sana pamoja na kilimo cha pareto, je, Serikali itatusaidiaji katika kuhakikisha kuwa wakulima wanajiunga katika vikundi na vyama vya ushirika ili iwe rahisi kuwapelekea teknolojia za kilimo bora na taarifa za masoko ya mazao hayo kwa ufanisi zaidi?

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Ludewa ina mazingira yanayoruhusu uzalishaji matunda na mboga mboga hususan yanayostawi maeneo ya baridi, je, Serikali itatusaidiaje kupata wataalam na uzalishaji bora wa mazao ya bustani hususan kuanzisha bustani za Serikali ya kutunza nasaba na kuzalisha vipande bora vya mazao ya bustani kwa ajili ya wakulima waliohamasika sana katika kilimo hiki kama inavyoelekeza katika kifungu 132 ukurasa wa 85.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Spika, kabla ya kuunga mkono napenda nieleze yafuatayo ambayo nimekuwa nikiieleza Serikali bila utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, Geita, hususan jimbo la Geita na Busanda kuna kilimo cha matunda ya nanasi, maembe na tikiti maji ambayo hayana soko na hayana walaji. Tumeiomba Serikali isaidie kuleta kiwanda cha kusindika matunda. Hakuna sababu ya kuagiza *juice* kutoka Uganda, Afrika ya Kusini au Kenya. Matunda ya Geita yanatosha kabisa kuingiza pesa za kigeni. Tunaomba Serikali isaidie kutangaza utajiri huu kwani eneo hili ni pembezoni.

Mheshimiwa Spika, umetaja suala la kilimo cha umwagiliaji. Busanda kuna maeneo mazuri sana na yana rutuba. Yamekuwa yakisemwa kwa kila hotuba lakini utekelezaji ni dhaifu. Maeneo ni ya mbuga za Isima, Daragulwa (Nungwe), Nyanyeye, Buzanaki, Kaseme, Hobora na Ibanda. Maeneo haya ni mazuri sana na yanaweza kulisha Kanda ya Ziwa. Je, umwagiliaji umefikia wapi? Hivi sasa Uganda, Burundi, Rwanda na Zaire wananunua mpunga kupitia soko la Katoro la Geita. Kwa nini Serikali isijenge soko la Kimataifa katika mji wa Katoro na wageni wakaruhusiwa kununua kwa kutumia dola. Tunaomba soko la Kimataifa katika mji wa Katoro, Geita.

Kwa nini Geita haimo katika mpango wa vocha kwa mkulima ili waweze kupata hati punguzo ya pembejeo. Inaonekana Serikali haielewi vizuri maeneo yanayotoa mpunga kwa wingi. Serikali haitendei haki Geita. Kabla hujajibu hebu pata taarifa ya bonde la Isima, Itobora na Ibanela waulize wakwambie ukweli. Katika mabonde hayo mwaka huu walivamiwa na ndege aina ya kwelea kwelea. Nikatoa taarifa ofisi ya kilimo ya Wilaya na Mkoa. Afisa kilimo alitoa taarifa ofisi ya Shinyanga kuchukua hatua za dharura; cha kusikitisha walipokuja walifika saa 6 wakaone ndege ni wachache. Matokeo ekari zaidi ya 200 zikaharibiwa na ekari zangu tatu sikuvuna kwani nami ni mkulima. Ndege hiyo iliyo Shinyanga inatusaidiaje wakulima? Naomba maelezo. Je, sisi waathirika tutafidiwa nini? Kwa sababu ya uzembe wa wataalam hawa.

Mheshimiwa Spika, wataalamu walio Shinyanga hawako *serious* kusaidia wakulima walipofika saa za mchana na kuamua kuwa wananchi hawahitaji msaada sikuwaelewa. Wakati huo ndege wanapumzika.

Naomba wataalam hao wabadilishwe hawatusaidii. Wametia hasara kubwa kwa kutopeleka ndege kuua ndege waharibifu. Naomba baada ya kikao hiki Mheshimiwa Waziri tembelea bonde la Isima ujionee mwenyewe. Ni eneo ambalo ni mkombozi wa nchi na nchi jirani. Naomba msimu ujao kosa kama hilo lisirudiwe. Inakatisha tamaa wakulima.

Mheshimiwa Spika, kwa kifupi, naomba kiwanda cha kusindika matunda, tunaomba soko la Kimataifa Katoro na mradi wa umwagiliaji uimarishwe katika bonde la Geita. Naomba ndege *please* itumike kudhibiti ndege waharibifu, (waelewe dharura).

**MHE. MARGARET A. MKANGA**: Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi na watendaji wote wa Wizara hii kwa kufanya kazi nzuri hasa katika eneo la kufufua ushirika wa wakulima nchini na hatimaye kuandaa hotuba nzuri yenye matumaini ingawa Bajeti bado haitoshelezi kikamilifu.

Napenda kuchangia baadhi ya maeneo machache kama yafuatavyo, upatikanaji wa pembejeo. Nimefarijika sana na mpango wa Serikali wa kusambaza mbolea kwa wakulima kwa kutumia mfumo wa vocha. Hata hivyo nashauri kwa njia yoyote ile itakayoamuliwa kutumika na Wizara cha msingi mbolea hiyo hata mbegu bora ziwahi kutawanywa kwa wakulima kabla ya msimu husika kuanza.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano mara nyingi kila mwaka wakulima wa korosho na kadhalika wamekuwa wakilalamika kuhusu ucheleweshaji wa dawa za kupulizia mikorosho kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, nimefurahi sana kusikia kuwa Serikali imepania kumalizia mchakato wa kuanzisha benki ya maendeleo ya kilimo kwani itakuwa ni mkombozi wa wakulima ambao wanakosa mtaji wa kuendeleza kilimo hapa nchini hivyo kwa benki hii tarajiwa ukombozi utapatikana.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeazimia kuandaa mwongozo wa kutumia zana za kilimo kwa faida zaidi. Ninachoomba mwongozo huo uandaliwe haraka kabla ya msimu wa kilimo ujao haujaanza ili ulimaji huo wa mashamba katika eneo moja *(block farming).*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli yaliyomo ndani hotuba hii ni mazuri kuanzia uanzishaji wa bodi ya nafaka na mazao mchanganyiko, usindikaji wa mazao, kuongeza idadi ya wataalam wa ugani na kadhalika. Rai yangu ni kwamba yote haya yapaswa kutekelezwa kwa vitendo ili tusiishie maneno matupu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya naunga mkono hoja.

**MHE. JUMA SAID OMAR:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima na afya na kushiriki kikao cha leo.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani kwako wewe Naibu Spika, Wenyeviti wa Bunge pamoja na viongozi wa Kambi ya Upinzani kwa kutuongoza vizuri.

Mheshimiwa Spika, pamoja na umuhimu wa sekta ya kilimo, ukuaji wake haulingani na mahitaji ya nchi kwani hatujaweza hata kujitosheleza kwa chakula. Hivyo Serikali inapaswa kuongeza Bajeti ya kilimo badala ya kupunguza pamoja na kutoa pembejeo kwa wakulima.

Mheshimiwa Spika, ili tuweze kujitosheleza kwa chakula na kupata ziada ni vyema Serikali ikatilia mkazo kilimo cha umwagiliaji maji badala ya kutegemea mvua ambayo wakati mwingine inakosekana, haitoshi au kuwa nyingi inayosababisha kuharibika kwa mazao mbalimbali na hivyo kusababisha upungufu wa chakula.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa nchi yetu ina ardhi nzuri, maji ya kutosha kutokana na maziwa na mito isiyokauka pamoja na utumiaji wa zana bora za kilimo kama vile matrekta, majembe ya kukokotwa na ng’ombe, utumiaji wa mbolea na kadhalika na

kwa kupitia kilimo cha umwagiliaji maji, nchi yetu itaweza kujitosheleza kwa chakula na kupata ziada na hivyo kuweza kuongeza Pato la Taifa na kukuza uchumi.

Mheshimiwa Spika, tangu uhuru hadi leo kilimo kimekuwa kikipewa majina mbalimbali kama vile siasa ni kilimo, kilimo cha kufa na kupona, kilimo ni uti wa mgongo na kadhalika, lakini bado hakijepewa umuhimu unaostahili. Mabadiliko na mafanikio katika uzalishaji wa mazao mbalimbali ya kilimo bado hayajafikiwa.

Mheshimiwa Spika, ili sekta ya kilimo iweze kukua ni muhimu sana kuanzishwa kwa benki ya kilimo itakayowasaidia wakulima kukopa na hivyo kuweza kuzalisha zaidi, kuongeza Pato lao la Taifa na kukuza uchumi.

Mheshimiwa Spika, masoko pamoja na miundombinu hasa vijijini ni muhimu ili wakulima waweze kusafirisha mazao yao kuyapeleka kwenye masoko ya uhakika.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa viwanda vya kusindika mazao mbalimbali ni muhimu ili mazao ya wakulima yasiharibike na hivyo yaweze kuchangia pato la wakulima na Taifa kwa jumla.

Mheshimiwa Spika, utumiaji wa vocha kwa wakulima ni jambo zuri lakini Serikali inapaswa kuwa makini ili utaratibu huu uwafikie walengwa. Ahsante.

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri na Naibu wake pamoja na watendaji wa Wizara kwa kazi nzuri ya kuandaa hotuba hii yenye mambo mengi mazuri.

Mheshimiwa Spika, matumizi bora ya wataalamu, kila mwaka tunazalisha wataalamu wenye digrii kutoka Chuo Kikuu cha Sokoine lakini sijui hawa wanaishia wapi. Kazi yao nini mbona hatuoni wakiwa na mashamba makubwa, wakiwa na mifugo ya kisasa? Sioni wakiendesha matrekta huko mashambani? Mbona hawaonyeshi mifano. Nashauri wakope toka katika mabenki waanze kilimo kikubwa cha kisasa. Mbolea imekuwa ghali sana duniani.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya mbolea yataleta tija na faida kama tutakuwa na mashamba makubwa ya kilimo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, naomba ueleze Bunge hili hawa wataalam wanaozalishwa kila mwaka mashamba yao yako wapi? Kama hakuna je, wamesoma ili wafanye nini?

Naomba mashamba yaliyoko mkoa wa Kilimanjaro wapewe wazawa hawa waliojaa huko kwenye ofisi za kilimo walime kitaalamu ili wengine waige. Nashangaa wazungu wanatoka Ulaya kukodisha mashamba haya kutoka vyama vya ushirika. Niko tayari kuwashawishi wazawa hawa waache suti zao ofisini wakaendeshe matrekta, wazalishe kahawa na mazao mengine.

Kuhusu Bodi ya Kahawa, imekuwa haina meneja mkuu kwa zaidi ya miaka miwili, namwomba Mheshimiwa Waziri ateue meneja mkuu wa bodi ya Kahawa ili bodi ile iwe na maamuzi ya kuwajibika. Bodi ipewe fedha za kutosha ili iweze kutafuta masoko mazuri ya Kahawa. Naomba kila mkoa upewe malengo ya uzalishaji ya mazao ya chakula na ya biashara. Kama mkoa hautafikia malengo bila sababu basi viongozi wake wawajibishwe. Tuna ardhi nzuri, mito mingi, mvua ya kutosha kwa hiyo hakuna sababu ya kutokuwa na chakula cha kutosha na ziada tukauza nje.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali badala ya kuuza mahindi Kenya tuwauzie unga ili mashine zetu za kusaga zipate kazi na ajira kwa Mtanzania na pia tubaki na pumba kwa mifugo yetu. Hata wafanyabiashara washauriwe wawe na uzalendo kama kweli kuna ulazima wa kuuza Kenya basi na wao wauze unga.

**MHE. KHADIJA SALUM ALY AL-QASSMY:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha siku ya leo kufika hapa Bungeni bila ya kukamatwa mkono.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo yangu hayo sasa naomba nianze kutoa mchango wangu kama ifuatavyo. Hotuba ya Waziri itabaki kuwa historia iwapo kama Serikali haikuwa tayari kuwaondolea Watanzania kilimo cha kutumia jembe la mkono, pia kuwapatia bei nzuri pamoja na soko la uhakika.

Mheshimiwa Spika, wakulima wetu wamekabiliwa na matatizo makubwa jambo ambalo hupelekea kukata tamaa kwa kazi yao, na ndio maana miji yetu ikawa na idadi kubwa ya watu wasio na kazi. Laiti kama Serikali inawapatia soko la uhakika, bei na kadhalika wataweza kuiondolea matatizo ya njaa nchi yetu. Pia tuachane na kilimo cha mvua kwa miongo. Hii mara nyingi sana wakulima hukosa mavuno kutokana na ukosefu wa mvua. Sasa ni wakati wa kilimo cha umwagiliaji maji.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ukosefu wa benki ya wakulima nchini ni doa kubwa kwa wakulima, wakulima wetu wengi ni wadogo wadogo wanahitaji mikopo ili iwawezeshe wakulima wetu kulima kwa kilimo cha kileo.

Mheshimiwa Spika, kuna ukosefu wa viwanda nchini jambo ambalo hupelekea baadhi ya mazao kuharibika kwa mfano, machungwa, maembe, mananasi na kadhalika. Msimu wa mazao haya ukifika utajua jasho la mkulima Serikali halilijali. Hakuna sababu yoyote kuharibika kwa mazao haya ila ni mwenendo wa Serikali yenyewe. Laiti kama tunakuwa na viwanda vya kutosha mazao yetu yasingeharibika, pia uhuru wa biashara. Mkulima kuruhusiwa kuuza mazao yake popote ama ndani ya nchi au nje ya nchi hili lisingelitokea.

Kuna baadhi ya wakulima waliojaribu kumpa mazao yao nje ya nchi wamekamatwa na mali yao inataifishwa yote. Hii ni kumuenzi mkulima au kumkomoa? Ahsante.

**MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kusema naunga mkono hoja hii. Hoja ya Wizara hii inaleta matumaini kwa kilimo kuendelea kukua na kuleta manufaa kwa wananchi ambao 70% wameajiriwa na sekta hii.

Pamoja na hayo napenda kutoa maoni yafuatayo, kilimo katika maeneo yangu mvua kidogo *(arid areas)* Ukanda wa Kati (Dodoma, Singida na sehemu ya Mikoa ya Tabora na Shinyanga) ni ukanda wenye mvua kidogo. Mazao yanayovumilia hali hii ni mtama, uwele, muhogo, na mazao ya mbegu za mafuta ambayo ni karanga, nyonyo, ufuta, alizeti na kadhalika. Lakini msukumo wa kuendeleza mazao haya bado hautoshi kwa maana ya mbegu bora, huduma za ugani, soko na kadhalika. Wizara itoe msukumo muhimu kwa mazao haya ili kuwaondoa wakazi wa mikoa hii katika umaskini na njaa za mara kwa mara.

Kuhusu kupambana na kwelea kwelea, ukanda wa kati mtama na uwele unalimwa japo kwa njia za jadi, lakini pia kwelea kwelea hushambulia kila mwaka, Wizara lazima iwe na maandalizi ya kupambana na tatizo hili kila mwaka. Mwaka huu kwelea kwelea walishambulia sana mtama katika jimbo langu la Manyoni Mashariki (Bonde la Ufa). Binafsi nilipiga simu kila siku kwa wiki mbili mfululizo kuomba ndege ije kunyunyuzia dawa. NilIishia kupata ahadi, nilishaeleza ndege ipo Dodoma inasubiri dawa Za kunyunyuzia. Tulizidi kusubiri na hadi ilipokuja kwelea kwelea walishmbulia mtama na kuhama! Maeneo hayo kwa sasa wana upungufu mkubwa wa chakula kwa sababu tu, ndege haikuja kwa wakati. Hali hii Wizara ijipange isitokee tena!

Mheshimiwa Spika, kuhusu kilimo cha umwagiliaji, Wilaya ya Manyoni tunazo *scheme site* za kilimo cha umwagiliaji (kilimo cha majaruba ya mpunga) lakini umwagiliaji hufanywa wakati wa mvua tu kwani hakuna mabwawa ya kuhifadhi maji. Wizara ya Kilimo ishirikiane na Wizara ya Maji na Umwagiliaji kupandisha hadhi ya *scheme* hizo ili zitumike hata wakati wa kiangazi ili kuinua kipato cha wakulima. Ombi ni kwamba mabwawa yakijengwa yatasaidia sana *scheme* hizi kuwa na kilimo cha masika na kiangazi.

Mheshimiwa Spika, narudia kusema naunga mkono hoja hii.

**MHE. DR. CHARLES O. MLINGWA:** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri, katibu Mkuu na watendaji wakuu wote kwa kazi wanazofanya.

Mheshimiwa Spika, nimeangalia kitabu cha hotuba ya Wizara sijaona baadhi ya mambo muhimu, nini, dira ya maendeleo ya kilimo nchini? Nini dira ya chakula nchini na nini dira ya ushirika nchini?

Mheshimiwa Spika, haya mambo ndiyo msingi wa kazi za Wizara hii ya kuongoza maendeleo ya Kilimo, Chakula na Ushirika nchini. Naomba Wizara inijibu katika haya.

Kwanza ni kuhusu ushirika, ushirika ni taasisi ya biashara yenye uhuru wa kujiunga kwa hiari baada ya mhusika kuamini na kukubali malengo makuu ya ushirika husika na huduma za wanachama ndani ya ushirika wao. Vyama vya ushirika siyo taasisi za Serikali. Serikali ni mhamasishaji tu na mwezeshaji pale panapohitajika. Si vizuri Serikali kuendelea kulea vyama vya ushirika vilivyoshindwa kazi kwa ubadhirifu na uongozi/utendaji mbaya wa wahusika na hivyo, hatima ya ushirika imara ni elimu sahihi ya ushirika na biashara. Bila elimu hii, ushirika ambao unakuwa kila siku, hauwezi kuleta manufaa yanayotarajiwa kwa maendeleo ya nchi. Bahati nzuri tuna Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika Moshi.

Nashauri Wizara hii ishirikiane na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi katika kuona upanuzi wa mafunzo ya ushirika na biashara yanakwenda kwa kasi na kusema kweli chuo hiki kiwe Chuo Kikuu kamili baada ya mwaka huu wa 2008/2009. Hii itawezesha Chuo Kikuu hiki kuongeza mafunzo ya ushirika na biashara kutoka ngazi cheti (astashahada), stashahada na Shahada.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kuongezeka kwa watu/wananchi waliosomea ushirika na biashara ndipo tutakapopata wanachama waelewa wa ushirika, viongozi waelewa wa kusimamia vyama vya ushirika na watendaji bora wa vyama vya ushirika. Ongezeko la vyama vya ushirika ni changamoto kubwa, bila ya elimu ya ushirika na biashara hatutafika!

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na biashara cha Moshi kina kampasi kubwa pale Kizumbi. Wizara hii isisitize upanuzi wa mafunzo ya ushirika katika chuo hiki katika kampasi ya Kizumbi (Shinyanga),

**MHE. DR. LUKA J. SIYAME:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii awali ya yote nimshukuru Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika kwa hotuba yake nzuri. Napenda pia niwashukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, katibu Mkuu, wakurugenzi, wakuu wa taasisi na asasi zilizo chini ya Wizara hii na wadau wote wa sekta ya kilimo kwa mchango wao mkubwa katika kufanikisha matayarisho ya hotuba Bajeti ya Wizara hii, na pia kwa juhudi zao katika kuhakikisha nchi hii inapiga hatua mbele katika maendeleo ya kilimo na uchumi kwa jumla.

Naishukuru sana Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kwa ushauri wake mzuri sana. Napenda kusema naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, pamoja na uungaji wangu mkono Wizara hii, naomba nijielekeze katika mambo yafuatayo, program ya kuendeleza sekta ya kilimo, upatikanaji wa pembejeo za kilimo, mfuko wa Taifa wa pembejeo, uzalishaji wa chakula, wataalam wa huduma za ugani na ushirika.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ufasaha uliopo katika maelezo ya Ilani ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005 ya Chama cha Mapinduzi, kuhusiana na umuhimu wa kufanya mapinduzi makubwa katika kilimo ili kumletea mwananchi mkulima maisha

bora, mpaka sasa miaka miwili na nusu imepita bila ndoto hiyo kuonyesha mwelekeo wa matumaini kwa wakulima wengi nchini. Sababu ni wazi ikiwa pamoja na kutotekeleza mipango yetu ya kuendeleza sekta ya kilimo kutokana na ufinyu wa Bajeti yetu, upungufu mkubwa wa wataalam wetu wa kilimo, kutopatikana kwa pembejeo za kilimo au kupatikana pembejeo hizo baada ya muda unaofaa kupita tena kwa bei mbaya mno inayowakatisha tamaa wakulima wetu.

Mheshimiwa Spika, pale ambapo wakulima wetu wamejitahidi kuomba mikopo ya mfuko wa pembejeo kwa ajili ya kununua mbolea au zana za kilimo, umetokana na usumbufu mkubwa wa ukiritimba kuanzia Wilayani hadi Makao Makuu ya mfuko wa pembejeo. Kwa namna ya kushangaza kabisa, wakulima kwa mfano wa jimbo la Mbozi Magharibi waliotaka kukopa fedha kwa ajili ya mbolea na matrekta waliambiwa hawawezi kukopeshwa kwa sababu kuna watu Wilayani Mbozi ambao hawajarejesha mikopo yao. Jimbo la Mbozi Magharibi mpaka sasa lina watu watatu tu, tena Madiwani waliokopeshwa matrekta. Naamini hao hawawezi kuwa kigezo cha kuwanyima watu, wengine wenye kila sifa ya kukopa na kurejesha fedha hizi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uzalishaji wa mazao ya chakula na ya biashara, napenda kusema wakulima wetu wana ari kubwa ya kufanikisha azma hii lakini mfumo mbaya wa miundombinu iliyoko kwenye maeneo ya wakulima, kwa mfano barabara mbaya, ukosefu wa umeme, huduma duni za maji na afya na elimu kuhusu kilimo chenye tija kwa wakulima, hatima yake ni kuwakatisha tama.

Mheshimiwa Spika, jimbo la Mbozi Magharibi na ukanda mzima wa Bonde la Ufa la Rukwa, ni eneo zuri sana kwa kilimo cha mazao ya chakula yakiwemo mazao ya nafaka kama mahindi, mpunga, mtama na ulezi bila kusahau matunda ambayo hulimwa bila kutumia hata mbolea. Tatizo kubwa wanalolipata wakulima wa maeneo hayo ni bei ndogo ya mazao yao kutokana na miundombinu mibaya inayosababisha ukosefu wa soko la mazao yao. Wafanyabiashara wachache wanaofikisha magari yao huko kuishia kununua mazao hayo kwa bei ya kutupa. Kwa bahati mbaya, kutokana na ushauri mbaya wa wataalam wetu wa sekretarieti za mikoa, hata pale ambapo Serikali ilikuwa inapanga kuainisha maghala kwa ajili ya hifadhi ya mazao hayo kwa utarabitu wa stakabadhi za mazao ghalani, maghala hayo yameamuriwa kwenda kujengwa kwenye barabara kuu ambako wala tatizo la hifadhi ya mazao haliko.

Mheshimiwa Spika, wakulima wetu wakihamasishwa wakapewa elimu bora kuhusu kilimo cha kisasa maeneo mengi ya Bonde la Ufa la Rukwa yatakuwa mkombozi wa uhakika wa tishio la upungufu wa chakula nchini. Maeneo haya yanaweza kulimwa mara mbili kati ya Novemba na Juni kila mwaka kwani mazao kama mahindi na mpunga huchukua miezi miwili hadi mitatu tu kukomaa.

Kwa upande wa ukanda wa juu *(Plateau)* ambao ni uwanda wa baridi kiasi, kilimo cha mahindi, mpunga na maharage kinahitaji mbolea. Ukanda huu una eneo zuri na kubwa la kilimo hicho lakini kama ilivyojitokeza kwa mfululizo wa miaka mitatu iliyopita, ukosefu wa mbolea umetugharimu kwa kiasi kikubwa na kuwarudisha wakulima hawa kimaendeleo. Wakulima wa ukanda huu wanahitaji na wana haki ya

kupata mgao wa mbolea kama wananchi wengine. Miaka mitatu mfululizo, ukosefu wa mbolea umezua biashara mbaya ya ulanguzi wa hali mbolea ya ruzuku. Kata za Tunduma, Chiwezi, Nkangama, Kapelo, Ndalambo na Myunga zinahitaji kivunge maalum cha mbolea kwani bila hivyo maisha ya wananchi wa kata hizi yako hatarini kukumbwa na umaskini mkubwa mbali ya tishio la kufa kwa njaa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kuwa pembezoni Jimbo la Mbozi Magharibi lina upungufu wa watumishi wa ugani wa kilimo. Mazao yote yanayolimwa jimboni kwangu yanapatikana kwa kiasi kikubwa kutokana na juhudi binafsi za wananchi ambao wanatumia mbinu za enzi za ujima. Naomba wataalam wa kilimo kule Mbozi Magharibi.

Mheshimiwa Spika, huduma za ushirika zienezwa vijijini kwani bila hivyo hata soko la mazao ya wakulima litaendelea kuwa baya. Maafisa ushirika mia Wilayani wawezeshwe kuwafikia wakulima vijijini ili kuwapa elimu ya ushirika na kuwawezesha kuanzisha ushirika sehemu zao.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii kumpongeza sana Waziri Mheshimiwa Stephen Wasira, Naibu wake Mheshimiwa David Mathayo David, Katibu Mkuu Ndugu Peniel Lyimo na Naibu Katibu Mkuu Bi. S. Kaduma na watumishi wote wa Wizara kwa kuandaa a *well-detailed budget speech* ambayo nimeridhika nayo kwa vigezo vyote vilivyoelezwa ndani ya hotuba hii. Naunga mkono hotuba hii na maudhui yake.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi kirefu sera za kilimo kuanzia miaka ya 1970, imeendelea kutoa majukumu ya Wizara hii ambayo hayatofautiani na maagizo ya Ilani kama yalivyoainishwa kwenye ukurasa wa 63 *items (i)* hadi (x) kwenye hotuba hii ya Waziri. Yote hayo yanajulikana lakini tumeshindwa kuyasimamia sababu tumefanya kilimo kiendeshwa bila sheria, taratibu za kuwataka wakulima wasiendeshe kilimo bila kuzingatia miongozo. Uamuzi wa kuwa na tamko la siasa ni kilimo na siyo kilimo ni siasa, hatujaupatia tafsiri sahihi. Turudi tena kwenye chama tawala, tupangane na viongozi wote ili kila mmoja ajue wajibu wake na kuzingatia yafuatayo, kwanza, tusiogope kuwa na wawekezaji wakubwa katika kilimo. Tusiogope waje toka kokote kule ili wakisaidiana na wakulima wadogo wadogo waweze kufanikisha kilimo cha kisasa.

Pili, tusikubali maeneo mazuri na yenye mabonde mazuri yakatumika kwa mifugo. Tuyatumie kuzalisha chakula tu. Nia yangu kwa nguvu zote utekelezaji wa mipango ya matumizi bora ya ardhi *(Land use planning).* Tusitumie ardhi yetu bila mpangilio wa kisheria na kanuni bora za kilimo. Mifugo ipangiwe maeneo mengine kwenye *highlands.*

Mheshimiwa Spika, tuandae wataalam wengi Wilayani ili wawe na uwezo wa kuandaa miradi ya maendeleo kwa kila Wilaya. Baada ya haya, tuandae wataalam (vijana) ambao tunaweza kuwapa mafunzo ya angalau mwaka mmoja ili tuwape nyenzo

za kusimamia miradi hiyo. Sioni tatizo kwa kuanza na vijana wanaotoka vijijini ambao wamemaliza *Form IV* kwa kuanzia.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kuamua mbolea ya Minjingu ianze kutumika rasmi kwa kuiongezea virutubisho kwa faida ya wakulima. Tunaomba mbolea hii ianze kupelekwa Rukwa na kwenye mikoa ya *the big four*. Tutumie pia vocha za mbolea ya ruzuku mkoani Rukwa.

Mheshimiwa Spika, naipongeza pia Serikali kwa kuanzisha rasmi *National Food Reserve Agency* ambayo imechukua nafasi ya *SGR*. Nampongeza pia Mkurugenzi wa taasisi hii ambaye naelewa ana uwezo mkubwa wa kuendesha taasisi kama hii.

Ombi langu kwa sasa ni kuiomba Wizara iisaidie taasisi hii ili ianze kununua nafaka Sumbawanga kwa nia ya kupisha eneo la kununua tena mahindi ya mwaka huu toka kwa wakulima ambao hawaruhusiwi kuuza nje ya nchi. Ukombozi wetu kwa sasa ili kitengo hiki kianze kununua mara moja. Naelewa kwa sasa tuna tani 76,000 za mahindi na tani 6,000 za mtama, nashauri jitihada za kuongeza ununuzi ili ifikie tani zaidi ya 150,000 ili kujiandaa na upungufu wa chakula: ununuzi uanze mara moja. Ombi la wenzetu wa Kenye kutaka mahindi, liangaliwe upya.

Mheshimiwa Spika, bado suala la kuwapa motisha watumishi lazima lipewe umuhimu wa kwanza. Mtetezi wa hali ya maslahi ya wakulima ni Waziri mwenyewe. Wakati Wizara nyingine zinaandaa mikakati ya kuboresha maslahi ya watumishi wake, mbona kilimo haiende kwa kasi ile ile na ya walimu, waganga na kadhalika? Nini hatma ya kuanza kutumia *uniforms* kwa watumishi vijijini na hasa mabwana shamba wa kata/vijijini?

Mheshimiwa Spika, nini mipango ya Wizara kuongeza idadi ya watumishi wa ushirika? Mbona sehemu nyingi katika Wilaya zetu maafisa hawa wako kidogo sana. Kwa nini kusiwe na *crash programme* ya kuwafundisha, vijana wetu huko huko vijijini ili wasaidie kuanzisha *SACCOS* na vikundi (vikoba/vibindo).

Mheshimiwa Spika, mwisho nashauri Waziri aagize kila mkoa, wilaya, kata na vijiji wawe na siku za wakulima rasmi katika maeneo yao. *TASO* iratibu na itoe maelekezo ili mipango ya zawadi tuifanye wenyewe katika maeneo yetu wenyewe.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA**: Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa kunipa nafasi nami nitoe mchango wangu wa maandishi.

Nampongeza sana Mheshimiwa Stephen Wasira, Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, Naibu Waziri Mheshimiwa David Mathayo David, Katibu Mkuu wa Wizara na mkurugenzi pamoja na wadau wote wa Wizara hii kwa kazi ngumu na nzuri.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu ulitolewa wakati nachangia Bajeti ya Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana. Nategemea taarifa hizo mmezizingatia vile vile, labda kwa kukumbusha, mara ya mwisho nilifuatilia sera yenu, nikapewa ya mwaka 1997. Nimeipitia, nimeona bado inatakiwa kuongezewa yafuatayo, kuwepo *profile* ya wakulima ili waweze kupata *supports* zinazostahili. Mfano *some policy* inasema *micro - 1 to 4 employees, capital up to 5 million, small – 5 – 49 employees, 5 – 200 million, large….*

Mheshimiwa Spika, sera hiyo inazungumzia zaidi Wizara ita…, haionyeshi vizuri jinsi inavyo *link* na *local government* pamoja na usimamizi wa jumla katika kazi za kilimo. Nashauri ni vyema ifanyiwe kazi, wakati wa marekebisho.

Mheshimiwa Spika, narejea umuhimu wa kutoa motisha ya wawekezaji wa ndani katika kuwekeza mashine na viwanda katika maeneo ya kilimo ili kuongeza thamani mfano kodi na kuwafahamisha watu mahli ambapo mashine za kusindika matunda zinapatikana na bei zake.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Ruvuma umeonyesha mafanikio makubwa katika kilimo cha uyoga kupitia kutamizi cha ujasiriamali *(better life Tanzania).* Tuna tatizo la mashine ya kuzalisha mbegu. Tunaomba msaada wenu, kwa sasa tuna wakulima zaidi ya 800 na tungetamani kuona zao hili llinakuwa zao kuu kama ilivyo tumbaku au kahawa kwani lina faida kubwa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kutenga muda ili tutoe mchango wetu katika sekta hii muhimu.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kupongeza shughuli zote ambazo Mheshimiwa Waziri amekuwa akizifanya kuanzia Wizara zingine ambazo amewahi kuzisimamia ni mtu shupavu na muwazi, pia pongezi kwa Naibu Waziri mchapakazi asiye na matatizo na mtu anayekubali kufundishwa. Niwapongeze wakurugenzi wote chini ya Katibu Mkuu Ndugu Peniel Lyimo ni mzoefu na mbunifu nawaomba wasaidizi wake wampe ushirikiano.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo mchango wangu wenye lengo la kuunga mia kwa mia kwa utekelezaji. Niipongeze Serikali kwa kuvilea na kuvipunguzia mzigo wa madeni ambayo yalilimbikizwa kwa miaka mingi.

Mheshimiwa Spika, nia ya Serikali kufufua ushirika ni nzuri sana pamoja na nia hiyo yapo mambo muhimu ambayo tukizingatia tutafikia lengo mapema.

Mikopo ya benki ni mizuri lakini riba yake bado ni kubwa mfano *NCU* iliomba shilingi 6,000,000,000/= na imepewa shilingi 3,000,000,000/= kati ya hizo imeruhusiwa kuchukua shilingi 1,000,000,000/= na kuzipeleka kwenye vyama vya ushirika kununua pamba ili warudi kuchukua pesa zingine lazima wasombe pamba 65% ya manunuzi.

Mheshimiwa Spika, si rahisi mahala ulipopeleka shilingi 2,000,000/= ukapata pamba ya kutosha kubebwa na lori tani 10 wakati shilingi 2,000,000/= ni kama tani tano tu kwa bei ya shilingi 400/=.  Mfano huo tayari unaashiria hasara zifuatazo kuchelewa kusomba pamba kuna malipo ya wasimamizi wa mkopo waliowekwa na benki ambao kila *ginnery* hupaswa kulipwa dola 1,800 kwa kila mwezi.  Ushauri ni vyema Serikali ilione tatizo hilo na kutafuta namna ya kuepusha hasara zisizo za lazima yapo mema mengi iwapo vyama vya ushirika vitaepushwa na riba za benki.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kupitia bodi ya pamba kufuta *passbook*, chombo hiki kilianzishwa kwa nia nzuri na malengo mazuri lakini chombo hiki kimedhulumu watu/wakulima wengi sana hivyo kufutwa kwake ni kheri kwa wakulima, swali je, wakulima waliopoteza pesa zao kupitia *passbook* watarejeshewa haki zao au ndio basi?

Mheshimiwa Spika, mrajisi wa vyama vya ushirika anayo majukumu yaliyoainishwa kisheria ili ayatekeleze, ni vyema utaratinbu uangaliwe vizuri kwani maafisa ushirika wa mikoa walio chini ya *RAS* hivyo hufanya kazi za jamii nzima hivyo kazi za ushirika huduma au kutofuatiliwa kwa usahihi.

Maafisa ushirika wa Wilaya walio chini ya *DED* wakati mwingine huwa makaimu *DED* hivyo hushughulikia makusanyo ya ushuru wa mapato hivyo kazi za mrajisi huishia Wizarani tu.  Kama watu wa kumsaidia huku chini ni vyema akapewa watumishi hawa wote na akawa na wajibu wa kuwawajibisha ikibidi hii itasaidia kufikia lengo.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa mradi wa maji wa kituo cha utafiti na Chuo cha Kilimo Ukiriguru umekuwa wa kusuasua katika mchango wangu wakati wa hotuba ya Waziri Mkuu nilielezea matatizo yaliyopo hapo pia kamati imesisitiza jambo hilo, naomba Bunge lielezwe utekelezaji ukoje kwa sasa.  Mheshimiwa Waziri naomba majibu ya hatua ilivyo kwa mradi huo.

Mheshimiwa Spika, mfuko wa pembejeo ni chombo muhimu sana kama kitapewa mtaji wa kutosha mfano mwaka 2008/2009 ni kiasi kidogo Serikali ione namna ya mfuko wowote uongezwe katika mfuko wa pembejeo ni chombo muhimu na ni mkombozi wa wakulima wadogo.

Mheshimiwa Spika,  suala la benki ya wakulima ni muhimu kama kuna ugumu basi benki ya *TIB* ihudumie Watanzania wengi na pia chombo hiki ni cha Watanzania ni kuamua tu matumizi kuhusu benki ya wanaushirika ni vyema vyama vikijipanga vizuri viwe na benki yao itakayowahudumia kwa riba nafuu hivyo mrajisi aione hoja hiyo siku za usoni kwani sasa vyama bado vinajiimarisha.

Mheshimiwa Spika, mazao mchanganyiko kuwa na bodi yake Serikali inaandaa Mkoa wa Mwanza na Shinyanga ni mikoa inayolima zao la dengu kwa wingi sana mara kwa mara huwa linakosa soko ni wajibu wa Serikali kutafuta masoko.

Pia ni vyema Serikali ikapokea shukrani kwa mpango wake wa stakabadhi ya mazao ghalani kwa zao la dengu ni sahihi kwani linaweza kutunzwa kwenye stoo moja na ni rahisi kutunza. Ushauri maghala hasa kwa vyama vya ushirika vya pamba yanahitajika ni vyema Serikali ifanye kila liwezekanalo wapate pesa za kujenga maghala vijijini ili maana ya stakabadhi ya mazao ghalani iwe sahihi sasa hivi, pamba inayonunuliwa kwenye baadhi ya maghala huwa nusu iko nje maghala ni ya zamani yamezeeka.

Mheshimiwa Spika, mwisho bei ya zao la pamba ukweli ni ndogo sana juhudi za Waziri zimesaidia kiasi kwa sasa ni 420 kwa kilo, lengo ikifika 500 itasaidia.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono.

**MHE. YUSUF R. MAKAMBA**: Mheshimiwa Spika, maeneo ya wafugaji na wakulima, Morogoro kuna ugomvi mkubwa wa wakulima na wafugaji. Vijiji vya Twatwatwa, Kiduki, Kambala, Mabwegere vilitengwa kwa ajili ya mifugo. Kwa kuzorota kwa huduma wafugaji wanahamia katika maeneo ya wakulima Serikali ipeleke huduma ili wafugaji wasihamie maeneo ya wakulima.

Kuhusu uhaba wa ardhi, vijiji vya Makorora, Mashewa, Kulasi, Kwagunda, Magunga Cheke, Mkwakwani na Mnyuzi, vijiji hivi vimezungukwa na mashamba ya mkonge mwaka 1974 kijiji cha Makororo kilimegewa ardhi ya mkonge na baadaye kikanyanyanywa ardhi. Naomba Mheshimiwa Waziri, utembelee kijiji cha Makororo ukaone hali halisi.

Mheshimiwa Spika, umwagiliaji, Serikali ilikuwa na mpango wa kujenga Bwawa la Manga – Mikocheni (Mkonazi Korogwe). Bwawa hili lingesaidia umwagiliaji katika hekta 11,000 katika vijiji vya Mkomazi, Mkumbara, Mazinde, Mombo, Chekelei, Makuyuni, Kwagunda – mpango huu umeishia wapi, ningependa maelezo.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Pamoja mchango wangu wa kusema pia nieleze yafuatayo kwa maandishi, mgawanyo wa mbolea kwa mwaka 2008/2009 ni vizuri Wabunge wote tugawiwe kiasi cha mbolea ya ruzuku kinachotolewa ili kila Mbunge afahamu mgao wa mkoa wake.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha kilimo cha Bugaga Wilayani Kasulu kifanywe cha Kitaifa kama ilivyo Ilonga, Tumbi na Ukiriguru. Kituo hiki kuendelea kuhudumiwa na halmashauri ya Wilaya kitakosa tija na msaada wake kwa walikuma ni mdogo sana. Hapo zamani kituo hiki kilipewa nafasi kubwa kwa kupewa fedha na watumishi.

Mheshimiwa Spika, ushauri, kituo hiki kipewe *priority* ya Kitaifa. Halmashauri ya Wilaya iwe mdau mkuu tu. Mkakati wa Wizara ujikite katika kuanzisha na kushirikiana na Halmalshauri ya Wilaya, miji kuanzisha, *form centres*, maksai/*place*, trekta, mbegu, ujenzi wa maghala na shule za wakulima (mashamba darasa) na wasomi wetu wengi wapelekwe ku-*support/manage* hizo *centres* ili kuongeza tija katika uzalishaji iwe ni dhambi, wasomi wa kilimo kuishia maofisini na kuhudhuria warsha na semina tu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuzuia uuzaji wa mazao ya kilimo nje ya nchi yetu, hili ni sawa kabisa, hoja ni kwamba maeneo/mikoa ambayo bado kufikiwa na stakabadhi ya mazao vocha hawana wananchi wanaoishi mipakani ambao maisha yao ni kuuza mazao nje ili waboreshe maisha na familia zao *what is the way forward, what should they do?* Hawana masoko ya ndani kwa sababu ya miundombinu duni, tegemeo lao ni nchi jirani watafanya nini. Ni kwa nini usibuniwe mkakati wa haraka kwa wananchi wa vijijini kule Kibondo, Kasulu na Kigoma ili mazao yao yanunuliwe na *SGR* yetu *(Agency).*

**MHE. JOHN P. LWANJI:**Mheshimiwa Spika, chakula. Mmetuhabarisha kuwa bei ya vyakula zitaendelea kuwa juu kwa karibu miaka kumi ijayo. Kuna upungufu mkubwa wa chakula duniani na pia nchini, magazeti yaliripoti kuwa Ngara debe moja la mahindi limebadilishwa na *SMG.* Nashangaa magazeti ya jana na leo yameripoti kuwa Serikali imekubali kuiuzia Kenya mahindi.

Sisi (Wabunge) tunawahubiria wananchi wetu wasiuze chakula au kutumia chakula vibaya kama pombe na kadhalika. Sasa wanasema kwamba Serikali inauza chakula nje ingelifaa Serikali itoe msimamo kuhusu mkanganyiko huu. Tatizo la nchi yetu tumekuwa wakarimu sana kwa majirani zetu wakati wananchi wetu wanaumia. Pia tumekuwa na mazoea ya kulea *shortages* (mapungufu), *chronic shortages* za makusudi. Bila shaka wanaolea *shortages* hizi wananufaika na uagizaji wa chakula kutoka nje kwa gharama kubwa *at the expense of the masses.*

Mheshimiwa Spika, wakulima wetu wadogo wadogo wana vikwazo lukuki zaidi ya kumi kuanzia wanapopanda mazao ambavyo ni majongoo, panya, kwale, ngedere, tembo, dumuzi/kweleakwelea, vizuizi wakati wa kusafirisha mazao, walanguzi wanaonunua mazao yangali shambani na baada ya kuvuna, bei mbaya/kukopwa mazao na makato ya ushuru.

Mheshimiwa Spika, vikwazo vyote hivi vinamwacha mkulima huyu hoi Wizara inajishughulisha zaidi na mambo ya utafiti kuliko kuja na hatua za kumuondolea mkulima aza hizi. Mkulima anaachwa kuhangaika peke yake. Wizara inaonekana kuja na mipango wa tafiti za wakulima wakubwa wa si wadogo wadogo. Ukombozi wa kilimo chetu ni plau na si matrekta kwa wingi kwa sababu mkulima wa kawaida hawezi ku-*maintain tractor* hata akipewa bure kutokana na gharama kubwa, bei ya mafuta haishikiki. Ni heri Serikali isambaze plau zaidi, hata milioni 10 na maksai kuliko matrekta kuliko *target* ya plau 100,000. Pia Serikali inunue ndege zake za kupambana na Kwelea kwelea ili wananchi walime na kuvuna chakula kwa wingi (mtama na uwele).

Mheshimiwa Spika, ushirika umeipa kipaumbele zaidi *SACCOS* na si kilimo cha uzalishaji, mamlaka makubwa ya Mrajisi wa vyama vya ushirika yana-*overide* mamlaka ya bodi za vyama vya msingi. Uwakilishi wa wajumbe 6 mpaka 9 kuwakilisha chama cha msingi hata chenye idadi kubwa ya wanachama inakwenda kinyume na dhana ya demokrasia. *Ratio* ya uwakilishi iendane na idadi ya wanachama wa chama cha msingi husika. Marekebisho yaletwe Bungeni kufanyiwa marekebisho yanayoostahili.

Mheshimiwa Spika, tatizo la kilimo cha tumbaku Mgandu Mwaka imeuza tumbaku ya shilingi bilioni mbili, lakini ni shilingi milioni 20 tu zimetengwa na Halmashauri kama *cess* kwa ajili ya kujenga mabwawa ya kumwagilia miche. Kiasi hiki ni kidogo sana wakati halmashauri imepata *cess* ya shilingi milioni 150 kwa maana ya *percent* ya asilimia tano kwa kila belo la tumbaku.

Naiomba Wizara isaidie kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya ujenzi wa mabwawa ya umwagiliaji wa miche.

**MHE. BERNADETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kumpongeza Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara hii kwa hotuba nzuri lakini vile vile kwa mipango mizuri inayoendelea katika sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, kilimo ni sekta inayoajiri Watanzania walio wengi. Njia pekee ya kuondoa umaskini ni kuboresha kilimo, hotuba ya Bajeti hii imesheheni mipango mizuri na mikubwa. Lakini Bajeti ya shilingi bilioni 113.737 ni ndogo sana haiwezi kuyatekeleza kikamilifu. Tunaomba Serikali, iangalie sekta hii upya ili kusudi wapangiwe fedha nyingi zaidi.

Mheshimiwa Spika, ili tuweze kuboresha kilimo lazima tuhakikishe tunaongeza uzalishaji, tulime kwa matrekta na majembe yanayokokotwa na wanyama, uwezekano wa watu wa kawaida kununua matrekta ni mdogo. Trekta zuri na kubwa liko kati ya shilingi milioni 35 mpaka 50. Serikali imejitoa kwenye biashara, lakini kwa hili naomba Serikali ifumbe macho, inunue matrekta ili tupanue kilimo (angalia mfano wa ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma, Serikali imekopa kwenye mifuko ya hifadhi wameanza kujenga. Baadaye sehemu nyingine watawaachia wawekezaji wa nje na ndani). Nashauri kwa hili, kwa kuanzia, Serikali itafute fedha, inunue *tractor* za kuanzia.

Pili, Serikali iwekeze kwenye miundombinu ya umwagiliaji. Je, Serikali iko tayari kupokea ushauri wangu huo? Tuhakikishe watu wawekeze kwenye viwanda vya kusindika mazao. Soko lipo, kwani nchi nyingi duniani wana uhitaji wa mazao mbalimbali na ziwepo benki zilizo na masharti nafuu, walio tayari kukopesha wakulima.

Mheshimiwa Spika, upungufu wa wataalamu hatuwezi kuboresha kilimo kama hatuna wataalamu waelekezi. Mkoa wa Kagera una maafisa ugani 148 tu wakati wanahitajika zaidi ya 700. Je, Serikali iko tayari kuupatia mkoa wa Kagera maafisa ugani wangapi na lini? Wananchi wa Kagera, kihistoria ni wakulima na walaji wa zao la ndizi, wamefanya hivyo kwa miaka mingi sana sasa hivi migomba hii inashambuliwa sana na magonjwa hatari ya mimea, migomba inaugua mnyauko bakteria *(banana*

*manthomonas wilt)* mihogo yetu ya asili inashambuliwa vibaya na batobato kali *(cassva mosail disease)* na mibuni inashambuliwa na nyauko fuzari *(coffee fusarium wilt).* Magonjwa haya yamewatia wananchi wengi umaskini. Wamelima, mazao yote yameharibika. Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa fedha za kutosha ili kufanya uhamasishaji kwa wananchi ili kuwaandaa waweze kuwa tayari kulima sasa mbegu za kisasa za migomba, mibuni, mihogo na kadhalika?

Mheshimiwa Spika, vipo vituo mbalimbali vinavyozalisha mbegu hizi za migomba, mihogo na mibuni lakini viko mbali kwa mfano *TACRI*, Maruku, Ibwera, Biharamlo na kadhalika. Je, Serikali itatoa fedha kiasi gani ili kuhakikisha mbegu bora zinawafikia wakazi wa Kagera wasio na fedha au uwezo wa kuzifuata huko zinapozalishwa?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri ambayo inaonyesha kutia matumaini ya maendeleo katika sekta ya kilimo nchini. Pia nimpongeze kwa kutokuja na programu mpya, maana tumezoea kuletewa programu zisizo na tija yoyote.

Mheshimiwa Spika, nina mambo matatu. Kwanza hali ya ushirika nchini na *COASCO.* Hadi sasa, ushirika wa kuweka na kukopa umeendelea vizuri na hizi ziko kwenye *level* ya chini ya kata takribani zote nchini. Tatizo kubwa katika ushirika lipo kwenye ushirika wa uzalishaji unaotokana na kilimo, tatizo hili halitakwisha kama Serikali haitakuwa tayari kufanya marekebisho makubwa na kwa haraka sana katika mtizamo wa kuondokana na nadharia na kuzungumzia ushirika wa vitendo. Eneo lingine ambalo linachangia kuzorotesha ushirika wa vyama mbalimbali vya ushirika hapa nchini ni pamoja na *COASCO* kushindwa kufanya majukumu sawa sawa. *COASCO* imechoka katika kila hali, watumishi, tangu Juni, 2006 *COASCO* haina bodi, uongozi uliopo kugeuza *COASCO* ni shirika lao binafsi.

Mheshimiwa Spika, namuomba Mheshimiwa Waziri anieleze, kuhusu yafuatayo, katika Bajeti hii *COASCO* imetengewa shilingi ngapi? Ni hatua gani za dharura atakazozichukua kuleta mabadiliko katika *COASCO.*

Mheshimiwa Spika, kuhusu programu za kilimo zilizopo na tija yake. Programu hizi hazitumiki kwa malengo yake, programu zinatengenezwa vizuri tatizo ni utekelezaji, programu kama *DADPS, DASIP* na hata *ASPS,* tatizo ni utekelezaji kwa msingi wa nani anasimamia kilimo kikitekelezwa kwenye halmashauri kama ilivyo sasa ni tatizo kubwa, hakutakuwa na ufanisi, hii dhana ya *D by D* katika kilimo Serikali iangalie na ifikirie upya kuwa tunataka mapinduzi hasa. Mapinduzi yoyote hayana demokrasia. *ASPS* wataalamu wameelemishwa, wamerudi wamekaa tu, maafisa ugani moyo wa kazi umekufa, hawana chochote wanachokifanya anafahamu afisa kilimo wa Wilaya tu, sehemu muhimu katika programu hizo ni ile ya shamba darasa, semina na kadhalika ambazo zinawapa posho na si sehemu inayomhusisha mkulima na kilimo kwa maana ya tija.

Mheshimiwa Spika, bodi ya mazao mchanganyiko *(grains)* mwaka jana nilipokuwa nachangia katika Bajeti ya Wizara ya Kilimo, niliuliza kuhusu bodi hii, majibu yalikuwa kwamba Serikali ipo katika mchakato wa kuandaa bodi hiyo, je, bodi hiyo mchakato wake umefikia wapi?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DR. FESTUS B. LIMBU:** Mheshimiwa Spika, napongeza kwa hotuba nzuri iliyosheheni mwelekeo mzuri wa kuhakikisha maendeleo ya kilimo, ushirika na chakula.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Kuhusu pembejeo namba moja ni maji, pembejeo namba mbili ni maji, pembejeo namba tatu ni maji. Wakulima wa mazao mbalimbali ya chakula na biashara wapewe mikopo ya kuchimba visima virefu (bore holes) kwenye mashamba. Hili litatupa uhakika wa kuvuna. Maji yaliyo chini ya ardhi Mwenyezi Mungu anatushangaa kwa nini hatuyatumii kwa kilimo? India wamefanikiwa sana.

*Power Tillers* ni mkombozi wa mkulima mdogo (maskini) mwenye ardhi. *Tillers* hizi zinalima, zina *hallow*, zina tela la tani moja na uwezekano wa kuzalisha umeme. Makadirio yanaonyesha mkopo wa shilingi milioni sita unaweza kurudishwa ndani ya mwaka mmoja. Sambamba na plau la ng’ombe ingefanywa mikakati kwa mfano kuzitaka halmashauri za wilaya zote hasa za pamba ziagize walau *power tiller* moja kila kata kwa kuwakoposha *selected/trusted individuals* ili kuhamasisha wananchi wengi kuzikopa/kuzinunua. Wananchi/wakulima hujifunza kwa kuona (Mpaga Bona). Mkulima atalima atasomba mazao/mavuno toka mashambani na pia kusomba mbolea ya samadi na kadhalika kupeleka mashambani. *CRDB* wameanza mazungumzo/mikakati ya kumwaga *power tillers* kwenye maeneo ya pamba. Serikali ilifuatilie hili kwa uharaka na umakini.

Mheshimiwa Spika, *DADPs*, *DASIP*, bado haijaleta *impact* kabisa vijijini ikilinganishwa kwa mfano na *TASAF*. Pesa nyingi zilizokwisha tumika hadi sasa sana sana zimetumika kwenye *software* ya kujenga uwezo, mradi huu ufanyiwe tathmini ya haraka ili uweze kuleta manufaa yanayotarajiwa shilingi bilioni 5.5 za *DASIP* 2007/2008 hazitoshi kabisa.

Kuhusu usindikaji wa mazao nchini hasa ya chakula umejikita kwenye mambo madogo madogo *subsistence.* Tunatakiwa tusindike mazao kibiashara ili yajaze *supermarkets* zetu kuliko ilivyo hivi sasa vingi (80%) ni *imported.* Uchumi wa Zimbabwe umedidimia kwa sababu ya kuporomoka kwa uzalishaji na usindikaji wa mazao ya kilimo (hasa ya chakula). Usinidikaji wa mazao ya chakula ndani ya nchi utawahakikishia wakulima soko la uhakika. Kiwanda cha Mvinyo hapa Dodoma kimetoa soko la uhakika kwa wakulima wa zabibu hapa Dodoma mfano huu uigwe haraka kwenye mazao na maeneo mengine. Hivi sasa uzalishaji ukiwa mkubwa tu, bei zinaporomoka na mkulima anakula hasara na kukata tamaa.

Mheshimiwa Spika, *exchange rate* inavyokwenda hivi sasa inampunguzia mkulima wa pamba pato lake. Mwezi Juni mwanzoni *rate* ilikuwa shilingi 1,185/= kwa dola moja. Hivi sasa ni shilingi 1,160/= kwa dola moja na bado inaendelea kushuka. Nini kifanyike? *BOT* wa-*intervene* kwenye *open market operations* kumnusuru mkulima. Bei ya pamba kwenye soko la dunia imeendelea kupanda lakini *exchange rate* inaleta vurugu tena.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *large scale commercial farming.* Bado haijatiliwa mkazo hasa kwenye maeneo yenye ardhi kubwa. Tuepuke ya Zimbabwe kwa kumilikisha ardhi kwa wazungu peke yao. Wazungu wakija, waingie ubia na Watanzania/wazalendo.

Pili *graduates (B.Sc, M.Sc* na *PhDs)* wa kilimo wawezeshwe kuingia katika kilimo kikubwa cha kibiashara. Wapewe mikopo, watengewe maeneo yaliyoainishwa na wawe *exposed* kwenye *entrepreneurial skills/seminars/visits* na kadhalika. Hivi sasa wengi wako *jobless* au wanafanya shughuli zingine zisizohusiana na kilimo.

Tuna *success stories* kadhaa kwenye sekta ya kilimo na ushirika ambazo zinaweza kuenezwa maeneo mengine. Hizi ziainishwe na zitumike kwa manufaa ya maendeleo ya kilimo. Tuna *appropriate technologies* nyingi kwenye kilimo ambazo ziko bado kwenye makabati ya vyuo vya utafiti. Kuna mbegu nyingi zilizopasishwa za mazao mbalimbali lakini hazijamfikia mkulima. Juhudi za makusudi zifanywe kuzipeleka teknolojia hizi kwa wakulima.

Mheshimiwa Spika, nampongeza tena Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, wakurugenzi na kadhalika kwa hotuba nzuri. Nawatakia kila la kheri na naunga mkono hoja.

**MHE. AMEIR ALI AMEIR:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uzima na kuchangia hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri na timu yao kwa kutuletea hotuba yenye dira ya Taifa ya mwaka 2025 ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya 2005.

Mheshimiwa Spika, hali ya chakula nchini imeelezwa si nzuri kwa baadhi ya mikoa, hali iliyosababishwa na mvua za vuli kunyesha kwa kiwango cha chini. Upatikanaji wa mvua ni majaliwa ya Mwenyezi Mungu kwa hiyo Wizara ijiandae kwa kila hali nchi isikumbwe na balaa la njaa.

Mheshimiwa Spika, nashauri Wizara itoe kipaumbele ile mikoa iliyofaya vizuri kuzalisha chakula kwa kuipatia pembejeo za kilimo mapema ili iweze kuandaa mapema na ili lengo la Serikali liweze kufikiwa la uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, mfuko wa pembejeo, kuna malalamiko mengi kuhusu upatikanaji wa mikopo ya pembejeo kwa wakulima na zana za kilimo kwa kuwa wakulima wengi hauwafikii. Kwa hivyo, Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali izidi

kuuimarisha mfuko huu kwa kutenga fedha nyingi ili uweze kupanua uwezo wa kuwafikia wakulima wengi zaidi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ardhi ya Tanzania na kutokana na mashamba makubwa tuliyonayo na kuwapatia wakulima zana na pembejeo za kilimo mapema na kwa wakati Tanzania hakuna njaa na ziada tutauza nje.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. FUYA G. KIMBITA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Hai nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wengine wote hapo Wizarani kwa kutuletea hoja inayoleta matumaini, hongereni sana.

Pili, nishukuru kwa mradi wa *PADEP* kule Wilayani Hai na niombe kuendeleza miradi hii ya *PADEP* katika vijiji ambavyo havikupata kwa sababu miradi hii ya *PADEP* imeonyesha mafanikio makubwa sana hivyo ninaomba muendelezo wake.

Naomba nitoe mchango wangu wa ujumla katika maeneo machache yafuatayo, kwanza, hali ya chakula duniani. Kama inavyofahamika ni jukumu letu sisi tuliojaliwa ardhi nzuri inayofaa kwa kilimo kuitumia vizuri na kwa uangalifu mkubwa nikiwa na maana ya yale maeneo yanayofaa kwa kilimo cha mazao ya chakula tusiyatoe kwa ajili ya kilimo cha mazao ya nishati kama ambavyo katika baadhi ya maeneo mazuri tayari yanatumika visivyo.

Kuhusu benki ya kilimo, nashauri uanzishwaji wa benki itakayowasaidia wakulima wetu katika kilimo cha mazao na ufugaji ili kuwapunguzia adha kubwa wanayopata na lini itawapa moyo zaidi wasomi wetu waliosomea kilimo waweze kuendeleza fani zao na wasikimbie kilimo cha mazao na ufugaji, naunga mkono kusudio la Mheshimiwa Rais la kupeleka pesa kiasi katika benki ya *TIB* ili kuanza kuwasaidia wakulima wetu lakini napendekeza iwepo benki rasmi ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, bodi ya mazao mchanganyiko, napendekeza uanzishwaji wa bodi ya mazao mchanganyiko kwa maana ya uendelevu wa haya mazao natumaini utaalamu na manufaa yake mnayafahamu vizuri hapa Wizarani.

Kuhusu mbolea ya ruzuku na mbegu bora, upungufu mkubwa wa mbolea na mbegu umeonekana katika msimu huu unaoisha pamoja na usimamizi ambao haukuwa mzuri au hafifu, kutokufika kwa wakati pamoja na mambo ya bei kama ambavyo Mheshimiwa Waziri alivyokiri katika hotuba yake. Lakini bado hakusema ni nini kifanyike au ni mikakati gani ilivyowekwa au kutayarishwa ili yasitokee matatizo tena, ninaomba majibu.

Kuhusu masoko, ni muhimu kuwa na mkakati ulio imara wa masoko ya mazao ya wakulima wetu, ikiwa ni kujenga masoko mapya pamoja na kuwaruhusu wakulima wetu kuuza ziada ya mazao yao nje ya nchi kwa maana ya kupata bei nzuri zaidi. Lakini kwa maana ya kuongeza thamani ya mazao yetu na kupata bei nzuri zaidi ni muhimu sana kuwa na viwanda kwa mfano *agro processing,* usindikaji wa mazao yetu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ushirika, ushirika ni muhimu sana katika maendeleo ya kilimo hapa nchini hivyo tuna kila sababu ya kuufufua ushirika pale ulipokufa na kuanzisha pale ambapo haupo.

Naomba niishauri Wizara iingilie kati mgogoro uliopo kati ya *KNCU* na Chama cha Msingi cha Lyamungo kuhusu umiliki wa shamba la Uremi ili kile chama cha msingi cha Lyamungo waweze kurudishiwa shamba lao, vinginevyo huu mgogoro unaweza kuvuruga ushirika hapa nchini na hivyo kuwakatisha tamaa wananchi wa maeneo mengine kuwa ushirika siyo kitu kizuri. Naomba sana jibu ya hili suala tupate ufumbuzi wa haraka kwa sababu lile shamba hivi sasa ni hasara tupu kwani hakuna uzalishaji wowote unaoendelea na kubaya zaidi ni uhasama kati ya uongozi wa *KNCU* na wananchi wa Lyamungo.

Kuhusu huduma ya ugani, umuhimu wa huduma za ugani ni muhimu sana, lakini lazima tuwape vitendea kazi hawa wataalamu wetu wa ugani ili waweze kutenda yale tunayoyatarajia. Suala la utafiti, kuna kila sababu ya kupanua utafiti wetu na kuviwezesha vyuo vyetu vya utafiti kwa maana ya kuwapatia vifaa vinavyohitajika pamoja na pesa za kutosheleza kwani utafiti ni dhahiri unahitaji pesa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na kuwatakieni kila la kheri.

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Mheshimiwa Spika, napenda kuwa mmoja wa wachangiaji katika Wizara hii muhimu katika maendeleo ya Taifa letu na vile vile ningependa kumpongeza Mheshimiwa Waziri mhusika na jopo lake katika hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hotuba nzuri na mipango mizuri na nia njema kabisa ya Wizara hii mimi naamini haitatekelezeka kama kila vitu vingi vitategemea Halmashauri za Wilaya.

Mheshimiwa Spika, pamoja na sisi Wabunge tumekuwa ni Madiwani katika halmashauri zetu lakini kutokana na shughuli nyingi za Ubunge mara nyingi Wabunge wamekuwa hawahudhurii vikao vya halmashauri kwa ajili ya kazi zingine za Kitaifa au kutopewa taarifa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na sababu hizo na zinginezo saa nyingine husababisha ushiriki wa Mbunge kuwa wa mara chache na kukuta mambo mengi ya maendeleo yamepita kwa kupitishwa na Madiwani waliopo au kupitishwa bila ushiriki wa Madiwani.

Mheshimiwa Spika, nasema hivi kwa ushahidi wa vitu viwili ambavyo vimejitokeza katika Wilaya yangu kwa mfano, kwanza maafisa ugani wapo katika baadhi

ya vijiji, pamoja na kuwa hawatoshi lakini waliopo hawana kazi ya maana wanayoonyesha kwa wananchi na hasa utaalamu wao wa kilimo.

Mheshimiwa Spika, utakuta kwa ushahidi wa kutosha afisa ugani hajulikani na wakulima katika kijiji husika kwa asilimia tisini ya wakulima waliopo na mfano katika jimbo langu la Gairo, huwezi ukaona mabadiliko yoyote katika kilimo kuwa cha kitaalamu siku zote na ukiuliza wakulima watakuambia hawana mtaalamu wakati yupo lakini hajulikani.

Mheshimiwa Spika, hili ni tatizo kubwa linalosababisha kilimo kutokubadilika miaka nenda na utashangaa ripoti wanavyoiandika kwa ustadi kuipeleka wilayani. Cha kushangaza afisa kilimo Wilaya hana habari na hastuki, mradi ripoti zipo ambazo nyingi si sahihi yeye hujirizisha kwa kuona Wilaya yake inafanya vizuri.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni kuhusu pikipiki zilizoletwa katika Wilaya ya Kilosa ambazo ni 40 na katika Wilaya ya Kilosa kuna kata 37 cha ajabu ugawaji huu umezingita urafiki kuliko malengo ya maendeleo ya kilimo angalau kila kata zingepewa pikipiki moja tu zote 37 zingeenea lakini kata zingine hazikuweza kupata kabisa pikipiki hata moja na nyingine zipo zinazunguka tu makao makuu ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo tu inaonyesha umuhimu wa Wizara yenyewe ishughulike na mipango yote ya kilimo kuliko kutegemea halmashauri ambazo nyingi haziko makini katika kukuza kilimo chetu na naamini hizi halmashauri ndio zinazoharibu utaratibu wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kuhusu mfuko wa pembejeo ambao kwa maelezo ya hotuba umetengewa shilingi bilioni 3 tu na inategemea kukusanya shilingi bilioni 4.7 na jumla ni shilingi bilioni 7.7 ambazo zinaweza kununua matrekta madogo 107 na makubwa 124 ukiagalia matrekta makubwa ambayo ni tegemezi hata kila Wilaya ukigawa moja tu hayatoshi. Sasa ni kweli tuna nia ya kweli ya kutoka katika kilimo cha jembe la mkono kwenda kutumia trekta wakati kuna Wilaya zina zaidi ya kata 37 vijiji 200 lini tutafika kutumia kila kijiji matrekta matano? Hii ni ndogo.

Mheshimiwa Spika, naomba mfuko huu uongezwe pesa ya kutosha na nataka majibu. Naiomba Serikali sasa iangalie kwa makini ili iongeze fedha katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, la mwisho naomba sasa ndani ya msimu huu wa ununuzi wa mahindi ya hifadhi tuangalie bei mtakayotoa kwa wakulima ya ununuzi wa mahindi. Sio ya miaka miwili iliyopita ya shilingi 190/= kila mwaka wakati likitokea tatizo la njaa wakulima huuziwa shilingi 300/= kwa kilo hili liangaliwe.

Mheshimiwa Spika, mwisho naunga mkono hoja.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA**: Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na wataalamu wake wa Wizara hii kwa kuandaa hotuba hii na kuleta hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi zinazofanywa na Wizara hii kuboresha kilimo hapa Tanzania bado Serikali haijaweka nia ya kweli ya kuleta mapinduzi ya kweli ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, hili linajionyesha wazi kwa kuona jinsi kilimo kinavyokuwa taratibu na wakati mwingine kwa kiasi kikubwa kimekuwa kikishuka. Katika karne hii tuliyonayo na ndani ya miaka 45 ya Uhuru kilimo hukua kwa 4.5% kwa mwaka 2007 inaonyesha wazi sekta hii inadumaa.

Mheshimiwa Spika, tuna maanisha nini tunavyosema kilimo ni uti wa mgongo wa Mtanzania? Kwa kushindwa kuwekeza vya kutosha kwenye kilimo tumeshuhudia madhara yake. Miaka ya nyuma nchi yetu haikuwa inakumbwa na njaa na wakulima waliweza kuendelea sana na kuweza kusomesha watoto wao bila wasiwasi kwa kilimo. Hili liliwezekana kutokana na umuhimu ambao uliwekwa kwenye kilimo.

Mheshimiwa Spika, tunahitaji kuweka kipaumbele na kutenga fedha za kutosha kwenye kilimo. Tunatakiwa kuweka kipaumbele kwenye mazao ambayo kwa hakika yatawanyanyua wananchi walio wengi. Mazao haya yakishaainishwa Serikali iweke nguvu zote, utaalumu wote, ugani wote, yalimwe kwa wingi na ubora unaotakiwa. Tutafute masoko ya uhakika ndani na nje ya nchi ili wakulima wapate bei nzuri ya mazao yao.

Mheshimiwa Spika, nchi ya Vietnam wanazalisha sana mchele, kahawa na korosho. Cha kushangaza mbegu ya kwanza ya kahawa na korosho waliipata hapa Tanzania. Kwa kuwa waliweka malengo na mikakati madhubuti leo Vietnam ni *first producer* wa korosho duniani na ni *second producer* wa kahawa duniani.

Mheshimiwa Spika, wataalamu wa ugani, tatizo kubwa tulionalo ni ukosefu wa maafisa ugani wa kutosha kusaidia wakulima walime kitaalamu zaidi, kwenye hotuba watumishi walioajiriwa ni 330 mwaka 2008. Hakuna mahali ambapo tumeambiwa maafisa ugani wangapi wameajiriwa kwa mwaka mzima wa 2007/2008.

Mheshimiwa Spika, msimu wa matunda kama sasa mengi yanaoza masokoni na mashambani. Msimu ukiisha hatuna *juice* zilizohifadhiwa na tunakwenda kununua *juice artificial* tena kwa bei ghali sana kutoka nchi za nje kwenye *supermarkets* zetu.

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu kujitoa kuwekeza kwenye viwanda vya kusindika vyakula pamoja na kununua pembejeo kama matrekta na kujiacha kwa wawekezaji hili sikubaliani nalo kabisa. Wawekezaji hatuwezi kuwalazimisha kuwekeza eneo ambalo hawajapanga. Eneo muhimu kama hili ambalo linamkomboa mwananchi moja kwa moja ni vizuri Serikali ikaweka mkono wake asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, kuhusu wakulima wa tumbaku mkoa wa Tabora. Tumbaku ni zao la biashara ambalo linaliingizia Taifa hili fedha nyingi sana. Hata kwenye hotuba ya Wizara wa fedha kwa mwaka 2008/2009 ushuru wa bidhaa za tumbaku zimeongezeka sana. Pamoja na Taifa kunufaika wakulima wa zao hilo wameendelea kubaki maskini. Makampuni yanayonunua tumbaku Tabora wamekuwa wanajinufaisha bila kumjali mkulima.

Kwanza wakulima wanapewa mkopo wa mbolea kwa bei ghali sana na bei inapanda kuendana na kupanda kwa dola. Wakati wa kununua tumbaku hii makampuni wanapanga bei wao, madaraja yanapangwa manne. Bei haiangalii kupanda kwa dola wala kupanda kwa mbolea. Gunia wananunua/wanalipia na kampuni inakata kilo moja kwenye tumbaku eti ni uzito wa gunia. Mwaka unaofuata lile gunia wanalipia tena. Kampuni ya Pimori imekuwa inafikisha tumbaku kiwandani na tena wanarudisha kwa wakulima. Mipango iliyoelezwa ni Wizara kushirikiana na TAMISEMI kutoa mafunzo kwa vijana na kutoa ajira kwa wahitimu hao, lengo ni kuajiri watumishi 2500 kwa mwaka. Hivi sasa kuna wataalamu wengi wenye fani za kilimo ambao wanafanya kazi tofauti na fani zao.

Kwa nini Wizara isiwe na mpango mahususi wa kuwavutia hawa ili waje wafanye kazi waliyosomea kama mpango wa haraka wa kupunguza upungufu wa wataalamu na huo mpango wa kuwasomesha ukiwa mpango wa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri alieleze Bunge hili ni kwa jinsi gani Wizara ya Kilimo inashirikiana na sekta ya utalii hapa nchini kwa ajili ya kupata masoko mazuri ya mazao ya wakulima wetu?

Mheshimiwa Spika, ni kwa nini hoteli za kitalii wananunua nafaka, mboga mboga na hata matunda kutoka nje ya nchi? Ni kwa nini ukienda kwenye *supermarkets* zetu karibu zote zimejaa vyakula kutoka nje? Kuna tatizo gani? Hii inamaanisha vyakula vinavyozalishwa hapa nchini havina ubora? Kama havina ubora Wizara inafanya nini kusaidia tatizo hili au Serikali inaona ni vizuri kuwepo na hali kama hii?

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Spika, naunga hoja mkono mia kwa mia. Awali ya yote naomba kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara, kwa hotuba nzuri inayoeleweka, iliyoletwa mbele yetu kuijadili. Aidha, nampongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Chakula na Ushirika.

Mheshimiwa Spika, leo nitazungumzia maeneo mawili tu, ambayo naona yana matatizo makubwa yanayohitaji msaada wa dharura ambayo ni ushirika na mafao ya wafanyabiashara.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ushirika pamoja na juhudi za Serikali kuhamasisha ushirika nchini, ushirika umekuwa ukididimia siku hadi siku ukilinganisha na hali ilivyokuwa miaka ya 1970.

Mheshimiwa Spika, idara za ushirika/ofisi zilizo mikoani na Wilayani zinatisha. Maafisa wenyewe hawana hamu kabisa ya kuhamiasisha wananchi kwenye elimu ya ushirika. Mbaya zaidi hawawatembelei wananchi kwenye maeneo yao kwani wanadai hawana vitendea kazi, yakiwepo magari, pikipiki hata *stationeries.*

Mheshimiwa Spika, naomba utakapokuwa unajumuisha, unieleze ni jinsi gani eneo hili litasaidika.

Mheshimiwa Spika, wananchi wamehamasika sana kujiunga kwenye *SACCOS.* Tatizo tunalopata kwa maafisa ushirika ni *speed* ya kuandkisha *SACCOS* hizo kutokana na baadhi ya maafisa ushirika kudai kuwa zina harufu ya siasa kisa ni kwa vile tu baadhi ya wanachama hao kuwa wanachama au viongozi kwenye vyama vya siasa. Hapa nina mfano hai, japo nisingependa kuutumia.

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri anieleweshe endapo ni sheria ya ushirika kuwa ukiwa kwenye siasa, huruhusiwi kuwa mwanachama wa *SACCOS.*

Mheshimiwa Spika, vipimo vya mazao yetu. Hapa naipongeza Wizara kwa kupiga vita rumbesa na kudhibiti hali ya kudanganya wakulima.

Mheshimiwa Spika, hapa kilio changu ni kipimo cha mazao kama ndizi, zao hili limekuwa mateso kwa wakulima wote Tanzania ifikie mahali sasa zao hili lianze kupimwa kwa kilo. Naomba Waziri atakapojumuisha anipe mwanga kwenye hilo.

Mheshimiwa Spika, malipo kwa wastaafu *TCB,* Moshi. Mimi binafsi nilishazungumza na Mheshimiwa Waziri jambo hili mara tatu kuanzia mwaka 2007, wakati wa Bajeti na kumuomba aingilie kati watu hao walipwe. Kati yao hao, 12 kuna wanawake wajane wanne nao wananigusa sana nikiwaona kama Mbunge wao. Je, ni lini wastaafu hao watalipwa haki zao wapate amani? Naomba jibu wakati wa majumuisho.

**MHE. EUSTACE O. KATAGIRA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri na maofisa wote wanaomsaidia kwa Bajeti iliyoandaliwa na kuwasilishwa vizuri. Pia uendeshaji wa shughuli za Wizara.

Mheshimiwa Spika, jembe la mkono, kama inavyohimizwa kila mara, jitihada ifanywe ili wananchi wapunguze kilimo cha jembe la mkono, twende kwenye kilimo chenye kutumia nyenzo bora zaidi.

Kuhusu maafisa ugani, tunaona na kushukuru jitihada za Wizara, kwa muda mrefu itakuwa ni kazi ngumu kuwa na afisa ugani kila kijiji. Nashauri baadhi ya watendaji wa vijiji wenye mwelekeo wapewe mafunzo ili waweze pia kutoa utumishi wa ugani kwa ngazi za kijiji. Kama tuna maafisa ugani wasomi kwenye ngazi za juu, Wilaya na tarafa basi watawaongoza hawa wa vijijini.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Spika, kilimo mabondeni, nchi yetu imebahatika kuwa na mabonde mazuri sana yanayofaa kwa kilimo, mfano Bonde la Mto Rufiji, bonde la mto Malagarasi na mengineyo. Napenda kuishauri Serikali ione umuhimu wa kuwekeza katika mabonde hayo na Wizara iweke mikakati mahsusi ya kufanikisha kilimo kwenye mabonde ya mito ambapo umwagiliaji hautahitajika kwani kuna unyevu wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, kilimo cha umwagiliaji, nchi yetu haina tatizo la maji, tunayo maziwa, mito na vyanzo vingi tu. Vile vile tunayo ardhi ya kutosha kwa kilimo hicho cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kumkumbusha Mheshimiwa Waziri kuwa Bajeti ya mwaka 2006/2007 alitoa ahadi Bungeni ya kuendeleza hekta milioni moja kwa kipindi cha miaka mitano (2006 – 2010). Lakini mpaka sasa eneo la umwagiliaji ni hekta 275,388 tu ambapo ni kiasi cha 27.5% ya lengo hilo na imebaki miaka miwili tu kufikia mwaka 2010. Je, Waziri anasemaje juu ya hilo?

Mikoa kama ya Mbeya na Morogoro ni *potential* sana ina vyanzo vingi vya maji ikiwemo mito. Lakini bado Serikali haijafanya *homework* yake vya kutosha na pamoja na vyanzo vingi vya maji na ardhi nzuri na wanajitahidi sana kwa shughuli za kilimo, kwa nini Wizara isiharakishe kuanzisha kilimo cha umwagiliaji katika mikoa hiyo? Na ishangaza katika mikoa iliyokumbwa na njaa na mikoa hiyo iliathirika na janga hilo.

Mheshimiwa Spika, Serikali itueleze itawezaje kuleta mapinduzi ya kijani ikiwa kilimo cha umwagiliaji hakipewi nafasi inayostahili?

Mheshimiwa Spika, kilimo vijijini bado ni duni na hakimsaidii mkulima, kinamdhalililsha, kinamdhoofisha na kinamnyonya kwani anafanyakazi kubwa lakini tija kidogo sana. Umaskini unaendelea kukithiri maisha yake yanakuwa ya taabu siku hadi siku. Serikali ichukue hatua, jembe la mkono halitamwinua mkulima na inasikitisha mikopo ya JK inaishia kwa wajasiriamali wajanja, mkulima ataendelea kibaki nyuma mpaka lini? Kutokana na matatizo hayo wimbi la vijana (machinga) litaendelea kutorokea mjini na mapambano kati ya mgambo na machinga hao yataendelea kwani kijana hawawezi kukaa vijijini kwenye kilimo cha jembe la mkono ambacho hakijamnufaisha babu yake, wazazi wake na yeye hakitamnufaisha kwani maisha yake yanaenelea kuwa duni.

Mheshimiwa Spika, Serikali iangalie uwezekano wa kuanzisha mikopo ya riba nafuu kwa wakulima na benki ya wakulima ianzishwe haraka kwani ni muda mrefu wakulima wameishi bila ya benki ambapo ni chombo muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, Wizara ishirikiane na Wizara ya Viwanda na Biashara kuangalia uwezekano wa kuanzisha viwanda vidogo vidogo kwenye eneo la kilimo mfano kiwanda cha kusindika korosho Mtwara matunda, Tanga na kadhalika ili kilimo kiwe na tija kwa mkulima.

Mheshimiwa Spika, natarajia majibu kutoka kwa Waziri yaliyojitosheleza.

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Spika, napongeza Wizara kwa mikakati mizuri ya kuboresha mageuzi katika kilimo hasa katika suala zima la kuanzisha utaratibu wa stakabadhi ya mazao ambao utamwezesha mkulima kuweza kuuza mazao yake wakati bei inapokuwa nzuri na pia kumuwezesha kukopa katika vyombo mbalimbali vya fedha. Hii ni hatua kubwa ya kuipongeza Serikali, utaratibu huu utakuwa wa mafanikio makubwa kama utaendana na upatikanaji wa pembejeo za kilimo kwa wakati na ushauri wa wataalamu ili kuweza kuongeza uzalishaji (mavuno) kwa eka.

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa mbolea ya *DAP* kwa ruzuku pia ni muhimu hasa kwa Wilaya ya Njombe ambako wanazalisha viazi kwa wingi na kuuza nje ya mkoa na nchi. Ni vizuri mbolea hii pia ikaingizwa kwenye utaratibu wa vocha.

Mheshimiwa Spika, kwa vile hii Wizara inashughulikia masuala ya chakula, sijaona mkakati mahususi ulioandaliwa kuhusu utayarishaji wa vyakula, elimu kwa wananchi kuhusu upatikanaji na ulaji. Watanzania wengi wanakabiliwa na lishe duni. Kitengo cha lishe Wizarani hakipewi umuhimu unaostahili. Sasa ni wakati muafaka kwa Wizara kutoa elimu ya lishe kwa jamii. Hii ni nini kilichotokea na kusababisha Wizara kuacha kutilia umuhimu elimu ya lishe kwa jamii ikiwa pamoja na upangaji wa milo, lishe kwa watoto na akinamama wajawazito? Wizara ifufue vitengo hivi. Wananchi wahimizwe kulima kutumia vyakula vya asili.

Mheshimiwa Spika, vyuo vya kilimo Uyole na Ukiriguru vitoe pia shahada pamoja na kutoa astashahada, stashahada na kozi fupi maalum kutegemea na mahitaji. Suala la jinsia lipewe umuhimu unaostahili badala ya kujumulisha tu wakulima wangapi wanawake?

Mheshimiwa Spika, mafunzo kwa wataalamu wa kilimo ujuzi wa cheti. Ili kupata vijana wengi wa kidato cha nne kujiunga, matangazo yatolewe katika ofisi za kilimo Wilaya, Ofisi za Wakuu wa Wilaya/*DED* ili kupata uwiano na kuweza kupata wataalamu watakaokuwa tayari kurudi katika maeneo yao wamalizapo mafunzo. Wakati huo programu ya kutoa mafunzo kwa zao fulani mfano mahindi kama ndiyo mahitaji ya eneo husika mfano mahindi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Nampongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na viongozi wote Wizarani.

Mheshimiwa Spika, naomba kwanza kuzungumzia pembejeo. Naishukuru Serikali kwa kuongeza ruzuku katika pembejeo hasa mbolea. Msimu wa kilimo unakaribia, muundo mpya wa stakabadhi bado haujafikishwa kwa walengwa na huko Wilayani hatuna mabwana shamba wa kutosha, nashauri tuanzeni sasa. Lakini kwa kuwa Wabunge na Madiwani ndio wanaoishi na wananchi, tafuteni namna makundi haya yaelimishwe ili yasaidie kuelimisha na kutoa hamasa maeneo husika.

Kuhusu kilimo cha miwa, Halmashauri yangu kupitia Mbunge na wananchi tumeanzisha kilimo cha miwa ya sukari. Hali inaenda vizuri lakini fedha pekee tunayotegemea ni fedha ya *DADPS* toka Halmashauri ya Wilaya mara nyingi ninapouliza maswali Bungeni nimeambiwa kuna fungu maalum la kufundisha wakulima Wizarani lakini miaka inapita - naomba yafuatayo, kwanza kwa kuwa kilimo hiki kinahitaji upanukaji wa haraka na uwepo wa mashamba makubwa, naomba Wizara ione namna ya kusaidia hilo.

Pili, kwa kuwa fedha ya maendeleo ya kilimo ni ndogo Wilayani tunaomba Wizara itusaidie eneo la mafunzo na mashine ndogo ndogo za usindikaji. Kuhusu ushirika wa *SACCOS*, ushirika ni ukombozi. Ni kweli kupitia ushirika maendeleo yapo. Naomba kushauri yafuatayo, *SACCOS* zimeanzishwa *resources* za Halmashauri ni kidogo hivyo hakuna uwezo wa kutosha wa kujengea uwezo wa kiuendeshaji. Pia hatuna maafisa ushirika wa kutosha, zamani tulikuwa na maafisa ushirika mpaka vijijini sasa miundo ya madaraka inabadilika inatupa shida. Vijana watakaosomeshwa kilimo wafundishwe na *ABCDs* za ushirika watusaidie vijijini.

Kuhusu *SGR*, katika Jimbo la Peramiho linaongoza kwa uzalishaji wa mahindi Mkoa wa Ruvuma na kwa kuwa hiyo ndio hali halisi naomba sana Serikali ituongezee vituo vya ununuzi maeneo yafuatayo, Mpitimbi eneo la kuelekea mpakani mwa Tanzania na Msumbiji kwa kuwa mpaka sasa unafunguliwa itasaidia kudhibiti uuzwaji wa chakula nje ya nchi. Pia Magagura, kwa kuwa eneo hili linaunganisha wakulima wa Wilaya ya Mbinga na Songea linafaa kutumiwa kama *centre* ya kununulia mahindi.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni eneo la Madaba kwa kuwa eneo hili Kaskazini limekuwa mbali na maeneo yote ya Jimbo na wafanyabiashara wamekuwa wakinunua hapo kwa kuwanyonga wakulima na kuuza wao *SGR*, ni bora wakulima hao wasaidiwe.

Kuhusu ubora wa mbolea, mara nyingi mbolea inayoletwa na wafanyabiashara haina ubora mwaka jana Jimbo la Peramiho na mkoa tulipata tatizo hilo, Wizara inasemaje na imechukua hatua gani kudhibiti hilo? Wakulima wa Ruvuma wanapenda kujua hatma ya hasara waliyopata.

Mheshimiwa Spika, suala la mazao mchanganyiko, mazao mchanganyiko yamekuwa na tija kwa wakulima tatizo kubwa hayana *coordinating point,* tunaomba bodi ya mazao mchanganyiko ianzishwe haraka.

**MHE. DR. SAMSON F. MPANDA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naunga mkono hoja mia kwa mia.

Mheshimiwa Waziri, je, ni taasisi gani inayosimamia kurasimu mazao mchanganyiko kama vile ufuta, matunda, maua na vyakula vya nafaka, na wakati bodi ya mazao hayo haijaundwa?

Ni lini Mheshimiwa Waziri au Naibu Waziri atazuru katika Jimbo la Kilwa Kaskazini ili aweze kujionea mwenyewe jinsi machungwa, malimao, ndimu yanavyooza ovyo jimbo lote la Kilwa Kaskazini.

Mheshimiwa Spika, ni lini Kilwa itapata pembejeo ya ruzuku kwa mazao ya chakula na biashara?

**MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA:** Mheshimiwa Spika, nampa hongera Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri na yenye matumaini mema. Naomba nipate ufafanuzi wa maelezo yako kuhusu madeni ya wakulima katika ukurasa wa 62.

Mheshimiwa Spika, je, wakulima wa Jimbo wa Songwe wamo kama ulivyoahidi na kuuthibisha ujumbe uliokutana nao? Je, maendeleo ya utafiti juu ya kuwepo kwa funza mwekundu aliyesababisha kusitisha kilimo cha pamba jimboni Songwe umefikia wapi?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MCH. DR. GERTRUDE P. RWAKATARE:** Mheshimiwa Spika, ninaungana na wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Waziri na wasaidizi wake kwa hotuba nzuri sana inayokidhi malengo na mahitaji ya Watanzania. Naomba nichangie kama ifuatavyo.

Kwanza tatizo kubwa la wakulima wa mpunga Kilombero ni walanguzi. Wakati wa kuvuna nafaka hizi zinanunuliwa na walanguzi na kuuza tena kwa bei nne ya waliyonunulia. Je, hakuna uwezekano wa kuunda Bodi ya Nafaka ili wananchi waweze kunufaika na jasho lao badala ya kununua walicholima wenyewe mara nne ya bei ya mauzo.

Mheshimiwa Spika, je, Serikali haiwezi kusogeza ushirika kwa mazao ya nafaka pia? Wakulima wa miwa wa Kilombero wananyanyasika sana. wanauza kwa bei ya kutupwa na mara nyingi miwa inakatwa hawaji kuchukua mpaka inakauka na kukataliwa. Hivyo wanapoteza nguvu yao bure, wanahitaji Kiwanda kingine. Sukari imepanda bei je, miwa pia itapanda bei kwa manunuzi?

Mheshimiwa Spika, suala la soko, mazao kama ndizi, nyanya, vitunguu havina soko la kudumu. Kwa sasa wanategemea soko la kuweka barabarani kutegemea wasafiri. Serikali ituwezeshe kuweka viwanda vidogo vidogo vya kusindika mboga na matunda kama *juice* au *paste* au *BET* wasaidie kuwatafutia masoko ya matunda na mboga. Njia ya Dodoma kwenda Dar es Salaam imejaa mazao yasiyo na soko tuwasaidie.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja mia kwa mia.

**MHE. STEPHEN J. GALINOMA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Waziri na timu yao yote kwa hotuba nzuri iliyojaa matumaini kutokana na utekelezaji wa mwaka uliokwisha na malengo ya mwaka mpya. Kwa hiyo, naunga mkono hoja hii.

Hata hivyo nina mchango katika maeneo machache. Kwanza ni kuhusu ushirika: ni kweli kwamba ushirika umekufa au kuzorota ingawa dalili zinaonyesha maendeleo lakini bado tuko mbali sana tukifahamu kuwa idadi ya wakulima ni 70% – 80% ya watu wote. Iko haja ya kuzidisha jitihada zetu. Pia si vibaya kutazama upya sheria ya ushirika *vs SACCOS, para 23.*

Kuhusu chakula katika kifungu 15(ii) hotuba inasema kuwa Wizara imesitisha uuzaji nje ya mazao yetu ya chakula. Lakini katika siku mbili zilizopita imetangazwa kwamba tutawauzia Kenya tani ningi tu kwa lengo la kuiuzia *WFP*. Kama ni kweli hii ni kujipinga sisi wenyewe na ni vyema kuangalia upya sera yetu hiyo.

Mheshimiwa Spika, *green revolution,* nimevutiwa sana na kifugu 51 kinachozungumizia mageuzi ya kijani. Niulize tu kwamba kwa kuwa Wilaya chache sana zimehusishwa, Wilaya zingine kama Iringa zitafikiwa lini?

Suala la mbolea, pia nimepata matumaini juu ya mfumo mpya wa mbolea za ruzuku. Kubwa ni utekelezaji ili isiwe ahadi hewa. Labda niseme kwamba pamoja na matatizo tuliyopata kuhusu mbolea, ile aina ya *Urea* imethibitika kutokuwa na nguvu.

Mheshimiwa Spika, tukizingumizia suala zima la pembejeo, lazima tuguse *mechanization.* Siridhiki na kasi kama inavyoelezwa. Tunahitaji ubunifu zaidi wa kuhakikisha uingizaji wa matrekta na zana zaidi. Njia ya kuharakisha ni kuziwezesha Halmashauri kukopa kwa ajili ya watu wao. Kasi ya ukuaji wa 4% badala ya 10% itatupeleka hadi karne ijayo.

Mwisho nihitimishe kwa kuhoji wingi wa miradi au programu. Tuna *ASPD, ASPS, DADPS, DASIP, PADEP* na sijui nini. Kwa nini tusiondoe au kupunguza utatanishi uliopo? *Why not synchronise to one or two?* Inaongeza urasimu na pia gharama za kuweka au kushughulikia mradi mmoja mmoja hasa ikizingatiwa kwamba mtekelezaji ni yule yule *District Council.*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na kutakia Wizara kila la kheri ipitishwe na utekelezaji mwema. Wizara ina mipango gani ya kutumia maghala *(SILOS)*yaliyoko *ex- NMC* Iringa?

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi hii ya kuchangia hotuba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Waziri kwa hotuba Nzuri. Aidha, niwapongeze Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara kwa kazi yao nzuri.

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno haya ya utangulizi sasa naomba nichangie machache kuhusu Wizara hii. Kuhusu kilimo cha umwagiliaji maji katika Mkoa wa Dodoma.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Dodoma ni kati ya mikoa mikame sana nchini. Wakulima katika mkoa huu wamejitahidi kujitosheleza mahitaji ya chakula kwa kutumia mvua chache zinazoonyesha kila mwaka bila mafanikio kwa kutambua hili Serikali miaka 1980 ilibuni mikakati ya kuweza kumsaidia mkulima wa mkoa huu. Moja ya mikakati iliyobuniwa ilikuwa ni kuanzisha miradi ya umwagiliaji katika mabonde mbalimbali mkoani Dodoma.

Mheshimiwa Spika, mmoja wa mradi wa umwagiliaji uliobuniwa ni ule wa Bonde la Mto Bubu maarufu kama *Farkwa Multi purpose dam scheme*, madhumuni ya mradi huu ni pamoja na kuanzisha mradi wa umwagiliaji wa mashamba yenye ukubwa wa hekta 10,000 wenye uwezo wa kuzalisha tani 24,839 mazao mbalimbali kwa mwaka kama ifuatavyo mahindi tani 13,100, mpunga tani 9,450 na karanga tani 2,128.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mazao haya kuna uwezekano pia wa kuzalisha wengine yakiwemo alizeti, mtama na mbogamboga. Aidha, ufugaji wa samaki utakuwa ni moja ya faida. Mradi huu utaondoa tatizo kubwa la maji katika vijiji zaidi ya 30.

Mheshimiwa Spika, mradi huu haukuweza kutekelezwa wakati huo kwa sababu mbalimbali. Hata hivyo umuhimu wa kutekeleza mradi huu sasa ni bayana. Serikali lazima iwekeze ili kuwasaidia wakulima wa Mkoa wa Dodoma kwa sababu ndiyo njia pekee ya kuwaondolea umaskini wa kukithiri na njaa za mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, nafahamu kuwa mradi huu una gharama kubwa lakini unaweze kutekelezwa kwa awamu. Hatua ya kwanza ni kuchimba bwawa lenyewe; baada ya bwawa hatua zingine zinaweza kutuata.

Kuhusu uundwaji wa vyama vya ushirika mkoani Dodoma. Mkoa wa Dodoma ni kati ya mikoa ambayo haina Vyama vya Ushirika vya mazao. Kutokana na hali hii wakulima wa Mkoa huu ni kama watoto yatima. Hawana mahali pa kukimbilia pale wanapopata matatizo. Aidha, hawana chombo cha kuwasaidia pembejeo, utaalamu na hata kusimamia bei za mazao yao. Wakulima hawa wanalanguliwa bei na hivyo kudidimiza maendeleo yao.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara hii isaidie elimu ya ushirika ili wakulima waweze kuunda vyama vyao vya ushirika ya mazao. Kuhusu uundwaji wa bodi ya mazao mchanganyiko, naomba Wizara iharakishe uundaji wa bodi ya mazao mchanganyiko nchini.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuchangia haya machache naomba kuunga mkono hotuba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika.

**MHE. HAJI JUMA SEREWEJI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniruhusu kuchangia hoja ya Waziri wa Kilimo, Chakuna na Ushirika. Kabla sijaanza kuchangia hoja hii, naunga mkono asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, nchi ya Tanzania ina ardhi kubwa sana ambayo inayotumika kwa kilimo kwa ajili ya mazao mbalimbali na kwa bahati wananchi vijijini wanajitahidi sana kulima mazao mbalimbali. Lakini hadi leo wananchi wengi wanatumia jembe la mkono jambo ambalo limepitwa na wakati kwa kilimo cha kileo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mbolea ni vizuri mbolea iwafikie kwa wakati wakulima ili wawahi msimu wa kilimo.

Mheshimiwa Spika, tuna matunda mengi sana ambayo wakulima wetu wanazalisha wakati wa msimu wa matunda hayo kama vile mananasi, chenza, machungwa na kadhalika. Matunda hayo huwa yanaoza na kuharibika vibaya sana kwa kukosa soko kutokana na wingi wa matunda hayo jambo ambalo wakulima wanapata hasara na wengine kuvunjika moyo.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali ingefanya mpango wa kuweka viwanda vidogo vidogo kwa ajili ya kutengeneza *juice*.

Mheshimiwa Spika, hata maziwa ya ng'ombe baadhi ya mikoa hukosa soko na kumwagwa, haya yanatokea sehemu ya vijijini.

Mheshimiwa Spika, ili kilimo kuendelea vizuri wakulima wetu wapate mikopo ya mbolea na hata kwa fedha taslimu ili waweze kununulia vifaa vinavyohitajika kwenye kilimo.

Mheshimiwa Spika, baada ya haya, kwa niaba ya wanachi wangu wa Mwanakwerekwe nazidi kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naunga mkono hoja. Hata hivyo pamoja na kuunga mkono hoja nina mambo kadhaa ambayo ninaoma hayajakaa sawa na yakipewa umuhimu unaostahili basi tija katika kilimo itapatikana.

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 80 wa hotuba ya Waziri amezungumzia uzalishaji wa pamba. Ni kweli uzalishaji umeongezeka kutokana na wakuliwa kulima zao hilo kwa utaalamu. Hata hivyo pamoja na kuongeza uzalishaji bei ya pamba mwaka huu hailengi katika kumhamasisha mkulima wa pamba kuzalisha zaidi zao hilo mwakani.

Suluhu ya tatizo hili la bei kwa mujibu wa hotuba ya Waziri ni Serikali (Wizara) kuwahimiza wakulima kuuza pamba yao kwa utaratibu wa stakabadhi za mazao ghalani. Swali ni kwa nini Serikali haikuliona tatizo hili mapema hivyo kuanza kuwahimiza wakulima kuuza pamba yao kwa utaratibu huo? Nina ushahidi kwamba sio Wizara wala Bodi ya Pamba licha ya kutambua mwenendo wa bei ya pamba katika soko la dunia haikufanya jitihada zozote kuwasaidia wakulima.

Mheshimiwa Spika, vile vile katika maeneo mengi kuna kuzalishwa pamba, wakulima wamekata tamaa na wametishia kuacha kulima pamba msimu ujao. Serikali itabadilisha vipo mwelekeo huu?

Mheshimiwa Spika, katika ukuraza 62 wa hotuba ya Waziri amezungumzia madeni ya wakulima kwa kusema Serikali ilitenga shilingi milioni 2.5 katika Bajeti ya mwaka 2007/2008 na hatua za kuwalipa wakuilima zimeanza kuchukuliwa. Chama Kikuu cha Ushirika cha *KACU* kinadaiwa na wakulima wa Kahama, Bukombe na Uyuwi takriban shilingi 130,000,000/= tangu mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kila mwaka tangu mwaka 2006 Serikali kupitia Bunge hili imekuwa ikiwaahidi wakulima hawa kwamba itawalipa kwani uhakiki umekamilika lakini zimebaki kuwa ahadi ambazo haziaminiki. Napenda wakati Waziri anahitimisha hotuba yake aniambie kwa usahihi kabisa lini wakulima wa Kahama (wa pamba) watalipwa fedha zao?

**MHE. KHERI KHATIB AMEIR:** Mheshimiwa Spika, kwanza namie nitoe pongezi zangu za dhati kwa Waheshimiwa Mawaziri wa Kilimo (Waziri na Manaibu wake), Katibu Mkuu, Wakurugenzi wa Wizara hii kwa kuwa mstari wa mbele kulisaidia Taifa hili kulilisha, pamoja na matatizo yote ya Bajeti finyu inayotengwa. Nawapongeza vile vile Wakurugenzi na Wasaidizi wao wa taasisi mbalimbali zilizomo chini ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, tengeo la 6% tu ya Bajeti iliyotolewa kwa Wizara hii halikuwa sahihi na si halali, halingepaswa kupewa Wizara hii. Kilimo ni kila kitu, kilimo ni usalama wa nchi, elimu na afya na ni mwajiri mkubwa wa walalahoi. Bila kilimo hakuna Serikali.

Mheshimiwa Spika, naelewa fika kwa sababu hakuna la kufanya mazoea yanatueleza kuwa Bajeti ikishapita hakuna cha kubadilisha lakini kwa siku za baadaye naomba Wizara hii itengewe angalau 10% – 15% za Bajeti yote.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu kwa sasa, Wizara ijitahidi kujipanga vizuri zaidi kwa hiki kidogo kilichopatikana na tujielekeze zaidi katika kilimo cha umwagiliaji na ikiwezekana, tupanue mashamba kwa kushirikisha taasisi za Magereza na JKT kwa kuanzia.

Mheshimiwa Spika, kwa siku za baadae Wizara ijielekeze pamoja na kuwashirikisha wawekezaji binafsi mfano, Misri, Libya na hata Israel wana programu maalum ya umwagiliaji inayowashirikisha wataalamu na wafabiashara ya kuandaa mashamba maeneo ya jangwani ya umwagiliaji (mashamba makubwa tu), ama kwa kutayarisha visima *(bow holes)* au kutumia mto mkubwa wa Misri pamoja na *Lake Victoria.* Kuchimba mitaro ya maji na kutengeneza mashamba na baadaye huyakabidhi mashamba hayo kwa Serikali na Serikali yenyewe nayo kuandaa vijana ambao wamebobea katika taaluma ya kilimo watokao vyuoni na kuwakabidhi kama mali zao kimikataba. Lakini vile vile kwenye programu hizi asasi hizo baadae huwaajiri vijana kama wamanchinga kufanya nao kazi.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huu unaondoa tatizo kubwa la ajira, tutatumia nguvu kazi iliyopo kikamilifu na nchi yetu itakuwa na chakula na si kwa matumizi ya ndani tu bali hata matumizi ya nje ya nchi (kwa biashara).

Mheshimiwa Spika, tatizo letu ni nini Tanzania? Ardhi tunayo, mabonde yaani maziwa kwa ajili ya maji tunayo ni jambo gani linatusonga? Mie nadhani bado hatujakuwa na dhamira ya kweli kulitumia suala hili, njaa inakuja na hakuna chakula duniani. Dunia inapiga kelele, wanatuuzia, wamesitisha kuuza vyakula kwa Mataifa mengine, je, hawa kweli watakuwa tayari kulipa misaada ya kutusaidia? Twangojea nini maafa?

Mheshimiwa Spika, nashauri tena kuwa Bajeti hii ama iongezwe au tuhakikishe Bunge linachukua nafasi yake kwa Bajeti ijayo kusimamia Serikali ni muafaka lazima Bajeti ya kilimo kufikia angalau zaidi ya 15% ya Bajeti ya Taifa.

**MHE. FELIX N. KIJIKO:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kutamka wazi kwamba naunga mkono hoja ya Waziri na wataalam wake kwa sababu hoja yenyewe imetayarishwa vizuri na kueleweka. Hata hivyo napenda kuchangia katika hoja hiyo kwa maana ya kuboresha kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mafunzo kwa maafisa wa vyama vya ushirika, ili kuweza kuwapa usimamizi mzuri wa usimamizi wa vyama vya ushirika na *SACCOS* inashauri watu hawa ambao ndio wanatakiwa kuwa wasimamizi wao. Aidha, lipo kundi la mabwana shamba ambao nao ni wasimamizi wakuu wa kilimo ambao hao wanatakiwa kupelekwa kwenye kozi mbalimbali zinazohusu uboreshaji wa kilimo. Kwa sasa hivi kundi hili ambalo ni la wataalamu hawapelekwi kwenye mafunzo hali ambayo inaathiri maendeleo na usimamizi bora wa sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, lipo tatizo kubwa la kuuza chakula hadi kujisahau kwa kuuza chakula chote na kutokubakiza akiba. Mikoa mingi imekuwa ikikabiliwa na njaa kutokana na kuuza chakula na hasa ile mikoa ambayo imekuwa na hali nzuri ya hewa. Ili kuzuia hali hiyo ambayo huwa inasababisha Serikali kugharamia kwa kutafuta chakula cha msaada Wizara isimamie kutokuuzwa kwa chakula kiholela na ikibidi kutumia vyombo vya habari kwa tahadhari.

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Spika, nimfahamishe Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, hivi sasa mradi wa *ASDP*, kwanza halifahamiki sana na viongozi wa ngazi za chini. Pia inaonekana ushirikishwaji wa viongozi na wananchi katika kuteua miradi ya kilimo ni mdogo au hakuna ushirika kabisa. Miradi mingi ya kilimo hupendekezwa na watendaji wa wilaya.

Ombi langu tutafute mkakati wa kuhakikisha wananchi wanaelimishwa juu ya mradi huu wa *ASDP* na jinsi unavyokuza uchumi na kuongeza uchumi. Serikali imelenga pesa nyingi zisipofahamika na wahusika pesa hizi zinaweza zikatumiwa na wajanja wachache.

**MHE. SULEIMAN O. KUMCHAYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naipongeza Wizara kwa mpango mzuri wa kuendeleza kilimo katika nchi yetu.

Kwa kuwa kilimo ndio msingi mkubwa wa maisha yetu na asilimia 85 ni wakulima walioko vijijini na kwa maana hiyo vijijini ndiko yanakotoka mazao yote. Naiomba Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na Wizara ya TAMISEMI kuboresha barabara za vijijini ili mazao yaweze kusafirishwa kirahisi na kufanya hivyo bei zitapungua na kuleta unafuu kwa wananchi wote.

Naomba suala la wakulima kusaidiwa/kukopeshwa zana za kisasa litiliwe mkazo na Wizara iwe na utaratibu wa kufanya tathmini kila baada ya miezi minne ili kujihakikishia kwamba eneo hili la zana za kisasa linaendelea vizuri. Suala la mbolea bado linazungumzwa sana kuliko utekelezaji wake. Bado haifiki kwa wakati na inauzwa kwa bei ya kawaida na sio ya ruzuku. Naomba Wizara ifuatilie kwa makini.

Mheshimiwa Spika, katika mkoa wa Mtwara bado muuzaji mbolea/*sulphur* ni mmoja naye ni *Abbas Export* na kwa maana hiyo anaweka bei anayotaka yeye na kwa kufanya hivyo wakulima wanaumia.

Katika msimu huu wa ufuta, wakulima wa Wilaya ya Masasi walihangaishwa kwa kutumia bei ya aina mbili kwa msimu huo huo. Mara ya kwanza waliuza kwa shilingi 1,300/= na baadaye wakauza kwa shilingi 700/= tunaomba maelezo ya Wizara itakapokuwa inajibu hoja mbalimbali.

Pia tunaomba kuanzishwa kwa bodi ya mazao mchanganyiko ili kuleta unafuu wa bei kwa wakulima wa mazao hayo kama vile ufuta, choroko, kunde, nyonyo na kadhalika.

Napenda kuchukua nafasi hii kuipongeza Wizara ya Kilimo, Mkoa na Wilaya kwa kusimamia vizuri mfumo stakabadhi za mazao shambani kwa zao la korosho na kuwafanya wakulima wafaidike.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Spika, ni miaka mingi nchi yetu iko katika lugha ya kuwa kilimo ni uti wa mgongo wa uchumi. Lakini na kauli hiyo ni hizo nyingine bado hali ya kilimo na wakulima bado ni duni. Inavyoonekana mpango huu ni mzuri lakini utekelezaji wake ndio matatizo ya nchi yetu. Kutokana na hali hiyo uwezekano wa ukuaji wa uchumi kwa mwaka 2010 kwa asilimia 20 ni ndoto kama inavyoeleza Ilani ya CCM ya mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika, bila ya ukuaji wa kilimo wakulima wenyewe wataendelea kuwa na maisha duni na nchi yetu likitokezea tatizo dogo tu basi nchi yetu itakabiliwa na upungufu wa chakula. Tatizo moja ninaloliona hapa nchini kwetu ni utumiaji wa raslimali ndogo tuliyonayo ya fedha kwa kutaka kuimarisha kula zao. Hali hiyo inasababisha ushughulikiaji mdogo wa kila zao.

Mheshimiwa Spika, nashauri Wizara ifikirie uwezekano wa kuweka kipaumbele kwa mfano mazao mawili kwa kila mwaka. Ikiwezekana mpango huo ukaanzia na mazao ya chakula.

Mheshimiwa Spika, hali hiyo itawezesha kuyashikilia mazao kwa namna inayostahili. Nchi ikishapata chakula na kuanza kusafirisha chakula nchi za nje itawezesha kujenga uwezo wa kuwezesha mazao mengine kushughulikiwa

Mheshimiwa Spika, licha ya sekta ya umwagiliaji kuwepo Wizara ya Maji na Umwagiliaji lakini bado kilimo cha leo bila ya umwagiliaji huna kilimo chenye uhakika.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii inahusiana au inashirikiana vipi na Wizara ya Maji na Umwagiliaji katika utekelezaji wa shughuli zenu hasa katika sekta ya umwagiliaji?

**MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naunga mkono hoja na nampongeza sana Mheshimiwa Stephen Masato Wasira, Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika kwa kuwasilisha Bungeni hotuba nzuri inayoeleweka na kujitosheleza kwa vigezo vyote. Nina maoni mawili tu yanayodai kuzingatiwa na Serikali.

Kwanza, ukurasa wa 13 na 14 wa hotuba ya Waziri inaongelea; "hali ya ushirika nchini." Sehemu kubwa ya maelezo ya Waziri inahusu *SACCOS*, idadi yake na ongezeko la mikopo la vyombo hivyo. Wizara imeshindwa kutambua uwepo wa vyombo vingine vya ushirika ambavyo vinakubalika zaidi na wananchi wa kipato cha chini kuliko *SACCOS*. Vyombo hivyo vinaitwa *VICOBA* ambavyo unaweza sema, ashaakum si matusi *SACCOS* za walalahoi. Vyombo hivi vya ushirika vilianzishwa na Serikali miaka sita iliyopita chini ya mpango wa kuondoa umaskini, Ofisi ya Makamu wa Rais. Inasikitisha kuwa Serikali haifuatilii mipango inayoianzisha yenyewe!

Kwa taarifa, *VICOBA* vimeshamiri mikoa ya Ruvuma, Mbeya, Kilimanjaro, Pwani, Kagera, Dodoma na kadhalika na kuonyesha mafanikio makubwa. Wilaya ya Kyela, mathalan, imeanzisha vikundi hivi vya ushirika mapema mwaka jana kwa jumla ya shilingi 100,000/= kama mtaji. Leo hii Kyela ina zaidi ya vikundi hivyo 150 vyenye zaidi ya shilingi biliobi moja benki na sehemu kubwa ya fedha hiyo ikiwa inazungushwa kwa wanachama wapatao zaidi ya 4,000. Pamoja na kwamba vikundi hivyo havitambuliwi na Wizara na hivyo havipewi msaada wowote wa kuviwezesha, vikundi hivyo vimekubalika sana kwa wananchi, hasa wa kipato cha chini. Wakati umefika kwa Wizara kuvitupia jicho vikundi hivyo muhimu.

Mheshimiwa Spika, pili, zao la kokoa ambalo limeshamiri Wilaya za Kyela na Rungwe, linahitaji mkono wa Serikali kuliendeleza na kulipatia soko la uhakika litakalokuwa na tija kwa wakulima. Aidha, umuhimu kwa Serikali kuvutia wawekezaji kujenga *processing plant* ya kokoa Wilayani Kyela inajitokeza ili kuongeza thamani ya zao. Hatua hiyo itachochea uzalishaji zaidi wa zao hili na kuongeza kipato cha mkulima.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MWANAKHAMIS KASSIM SAID:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uzima wa afya na kuniwezesha kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri pamoja na timu nzima iliyoandaa hotuba hii, hutuba ambayo inaendana na dira ya mwaka 2025 ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mfuko wa pembejeo, licha ya kazi nzuri inayofanywa na mfuko huu wa kuwakopesha wakulima pembejeo na zana za Kilimo bado kuna malalamiko ya uwezo mdogo ya mfuko na kushindwa kuwafikia wakulima wengi, kwa hivyo hakuna budi Serikali iongeze Bajeti ya mfuko ili mfuko uweze kuwafikia wakulima wengi.

Mheshimiwa Spika, pia naishauri Serikali kuazisha benki ya wakulima ili wakulima waweze kukopa fedha na kuweza kumudu gharama za kilimo kwa sababu wakulima wapo, maeneo ya kilimo yapo lakini inashindikana kutokana na uwezo mdogo.

Kuhusu janga la UKIMWI, hili ni janga la Taifa na kila mmoja wetu linamgusa, naipongeza Serikali kwa kuendeleza kutoa elimu kwa watumishi kuhusu mbinu mbalimbali za kujikinga na maambukizi mapya ya virusi vya UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, fedha zilizotengwa na Serikali kwa ajili ya janga hili dhalimu naiomba Wizara izitumie kwa kuwapatia huduma ya chakula na virutubisho waathirika ili kuimarisha kinga za mwili pamoja na kuwaongezea nguvu na siyo vinginevyo kwa sababu elimu imetolewa vya kutosha na bado inatolewa kwa vyombo mbalimbali.

Mheshimiwa spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uzima na afya hadi ninapotoa mchango wangu huu leo.

Mheshimiwa Spika, kama tunavyoelewa kilimo ni uti wa mgongo na asilimia themanini ya Watanzania ni wakulima, lakini inaonekana hali zao za maisha ni duni kwani bado wakulima wengi ni wakulima wadogo wadogo wanaotumia jembe la mkono, huku tija na soko likiwa tatizo.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kuanzisha benki ya wakulima ambayo itatoa mikopo kwa wakulima wadogo wadogo, mikopo ambayo isiwe na riba na ni vema mikopo iwe ni ya muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, *Tanzania Investment Bank (TIB)* imewekwa kuwasaidia wakulima lakini haiwasaidii wakulima kwa sababu *TIB* inaonekana zaidi iko kibiashara

na imekuwa na riba kubwa, jambo ambalo wakulima wetu ni masikini hivyo kupelekea wakulima kutofaidika na *TIB.*

Mheshimiwa Spika, wakulima wa mazao ya matunda kama vile machungwa na nyanya bado hawajanufaika ipasavyo kwani ni mazao ambayo yanastahimili kuharibika muda mdogo sana. Hivyo nashauri Serikali kuanzisha viwanda vidogo vidogo vya mazao haya vijijini ili kuweza kusindika na kuhifadhi na kufanya wakulima kuongeza kipato katika dhana nzima ya MKUKUTA.

Mheshimiwa Spika, kilimo cha bustani ya maua kama kikipangiwa mkakati madhubuti kinaweza kuchangia kwa kiasi kikubwa kuongeza kipato cha wakulima na kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Spika, napenda kujua mchango wa kilimo cha maua katika Bajeti ya Wizara na ni kiasi gani Serikali inamkakati wa kuboresha kilimo hiki cha maua ili kuongeza ajira hasa akinamama katika azma nzima ya MKUKUTA na je, kwa mwaka wa fedha 2007/2008 kilimo cha maua kimeingizia fedha kiasi gani kwa kuuza maua nje ya nchi?

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana na naomba kuwasilisha.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Spika, suala la mbolea kuwafikia wakulima kwa wakati ni jambo la muhimu sana. Juhudi zifanyike ili mbolea ya ruzuku iwafikie walengwa.

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA:** Mheshimiwa Spika, pongezi kwa timu nzima ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika.

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 45 wa kitabu cha Bajeti imezungumiziwa udhibiti wa visumbufu vya mimea na mazao ya kilimo kwa kuvitaja visumbufu hivyo kuwa ni nzige, kwelea kwelea, viwavijeshi, panya na magonjwa. Kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Tunduru nasikitika kwa Wizara kutotamka rasmi kuwa mnyama tembo ni miongoni mwa visumbufu vya mimea na mazao ya kilimo ambaye anastahili kuwekewa mkakati wa udhibiti.

Mheshimiwa Spika, tunaomba Wizara ituambie ina mkakati gani wa kuwadhibiti tembo wanaoharibu mazao ya kilimo?

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri alifikishe wazo hili kwenye Baraza la Mawaziri.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali, iahirishe walau kwa mwaka mmoja fedha za JK zikatumika kununua matrekta. Kama fedha hizo shilingi bilioni 21 zitatumika kununua matrekta moja kwa moja toka kwa watengenezaji, yatapatikana matrekta 840 yaani kila trekta shilingi milioni 25 kiasi hicho hicho cha pesa kinaweza kununua *power*

*tiller* 4,200 ambapo kila *Power Tiller* ni shilingi milioni tano. Kiasi hiki cha matrekta chaweza kuleta mapinduzi makubwa ya kilimo kwa kuongeza maeneo ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, panya ana kiwango kikubwa cha protini na protini inayotengeneza *amino acids* ambayo vimelea vyake ni pamoja na *nitrogen.*

Mheshimiwa Spika, *nitrogen* ni rafiki mkubwa wa mimea. Napenda kutoa ushauri kwa Wizara kwamba iwaagize wataalam wetu wa Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine kifanye utafiti wa kuwakausha panya halafu kurutubisha mimea. Faida mbili zitapatikana ni kwanza, panya ambao ni wasumbufu watadhibitiwa na pili, udhibiti utatumika kurutubisha mimea.

**MHE. DR. BINILITH S. MAHENGE:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kutoa pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara kwa maandalizi ya hotuba nzuri.

Mheshimiwa Spika, upimaji wa sumu ya zao la Pareto. Kwa niaba ya wananchi wa Makete naipongeza Serikali kwa kupata soko la Pareto. Wananchi wa Makete tayari wameanza kulima Pareto kwa wingi na uzalishaji umeanza kuongezeka. Malipo ya zao la Pareto yanatokana na kiwango cha sumu iliyomo ndani ya ua la Pareto. Kiwango cha maabara ya kupima sumu ni cha kampuni inayonunua hiyo Pareto. Mkemia wa Serikali anayesimamia upimaji wa sumu ili kulinda maslahi ya wananchi hawezi kufanya kazi yake kwenye maabara ya wanaonunua zao la Pareto.

Mheshimiwa Spika, napendekeza, Serikali ijenge Maabara ya Serikali ya kupima kiwango cha sumu kwenye zao la pareto. Hii itasaidia kuwalinda wananchi katika kupata bei sahihi inayotokana na kiwango cha sumu. Mazao mengine kama korosho, Serikali imeweka maabara hivyo ni vema zao la Pareto pia likawa na maabara yake. Pia Serikali kusaidia kutengeneza barabara kwenye maeneo yanayolimwa Pareto ili ziweze kupitika wakati wote na kuwawezesha zao la Pareto kusafirishwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara isaidie kuwajengea wakulima wa Pareto Maabara ya kukaushia Pareto kwa ubora zaidi badala ya kukausha kwa jua, hasa ukizingatia hali ya hewa ya mvua.

Suala la mbolea, Serikali inapendekeza kutumia utaratibu wa vocha kwa kugawa mbolea ili iwafikie wakulima. Wananchi wangependa kujua gharama halisi za maandalizi ya hizo vocha pamoja na kuzisafirisha ni kiasi gani? Ni kwa nini Serikali ijiingize kwenye gharama hizo badala ya kujikita zaidi kusimamia ugawaji wa mbolea. Fedha za kutengeneza na kusambaza vocha zingetumika kuongeza mbolea. Pia bei ya mbolea ni kubwa mno mbolea aina *DAP* inatumika sana Kwa wakulima wa Makete, lakini bei yake ni kubwa mno yaani shilingi 95,000/=, wananchi kipato chao ni kidogo, hawawezi kumudu bei hii. Serikali itaendeleza vipi kilimo katika mazingira haya?

Mheshimiwa Spika, mapendekezo yangu ni kuwa Serikali ijenge kiwanda cha mbolea Nyanda za Juu Kusini, kwa sababu zinaweza kuzalisha sana. Pia Serikali iendeleze kilimo cha umwagiliaji, isambaze umeme vijijini, umeme utawezesha matumizi ya pampu za umeme katika umwagiliaji na hivyo kuongeza *efficiency* na *productivity*.Mbolea nyingi ipelekwe Nyanda za Kusini ambako mazao mengi yanastawi na uzalishaji wake unaweza kutoa chakula cha kutosha.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MOHAMEDI ALI SAIDI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kilimo ndio uti wa mgongo wa uchumi wa Tanzania, na kwa kuwa zaidi ya 80% ya Watanzania ni wakulima. Bado kilimo hakijapewa umuhimu unaostahili. Kwanza kilimo chetu bado ni cha zamani, watu wanalima kwa majembe ya mkono na yale ya kuburuzwa na ng'ombe. Ukulima wetu bado haujawa wa kitaalamu yaani wa kisasa. Hatujaweza kutumia mbolea ipasavyo wala hatujakuwa na mipangilio mizuri, na kwa sababu hiyo, bado hatujaweza kujitegemea kwa chakula na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Tanzania Mwenyezi Mungu katubariki kwa kuwa na ardhi kubwa na nzuri kwa kilimo cha aina mbalimbali. Kama ardhi hii tungeitumia vizuri, sisi tungeweza kujitosheleza kwa chakula na kingine tungeweza kusafirisha nje kwa kupata pesa za kigeni kuongeza pato letu la Taifa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa nchi yetu imebahatika kuwa na mito mingi na maziwa, kilimo ambacho kinaweza kutunyanyua haraka katika uchumi wetu na pia kuondokana na njaa na kupata chakula cha ziada ni kilimo cha umwagiliaji. Naiomba Serikali iwekeze nguvu zake zaidi katika kilimo cha umwagiliaji, na hata kuwaruhusu wawekezaji binafsi wawekeze katika kilimo hicho. Kwani kwa kufanya hivyo tutaweza kupiga vita umaskini kwa kuongeza ajira kwa vijana wetu, na kuondoa kabisa balaa la njaa.

Mheshimiwa Spika, vile vile naiomba Serikali iboreshe miundombinu ya barabara hasa vijijini, ili bidhaa zinazozalishwa ziweze kufika kwenye masoko.

Mheshimiwa spika, pia naiomba Serikali ianzishe viwanda vya kukamulia matunda yaani *juice* ili matunda yetu yaweze kusafirishwa bila kuharibika ovyo na pia tuweze kusafirisha *juice* badala ya kuagizia kutoka nje. Ahsante sana.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naunga mkono.

Pongezi kwa Mheshimiwa Stephen Wasira ambaye ni Waziri, Mheshimiwa Dr. David Mathayo David, Naibu Waziri, Katibu Mkuu Bwana Peniel Lyimo, Naibu Katibu Mkuu Sophia Kaduma na watendaji wote wa Wizara yote, kwa hotuba nzuri ambayo imefafanua mahitaji muhimu ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, matarajio ya upatikanaji wa chakula. Pamoja na maandalizi mazuri ya Serikali ningependa nitoe maelezo yangu na ushauri kama kuwezesha mabwana shamba/mabibi shamba kuwafikia wakulima kama inavyofahamika jiografia ya vijiji vyetu. Kwa mfano hata kuwakopesha pikipiki ili waweze kutumia elimu yao na utaalamu wao kwa ukaribu zaidi, kuwapa pembejeo ili waweze kulima mashamba darasa kwa kila tarafa ambayo yatakuwa ni mfano kwa kila tarafa kama kwenda kufudhishiwa pale kuliko wao kwenda kila kijiji au kutoa elimu kwa kila mwananchi mkulima hiyo itatoa lawama kwa wana ugani bila sababu kama ilivyo sasa. Pia wakopeshwe matrekta au majembe ya kukokotwa na ng'ombe (wanyama kazi).

Mheshimiwa Spika, pia wapewe motisha mbalimbali kama vile kupewa nyumba bora vijijini/tarafa, posho na mishahara. Waandaliwe ofisi bora kwani hawana ofisi za kisasa hata za zamani ni ovyo naomba ziangaliwe na kupewa kompyuta kwa ajili ya takwimu ili zitolewe kwa usahihi.

Mheshimiwa spika, hali ya uzalishaji na mazao ya biashara, ruzuku kwa kuwa hutolewa kwa mikoa michache hapa nchini ningeomba hata zao la tumbaku wapewe ili waweze kuzalisha zaidi, kilimo cha tumbaku kwa kawaida hulimwa kwa mwaka mmoja mwaka unaofuata hulimwa zao la chakula kwa kutumia mbolea hiyo hiyo. Hivyo na kuzalisha chakula.

Suala la mbolea usambazaji – Minjingu, kwanza niishukuru Wizara kwa kuamua usambazaji wa mbolea hapa nchini iwe *TFC*, ni kweli napongeza kwani wao ni wazoefu. Bei ya mbolea ya Minjingu iwe ya kawaida ili wananchi/wakulima wengi waweze kumudu gharama hizo, kwani malighafi ipo hapa hapa nchini, lazima Wizara iangalie gharama zake na bei inayopanda mara kwa mara.

Pia elimu itolewe ili wananchi waweze kuzoea hiyo mbolea ya unga. Kwa kutumia *TV*, redio, vipeperushi kwa kushauriana na hao wenye viwanda hata kama watazalisha bila kutoa elimu bado wakulima wataogopa kuitumia.

Mheshimiwa Spika, suala la bei ya tumbaku, naomba Wizara iangalie suala zima la uuzaji wa tumbaku kwa fedha ya Tanzania, kwani wao mpaka sasa hununua kwa dola, wanunuzi wote hapa nchini. Wizara isaidie kutatua uuzaji wa tumbaku kama ilivyosaidia zao la korosho, kwa kutumia stakabadhi. Kuna soko huria kwa wanunuzi wengine kama ilivyokuwa siku za nyuma/mwanzo kulikuwa na *TLTC*, *Dimond* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, wakulima wa tumbaku waondolewe au wasaidiwe na Serikali kulipa madeni yao ili wawe huru na kuuza popote. Kuuliza bei ya soko la dunia. Kabla ya kuuza.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja mia kwa mia.

**MHE. COL. FETEH SAAD MGENI:** Mheshimiwa Spika, kwa heshima kubwa ninapenda kumpongeza, Mheshimiwa Waziri, Naibu wake pamoja na watendaji wale

wote kwa kazi nzuri wanayoifanya katika Wizara hiyo pamoja na hotuba nzuri ya Bajeti walioiwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima naomba kuchangia maeneo machache yafuatayo, kwanza ni kuhusu kilimo, kauli ya Marehemu Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere, kwamba kilimo ndio uti wa mgongo wa Taifa. Je, tujiulieze tumeuenzi wito huo wa Baba wa Taifa kwa kiasi gani? Nadhani sasa umefika wakati tulitekeleze kwa dhati suala au kauli hiyo kwa nguvu zetu zote. Asiyelienzi la mkuu huvunjika guu.

Mheshimiwa Spika, matajiri wa duniani wameshatuacha mkono hasa nchi zetu zinazoendelea ambazo bado tegemezi. Naomba ushauri sana yafuatayo, kuimarisha kilimo cha umwagiliaji tena kwa utaalamu wa hali ya juu kabisa, kupatikana pembejeo za kilimo za uhakika kabisa aidha, mbolea safi itakayoendana na hali ya jiografia ya ardhi ilivyo na matrekta ya kutosha yapatikane. Pia wataalam wa kilimo watumike ipasavyo, azma ya mapinduzi ya kilimo/*green revolution* itekelezwe kikamilifu na upatikanaji wa mbegu bora za mazao uzingatiwe.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hifadhi ya chakula *(SGR)*kutokana na hali mbaya ya chakula duniani, naomba kushauri akiba ya chakula Kitaifa lazima iongezwe mara mbili zaidi aidha, maghala ya utunzaji wa nafaka yaongezwe zaidi na yawe ya kisasa.

Kuhusu mazao ya mafuta, mazao kama nazi, mawese, alizeti, pamba, karanga na kadhalika lazima tuyaimarishe kwa bidii sana. Mazao ya biashara lazima tuimarishe mazao ya biashara kama vile pamba, chai, ngano na kadhalika ili tuweze kuwa na ushindani mzuri katika soko la dunia.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango wangu huu ambao ni mchache sana, sasa kwa heshima kubwa kabisa, naunga mkono hoja hii kwa asilimia kwa mia.

**MHE. SIJARU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa ni kuhusu benki ya kilimo. Uwekezaji katika miradi mikubwa na ya kati ya kilimo inahitaji fedha nyingi kwa ajili ya kununulia zana za kilimo (matrekta, plau, mabomba ya umwagiliaji, pembejeo mbalimbali na kadhalika na fedha hizi hazipatikani toka kwenye mabenki ya biashara. Kwa nini Serikali isichukuwe uamuzi wa makusudi wa kutenga fedha kiasi kisichopungua shilingi bilioni 200 kwa kuanzia ili kuanzisha benki ya kilimo?

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba fedha hizi ni nyingi na Serikali inaweza kujitetea kuwa haina fedha hizo. Ndiyo maana napendekeza Serikali ichukue uamuzi wa makusudi kutafuta mtaji wa kutosha ili kuanzisha benki ya kilimo haraka sana. Mtaji huu kwa benki ya kilimo utakuwa na manufaa makubwa/mengi kwa uchumi wetu. Kwa hali hiyo nasisitiza Serikali ifanye haraka kuanzisha benki hii kwa manufaa ya uchumi mdogo na mpana.

Suala la viwanda vya mbolea, Tanzania ina rasilimali nyingi muhimu zinazohitajika kama vile gesi asilia, *phosphets* na kadhalika kutengenezea mbolea za chumvi chumvi hapa nyumbani. Kwa nini Serikali isihamasishe sekta binafsi kuanzisha viwanda vya mbolea hapa nchini badala ya kutumia fedha nyingi za Taifa kuagiza

mbolea toka viwanda vya nje.  Utaratibu huu utakuwa na faida nyingi za kiuchumi hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, *agro-based industries,* tunahitaji kuanzisha viwanda vingi hapa nchini vitakavyotumia malighafi zitokazo kwenye sekta ya kilimo. Si jambo zuri kwa uchumi wa nchi kuendelea kuuza nje bidhaa ghafi za kilimo bila kuziongezea thamani katika viwanda vyetu.  Kwa mfano, kwa nini tuendelee kuuza nje pamba badala ya nguo?  Au nyuzi za katani badala ya kamba zake na/au mazulia?  Kahawa (buni) badala ya Kahawa ya viwandani ambayo iko tayari kwa matumizi na kadhalika. Ni kweli kwamba Serikali haiwezi kuwekeza katika viwanda hivi.  Kwa hiyo, ni vema Serikali ikatengeneza mazingira rafiki kwa sekta binafsi kuweza kuwekeza katika sekta hii ya viwanda.

Kuhusu ushirika, naipongeza Serikali kwa kuweka mkazo juu ya umuhimu wa ushirika katika maendeleo ya sekta ya kilimo.  Hata hivyo napenda kusisitiza haja ya Serikali kusimamia kwa karibu sana utekelezaji wa sera ya ushirika hususan kuanzia ngazi za chini.  Bila kusahau uhumimu wa kuhamasisha uanzishwaji wa *SACCOS* nyingi hasa vijijini na mitaani.  Ili kutekeleza azma hii ni budi Serikali ikaajiri maafisa wengi wa ushirika watakaohamasisha uanzishwaji na uendelezaji wa *SACCOS.*

Mheshimiwa Spika, *Agricultural Sector Development Programme* dhana hii ni nzuri na inaweza kuwa injini ya kuleta maendeleo ya sekta ya kilimo.  Sina hakika kama Wizara husika imeweka utaratibu mzuri wa kuieneza dhama hii katika sehemu kubwa ya Tanzania na hasa vijijini ambako kuna wakulima wengi ambao wanastahili kufaidika na mpango huu. Nasisitiza umuhimu wa Wizara ya Kilimo kusambaza elimu ya mradi huu *ASDP* katika Wilaya na vijiji vyote nchini na ni vizuri zaidi kama kila Wilaya itakuwa na wataalam wa kutosha watakaohimiza wananchi utekelezaji wa programu hii.

Kuhusu kilimo cha umwagiliaji, hili ni eneo ni muhimu sana kwa maendeleo ya sekta ya kilimo ili tuachane na utaratibu wa kutegemea mvua tu ambazo wakati mwingine hazina uhakika. Ni kweli Serikali imekuwa inazungumzia umwagiliaji na kuna maeneo ambayo tayari miundombinu ya umwagiliaji ipo. Ninachotaka kusisitza ni haja ya kuongeza kasi ya uwekezaji katika eneo la umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, India ni moja ya nchi ambazo zimefanikiwa sana katika eneo hili la umwagiliaji hata katika maeneo yasiyokuwa na moto kwa kutumia visima virefu. Naishauri Serikali yetu ikaazime uzoefu wa umwagiliaji toka India.

Kuhusu kilimo cha mazao ya biashara/chakula, Tanzania ina eneo kubwa la kuweza kulima mazao mbalimbali kuliko nchi nyingine za Afrika ya Mashariki, lakini inasikitisha kwamba nchi yetu hajaiweza kuzalisha mazao mengi zaidi kuliko majirani zetu. Kwa mfano sielewi kwa nini nchi yetu inazalisha takriban 10% tu ya chai inayozalishwa Kenya?  Tukajifunze Kenya wanawezaje kuzalisha chai na mazao mengine kwa wingi zaidi kutushinda sisi. Hadithi ya zao la chai, inahusu pia mazao mengine ya kilimo.

Kuhusu *Tumbi Agricultural Research Institute,* Tabora naiomba Serikali itenge fedha za kutosha kwa ajili ya kukikarabati kituo hiki (majengo na miundombinu yake), ili kiweze kutekeleza majukumu yake ya kufundisha wataalam wa kilimo katika mazingira mazuri.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mradi mdogo wa umwagiliaji. Ili chuo chetu cha Tumbi kiweze kuainisha elimu ya darasani na ile ya vitendo hususan katika eneo la umwagiliaji, chuo kimetayarisha mradi mdogo wa umwagiliaji. Tatizo kubwa ni upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa chuo cha umwagiliaji.

Naoimba Wizara ifuatilie mradi huu kwa manufaa ya chuo chetu cha Tumbi, Tabora.

**MHE. ABDUL J. MAROMBWA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kuunga mkono hoja iliyo mbele yetu ya Waziri wa Kilimo. Hotuba hii imetoa mwelekeo mzuri wa namna ya kuinua kilimo katika nchi yetu na kuifanya isiwe omba omba.

Mheshimiwa Spika, nianze kuchangia hotuba hii kwa kuishukuru Serikali kwa kukipatia chama cha ushirika mkoa wa Pwani *(CORECU)* fedha za kununua mazao hasa zao la korosho. Kwa muda mrefu wakulima wa korosho, walikuwa wanatafuta mahali pa kuuzia mazao yao. Kwa ujumla wakulima wa korosho wanaishukuru sana Serikali kwa kuwawezesha kuuza korosho zao zote. Hakuna mkulima ambaye korosho zake hazikuuzwa.

Mheshimiwa Spika, wakulima wetu wana malalamiko kuhusu namna *CORECU* ilivyonunua korosho mwaka jana. Malalamiko hayo ni pamoja na korosho karibu zote zilizonunuliwa zilikuwa za daraja la “A”. Hii ni hatari kwani wakulima walijitahidi sana kuzipanga korosho zao katika madaraja lakini *CORECU* haikukubaliana na wakulima hao. Hata Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, alipofanya ziara Mkoa wa Pwani Desemba mwaka 2007 aliilaumu *CORECU* kwa kununua korosho karibu zote kwa daraja moja. Alitaka *CORECU* inunue korosho kwa madaraja.

Pia kuchelewa kupewa mkopo kwa chama cha ushirika Mkoa wa Pwani *(CORECU)* hapo mwaka jana fedha za kununua korosho zilichelewa sana kutolewa na benki zetu na hatimaye baadhi ya wakulima waliuza korosho zao kwa walangunzi.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali itoe fedha za kununulia korosho mapema msimu unapoanza ili walanguzi wasiwalangue wakulima Pembejeo za kilimo zitolewe mapema ili wananchi wawili kupulizia mikorosho yao kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine la kuhusu upatikanaji wa matrekta katika Wilaya ya Rufiji. Wilaya hii ni miongoni mwa Wilaya ambazo zina rutuba ya kutosha na bado ardhi yake haijaharibika. Kwa muda mrefu tafiti mbalimbali zimeonyesha kuwa kama utalima bonde la mto Rufiji, chakula kitakachopatikana kinaweza kulisha nchi hii kwa mwaka mzima.

Mheshimiwa Spika, tatizo lililokuwepo ni umaskini mkubwa unaowakabili wananchi wa Wilaya hii. Hadi sasa wakulima wa Rufiji wanatumia jembe la mkono. Kilimo hiki haina manufaa yoyote kwa wakulima wenyewe na Taifa letu kwa ujumla. Wilaya yote ya Rufiji ina matrekta si zaidi ya matao, hii ni hatari.

Naiomba Serikali inagalie uwezekano wa kuwasaidia wananchi ambao tayari wameainisha vikundi vya ujasiriamali waweze kukopeshwa matrekta ili walime maeneo makubwa na hatimaye waweze kupata mazao mengi.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya vikundi hivyo vimeshafanya michango mbalimbali na wana zaidi ya shilingi 8,000,000/= kwa kikundi. Ni vizuri Serikali ikatoa ufafanuzi juu ya vikundi hivi.

Aidha, Serikali iweke bayana matumizi ya fedha za *DADPS* kwani kuchangia vikundi vya kilimo ambavyo vinatumia jembe la mkono hakusaidii kuleta mapinduzi ya kilimo. Naishauri Serikali iangalie uwezekano wa fedha hizo kutumika katika ununuzi wa matrekta walau manne kila mwaka ili kuinua kilimo Wilayani Rufiji.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DORAH H. MUSHI:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mungu kwa kunipa uzima.

Naomba nitoe rambirambi zangu kwa familia ya Mheshimiwa Savelina Mwijage kwa ajali mbaya iliyotokea hatimaye kumpoteza mwanaye pamoja na dereva wake. Naomba Mungu ampe moyo wa uvumilivu.

Naomba sasa nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri wa Kilimo, Naibu Waziri pamoja na wataalam wake wote kwa hatua nzuri ambayo inajibu utekelezaji wa ahadi zilizoko katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze na suala la kilimo. Kilimo ni uti wa mgongo wa Taifa letu. Mwenyezi Mungu ametujalia ardhi nzuri, maeneo mazuri ya mabonde yanayopendeza, lakini inashangaza kwamba Watanzania bado hatujaweza kutoa kipaumbele kwenye kilimo.

Mheshimiwa Spika, vijana wengi wanakimbilia mijini kwenda kufanya biashara (umachinga) lakini wanasahau kuwa kilimo ni biashara.

Mheshimiwa Spika, wazazi wetu hawakujua kufanya biashara yoyote isipokuwa ni kilimo tu. Tulilelewa na kusomeshwa na kilimo tena cha jembe la mkono wala kulikuwa hakuna pembejeo. Lakini tuliishi kwa kutegemea kilimo. Kwa nini leo tunaona kilimo hakina faida? Kilimo kina faida kubwa sana. Tunataka kila mtu aende shambani wakati muafaka ikiwa ni Mbunge, daktari, mwalimu, mfanyabiashara na

wafanyakazi wote, twende shamba, Tanzania njaa mwiko. Kilimo ni uti wa mgongo wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, wakati umefika sasa kuhamasisha kilimo kama tulivyohamasisha kujenga madarasa na zahanati, tuhamasishe kilimo. Tunaiomba Serikali ielekeze nguvu upande wa kilimo kuongeza maafisa ugani kwa kuwa waliopo hawatoshi na wasikae mijini wakae mashambani ili waweze kutoa msaada kwa wakulima

Mheshimiwa Spika, Serikali iagize matrekta, mbolea, pembejeo na dawa za kuulia wadudu na wakulima wazipate kwa wakati. Serikali ianzishe benki ya wakulima kwenye vijiji kwa kuwa wananchi wakulima wameunda *SACCOS* zao ambapo itakuwa rahisi sana kukopesheka ikiwa Serikali itapeleka Benki Vijijini.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Manyara ni eneo la wakulima na wafugaji. Ni vyema Serikali iangalie miundombinu ya barabara zinazounganisha vijiji, kata hadi kata ni mbaya sana. Ni vigumu sana mkulima kuondoa mazao shambani na kupeleka ghalani. Serikali iangalie sana suala la barabara tunaomba halmashauri ziongezewe Bajeti kwa ajili ya kutengeneza barabara hizo. Ikiwa barabara za Manyara zitaboreshwa mkoa huu una uwezo mkubwa wa kuzalisha chakula cha kutosha kabisa na cha biashara.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Spika, kwanza naunga mkono hoja ya Serikali. Nawapongeza pia Waziri Mheshimiwa Stephen Wasira, Naibu Waziri Mheshimiwa Dr. David Mathayo David, Katibu Mkuu na Naibu katibu Mkuu kwa juhudi wanazofanya kuendeleza kilimo.

Mheshimiwa Spika, tunaweza kusimama na kufanya *stock.* Juhudi zilizofanywa na fedha yote iliyotumika kwa nini hatujaweza kubadilisha kilimo cha Mtanzania. Bado kwa kiwango kikubwa kilimo chetu ni jembe la mkono. Mapinduzi yatafanyika lini?

Pia tumetawanya sana rasilimali zetu, kwa vile tunaelekea kukubaliana Arusha ni mji wa kitalii na rasilimali zimeelekezwa huko. Kwa nini Serikali isielekeze rasilimali katika maeneo yatakayotupa mazao mengi ya chakula na mazao ya biashara? Katika hotuba mafunzo yameelekezwa katika mikoa mingi lakini Ruvuma haipo!

Mheshimiwa Spika, kuhusu zao la kahawa, sheria inataka *TCB* ifanye *registration* ya wakulima, hili halijafanyika pamoja na kuteua *coffee inspectors.*

Suala la ushirika Serikali ilifanya kazi nzuri ya kurejesha vyama vya ushirika Mtwara na Lindi, vyama hivi vilikuwa hoi sana lakini Serikali imesaidia kuviinua. Kwa nini juhudi hizi za makusudi hazijaelekezwa Mbinga ambako hata kihistoria ushirika ndio mtindo wanaoufahamu? Namshukuru sana Waziri Mheshimiwa Stephen Wasira kwa kuwa *very positive* na kufufua ushirika wa Wilaya Mbinga. Tayari vyama vya msingi 28 vimefanya mkutano na wamechagua Mwenyekiti wao na viongozi wengi.

Mheshimiwa Spika, mahitaji ni pamoja na Serikali iwasaidie *management* hasa hapo awali hatua ilivyofanyika kule Mtwara/Lindi. Shughuli za Mfilisi ziishe, madeni ya *NBC* yafutwe kama ilivyofanyika katika sehemu nyingine. Hawa pia ni Watanzania Serikali haishindwi kitu. Inawezekana. Tumsadie mkulima.

Mheshimiwa Spika, maombi yangu ni kwanza kuhusu mazao ya matunda/bustani/maua. Mbinga ina hali ya hewa nzuri shughuli hizi zinaweza kufanyika vizuri. Wizara isaidiane na Halmashauri kuhamasisha wananchi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. FRED M. TUNGU:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naunga mkono hoja. Pili, naipongeza Wizara kwa jitihada inayozofanya katika kutekeleza wajibu wake.

Naomba kuchangia mambo yafuatayo, bodi za mazao ya pamba, kahawa, tumbaku na kadhalika ni vyombo muhimu sana katika kuwasaidia wakulima kupata utaalamu na ushauri mbalimbali katika kuboresha kilimo cha mazao hayo. Bodi hizi kwa sasa zinafanya kazi katika mazingira magumu sana. Nashauri bodi hizi ziongezewe fedha ili ziweze kutekeleza majukumu yake. Vyanzo vilivyoondolewa virudishwe.

Kuhusu mfuko wa Taifa wa pembejeo, mfuko huu ni muhimu sana katika kumsaidia mkulima ili aweze kupata pembejeo. Mfuko huu upate fedha zake kutoka Hazina moja kwa moja. Aidha, *component* ya *ASDP* itumike kama moja ya chanzo cha fedha kwa mfuko huu wa pembejeo.

Mheshimiwa Spika, bodi ya mazao mchanganyiko ianzishwe haraka. Kuna mazao mbalimbali ambayo yanawasaidia sana wakulima lakini hayana usimamizi. Bodi ya mazao mchanganyiko itasaidia sana.

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ya Kishapu tarafa ya Negezi kulikuwepo kituo cha kilimo ambacho kwa sasa hakuna kitu kinachofanyika, yamebaki majengo tu. Naishauri Wizara itume wataalam waende waangalie uwezekano wa kukifufua kituo hicho ambacho kingeweza kutumika kama kituo cha kufundishia wakulima wadogo na pia kuanzisha kituo cha majaribio na kuelimisha wakulima walime kilimo cha kisasa.

**MHE. DR. MAUA A. DAFTARI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, umuhimu wa kuwekeza katika kilimo. Turejee kule nyuma wakati wakulima wakubwa waliokuwa wanalima na ku-*process products* zao kwa mfano, unga, ngano *(packed)* sembe *(packed) edible oil* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, *products* hizo zilitawala soko la nje na kuingiza fedha za kigeni nchini. Ni vyema basi yawepo mashamba makubwa ya Serikali ya mifano ambayo wakulima watajifunza.

Kuhusu usambazaji wa pembejeo hauendi kwa wakati, mboleo inachelewa sana kuwafikia wakulima. Uwepo usimamizi bora katika hili. Suala la matumizi ya hali ya

hewa katika kulima, inaelekea *data* za hali ya hewa hazimfikii mkulima wa kijijini, zinabaki katika mafaili ya *RC* na *DC.* Si kila mtu ana redio au *TV*.

Mheshimiwa Spika, maafisa ugani hawawatembelei wakulima ipasavyo, hivi sasa upo ugonjwa wa minazi kuanzia Kibaha hadi Morogoro. Minazi inakauka na majani yake yanabadilika. Hatuoni *efforts* zinazoelekeza utatuzi wa suala hili. Hivyo wakulima wanakosa maelekezo juu ya ukulima bora.

Pia hatuna mkakati wa uvunaji wa moja ya mvua na kuyahifadhi kwa matumizi ya baadae, licha ya mvua nyingi zinazonyesha, *in the end* hatuzitumii ipasavyo. Kuwepo na mkakati wa kukitumia kituo cha *Carmatec* kwa lengo kuwasaidia wakulima vijijini. Wanazo teknolojia muafaka mbalimbali za kumsaidia mkulima. Tatizo hakuna *coordination* baina ya Wizara ya Kilimo na Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko. Hivyo *investiment carmatec* ni kama ndoto. *Efforts* za Mwalimu Julius Nyerere za kumnyanyua mkulima zimegonga mwamba.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kilimo na ile ya Maji na Umwagiliaji lazima *in the end* waonane kilimo bila Maji si Kilimo. Wananchi wa Kiluvya Mkuranga wanalima kwa juhudi kubwa, hakuna maji kwa kunywa wala umwagiliaji. Ardhi inayo rutuba ila tatizo ndio hilo.

Mheshimiwa Spika, tuwekeze katika tafiti, vyuo vyetu vya *SUA* na vingine vipewe fedha za kutosha kufanya utafiti wa mbegu bora ambazo hatimaye zitasambazwa kwa wakulima. Viongozi mbalimbali katika ngazi zote lazima wawe mfano wa mkulima bora wawezeshwe kufanikisha hilo. Viongozi wa Kitanzania wengi wao ni maskini. Vipato vyao vingi vimeishia kwa wapiga kura.

Mheshimiwa Spika, *GMO* hivi Tanzania inasema nini katika hili? Kule China wanatumia *paddy field* ambazo wanalima mara tatu kwa mwaka, je, ukulima huu hauwafai wakulima wa Tanzania?

Mheshimiwa Spika, mazao ya biashara za nje ya nchi yapewe uzito sana na wawezeshwe na wa- *import* mazao nyumbani na kuuza nje.

Mheshimiwa Spika, Wizara imejitahidi sana katika kuboresha kilimo, nawapongeza viongozi wote wa Wizara kwa kazi nzuri.

**MHE. CHARLES N. KEENJA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuanza mchango wangu kwa kumpongeza Waziri wa Kilimo na wasaidizi wake kwa hotuba yake nzuri ambayo inafafanua vizuri mambo tunayotakiwa kufanya ili kuwezesha kuwapo kwa mapinduzi ya kijani katika kilimo.

Mheshimiwa Spika, tatizo langu ni kwamba maelezo hayo mazuri hayaendani na rasilimali zilizotengwa kwa ajili ya maendeleo ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, hali ya kilimo iliyopo nchini leo imekuwepo kwa miaka mingi iliyopita. Mwaka wa 1972 tulipitisha Azimio la Iringa lililojulikana kama siasa ni kilimo. Yanayosemwa kwenye Azimio lile ndiyo hayo hayo tunayoshauri leo. Hii ina maana kwamba hali ya kilimo haijabadilika na kwamba hatukutekeleza yale tuliyoamua miaka 36 iliyopita. Hili ndilo tatizo letu kubwa sana. Tunafanya maamuzi sahihi na mazuri lakini hatuyatekelezi na kwa hiyo, hatupati maendeleo yaliyokusudiwa.

Kuna mifumo mingi ya maamuzi ya aina hiyo. Ilani za Chama cha Mapinduzi za chaguzi kuu zinatoa ahadi ya maelekezo ya mambo ya kufanywa ili kuendeleza kilimo. Ilani ya mwaka wa 2008 inaeweka lengo la kukua kwa kilimo kwa 20% na inazitaka Serikali zitenge zaidi ya 10% ya Bajeti zake kwa ajili ya kilimo. Mwaka jana na kwa miaka minne iliyotangulia, kilimo kimekuwa kwa asilimia nne tu. Kutafanyika muujiza gani kukifanya kiongeze kasi ya kukua kufikia 20% ifikapo mwaka 2010! Mwaka jana Bajeti ya kilimo ilikuwa 6.2% na 6.4% mwaka huu. Hatukufikia 10% ya mapato na ambayo imekubaliwa na Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika, ni lazima Serikali na wadau wote wa kilimo wakubali kuongeza sana uwekezaji katika kilimo. Mawazo kwamba baadhi ya mambo muhimu yataachiwa sekta ya binafsi yanawezekana tu iwapo sekta hiyo itaandaliwa na kuwezeshwa, vinginevyo Serikali ndicho chombo pekee kilichopo chenye uwezo na wajibu wa kuendeleza kilimo. Kwa mfano tunahitaji viwanda vya kutengeneza mbolea, zana za kilimo za aina zote kuanzia na jembe la mkono, majembe ya kukokotwa na wanyama, matrekta na kadhalika na viwanda vya kusindika mazao ili kuyaongezea thamani. Kwa sasa tunauza mazao ghafi na tunaagiza mahitaji yetu karibu yote kutoka nje ya nchi. Hiii ni hali ya hatari sana.

Mheshimiwa Spika, kilimo cha kisasa kinahitaji ujuzi wa sanyansi. Katika nchi nyingi zilizoendelea, wakulima ni watu waliohitimu mafunzo ya kilimo kwenye vyuo vikuu au walioajiri wafanyakazi wenye elimu hiyo. Wakulima wa Tanzania hawana ujuzi wa kilimo cha kisasa au kilimo bora. Madai kwamba kuna wakulima wanaotumia kilimo cha jadi hayana msingi kwa kuwa kilimo cha aina hiyo hakipo. Wakulima wanapaswa kupewa mafunzo ya kilimo na sio ushauri usiokuwa na utaratibu. Wizara ina vyuo vinne vya wakulima zipo *EDC 56.* Hii ina maana kwamba kuna vyuo 60 ambavyo wanaweza kuvitumia kuwapa wakulima mafunzo.

Mheshimiwa Spika, tumeona mafanikio ya wakulima wa mpunga waliopewa mafunzo kwenye vyuo vya *KATC* na Mkundi na ninahakika kwamba mafanikio kama hayo yanawezekana kwa mazao mengine iwapo wakulima watapatiwa mafunzo. Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika ishirikiane na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na watoto kuweka ratiba ya kutumia *FDCs* kikamilifu kuwapa wakulima mafunzo.

Mheshimiwa Spika, matatizo ya kilimo yanajulikana na ufumbuzi wake unajulikana. Kinachokosekana na dhamira ya dhati ya kuendeleza kilimo. Bila ya kukipa kilimo rasilimali za kutosha, tusitegemee miujiza!

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MARIAM S. MFAKI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wa Wizara kwa kuandaa hotuba hii imeonyesha mwelekeo wa kilimo.

Mheshimiwa Spika sasa naomba nichangie mambo yafuatayo; kwanza ni miradi ya maji inayofadhiliwa na fedha za benki ya dunia bila ubishi nayo imekuwa ni tatizo. Kwa maelezo ya Serikali ni kwamba Halmashauri nyingi zinashindwa kukidhi vigezo vinavyotakiwa. Naishauri Serikali kuteua angalau afisa mmoja katika ofisi ya Kilimo Mkoa ili ashirikiane na Halmashauri zote mkoani ili wasifanye makosa katika kuomba fedha hizo.

Mheshimiwa Spika, naomba kupata ufafanuzi kutoka katika Serikali kwa sababu katika jedwali linaloonyesha hali ya hewa na mazao yanayofaa katika eneo hilo na kwamba Dodoma katika Kitongoji cha Chadulu ndio imeonekana maana yake nini ina maana ndio Mkoa mzima au vipi? Hata hivyo tunayo maeneo ambayo yanalimwa mahindi, mtama, uwele, alizeti, Karanga kwa wingi na kadhalika, tunaomba Serikali itupe mwelekeo wa hali ya hewa na mazao stahiki.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara kwa kuamua kuanzisha benki ya wakulima ambayo itakuwa mkombozi kwa wakulima. Naomba Serikali ieleze utaratibu mzima wa uanzishaji wa benki hiyo na lini itaanza. Kufanya hivi ni kuwawezesha wananchi kujiandaa hata kama ni kwa kununua hisa na muhimu ni kuharakisha sheria iletwe mapema Bungeni.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali itusaidie wananchi wa Mkoa wa Dodoma kuhusu matumizi ya mbolea za viwandani kama zinaweza kutumika Dodoma kutokana na mvua chache zinazonyesha na sisizo na mtawanyiko mzuri.

Mwisho naomba nitoe angalizo kwa matumizi yatakayoidhinishwa na Bunge leo kwani wananchi wanachotaka ni kuona vitendo na wala hawatahesabu usimamizi wa viongozi kwa kufanya safari nyingi zisizo na matendo ndio mafanikio. Wananchi waliopo sasa ni waelewa na wanachunguza kazi inayosimamiwa na Serikali kama fedha ilizotengwa zinalingana na kazi au miradi iliyokusudiwa. Wanapoona kuna tofauti wanalalamikia Wabunge wao.

Mheshimiwa Waziri, naomba Wabunge angalau tusaidiwe kupewa orodha ya miradi, fedha zitakazotumika katika vijiji gani na ratiba ya utekelezaji wa miradi. Naomba suala hili muhimu na vile vile kuna utaratibu wa shamba darasa vielezwe faida yake, gharama yake na vimewanufaisha wananchi wangapi wamefaidika.

Mheshimiwa Spika, suala la kuchimba mabwawa ya umwagiliaji ni muhimu sana hasa kwa sisi wa Mkoa wa Dodoma tunaomba fedha zilizotengwa zifanye kazi iliyokusudiwa bila senti hata moja kuvuja. Sisi Wabunge tutakuwa karibu sana.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. CLEMENCE B. LYAMBA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara kwa kuandaa Bajeti aliyoiwasilisha Mheshimiwa Waziri vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutambua juhudi kubwa ambazo Waziri Mheshimiwa Stephen Wasira na wasaidizi wake wamezionyesha katika utendaji wa kueneza elimu na huduma muhimu zinazolenga kuinua uzalishaji na ubora wa mazao ya chakula na biashara.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi nilizozitoa kwa dhati napenda kumjulisha Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika kuwa wakulima wa miwa na wenye viwanda vya kuzalisha sukari wana malalamiko makubwa ambayo sina hakika kama anayafahamu. Malalamiko yao yanahusu ukiukwaji wa vibali vinavyotolewa na Serikali vya kungiza sukari nchini kunakofanywa na baadhi ya wafanyabiashara wasio waaminifu, ukiukwaji huu husababisha ushindani usio wa haki baina ya wazalishaji wa sukari na wakulima wa miwa dhidi ya wafanyabiashara wanaoingiza sukari ya kawaida, nyingi nchini, kutoka nje ya nchi, na kuiuza kwa bei ya chini zaidi kuliko bei halisi ya sukari inayozalishwa nchini, kwa kuzingatia *fair cost of production.*

Mheshimiwa Spika, kitu kinachotokea ni kwamba baadhi ya wafanyabiashara hupewa vibali vya kuagiza *refined sugar* (sukari safi nyeupe) kwa lengo la kuitumia kama *raw material* kwa utengenezaji wa bidhaa nyingine. Vibali hivi huambatana na punguzo la ushuru wa 10%. Hili halina tatizo.

Mheshimiwa Spika, cha kushangaza ni kwamba baadhi ya wafanyabiashara wasio waaminifu, huagiza na kuingiza nchini sukari ya kawaida inayofanana na sukari inayozalishwa nchini, badala ya kuagiza na kungiza *refined sugar* kwa mujibu wa vibali vilivyotolewa.

Mheshimiwa Spika, ukiukwaji nilioueleza husababisha viwanda vya sukari nchini kushusha bei ya sukari yao chini zaidi ili iuzike. Kwa kuwa viwanda huwalipa wakulima wa miwa kwa uwiano wa bei ya sukari inayotawala katika soko, hivyo bei ya miwa ya wakulima hupunguzwa *accordingly in proportion to* bei ya sukari iliyoshushwa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hii wakulima wanapata hasara ambayo chimbuko lake ni ukiukwaji wa masharti ya vibali vyao vya kuagiza sukari kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, namuomba sana Mheshimiwa Waziri, wakati akiwasilisha hotuba ya majumuisho ya hoja za Wabunge alifahamishe Bunge lako Tukufu kama analifahamu tatizo hili na hatua zitakazochukuliwa na Serikali sasa baada ya taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha na uchumi alipokuwa anajibu hoja za Wabunge baada ya kuwasilisha Bajeti yake alikubali kimsingi hoja niliyotoa ya kuiomba Serikali iondoe *VAT* katika gharama kwa wakulima wa miwa, za kukata, kupakia na kusomba miwa, namwomba Mheshimiwa Waziri wa Kilimo asaidie kwa kushirikiana nami, kumwomba Waziri wa Fedha awasilishe marekebisho ya *Schedule II* ya sheria ya *VAT* ili kukidhi kuondolewa *VAT* katika huduma tajwa hapo juu.

Mheshimiwa Spika, marekebisho haya yakifanyika kabla ya kumalizika kwa Mkutano wa Kumi na Mbili yatakuwa yamewaletea wakulima unafuu mkubwa hasa ikizingatiwa kuwa kwa mUda wa miaka mitano wamekuwa wakitozwa *VAT unfairly* kwa huduma tajwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango huu na kwa kutegemea Mheshimiwa Waziri atatoa ufafanuzi niliouomba, naunga mkono hoja mia kwa mia.

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumpongeza Waziri, Naibu Waziri kwa hotuba nzuri yenye ufasaha. Aidha, napenda pia kumpongeza Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo kwa maandalizi mazuri ya hotuba hiyo.

Mheshimiwa Spika, wawekezaji katika sekta ya kilimo, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 inasema kuwa Serikali itatilia mkazo uwekezaji wa kutoka ndani na nje katika mashamba makubwa ili kuongeza uzalishaji katika kilimo. Miaka 10 iliyopita, wakati Serikali inabinafsisha Kampuni ya Sukari ya Kilombero, ilifanya hivyo bila kuhakiki mipaka ya shamba. Ndani ya shamba hilo, Serikali wakati wa *operation* vijiji iliwaweka wananchi katika vijiji vya Nyange, Magombera na *Msolwa station.*

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya *ILLOVO* ambayo ndiyo iliyonunua shamba hilo, ilipitia mipaka hiyo upya na kugundua kuwa vipo vijiji ambavyo viko ndani ya eneo la shamba. Baada ya majadiliano na Serikali ilikubaliwa kijiji cha Nyange, wananchi waendelee kuishi lakini wale wa Magombera watoke jambo ambalo lilileta usumbufu mkubwa kwa wananchi. Aidha, ilikubaliwa eneo la hekta 1976 ambalo ni eneo lao la Kijiji cha Nyange, lifidiwe na ardhi nyingine katika kijiji cha Mbingu katika bonde la mto Ruipa.

Mheshimiwa Spika, tarehe 4 Julai, 2008 hapa Dodoma, nilishudia Shirika au Mamlaka ya Ustawishaji wa Bonde la Mto Rufiji *(RUBADA)* wakitiliana sahihi na Kampuni ya *Infenergy Tanzania Ltd.* katika kuendeleza shamba la *KOTACO* ambalo halijaendelezwa kwa zaidi ya miaka 16. Lakini katika kutiliana sahihi palijitokeza tatizo la kitongoji cha Mbasa katika Kijiji cha Lukalongo.

Mheshimiwa Spika, mwaka 1974 wakati wa operesheni vijiji wananchi wa kitongoji cha Mbasa waliombwa na Serikali kuhamia makazi ya Kijiji cha Mchombe ili kuilinda reli ya *TAZARA*, ila kitongoji cha Mbasa kilibaki kama eneo la mashamba yao. Wakati wanapima shamba la *KOTACO* mnamo mwaka 1977, wapimaji hawakuzingatia kitongoji cha Mbasa na wakakipima kama eneo la shamba. Tulikubaliana tarehe 4 Julai,

2008 na *RUBADA* kuwa kitongoji hiki kibaki kwa wananchi ya Mbasa na utaratibu ufanywe wa kupata eneo mbadala nje ya kitongoji hiki ili kufidia ardhi hiyo.

Mheshimiwa Spika, hiki ni kitongozi cha asili na hapa ningependa wa-*declare interest* kuwa mimi nimezaliwa kitongoji hicho na Marehemu baba yangu alizaliwa katika kitongoji hicho mwaka 1922. Naomba Wizara iwasisitize *RUBADA* kutobadili makubaliano ya tarhe 04 Julai, 2008 ili kuleta mahusiano mazuri kati ya mradi wa wananchi ambao wanazunguka shamba hilo. Kutozingatia hilo kutaleta usumbufu kwa wananchi ambao ni sehemu ya mradi kwa sababu wao wanatakiwa kufaidika na utaalamu wowote utakaoletwa na wawekezaji hao. Naomba Waziri atakapokuwa anajumuisha hotuba yake, awahakikishie wananchi wa kitongoji cha Mbasa katika kijiji cha Lukolongo hawatahamishwa kutoka kitongoji chao cha asili, kama ilivyokubaliwa kati ya *RUBADA Iferergy* na mimi Mbunge wao tarehe 04 Julai,2008.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *Agro Processing Industries*, uwekezaji na uzalishaji wa mazao yawe ya chakula au bishara ni vizuri yauzwe yakiwa na ongezeko la thamani. Tunatakiwa sehemu ya uzalishaji, tuuze mchele badala ya mpunga, tuuze unga badala ya mahindi au ngano. Wakati Wizara inasimamia uwekezaji kwa ajili ya kuongeza uzalishaji na tija, napendekeza Wizara ishirikiane na Wizara ya Nishati na Madini ili miundombinu ya umeme iwepo pale ambapo uwekezaji wa mashamba makubwa upo.Kwa mfano katika Wilaya yangu kuna mashamba makubwa matano ambayo hanaya umeme kwa ajili ya kuanzisha viwanda vya kusindika mazao.

Mheshimiwa Spika, katika barabara ya Ifakara – Ngalimira kuna mashamba yafuatayo, Gereza la Idete ekari 10,000 zao la Mpunga, shamba la Tuipa ekari 20,000 zao la Miwa, shamba la *Rubada/Infenergy* ekari 5830 zao la Mpunga, shamba la JKT Chita ekari 6,000 zao la Mpunga na shamba la Mpunga ekari 10,000 zao la Mpunga.

Mheshimiwa Spika, mashamba hayo yote haya na miundombinu ya umeme licha ya kuwa karibu na vyanzo vya umeme vya uhakika vya Kihansi. Huwezi kuwa na mashamba makubwa bila kuwa na karakana za kutengenezea zana za kilimo. Huwezi kuwa na karakana bila kuwa na umeme. Bila kuwa na miundombinu ya umeme, viwanda vinavyosindika mazao haviwezi kuwepo. Kifaa kilichoharibika cha trekta lazima upeleke mbali kwa ajili ya kazi ndogo kama ya kuchomelea.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo wakati zinapotokea fursa za uwekezaji basi Wizara hii ishirikiane na Wizara nyingine kama ya Nishati na Madini, Miundombinu ya barabara ili vyote vitoe mchango katika uwekezaji uliopo. Miumbombinu ya barabara itasaidia kupeleka mazao yaliyosindikwa kwenye soko kwa urahisi.

**MHE. MAIDA HAMAD ABDDALLAH:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa taarifa yake, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, wataalam pamoja watendaji wote wa Wizara hii walioshiriki kuandaa hadi kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Wizara kuandaa taarifa hii bado nchini tumekabiliwa na changamoto kubwa za uzalishaji zaidi wa mazao ya kilimo. Juhudi za

ziada lazima zifanyike ili wakulima waweze kulima mazao ya chakula na biashara ili kuondokana na umaskini uliokithiri na kuweza kujikimu wakati wa njaa.

Mheshimiwa Spika, Serikali lazima iongeze elimu kwa wataalam wa kilimo kwa kubuni wenyewe mbinu za kupata mbegu bora hapa nchini. Serikali iandae mikakati ya ziada ya kusambaza mbegu bora kwa njia ya ruzuku ili kumwondolea mkulima usumbufu wa kutafuta mbegu.

Mheshimiwa Spika, wataalam waache tabia ya kukaa sehemu moja na kusambaa kote nchini kuwaelimisha wakulima kuondokana na kilimo cha kizamani. Serikali kusimamia ipasavyo vijana wanaokimbilia mjini wakiwa hawana kazi yoyote, kurudi vijijini kwenda kuungana na wazazi kuwasaidia katika kilimo na Serikali kusimamia wakulima kuwezeshwa mbegu, mbolea na dawa kwa njia ya ruzuku ili kuondoa malalamiko yaliyopo kuwa ruzuku haiwafikii wakulima.

Mheshimiwa Spika, pia kuweka mikakati ya ziada kuwa mkulima atakayezalisha zaidi Serikali kumuandalia zawadi ili kutoa motisha kwa wakulima bora nchini. Pia Serikali kununua mazao ya wakulima wanaozalisha kwa wingi kuweza kuweka akiba kwa mikoa ambayo inaathirika kwa ukame na kuendelea kuwashawishi wakulima kulima mazao yanayoendana na hali ya hewa iliyopo sehemu walipo wakulima.

Mheshimiwa Spika, kuzishawishi taasisi binafsi kuwekeza katika kilimo na kujenga miundombinu ya umwagiliaji katika sehemu husika. Tanzania tunalo eneo kubwa linalofaa kwa kilimo ni vyema Serikali ikaweka mkakati wa muda mrefu angalau 50% ya eneo hilo liwe limelimwa hii itaondoa umaskini kwa haraka sana. Serikali kuweka mkakati wa wataalam kuzalisha mbegu zaidi kwa ajili ya wakulima wote nchini.

Mheshimiwa Spika, pia utekelezaji ufanyike kwa mwaka huu wa fedha 2008/2009 kwa utaratibu uliowekwa wa kugawa mbolea ya ruzuku. Serikali kujiandaa ipasavyo hatua kwa hatua kuondokana na kilimo cha jembe la mkono ili kuwaondolewa usumbufu wakulima waliochoshwa na kilimo hicho.

Mheshimiwa Spika, kilimo cha mboga mboga na maua kiimarishwe zaidi wakulima wapatiwe fursa zaidi kuweza kuuza nje. Katika juhudi za kuimairsha zaidi mkulima ni vyema Serikali kuwekeza katika viwanda ili kumnyanyua mkulima kimapato.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya machache naunga mkono hoja.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, naomba kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na wafanyakazi wa Wizara hii muhimu. Naomba majibu kwa yafuatayo.

Mheshimiwa Spika, ni wazi kabisa wakulima wa zao la pamba wataongeza zao kama bei inaweza kuwa ya uhakika na inakidhi gharama za uzalishaji. Aidha, Serikali ni kimbilio la wakulima katika kupata ushauri juu ya bei. Mtindo wa sasa wa kuarifu

wakulima wakati wa msimu haifai kwani watu wameshalima na kuingia gharama halafu wanaelezwa bei pungufu. Serikali ina vyombo vyote vya kuwezesha kuuza pamba mapema *(forward sales)* na uwezo hata wa kuweka kiwango cha bei ya fedha za kigeni *(forward purchase of all foreign currency)* zitokanazo na pamba. Aidha, Serikali inaweza kuhakikisha kuwa vyombo vya kibenki vinavyoweza kukopesha badala ya kuwa na benki moja tu *CRDB* inayokuwa pia na mamlaka ya bei. Mkulima hana msaada juu ya bei – Serikali iangalie jambo hili na ichukue hatua na usikimbilie maamuzi ya kisiasa kama ushirika kama jibu.

Mheshimiwa Spika, malengo yasiyo ya chakula kama karanga, ufuta, Serikali iondoe amri ya kutouza nje. Kwa nini sasa yaoze na hakuna soko la ndani la kuridhisha?

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Napenda kuiomba Serikali kuangalia upya suala zima la kuongezeka kwa uzalishaji wa miche bora ya kahawa, bila kuwa na mashamba maalum *(individually or collectively)* inayoyafuatilia kuhakikisha matokeo mazuri ya uboreshaji huu.

Mheshimiwa Spika, wananchi/wakulima wanahamasishwa kuchukua miche bora ya Kahawa na kweli wanachukua. Lakini kwa mtazamo wangu, ukiacha kila mkulima achukue tu miche anayotaka mfano, huyu atachukua miche 10, mwingine 40, mwingine 100 labda na mwingine achukue 500. Swali hapa ni je, utafuatilia vipi wakulima wa hivi? Na je, ufanisi hapa una asilimia ngapi?

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali, iwatambue na iwashawishi wakulima wapande kwa wingi na miche bora katika shamba moja. Ni vema kiwepo kiwango cha miche mkulima mmoja kuchukua. Ingefaa, wakulima hao wakajulikama, mashamba yao yakakaguliwa ili matokeo ya miche hii yaonekane. Lengo ni kuboresha ongezeko la kilimo cha buni/kahawa mavuno bora katika ekari na ku-*improve* muda wa kuzalisha. Nashauri hili lifanyike.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuiomba Serikali ieleze katika Bunge hili ni kwa kiwango gani Serikali imetekeleza ahadi ya Rais Mheshimiwa Jakaya Kikwete, aliyoitoa wakati wa Kampeni zake aliposimama pale Kamachumu mwaka 2005. Nakumbuka alitamka kwamba zao la kahawa tunaelewa tatizo lake. Tupeni kura, tutaboresha bei na upatikanaji wa soko la uhakika la kahawa. Hili litolewe maelezo, tangu 06 Julai, 2008 na sasa mwaka 2008/2009, bei ya kahawa inayoambatana na upatikanaji wa soko la kahawa ikoje?

Mheshimiwa Spika, naamini ongezeko dogo la kilimo cha kahawa (japo miche ni bora) itatolewa bure unakuta muitikio ni mdogo. Tatizo ni bei ndogo ya kahawa. Pamoja na mashine zilizonunuliwa katika vyama vya msingi ili wakulima wakoboe kahawa, lakini kinachoongezeka ni kazi, bei haijaongezeka vizuri.

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri ajibu hoja yangu anapo-*wind up* jioni, maana nitasimama kutaka maelezo. Naomba Mheshimiwa Waziri ajiandae kunipa jibu la

ongezeko lipo/halipo kwa kiasi gani la bei ya kahawa za Mkoa wa Kagera, hasa chini ya Chama cha Ushirika *KCU.*

Mheshimiwa Spika, lingine naomba Serikali iwe makini na udhibiti wa njaa. Njaa kali inashinda vita.

Mheshimiwa Spika, ni kweli wote tunasikia habari ya ongezeko la bei ya chakula duniani hata kwenye masoko yetu hapa nchini bei imekuwa kubwa. Hali hii inatishia kuwepo kwa njaa. Hivi kinachofanya Serikali kutohakikisha kila mwenye uwezo wa kufanya kazi anazalisha mali na anachangia upatikanaji wa chakula ni nini? Hivi Serikali imejaribu kujiuliza ongezeko la vijiwe hata vijijini kuwa moja ya sababu ni kuwa na kizazi cha sasa ambacho hakitaki kuzalisha bali wanataka kula na lazima wale.

Mheshimiwa Spika, Serikali baada ya kuzuia wakulima wasiuze chakula nje, ikikusanye, ikinunue na ikiweke katika akiba yake. Kinachofanya wakulima wauze ni kujikimu! Sisi wote tunajua wakulima kipato chao ni katika mazao waliyozalisha, sasa unapozuia huyu mkulima asiuze unataka apate wapi mahitaji yake?

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali isiangalie kuzuia chakula kisiuzwe eti kuzuia njaa, wakati huo huo mkulima hajui atapata wapi mahitaji yake. Serikali itenge pesa za kununua mazao hayo mara tu yanapoiva badala ya kuwachia walanguzi ambao kwa vyovyote wamewapunja wakulima.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali iwaangalie vijana wengi wa Jimbo la Muleba Kaskazini ambao wana mashamba makubwa ya mananasi hasa kata za Muhutwe, Kata ya Izigo, Kata Ruhanga jinsi wanavyolima mananasi halafu wanahangaika na soko. Unataka kijana ashinde anakimbiza nanasi mkononi ili kuuza! Hii haiwezi kuondoa umaskini wetu hasa kwa vijana ambao ni Taifa la leo na kesho.

Mheshimiwa Spika, vijana wangu wako tayari kujiunga pamoja wakipata uhakika wa kusaidiwa kupata angalau kimashine kidogo cha kukamulia matunda na kuyatunza ili yauzwe kwa bei nzuri. Pia yanaweze kuuzwa hata mbali na pale walipo, lakini vyovyote vile itawapa tija nzuri na ajira mpya zitapatikana.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Spika, pongezi kwa kazi nzuri wanazozifanya katika Wizara ya Kilimo. Naomba maelezo na ufafanuzi kwa nini Wizara hii haianzishi Benki ya Wakulima ili kuwafikia wananchi wengi vijijini badala ya kupitia kwa mawakala wa mfuko wa pembejeo ambao wamegeuka kuwa walanguzi wa wakulima maskini.

Mheshimiwa Spika, Wizara itutafutie mwekezaji atakayewekeza katika uchimbaji wa *phosphates* Mpanda, kijiji cha Kapalamsenga ili Mkoa wa Rukwa tupate mbolea ya kutosha, mimi niko tayari kushirikiana na mwekezaji wa aina hiyo. *Green Revolution* hawezekani kama hatutawekeza zaidi fedha kama India, Misri na nchi nyingine walivyofanya. Tusiandike kwa nadharia pekee, twende sasa.

Mheshimiwa Spika, ni aibu kwa Nyanda za Juu Kusini kutegemea mbegu ziendelee kupatikana toka Arusha na Kilosa wakati yapo maeneo katika Mkoa wa Rukwa yangetoa mbegu bora. Nimewahi kukuomba Mheshimiwa Waziri shamba langu lililopo Katuka uniunganishe na Makampuni ya Mbegu ili tuzalishe mbegu katika Mkoa wa Rukwa badala ya kutoka nje.

Suala la umwagiliaji mashamba Nyanda za Juu Kusini usifanyike Kikanda badala yake ufanyike kimkoa ili wataalam waweze kuwa ni wale wa Mkoa unaohusika. Wizara iendelee kusomesha maofisa ugani wa kutosha katika vijiji vyetu.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa stakabadhi ya mazao ghalani uendelezwe katika Jimbo la Kalambo ambao ndio wazalishaji wazuri wa mahindi, alizeti, karanga na maharage. Dawa za wadudu zipatikane mapema, mbolea aina zote zipatikane kwa wakati na iwafikie wakulima vijijini na si kupeleka mijini.

Mheshimiwa Spika, kuongeza kiwango cha chakula cha akiba cha *SGR*. Tani 150,000 si chochote kwa nchi yetu isiyojitosheleza kwa chakula. Bei nzuri ya mahindi na alizeti itapatikana tu kama masoko ya nje yataimarishwa hasa kwa mkoa wa Rukwa, masoko ya Kongo, Burundi, Zambia hadi Angola. Kwa taarifa yako Mheshimiwa Waziri mazao ya Rukwa yanafika Angola na Namibia.

Kuhusu kuimarisha *SACCOS* za Rukwa na baadaye tuwe na Chama cha Ushirika. Tunaomba Wizara isaidie kupata makampuni yanayoweza kuingia mkataba na wakulima kwa mikataba maalumu na watakaotoa bei nzuri kuliko walanguzi. Zana za kisasa kama matrekta, *harvestern* na dawa za kuboresha kilimo nchini.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na dhamira njema ya kuleta mapinduzi ya kilimo, ningependa kupata ufafanuzi wa ziada ni kwa namna gani tutaleta mapinduzi iwapo fedha iliyotengwa kwa ajili ya maendeleo shilingi 20,032,832,400/= fedha za ndani tumetenga shilingi 2,516,709,000/= na kiasi kilichobakia shilingi 17,516,123,400/= toka nje, hivi kweli mapinduzi haya yatapatikana kwa kutegemea hisani ya wafadhili?

Mheshimiwa Spika, kuhusu mpango wa maendeleo ya kilimo *(ASDP)* na hasa kilimo cha umwagiliaji pale ambapo miradi imeibuliwa na kuombewa pesa hivyo basi kusiwe na urasimu usio wa lazima na utekelezaji uanze mara moja ili maeneo haya yaweze kuendelezwa.

Mheshimiwa Spika, ufanisi wa stakabadhi ghalani ni vema ukasambazwa kwa kasi hasa katika maeneo ambayo wanazalisha kama vile mpunga au mahindi na tayari vijiji vyao vina maghala yanayofaa kutunza/kuhifadhi nafaka hizo waelimishwe kuhusu mpango huo hasa Mkoa wa Rukwa ambao unayo maghala ya kutosha vijijini kwa kufanya hivyo kutakuwa tumewasaidia sana wakulima wetu ambao ni maskini sana.

Mheshimiwa Spika, mwisho uendelezaji wa zao la kahawa kule Mwese, Mpanda, kwa kuwapa ushauri wa mara kwa mara na ufuatiliaji kutoka katika kituo cha Mbozi au kwa njia yoyote ile ili mradi kilimo cha kahawa kiweze kupanuka na kuwanufaisha wananchi hao na kukuza uchumi wa Wilaya ya Mpanda.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Spika, tuongeze mbolea ya ruzuku na kupeleka kwenye mikoa yenye uhakika wa mvua. Tazama maeneo yenye upungufu wa chakula licha ya mafanikio ya asilimia 104. Iringa, Mbeya, Rukwa na Ruvuma hakuna shida au upungufu huo, ukurasa wa10 – 11.

Mheshimiwa Spika, mabonde yote nchini ni Ihefu na maghala yetu ya chakula tuyatumie kuzalisha chakula ili tujitegemee kwa chakula na kuuza nje, Rufiji, Kilombero, Pangani, Luiche, Rukwa, Mbarali, Ruvuma, Malagalasi ng'ombe wafugwe Dodoma, Singida, Tabora, Shinyanga, Mwanza na kadhalika, *need for specialization.*

Mheshimiwa Spika, tuwe na ramani ya matumizi ya ardhi nchini na tuzingatie matumizi bora ya ardhi. Jatropha au Chakula (sera haraka).

Mheshimiwa Spika, natoa pongezi, tusipuuzie maonyesho ya kilimo. Maonyesho ya kilimo ni shule kwa wakulima hivyo tuwe na ngazi mbili Taifa na wananchi vijijini. Maonyesho ya sasa ni kama *trade fair*, yapo mijini na yanawasaidia wakazi wa mijini kama *trade fair*. Nashauri ngazi nyingine iwe Wilayani (Wilaya zichukue eneo) ili wakulima wafaidike. Kuwe na mkakati wa kujenga mabwawa makubwa kama Hombolo, Mwamapuli nan kadhalika kwa kushirikiana na Wilaya au miji.

Mheshimiwa Spika, suala la kujitawala ni kujitegemea hasa katika chakula ni uhai, chakula ni uhuru, tafuteni kwanza maendeleo ya kilimo na mengine yote yatafuata. Kilimo cha kisasa ndio msingi wa uchumi wa kisasa kwa Tanzania.

**MHE. MARIAM R. KASEMBE:** Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kukushukuru wewe binafsi kwa kuongoza vizuri vikao vyetu. Pia nimshukuru Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Naibu Waziri, Katibu Mkuu, pamoja na watendaji wote katika Wizara hii bila kuisahau Kamati husika kwa kuandaa mipango mizuri ya utekelezaji wa shughuli za kilimo na ushirika kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kuchangia upungufu wa chakula unaikabili nchi yetu. Pamoja na sababu ya ukame ambao umekuwa ukijitokeza sehemu mbalimbali katika chini yetu, sababu ya pili ambayo ni kubwa na inafaa ifanyiwe kazi ni Watanzania kutowajibika kikamilifu katika kushiriki shughuli za kilimo, wakiona kwamba shughuli ya kilimo ni adhabu, au kilimo ni kazi ambayo ni watu ambao hawana ajira au kwa lugha nyepesi ni ya watu walioshindwa maisha, hili ni kosa kubwa na linafaa lichukuliwe hatua za haraka kuwaelimisha wananchi hasa wenye uwezo kama wafanyabiashara, viongozi, kuelekeza nguvu zao katika kilimo kwani wao wanao uwezo wa kuwa na zana za kisasa,

pembejeo hivyo wakaweza kuzalisha chakula cha kutosha na wakafanya biashara na nchi ikapata chakula cha kutosha kuweka hifadhi ili kusaidia wakati wa tatizo kama hili linalotukabili.

Mheshimiwa Spika, pamoja nao vile vile kundi lililobaki ambalo si wafanyabiashara/watumishi/viongozi hawa wangewekewa utaratibu mahususi wa kuwawezesha kupata vifaa vya kuwarahisishia kazi ya kilimo kama matrekta madogo madogo, majembe ya kuvutwa na ng'ombe, pembejeo na kuwasimamia kwa kutumia sheria ndogo ya nguvukazi inayomtaka kila mtu mwenye uwezo wa kufanya kazi ashiriki kikamilifu katika kulima mazao ya chakula na biashara ili kuhakikisha kila kaya kuwa na hifadhi ya chakula cha kutosha kwa kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, hili nimelizungumza kwani bado tuna kundi kubwa la watu ambao hawawajibiki kabisa katika kilimo, kilimo kisiwe hiyari kiwe ni lazima. Katika kupanua shughuli za kilimo ningependa kushauri wawekezaji ambao wanataka kuwekeza katika kilimo cha biashara wawekewe sharti la kutenga maeneo kwa ajili ya chakula ambacho kitauzwa hapa nchini ili kusaidia pia upungufu huu uliopo kwani wawekezaji hawa wanachukua maeneo makubwa ambayo wanaweza kulima mazao ya biashara na chakula, naomba ushauri huu uzingatiwe.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la pembejeo hasa katika Mkoa wa Mtwara. Suala la pembejeo kwa mkoa wetu bado ni tatizo kubwa sana kwani pembejeo ni bei kubwa sana, hazifiki kwa wakati na hazitoshelezi kabisa hivyo tunaiomba Serikali kuangalia uwezekano wa kuwa na mpango maalum wa kuagiza na kusambaza pembejeo mapema zaidi, kwa Mtwara ingekuwa vizuri zaidi endapo pembejeo za korosho tungekuwa tunapata wakati wao msimu wa mauzo ya korosho yaani mwezi wa kumi mpaka mwezi Desemba ili mkulima aweze kununua na kuhifadhi pembejeo zake na ifikapo mwezi wa nne na wa tano mkulima aanze kupuliza korosho kwa wakati akiwa na uhakika wa pembejeo za uhakika.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la ubanguaji wa korosho kwa mtu mmoja mmoja au vikundi na kazi hii hufanywa zaidi na akinamama ambao hubangua korosho kwa kutumia utaalam wa chini sana (kienyeji) hivyo ningeiomba Serikali iweze kuwasaidia akimamama kwa kuanzisha viwanda vidogo vidogo ili kuwawezesha kubangua kwa urahisi na kuzalisha kwa wingi ili waweze kuuza kwa bei nzuri na kuongeza kipato hivyo kuwaondolea umaskini akina mama hawa na vijana.

Mwisho, naiomba Serikali mipango yote iliyopangwa kutekelezwa katika Bajeti hii ya mwaka 2008/2009 ili ifikapo Bajeti ya mwaka 2009/2010 tuweze kuona ni jinsi gani tumeweza kumsaidia mkulima na hali ya chakula iweze kuongezeka.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

**MHE. SALUM KHAMIS SALUM:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa bei ya dola imekuwa na mtindo wa kushuka kila inapofika msimu wa ununuzi wa pamba. Je, Waziri haoni kuwa bei ya pamba inashuka kwa zaidi ya shilingi 100 kwa kilo moja ya pamba? Bei ya dola hadi Mei ilikuwa shilingi 1250/= leo bei ya dola 1150 tofauti hii ndio inayofanya bei ya pamba mwaka huu kuwa shilingi 450/= hivyo naomba tuzungumze na *BOT* warejeshe dola 1200 ili bei ya pamba iwe zaidi yashilingi 500/=.

Mheshimiwa Spika, ahsante na naunga mkono hoja.

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze na kuwapongeza, Waziri pamoja na Naibu Waziri na watendaji wote kwa Bajeti nzuri yenye matumaini kwa wakulima wetu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuuliza Wizara hii ni kwa kiwango gani tafiti mbalimbali za kilimo zimewafaidisha wakulima hapa nchini. Kumekuwepo na tatizo kubwa sana la matumizi mabaya ya taarifa hizi ambapo badala ya taarifa hizi kuwafikia wananchi zimekuwa zikiandikwa na kufahamika kwa wataalam tu badala ya kwenda kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, hali hii imekuwa ikifanya wakulima wetu kutokana na *up date* na aina mbalimbali za mbegu au mipango mizuri ya kilimo na matokeo yake wamekuwa wakilima bila kuwa na ufahamu wa aina mpya za mbegu ambazo zingeweza kuboresha mavuno yao. Kadhalika lipo suala la utafutaji wa masoko.

Mheshimiwa Spika, yapo mazao mbalimbali ambayo yanaweza kuota hapa nchini na yana bei kubwa katika soko la dunia. Je, ni kwa kiwango gani Wizara imeweza kufanya utatifi wa aina hiyo ya mazao ili kujua bei zake katika soko la dunia ni imefanya uhamasishaji wa kulima mazao hayo kaika maeneo gani? Naomba kupewa jibu kuhusu suala hili

Mheshimiwa Spika, endapo kama Wizara hii ingekuwa inafanya utafiti na kujua aina ya mazao yenye bei nzuri ingeweza kusaidia wakulima kulima mazao kulingana na soko.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ina eneo kubwa sana linalofaa kwa kilimo. Naomba kuuliza hivi Serikali haioni umuhimu wa kutumia vijana waliopo katika mafunzo ya kijeshi ili waweze kutumia kuzalisha chakula katika maeneo ya mabonde na maeneo mengine. Wizara hii inaweza kuzungumza na Wizara ya Ulinzi kuangalia uwezekano mzuri wa kuwatumia vijana hawa kusaidia katika uzalishaji wa chakula hasa ikizingatiwa kuwa wanajeshi wetu wana nafasi ya kufanya kazi za uzalishaji kama huo kutokana na kuwepo na amani ya kutosha hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ijaribu kufanya utafiti wa maeneo hasa mabonde mazuri yenye rutuba ili kuyagawa kwa wanajeshi hawa kwa ajili ya uzalishaji, makambi ya jeshi yapo katika maeneo mengi nchini hivyo hilo linawezekana ili kukabiliana na uhaba wa chakula hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, suala la mwisho ni uanzishaji wa benki ya wakulima naunga mkono mkakati wa Serikali wa kuanzisha benki ya wakulima.

Mheshimiwa Spika, suala linalonipa shida ni kwa jinsi gani Serikali itafanya ili kuhakikisha kuwa benki hii kama itakuwa kati ya Serikali na *private sector* je, itakuwa haitozi riba kubwa? Wasiwasi wangu ni kwamba benki nyingi zilizopo nchini zimekuwa zikiona kuwa wakulima hawakopesheki? Je, huyo mwekezaji atakayekubali kushirikiana na Serikali katika uanzishaji wa benki hiyo haitakuja kubadilika hapo baadaye? Ataridhika kwa katika benki ambayo haiweki mbele maslahi ya faida na badala yake maendeleo ya wakulima? Kwa nini Serikali isianzishe benki hiyo kwa mtaji wake 100%?

Mheshimiwa Spika, kama tatizo ni mtaji, je, haiweze kuuza hisa kwa wakulima wenyewe? Naomba majibu yatakayonitoa wasiwasi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ila nipate majibu kabla ya kushika vifungu.

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Bariadi Magharibi, ningependa kuchangia hoja ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika kwa kifupi kama ifuatavyo.

Kwanza naunga mkono hoja hii. Pili, napenda kumpongeza Waziri kwa hotuba nzuri yenye mwelekeo wa kutoa matumaini. Kupitia kwake nimpongeze pia Naibu Waziri pamoja na wataalam wote wa Wizara hiyo waliofanikisha uandaaji wa hotuba hiyo.

Mheshimiwa Spika, sote tunakubaliana kwamba kilimo chetu hapa nchini bado ni duni na ukuaji wake bado ni mdogo sana, ukuaji wa sekta hiyo uko chini sana 4% pamoja na jitihada za Serikali za kuboresha uchumi *growth of about 6 – 7%* ikilinganishwa na miaka ya 1980 na 1990, bado ukuaji huo wa uchumi si wa kuridhisha katika kupambana na umaskini wa kipato *(income proverty).* Lazima tuongeze ukuaji wa uchumi ufike angalau kwa 8% mpaka 10% na tuchukue hatua za makusudi za kuongeza kasi ya uzalishaji na ukuaji wa uchumi na kasi hiyo tuifanye kuwa endelevu.

Mheshimiwa Spika, sekta ya kilimo ina nafasi nzuri sana ya kuchangia katika ukuaji wa uchumi wetu na hili litawasaidia sana wananchi wetu hasa wakulima vijijini. Wizara ya Kilimo ina mipango mizuri sana ya kuboresha kilimo. Nashauri mipango hiyo isimamiwe vizuri. Bahati mbaya mipango hiyo kwa sehemu kubwa imekuwa ya kinadharia tu. Mfano hai ni mpango wa kuligeuza eneo kando kando ya Ziwa Victoria kuanzia Bunda, Magu mpaka Mwanza kuwa ukanda wa kijani wa kilimo cha umwagiliaji.

Natambua na kuipongeza Serikali kwa uamuzi na kuzijengea uwezo halmashauri zetu za Wilaya kwa kupeleka rasilimali nyingi. Hata hivyo, tatizo lililopo kwa maeneo

mengi ni uwezo mdogo wa kutumia rasilimali hizo *(absorption capacity).* Programu ya kuendeleza sekta ya kilimo haikuwa na *impact* nzuri. Serikali isipochukua uamuzi wa makusudi wa kutoa mafunzo kuhusu mbinu za kuandaa mipango bora ya *DADPs* kwa Halmashauri zetu. Mbinu shirikishi zitakuwa na maana tu iwapo wananchi wetu hasa huko vijijini watajengewa kupitia Halmashauri zao uwezo wa kusimamia, kufuatilia na kuratibu utekelezaji wa *DADPS.*

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi kirefu Serikali inakuwa ikihamasisha uwekezaji katika sekta ya kilimo kwa kukaribisha wakulima wakubwa. Ukiondoa mashamba makubwa yaliyokuwa yanamilikiwa na Serikali na ambayo sasa yamebinafsishwa na yanafanya vizuri, sababu kuwa ni kutokuwa na *clear incentives* kwa sekta hii muhimu. Tuliangalie eneo hilo kwa haraka. Sababu nyingine ni ardhi yote sasa hapa nchini kuchukuliwa kwa dhana potofu kwamba ni ardhi ya kijiji. Suala hili tunapaswa tuliangalie kwa haraka maana limegeuka kuwa kero. Serikali kupitia Wizara hii ya kilimo kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi ilitolee ufafanuzi ili kuondoa makanganyiko uliojitokeza.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya nimalizie kama nilivyoanza kwa kumshukuru Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri ya Bajeti ya Wizara hii muhimu na naunga mkono hoja.

**MHE. MANJU S. MSAMBYA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na kutamka kuwa naunga mkono hoja iliyo mbele yetu ninayo machache ya kuangaliza na pia kutaka ufafanuzi toka Serikalini kama ifuatavyo, kwanza ni kuhusu mbegu za ruzuku. Kigoma ni miongoni mwa mikoa ambayo inayo mazingira mazuri ya kilimo ambayo yanajumuisha ardhi ya kutosha, hali ya hewa inayofaa kwa kilimo kutokana na kuwapo mvua zinazonyesha kwa wakati na za uhakika na nguvu kazi ihayojituma ambayo inazalisha kiuhakika.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo lipo tatizo la miundombinu ya usafiri (barabara) ambayo ni kikwazo katika kusafirisha mazao na mahitaji mengine ya kilimo kwenda na kutoka kwenye masoko. Taifa limekuwa linatoa ruzuku ya mbolea kwa wakulima, ni jambo zuri sana. Lakini ingekuwa vizuri zaidi kama Mkoa wa Kigoma ambao unayosifa ya kuzalisha maradufu mazao tangu ya chakula hadi yasiyoweza kuliwa moja kwa moja ingepatiwa mbegu za ruzuku ili waweze kuzalisha zaidi na kwa maana hiyo kuufanya mkoa huo kuwa ghala la chakula. Kuwapatia wakulima mbegu za ruzuku itakuwa ni kichocheo na hamasa kwa wakulima katika uzalishaji. Suala hili la ruzuku ya mbegu limekuwa wimbo miongoni mwa Wabunge, hususan wale watokao Kigoma. Hivi Serikali haiono kuhamasisha matumizi ya mbegu bora za ruzuku ni sawa na mbolea ya ruzuku?

Mheshimiwa Spika, Serikali inapata kigugumizi gani kutoa mbegu za ruzuku hasa za nafaka ili Taifa kupitia mkoa wa Kigoma tuachane na hali ya kulalamikia upungufu wa chakula nchini?

Suala la uhaba wa wataalamu wa ugani, tatizo la uhaba wa wataalam wa ugani ni la Kitaifa. Hata hivyo kama inavyojulikana na kama nilivyoeleza hapo juu ni kwamba Kigoma inafaaa kwa kilimo cha karibu mazao yote. Lakini wakulima pamoja na sifa ya uzalishaji waliyonayo hawana utaalamu. Wanalima kama walivyozoea. Mfano hai ni jimbo la Kigoma Kusini lenye Kata 12 na vijiji takribani 72, kuna wataalam wa ugani watatu ngazi ya kata na watano ngazi ya kijiji. Hivi kweli mapinduzi ya kijani yatapatikana kiuhakika kwenye upungufu huu?

Mheshimiwa Spika, ni vyema Wizara ikaweka mikakati ya uhakika ya kusambaza haraka wataalamu wa ugani ili kuwanusuru wakulima, kukinusuru kilimo na kunusuru uchumi wa Taifa ambao unachangiwa kwa sehemu kubwa na sekta ya kilimo. Suala La kilimo kutumia zana za kisasa (matrekta/majembe ya wanyamakazi), usemi wa kilimo ni uti wa mgongo wa Taifa letu hauna haja ya kusisitizwa sana. Taifa hili ni pamoja na wananchi wake ambao ndio wanaendeleza kilimo hicho. Wakulima hao kwa kutumia jembe la mkono watavunjika uti wa ngongo wa miili yao. Hivyo ipo haja ya kuwa na utaratibu wa makusudi wa kutawanya kilimo cha zana za kisasa kama vile wanyamakazi na matrekta. Kwa hali hiyo Serikali inawajibika kulegeza masharti ya mfuko wa pembejeo ili wakulima wakopeshwe matrekta kwa lengo la kulima kisasa na hivyo kuongeza tija. Sambamba na hiyo upo umuhimu wa kuanzisha/kuongeza vituo vya kilimo *(agro-mechanisation centres)* ili wale ambao wasio na uwezo wa kukopa/kununua waweze kukodi kulingana na mahitaji yao.

Kuhusu kilimo cha umwagiliaji, njia nyingine ya kuwezesha Taifa kuwa na uhakika wa uzalishaji katika kilimo ni umwagiliaji. Yapo maeneo ambayo kama yangepewa umuhimu tatizo la umaskini lisingekuwa wimbo bali ingekuwa historia. Mkoa wa Kigoma unayo mito mingi ambayo kama ingetumiwa kwa umwagiliaji Taifa kupitia mkoa huu lingefaidika sana. Mito hiyo imetawanyika vizuri mkoa wote na kuweka mabonde na Nyanda zifaazo kuendesha kilimo cha umwagiliaji. Miradi na juhudi za umwagiliaji ni michache/chache mkoani. Ni vyema Wizara ikaelewa kuwa ipo haja ya kuutazama kwa jicho la pekee mkoa huu katika eneo la umwagiliaji ili ajira ya kilimo ikue.

Suala la hali ya chakula nchini/duniani, baadhi ya maeneo nchini yanapata mvua za vuli na za masika. Maeneo haya ni pamoja na mikoa ya Pwani. Yapo pia maeneo yanayopata mvua moja lakini ndefu. Haya ni pamoja na mikoa ya Kati, Magharibi, Nyanda za Juu na sehemu ya mikoa ya Kanda ya Ziwa. Mtawanyiko huu unawezesha uzalishaji mzuri wa chakula. Hata hivyo kumejitokeza hali tete ya chakula duniani na nchini ambayo ndiyo kiini cha kupanda bei na hata kutia wasiwasi. Kenya wameiona hali hii hata kutuma ujumbe mzito kwa Mheshimiwa Rais alipokuwa mkoani Tanga. Wameomba kuuziwa chakula na kukubaliwa japo sio kwa idadi waliotarajia. Lakini siku moja baada ya kufanikiwa Kenya wametangaza kuuza mahindi yao nje kwa lengo la kupata kipato kikubwa kwa wakulima wao.

Mheshimiwa Spika, hivi wakulima wetu sisi hawahitaji kusaidiwa kuingia soko la nje? Wizara imemshauri vipi Mheshimiwa Rais katika kufikia uamuzi aliofikia ambao unaelekea kumkejeli mkulima wa Tanzania?

Mheshimiwa Spika, nitaomba wakati wa majumuisho Mheshimiwa Waziri anipatie maelezo yakuridhisha ni namna gani mkulima wa Tanzania amesaidiwa kwa mahindi yaliyouzwa Kenya na halafu Kenya wakamua kuuza ya kwao na yale waliyotoa Tanzania? Sio kejeli kwa mkulima wa Tanzania? Naomba maelezo sahihi.

**MHE. HAMZA A. MWENEGOHA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalam wote wa Wizara ya Kilimo, kwa hotuba nzuri sana.

Mheshimiwa Spika, hakuna ubishi juu ya umuhimu wa kilimo hapa nchini. Kwa umuhimu huo huo, ni lazima Taifa liamke sasa kwa hali ya ukosefu wa chakula na bei ya chakula kupanda duniani. Dawa kwa Tanzania ni kuwastua wananchi kwa hali hii ya hatari ili kuikabili hali hii mambo yafuatayo (kwa vile nionavyo mimi) ni muhimu Taifa bila kusita litangaze hali ya kilimo cha kufa na kupona. Hili jambo lilitumia mwaka 1974 na nchi hii ilizalisha chakula kingi sana mapaka tukauza nje, ili kuweza kuweka akiba ya kutosha ya chakula, ipo haja ya kila mkoa kuwa na akiba yake ya chakula. Ni maghala ya chakula kila mkoa tu, ambapo wananchi wa Tanzania watakuwa na uhakika wa chakula kwa bei zake pale ambapo panatokea upungufu, Serikali ikubali kuwekeza 10% ya Bajeti kama yalivyo maamuzi ya *SADC*. Hili tendo litatupa usalama mkubwa wa chakula. Nchi yenye njaa usalama wake kiutawala ni kidogo sana na kwa makusudi kabisa Serikali iwezeshe wananchi kwa mikopo rahisi na isiyo na riba kwa zana za kilimo na mbolea. Hapa lengo kubwa ni kumwimua mkulima na kuinua kilimo katika nyanja zake zote.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nizungumzie kilimo katika Jimbo langu la Morogoro Kusini, katika wilaya ya Morogoro vijijini tunashukuru kwa Wizara hii kutupa mradi mmoja wa kumwagilia katika kijiji cha Kongwa.

Mheshimiwa Spika, watu wa Morogoro Kusini wanataka sana mapinduzi ya kilimo. Lakini mkulima anayetaka kuendelea anahitaji nyenzo bora na elimu ya kutosha. Wakulima hawa hawana elimu wala maafisa ugani wa kuwaelekeza juu ya kilimo bora.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la masoko ya mazao. Wizara imeagiza wananchi walime pamba na ufuta na kadhalika, pamba imelimwa sehemu mbalimbali, lakini hadi sasa pamba haijanunuliwa. Tunaomba pamba ya mwaka huu ikanunuliwe.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la zao la ufuta, wapo watu wanaonunua ufuta mweupe. Lakini cha ajabu watu hawa wanachanganya ufuta mweupe na mweusi, matokeo yake tunapata ufuta chotara na hivyo kuzalisha zao hili na kupunguza thamani ya zao hili. Tunaomba wanunuzi hawa wadhibitiwe ama sivyo wananchi watakata tamaa. Naunga mkono hoja.

**MHE. YONO S. KEVELA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Nampongeza sana Mheshimiwa Stephen Masato Wasira, Waziri wa Kilimo, Chakula na ushirika. Hongera sana, pia nampongeza sana mdogo wangu Naibu Waziri Mheshimiwa Dr. David Mathayo David, anajibu vizuri sana maswali ya Wabunge na ana uwezo mkubwa sana kiutendaji. Nampongeza Katibu Mkuu wa Wizara na Naibu wake Kaduma na watendaji wote.

Mheshimiwa Spika, kilimo kiendane na viwanda vya kusindika mazao, pia viwanda vya mbolea. Mkoa wa Iringa uwekezaji wa mbolea ya *organic* kutoka Marekani, ameonyesha nia ya kuwekeza pale Wanging'ombe – Mgelenge, Njombe, Mkoa wa Iringa. Tunaomba Serikali ishirikiane na Halmashauri pamoja na Mbunge tuweze kufanikisha. Pale patahitaji umeme wa gridi na miundombinu na hauko mbali. Taarifa nyingi ziko ofisi ya Mbunge, ofisi ya Mkuu wa Mkoa na ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Njombe na halmashauri ya Njombe kwa Mkurugenzi. Mengi yameandikwa na kutolewa na hotuba yako Mheshimiwa Waziri. Hongera sana.

**MHE. VUAI ABDALLAH KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, kwanza naipongeza Serikali ya awamu ya nne kwa uongozi wa Rais Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete pamoja na uongozi wote wa Baraza la Mawaziri waliopo sasa madarakani kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Spika, kilimo ni uti wa mgongo, kilimo ni uhai wa binadamu kwani ndio tegemeo kuu kwa nchi yetu tangu mababu hadi leo tunategemea kilimo hasa wananchi wa vijijini pia kwa upande wa Ilani yetu pia imehimiza kilimo bora kwa kila Mtanzania tuhimizane kulima pamoja na hayo yote. Naomba Serikali hasa kupitia Bajeti hii tuwe na kilimo cha kisasa kutumia utaalamu na zana za kisasa matrekta, mbolea, ardhi nzuri na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa vyakula kama Tanzania sasa tuegeke au tufanye mapinduzi ya kilimo kwa kusimamiwa na Serikali kwa makusudi kuanzia viongozi hadi wananchi wa kawaid. Basi uandaliwe mpango kabambe kupatiwa ardhi ya kilimo, mbegu za aina zote na wapatiwe wananchi ikizingatiwa ardhi na udongo wenyewe, ili tuepukanae na umaskini.

Mheshimiwa Spika, Serikali isimamie kutaka mabenki watoe mikopo *NMB*, *CRDB*, *ADB*, *NBC* na mabenki mengine kuwapa uwezo zaidi Serikali na wananchi ili waweze kulima kilimo cha umwagiliaji kwa maeneo yanayokosa mvua.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa magogoni na mimi mwenyewe naunga mkono hoja.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, mabadiliko ya mfumo wa uchumi unaonesha kuwa sekta ya kilimo sasa inachangia 26% ya *GDP*. Ukuaji umekuwa

*stagnat* kwa miaka miwili sasa. Serikali imeweka mkakati gani maalum ili kuhakikisha kuwa ukuaji wa kilimo unafikia 8% mpaka 10%. Sasa miaka mitatu ijayo ili kuhakikisha kuwa tunapunguza umaskini. Chama cha ushirika Kanyovu kule Kalinzi, Kigoma ni chama cha mfano na kinajitahidi sana kuendeleza zao la kahawa. Kuna mradi mkubwa sana ambao unaendelea hivi sasa kubakia uzalishaji wa kahawa katika tuta la Manyovu.

Hata hivyo, mahusiano kati ya bwana shamba Misuzi na Kanyovu sio mazuri, tafadhali naomba Serikali ifuatilie suala hili ili wakuliwa wa Kanyovu wasikatishwe tamaa. Mwenyekiti wa Kanyovu Alhaji Yahya Mamvisa amejitahidi sana kufuatilia suala hili. Nadhani tumsaidie ili wakulima hawa wapate bwana shamba ambaye atashirikiana na chama cha ushirika kujenga uimara wa kilimo cha kahawa.

Kuna tatizo kubwa la mbolea ya ruzuku kutofika kwa wakulima wa mkoa wa Kigoma. Mbolea takriban yote inauzwa nchi jirani ya Burundi kupitia mipaka ya Mabamba na Munanila. Ninaomba Wizara iteue Kanyovu kuwa wakala wa mbolea ya ruzuku ili iweze kufika kwa wananchi. Suala hili ni tatizo kubwa sana na wakulima wa Kigoma hawapati kabisa mbolea hii ya ruzuku.

Mheshimiwa Spika, nawatakia kila la kheri.

**MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA:** Hongera Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wa Wizara.

Kuhusu kilimo ndio uti wa mgongo unaoajiri 80% ya wananchi. Tunaomba Serikali kuu iongeze Bajeti ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika. Aidha, Wizara lazima itumie rasilimali vyema. Kuna matumizi mabaya ya fedha za *DADPS*, kwa maana ya kukosa, *value for money small projects* kule Rufiji tungeweza kununua matrekta ili kupanua kilimo katika Wilaya zetu. Dawa ya *sulphur* ya kupulizia mikorosho. Bei ya *surphur* iko juu mno sasa wakulima wa Rufiji wanashindwa kabisa kuinunua *sulphur*.

Ombi, Wizara iruhusu vyama vya msingi vya ushirika katika Wilaya ya Rufiji vikopeshe dawa ya *sulphur* kwa wakulima wa Rufiji na kisha Serikali ilipwe mikopo hiyo wakati wa mauzo ya korosho zao. Hili linawezekana na ni lazima Serikali ichukue hatua hii ili kuokoa zao la korosho wilaya ya Rufiji kwa msimu huu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu matrekta wilaya ya Rufiji, katika ziara ya Mheshimiwa Rais Wilayani Rufiji, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika ilitoa ahadi mbele ya Rais na umma wa watu pale Mloka, Rufiji kuwa baada ya kuona ardhi ya Rufiji ilivyo, lazima tupate matrekta ndipo Naibu Waziri alisema kuwa sasa Wilaya ya Rufiji, itapatiwa vituo vya kukodisha matrekta kwa wakulima. Wakulima katika Wilaya ya Rufiji wanaweza kulipia eka zao na akalimiwa mashamba yao. Serikali haipotezi chochote. Fedha zake zitarejeshwa kwa mfumo huu.

Mheshimiwa Spika, namuomba Waziri maelezo ya hatua thabiti zilizokwishachukuliwa na Wizara katika kutekeleza ahadi hii ya Rais toka katika Wizara yake (nitashika kifungu kama maelezo yake yatakuwa ya juu juu). Rufiji inahitaji matrekta mengi na Serikali isikie kilio chetu.

Mheshimiwa Spika, mwisho naunga mkono hoja kwa asilimia mia. Lakini suala la matrekta Rufiji ni suala la kufa na kupona.

**MHE. DR. MZERU O. NIBUKA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naunga mkono hoja 100%.

Mheshimiwa Spika, naomba kwa heshima kubwa mno na mimi nijiunge na wenzangu katika kuchangia hoja hii ya Wizara muhimu ambayo ni uti wa mgongo kwa vile bado tunaamini kuwa kilimo bado ndiyo nguzo yetu.

Mheshimiwa Spika, kabla sijajikita katika uchangiaji wa hoja hii ningependa kumpongeza Waziri na Naibu wake ambao ni watu makini, mahiri, wasikivu na wawajibikaji.

Mheshimiwa Spika, mimi kama Mbunge wa Jimbo la Morogoro Mjini ninao mfano hai kwani mwaka jana pale Morogoro Mjini kulikuwa na kituo cha kununulia mazao na *SGR* kwa ajili ya ghala ya Taifa ya chakula kwa bahati nzuri wakulima na wafanyabiashara wadogo wadogo waliitikia wito kwani walileta mazao mengi kiasi kwamba *SGR* waliishiwa fedha kabla mazao hayajaisha.

Mimi ilibididi nimuone aliyekuwa Naibu Waziri wakati huo Mheshimiwa Christopher Chiza na yeye alimowana Waziri ambaye ndio yeye mzee wetu Mheshimiwa Stephen Wasira. Waziri alishughulikia suala hili kikamilifu mpaka akapata fedha ya ziada na wakanunua mazao yaliyobaki mpaka yakaisha. Ninampongeza sana sana kwani haikuwa kazi rahisi.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano huo sasa ingekuwa fundisho ili Wizara itenge fedha ya kutosha ili tatizo hilo lisijirudie tena, kwa vile naamini mwaka huu tutakuwa na mazao mengi zaidi kuliko mwaka uliopita. Kujiandaa ni bora zaidi kuliko kusubiri dharura.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni kwamba nchi hii tunahangaika sana jinsi ya kuboresha kilimo ili tuvune vya kutosha ili Watanzania wajikwamue na umaskini ulio kithtiri. Lakini Mheshimiwa Rais wetu mpendwa ametangaza kuwa Mkoa wa Morogoro uwe ghala la Taifa la chakula, kwa maana hiyo huu ni mradi kamambe na mkubwa sana ambao Mkoa wa Morogoro pekee hauwezi kufanikisha, jambo hili, je, Wizara hii imejipangaje katika kusaidia jambo hili ambalo ndiyo hasa ukombozi kwa sababu zifuatazo, kwanza Morogoro ina maeneo makubwa sana ya ardhi ambayo haijalimwa, pili, ardhi ya Morogoro haihitaji mbolea ina rutuba, tatu, Morogoro inayo mito ya kutosha ipatayo 148 ambayo haikauki mwaka mzima, nne, Morogoro ni njia panda ya karibu robo tatu ya mikoa yote ya Tanzania, tano, Morogoro iko karibu sana na Bandari kuu ya Dar es Salaam na pia ipo karibu na *Airport* kuu ya Tanzania ambapo ni rahisi sana kusafirisha mazao nchi za nje na sita, Morogoro inayo mvua ya kutosha karibu mwaka mzima.

Hata hivyo nilishauliza swali hilo hapa Bungeni kuhusu Wizara, jinsi itakavyosaidia mradi huu mkubwa na nilipata jibu kwamba katika mpango huo Wizara itaanza na shilingi bilioni 105 na ipo katika *Hansard* ya Bunge, sasa je, Wizara imeshatekeleza kiasi gani mpaka sasa? Hii ni changamoto, naomba Wizara iwekeze nguvu katika mradi huu muhimu ili kupunguza tatizo la chakula nchini. Nawatakia kheri.

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu kilimo cha jatropha ambacho kimeanzishwa Kilwa na wawekezaji na Serikali kuwapa maeneo makubwa kupita kiasi, wakati hatujaona faida ya ile sehemu ya kwanza haijaonekana; nashauri maeneo haya mengine yasitishwe libaki eneo moja tu la Mavuji. Kibaya zaidi maeneo haya tayari yamepimwa na vijiji.

Mheshimiwa Spika, je, hatimiliki ya kijiji itakuwa ndani ya hatimiliki ya wawekezaji? Hatimiliki ya miaka 50 isitolewe, hawana nia ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, bodi ya mazao mchanganyiko ianzishwe haraka iwezekanavyo ili kuondoa unyanyasaji wa wakulima wa ufuta wa Mkoa wa Lindi hususan Kilwa unaofanywa na viongozi kwa kutumia jina la chama cha ushirika cha Ilulu.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa mauzo ya stakabadhi ghalani ni mzuri, tumeona wenzetu wa Mkoa wa Mtwara wakati wa msimu wa korosho. Ningependa kuelezwa huu mtindo wa chama cha ushirika cha Mkoa wa Lindi - Ilulu wa kuchukua au kukopa ufuta kwa wakulima na kuwaorodhesha majina bila kuwapatia risiti (stakabadhi) au kitambulisho kinachomsaidia kama ushahidi kwamba amekopesha kwa chama hicho kiasi fulani cha ufuta na adai kiasi fulani ni sahihi?

Mheshimiwa Spika, je, chama kikikataa kwamba hawakukopeshwa na wananchi hao au hawakukopeshwa kiasi ambacho mwananchi anakitaja katika kumbukumbu yake ili mwananchi apate haki yake, uthibitisho utakuwa nini?

Mheshimiwa Spika, napenda kupata majibu ya maswali haya. Pia natoa pongezi kwa hotuba nzuri.

**MHE. ESTERINA J. KILASI:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Stephen Wasira, Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika kwa mpango mzuri uliotolewa kwenye hotuba yake. Nampongeza Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalam wa Wizara hii kwa jitihada kubwa ambazo wamekuwa wakifanya katika kutekeleza malengo ya Serikali katika sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Mbarali naomba kutoa shukrani kwa Wilaya ya Mbarali kuwa moja ya Wilaya zitakazokuwa za majaribio ya utaratibu wa kutumia *voucher system* katika utoaji wa mbolea ya ruzuku, napongeza sana.

Mheshimiwa Spika, nina mambo machache ninayoomba ufafanuzi kama ifutavyo; Serikali katika ahadi yake ya kujenga miradi ya *scheme* za umwagiliaji zipatazo tano ili kuongezea maeneo ya kilimo Wilaya ya Mbarali yenye jumla ya ukubwa wa ekari

10,000. Katika maeneo ya Kimoni, Leturo, Ukwavira, Lyandembela kuongeza ukubwa wa shamba la Madibira Mawindi na Kapunga Chimala.

Mheshimiwai Spika, mwaka wa fedha 2007/2008 hekta 1200 zilipewa pesa kujenga *scheme* ya Uturo na Mobodega. Naomba kujua kuna mpango gani wa kuanza eneo lingine ili kuendelea kukamilisha ahadi ya Serikali, kwa sababu sijaona imezungumziwa kwenye hotuba ya Waziri. Hali ya shamba la umwagiliaji la Madibira ambalo bado lina wataalam wachache wa Serikali, hali ya shamba hili ni mbaya sana kimiundombinu, barabara, mifereji inaelekea kufa kabisa, tatizo ni kuwa wataalam hawa hawana vifaa vyovyote vya kuwasaidia wakulima wadogo walioko kwenye Ushirika *(MAMCOS)* hakuna trekta, kijiko ambacho kingesaidia kusafisha mifereji mikuu ya kusambaza maji kwenye mashamba, kinachoendelea sasa ni wakulima kusafisha ile mifereji midogo inayopeleka maji kwenya maeneo wanayolima tu. Tathmini ya ghamara za kurekebisha miundombinu ya barabara, mifereji kufikia Aprili 30, 2008 ilikuwa inakaribia shilingi milioni 800.

Naomba kujua vile vile Wizara ina mpango gani wa kuwasaidia wananchi/wakulima wa shamba hili ambao wangeweza kusindika mpunga wao kwa kutumia kinu kilichoko kwenye mradi wa Madibira kwa muda wote, tofauti na ilivyo sasa, kinu kinawashwa saa tu kwa kuogopa gharama za mafuta yanayotumika. Serikali iangalie ni vipi watakifanya kinu hiki kifanye kazi iliyotegemewa.

Naomba Mheshimiwa Waziri utembelee ili uone hali halisi ilivyo kwenye shamba hili lililosaidia kupunguza umaskini wa wananchi wa kata ya Madibira.

Mheshimiwa Spika, mpango wa stakabadhi za mazao ghalani ni mzuri sana na unasaidia Serikali kujua kiasi cha mazao yaliyopo na inakuwa rahisi kutafuta soko la mazao yaliyoko. Tatizo tulilonalo ni ukosefu wa maghala bora kwa ajili ya kufanya mpango huu ufanikiwe na kwa sababu Serikali iliahidi kusaidia kwa upande wa Moyola naomba Waziri atoe utaratibu wa usaidiaji utakuwa vipi?

Mheshimiwa Spika, *power tillers* bado ni muhimu sana naomba Serikali iweke mazingira mazuri yatakayowawezesha wananchi wa kipato kidogo kupata trekta hizi kiurahisi hasa upatikanaji wake bado ni tatizo, kwa vile si rahisi wakulima kukusanya pesa pamoja na kulipia kwa mkupuo kwa hiyo Serikali isaidie.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Wizara yote kwa ujumla kwa juhudi za kufanikisha majukumu ya kilimo nchini.

Mheshimiwa Spika, naomba kueleza machache kwenye Wizara yako. Kwanza napenda kueleza kwamba hali ya chakula kwenye jimbo langi ni mbaya sana. Tarafa ya Enduimet hawajapata mvua mwaka huu. Hali ya njaa ni mbaya sana. Naomba Serikali waangalie hali ya wananchi wasije kufa njaa.

Pili, wananchi wa eneo hilo mwaka 2006/2007 Mzungu mmoja aitwahe Bwana Luka ametumia ndege kunyunyuzia dawa ya kuua magugu kwenye shamba lake, ndege yake inapozunguka kumwaga dawa upepo ukapeleka dawa kwenye mashamba ya wananchi ambao wameotesha mazao yao. Kwa hiyo, ngano, mahindi na maharage yamekauka kwa ajili ya dawa hiyo.

Mheshimiwa Spika, malalamiko ya wananchi yamepelekwa kwa Mkuu wa Mkoa na kwa Waziri Mkuu ambaye alikuwa Mheshimiwa Edward Lowassa wakati huo mpaka sasa hakuna kilicho fanyika. Naomba Serikali wachukulie malalamiko hayo kwamba ni tatizo kubwa na ni hasara kubwa kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ya Longido kuna wakulima wa ngano *West Kilimanjaro* katika tarafa ya Enduimet, Ketumbeine na Engarenaibor lakini Serikali hawatambui kabisa wakulima hao kwa Bajeti hii. Naomba Wizara watambue wakulima hao kwa kusaidia wakulima hao. Jimbo la Longido ni Watanzania kama walioko maeneo mengine siyo kweli wote ni wafugaji kama wanavyodhaniwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara imechimba bwawa kwenye Kijiji cha Kiserian kwa ajili ya umwagiliaji, bwawa hilo halijakamilika kwani udongo bado uko ndani ya bwana na hata miundombinu ya umwagiliaji bado haujamalizika. Naomba Wizara yako waweze kuja kumalizia utengenezaji wa bwawa hilo likamilike kwani bwawa limetumia fedha nyingi sana.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho upelekaji wa chakula nchi za nje. Chakula kinachopelekwa Kenya siyo kwamba Wakenya wana njaa kubwa kuliko Watanzania, kinachofanyika Wakenya wanauza chakula chao kwa *WFP*, haiwezekani tukaruhusu wafanyabiashara wa Kenya wapeleke chakula chote kuuza Somalia, Ethiopia, *WFP* huku Watanzania wabaki bila chakula au waruhusiwe Watanzania kuuza chakula *WFP* kama hao Wakenya.

Mheshimiwa Spika, naomba nipate ufafanuzi juu ya wananchi ambao mazao yameuliwa na mzungu huyo na hakuwalipa fidia. Ahsante.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika kwa hotuba yake nzuri ya Bajeti. Nawapongeza watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri ya ujenzi wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia kama ifuatavyo; maafisa ugani walioko wilayani hawafanyi kazi yoyote ya ushauri kwa wakulima. Wakulima bado wanalima kilimo kile kile cha mwaka 1947. Hakuna anayewafuatilia pamoja na uhaba wa maafisa ugani lakini hata waliopo hawafanyi kazi ipasavyo. Pamoja na uchache wao hawana vyombo vya usafiri. Serikali inadhani wananchi watajikwamuaje kutoka katika hali hiyo ya kilimo duni? Serikali iweke malengo ya uzalishaji kwa kushirikiana na halmashauri

zetu. Viongozi wa Wizara waache umangimeza, watembelee mikoa inayozalisha mazao mengi na kutoa ushauri.

Mheshimiwa Spika, wakulima hawa benki ili wakope fedha kwa ajili ya kuendeleza kilimo. Wizara ifanye upembuzi yakinifu kwa nia ya kuanzisha benki ya wakulima.

Mheshimiwa Spika, nashauri Wizara ianzishe *SGR* kila mkoa na hata kila Wilaya ili wananchi waweze kuuza mazao kwa faida *SGR.* Naamini Wizara ya Kilimo inajua faida ya kuuza mazao *SGR* na *SGR* inunue mazao mchanganyiko; sio mahindi tu.

Mheshimiwa Spika, namwomba Waziri alieleze Bunge lako Tukufu mafanikio yaliyopatikana kutokana na kuwepo kwa *RUBADA* takriban miaka 20 sasa. Tumefaidika vipi na *RUBADA?* Jibu la Waziri litasaidia kujua kama skimu 40 zilizoanzishwa zitalisaidia Taifa.

Mheshimiwa Spika, Serikali iangalie uwezekano wa kuanzisha bodi ya mazao mchanganyiko, bodi hiyo itawasaidia wakulima kupanga bei za mazao yao.

Mheshimiwa Spika, mwisho naunga mkono hoja.

**MHE. JOEL N. BENDERA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalam wa Wizara hii kwa kuandaa hotuba nzuri sana ambayo mimi naamini ikitekelezwa kwa vitendo nchi yetu itapiga hatua kubwa sana kwenye maendeleo ya kilimo.

Mchango wangu nitauelekeza katika mambo yafuatayo, kwanza ni maafisa ugani, lipo tatizo sugu vijijini bado hadi leo wakulima walio wengi vijijini wanalima kienyeji, tatizo hili linapunguza tija. Mimi ni mkulima sana wa mahindi. Sijawahi hata siku moja kupata msaada wa afisa ugani.

Nashauri maafisa hawa wawepo kila kijiji na mtindo wa shamba darasa uimarishwe. Kilimo cha kisasa bila maafisa ugani hatuweze kuendelea na kuwabadilisha wananchi wetu. Ufanyike utaratibu wa aina yoyote ile wa kuimarisha uwezekano wa wananchi hasa wakulima katika maeneo ya Kata kupata matrekta sio rahisi kila kijiji kuwa na trekta lakini kata nzima inawezekana. Bado hadi leo hii wakulima wa eneo langu wanatumia mbegu za mahindi ya kienyeji maafisa kilimo wapige marufuku kabisa. Bila kuwa wakali wananchi hawa wataendelea kupanda mbegu za kienyeji.

Skimu za umwagiliaji za Kwangumi na Mahenge. Skimu hizi Wizara ya Kilimo wamezitelekeza. Kilimo cha umwagiliaji ndio mkombozi. Skimu hizi mbili zikiendelezwa zinaweza kuzalisha mpunga wa kutosha kulisha mikoa mingi.

Mheshimiwa Spika, naomba sana kupatiwa maelezo ya namna Wizara itakavyoelekeza miradi hii muhimu. Mmiradi ikiendelezwa wananchi wa Korogwe umaskini kwaheri kabisa.

Ushirika, kama kuna eneo ambalo Korogwe na Mkoa wa Tanga limekufa ni ushirika. Ipo haja ya kuweka nguvu kwa mkoa huu na kuhakikisha ushirika umefufuka Mkoa wa Tanga. Maafisa ushirika Tanga na hasa Korogwe wameshindwa kabisa. Hakuna dalili zozote za kuendeleza ushirika. Kazi ya ziada inahitajika kuimarisha sekta hii.

Mheshimiwa Spika, ninaiomba Wizara ifikirie namna itakavyosaidia wakulima wa Korogwe na Mkoa wa Tanga watakavyopata kiwanda cha kusindika mazao yao, hakuna masoko, matunda yanaoza, Serikali isaidie kufanikisha zao hili muhimu. Naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Sasa ni wakati wa matangazo ambayo yako katika sehemu mbili, kwanza wageni. Wageni wa Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, Waziri wetu wa Maji na Umwagiliaji, ni kama ifuatavyo; Mama Lucy Mwandosya ambaye ni Mkewe, yule pale ahsante karibu sana. Mama Joyce Mwambungu na Bwana Josephat Mwaipopo, ndugu zake Waziri, wale pale. Mama Ngusekela Manase, Shangazi yake Waziri, yule pale ahsante, karibu sana mama. Yupo pia Mheshimiwa Jacob Mwakasole ambaye ni Mheshimiwa Diwani wa Kata ya Utengule Songwe, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, ahsante sana. (*Makofi*)

Tunaye ndugu Patrick Rutabanzibwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, yule pale, ahsante sana na Naibu Katibu Mkuu, Eng. Christopher Sai, Mkurugenzi wa Utawala, ndugu Samson Fimbo, ndugu Aloyce Nyenza, Mkurugenzi wa Sera na Mipango, Eng. John Mukumwa, Mkurugenzi Huduma ya Maji kwa Jamii, Eng. Mbogo Futakamba, Mkurugenzi wa Umwagiliaji, Eng. Samuel Lupimo, Mkurugenzi wa Huduma ya Maji Kibiashara, Dr. Hassan Mjengela, Mkurugenzi Maabara ya Maji, Dr. S. Kayombo, Kaimu Mkuu wa Chuo cha Maji, ndugu Washington Mtoyaba, Mkurungezi Rasilimali za Maji, Eng. Akadi Mutalemwa, Mkurugenzi wa *DAWASA*, *Eng*. Alex Kaaya, Mkurugenzi *DAWASA*, lazima mmoja atakuwa mkubwa, naona wamekosea kuandika *DAWASCO*, *Eng*. Dr. A. Mohamed, Mkurugenzi *DDCA*, sijui ndiyo kitu gani hiki *DDCA*!

**MBUNGE FULANI:** Wakala wa Visima.

**SPIKA:** Ahaa Wakala wa Visima. Huyu Dr. Mohamed, tunamhitaji sana vijijini. Wakurugenzi wa Mamlaka za Maji Mijini, Makao Makuu ya Mikoa, sijui wako wapi, Wakurugenzi wa Mamlaka za Maji Mijini angalau wa Dodoma basi asimame. Ohoo! Ahsante sana, loo! Leo nafasi imekuwa shida ahsante karibuni sana. (*Makofi*)

Kuna Wahandisi wa Umwagiliaji wa Kanda, Maafisa Maji wa Mabonde. Loo, hizi Wizara, wafanyakazi wa Umwagiliaji Kanda ya Kati na wafanyakazi wa Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Dodoma, *DUWASA* wakiongozwa na Mkurugenzi wao. Ahsante sana. (*Makofi*)

Nafurahi pia kumtambulisha kwenu Waheshimiwa Wabunge, Balozi Msaidizi wa Ubalozi wa Marekani Dar es Salaam, Mheshimiwa *Larry Andrew Junior*. *Deputy Ambassador, we welcome you to Dodoma and we are pleased to have you as representative of one the development partners for Tanzania. Thanks for the good works that you are doing. (Makofi*)

Pia wageni wa Mheshimiwa Gaudentia Kabaka, Naibu Waziri wa Elimu na Ufundi, ni mama Rehema Muzo, ambaye ni rafiki na ni mfanyabiashara mashuhuri wa suti za kike na za kiume Jijini Mwanza. Hebu asimame tumuone huyu. Yuko mama Rehema Muzo, naomba usimame, ahsante sana. Basi Waheshimiwa Wabunge, mambo ya suti ndiyo hapo tena. *(Makofi/Kicheko)*

Halafu wageni wa Mheshimiwa Sigifrid Ng'itu, ni Viongozi wa Mfuko wa Maendeleo ya Mikoa ya Kusini, *Southern Union Development Fund (SUDF),* Bwana Hamasi Chinyaka, Mwenyekiti, yule pale karibu sana na ndugu Ali B. Membe, Katibu, ahsante, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa Abbas Mtemvu na Mheshimiwa Mwinchoum Msomi, ni Mama Stella Sozigwa yule pale, mama Aisha Chiki, Mama Khadija Njechele na Bi Scolastica Mkenjwa, hawa ni Wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya UWT Wilaya ya Temeke. (*Makofi*)

Pia kuna mgeni wa Mheshimiwa John M. Cheyo, ni Mheshimiwa Mustafa Zambia, ambaye ni Mwenyekiti wa Mkoa, *UDP* Tabora. Sijui yuko wapi huyu?

Wageni wa Mheshimiwa Meryce Emmanuel, ni Mabelana Bashide, mume wake, Eng. Bashide, yuko wapi sijui, huyo hapa ahsante sana. Tunaendelea kuwapa pole kwa matatizo ya majeruhi ya vijana, tunaamini wanaendelea vizuri, ahsante sana. *(Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa John Paul Lwanji, ni Shaban Mlekwa, Peter Kukanza na Salum Abdulhaman, Mwenyekiti, Katibu na Mjumbe, sasa sijui ni wa kitu gani lakini ni viongozi kutoka Jimbo lake, nadhani Manyoni kule, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa Madeje, wako watatu lakini hawakutajwa majina. Wageni wa Madeje, naomba wasimame, wale pale, ahsante sana. *(Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa George Lubeleje, ni wanakwaya 30 kutoka Kikundi cha Uinjilisti cha Mtakatifu Maria Chimuli, Kanisa la Aglikana Dodoma wameambatana na kiongozi wa msafara, Mchungaji Richard Toroka. Wale wanakwaya wasimame, ahsante sana. Karibuni, kazi yenu ni ya baraka sana pamoja na kuimba ni vizuri muweze kutupa nafasi na sisi Wabunge siku nyingine tuwe tunasikiliza mambo haya.

Wageni Emmanuel Luhahula, Mchungaji Elikana Gonda na mke wake, wale pale, ahsante sana na Mwinjilisti Mbise Haruni kutoka *AICT* Dodoma, wale pale, ahsante karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, ambao ni Idd Mruru, Khamis Shaka, Ali Khamis kutoka Tawi la Kibondeni Jimbo la Fuoni. Karibuni sana ndugu zetu kutoka Zanzibar. (*Makofi*)

Pia tunao wanafunzi 40 kutoka shule ya *Central Secondary,* sijui ndiyo *Kiswanglish* chenyewe hiki. Sasa shule inaitwa *Central,* sina namna. Shule ya *Central* na Walimu wao. *(Makofi)*

Wanafunzi 64 kutoka shule ya Msingi Makulu, nadhani ni hao sasa na Walimu, ahsante sana, karibuni sana. Nashukuru tunawakaribisha na kuwatakia mema katika kuendeleza masuala ya elimu. *(Makofi)*

Sasa matangazo ya shughuli za kazi. Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa, Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa, anaomba wajumbe wote wa Kamati hiyo ya *LAAC*, kwamba kutakuwa na mkutano na wajumbe wa *CPA* ya Uingereza, saa 4.45 hadi 5.30, kwenye ukumbi namba 219.

Mheshimiwa Kabwe Zitto, Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu ya Mashirika ya Umma, anaomba wajumbe hao wa Kamati hiyo, waende sasa kukutana na wale wageni wetu ukumbi ule ule namba 219. Mkutano ni saa 4.00 hadi saa 4.45.

Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, Makamu Mwenyekiti, Kamati ya Fedha na Uchumi, anahitaji wajumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi, wakutane saa 8.45 mchana katika ukumbi namba 219. Huo ndio mwisho wa matangazo ya kawaida.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya hapo, tutakapoingia katika hatua ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo kujibu hoja, tutatumia dakika 75 ambazo ni haki yake pamoja na Naibu Waziri. Kwa hiyo, ni dhahiri tukiingia na Kamati ya Matumizi haitawezekana kwa Mheshimiwa Waziri wa Maji kusoma hotuba yake. Muda utakuwa ni mfupi mno. Kwa hiyo, inavyoelekea hotuba ya Waziri wa Maji itakuwa ni saa 11.00. Nimetangaza mapema kwa sababu watu wengi wa Wizara ya Maji wako hapa sasa wasiendelee kukaa, wakipenda kusikiliza mambo ya kilimo ni vizuri lakini niliona ni vema wajue hilo ili wajipange wanavyoona.

Waheshimiwa Wabunge, naomba nitangaze kwamba leo ni sikukuu ya kuzaliwa Mheshimiwa Mathayo David Mathayo, Naibu Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika. *(Makofi/Kicheko)*

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2008/2009 – Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika

*(Majadiliano yanaendelea)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nachukua nafasi hii, kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia katika Wizara hii ya Kilimo, Chakula na Ushirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai mpaka siku hii ya leo ambapo ni *birthday* yangu, nimefikisha miaka mingi tu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, pia namshukuru Mheshimiwa Rais kwa kunirudisha tena mwezi Februari, 2008 katika Baraza la Mawaziri jipya na kuwa Naibu Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika. Ninawashukuru wapiga kura wa Jimbo la Same Magharibi kwa kunipa heshima hii ya kunileta Bungeni na leo nimesimama hapa ninazungumza. Ninawashukuru sana wana-Same, ninakumbuka shida yao ya maji, ninakumbuka shida ya umeme katika vijiji vile vyenye shida ya umeme na ninakumbuka tatizo lao la kuuzwa kwa *PADECO*.

Mheshimiwa Spika, mwisho niishukuru familia yangu kwa kuni-*support* na kunitunza mpaka leo. Nianze kwa kuunga mkono hoja hii kwa asilimia 100. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapenda moja kwa moja kuchangia hoja za Waheshimiwa Wabunge. Kuna hoja kwamba Serikali iandae mpango wa kuongeza Maafisa Ugani na wapewe vitendea kazi na mafunzo.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekwishaandaa mpango huu tangu mwaka 2007 na mpango huu ni mpaka 2011 kusudi ifikapo mwaka 2011 Maafisa Ugani 11,703 watakuwa wamekwishaajiriwa nchini kote kwa ajili ya kutoa huduma za ugani. Mwaka 2007/2008, wameajiriwa Maafisa Ugani 309, na mwaka huu 2008/2009, wataajiriwa Maafisa Ugani 1,252, Maafisa Ugani hao watapelekwa maeneo ya Vijijini, Kata pamoja na Tarafa.

Mheshimiwa Spika, vyuo hivi kwa sasa hivi vinaendelea kukarabatiwa kusudi viweze kuchukua wanafunzi na kuhitimisha wanafunzi 3,000 kwa mwaka. Vitendea kazi kama baiskeli, pikipiki na nyumba kwa kupitia *DADPs* au *ASDP*, Halmashauri zitatoa fedha hizo kusudi vitendea kazi hivyo viweze kuwepo kwa ajili ya Maafisa hao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Maafisa Ugani kupewa malengo, Serikali kwa kutumia Sheria Na. 8 ya Utumishi ya Mwaka 2002, inataka wafanyakazi kufanya kazi kwa malengo. Aidha, hakuna ajira za Mkataba Serikalini, ajira zote ni za kudumu.

Mheshimiwa Spika, suala kwamba Maafisa Ugani wa Kilimo waliopo Wizarani waende vijijini. Napenda kusema kwamba chini ya utekelezaji wa *D by D*, Maafisa wote walihamishiwa kwenye Halmashauri za Wilaya na waliobaki Wizarani ni kwa ajili ya kuandaa Sera na Miongozo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, wataalam wanaohitimu *SUA* wanafanya nini? Wataalam wanaohitimu Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, huajiriwa Wizarani, wengine wanaajiriwa TAMISEMI, lakini wengine wanajiunga na Sekta Binafsi.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Mtwara, wataalam wa kilimo hawajapandishwa vyeo kwa muda wa miaka 10. Chini ya Sheria Na. 8 ya mwaka 2002, inampa *DED* mamlaka ya kuwapandisha vyeo wataalam hao. Kwa hiyo, hili ni zoezi ambalo lipo chini ya *DED* wa Halmashauri hiyo. Namshauri Mheshimiwa Mbunge aweze kuwasiliana na *DED*.

Mheshimiwa Spika, wakulima wanaoamua kulima alizeti na karanga na kuacha mazao ya chakula. Wizara inahimiza mazao ya chakula na ya biashara. Kwa hiyo, Halmashauri zihimize uwiano mzuri wa mazao hayo ya biashara na ya chakula.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Rombo kuendeleza kilimo cha mazao ya bustani, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, itatoa mafunzo kwa wataalam wa Wilaya hiyo na vipando bora vitatoka Seriani na Tengeru na mazao hayo itabidi yaingizwe kwenye Programu za *DADPs*.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kilimo cha mazao yanayostahimili ukame, sisi Wizarani tunahimiza uzalishaji wa mazao kutokana na hali ya hewa. Mbegu za mtama kwa mfano ambazo zinahimili ukame zipo kwenye ruzuku ya Serikali. Kwa hiyo, nazihimiza Halmashauri nchini katika maeneo yale kame ziweze kutumia fursa hii. Pia Wizara inatoa mafunzo ya uchanganyaji wa chakula yaani *breeding* kwa maana ya kuchanganya mtama pamoja na mahindi ili kuweza kuongeza chakula na kuongeza wigo zaidi wa matumizi ya mtama.

Mheshimiwa Spika, kituo cha Buganga kifanywe kuwa cha Kitaifa. Kituo hiki ni cha Kitaifa na kinazalisha vipando bora na ili tuweze kukiongezea hadhi kituo hiki wananchi wanashauriwa kununua vipando vya mazao ya bustani kutoka kwenye kituo hiki. Halmashauri zitoe mafunzo ya uzalishaji wa mazao ya bustani kwa kutumia kituo hiki cha Buganga.

Mheshimiwa Spika, kodi ya ushuru ya asilimia 10 inayoondolewa kwa uingizaji wa mafuta ya kula, irudishwe. Hoja hii tumemwachia Waziri wa Fedha, lakini mimi kama mchangiaji kwa kweli na mimi ninahimiza kwamba irudishwe hii asilimia 10 ili tuweze kulinda viwanda vyetu hapa nchini, lakini pia tuweze kulinda ajira ya watu wetu hapa nchini. Tutakaporuhusu watu hawa waingize mafuta bila kulipia asilimia 10 maana yake tunaua viwanda na tunapeleka ajira nje ya nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wakati nipo Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko tulituma watu kwenda kule wanakosema wanachukulia mafuta ghafi, hayo mafuta siyo ghafi yanakuja yakiwa yapo tayari wanayauza, kwa hiyo, kodi hii tunaomba irudishwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mauzo ya maua ya nje yaliingiza kiasi gani cha fedha? Mwaka 2006/2007, mauzo ya maua yaliingiza shilingi bilioni 52.

Mheshimiwa Spika, kilimo cha mibono kuchukua eneo kubwa. Serikali kupitia Wizara yetu na Wizara ya Nishati na Madini, tunaandaa mwongozo wa mazao ya nishati na pia Wizara imekwishawaandikia Wakuu wa Mikoa kuwa waangalifu kusudi wasitoe maeneo ambayo yanafaa kwa ajili ya mazao ya chakula kulimwa jatrofa au mazao mengine ambayo ni ya nishati.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa nini wananchi wawe waangalifu au kwa nini viongozi wawe waangalifu ili wasitoe maeneo yale? Mibono hiyo au jatrofa zinaota kwenye maeneo yasiyoota kitu chochote. Sasa kwa nini yasipelekwe kule mahali ambapo hakioti kitu chochote, yanapelekwa kwenye maeneo yenye rutuba? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, siyo lazima mwekezaji pia alime hii jatrofa hata maeneo yale ambayo hayaoti kitu chochote wananchi wale waliozunguka maeneo yale wanaweza kulima kwa kilimo cha mkataba kusudi waweze kujipatia kipato. Lakini wakati huo huo wale wawekezaji wakubwa wasipewe miliki ya maeneo makubwa sana kiasi ambacho vijiji vinapungua na hata Wilaya zinapunguza maeneo yake. Lazima tukumbuke kwamba sisi Watanzania tuliopo sasa hivi baada ya miaka 25 idadi itakuwa imeongezeka kwa kiasi kikubwa sana, wale watoto wetu na wajukuu watakwenda wapi? Kwa hiyo, hilo ni suala la kuangalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia kuna kitu kinaitwa *biodiversity*, uoto na wanyama wa asali waliopo pale, mtu akishapewa ekari 100,000, 200,000 maana yake akilima pale wale panya waliopo pale, wale nyani waliopo pale, wale wanyama waliopo pale na uoto wa asili na mimea iliyopo pale na yenyewe itapotea.

Mheshimiwa Spika, hatimiliki ya miaka 50, ni umri wa mtu mzima. Tunawapa katika maeneo ambayo ni *prime area*, niseme kabisa kwamba hatukatazi wawekezaji wa mazao hayo. Nasisitiza kwamba tunakaribisha wawekezaji, lakini siyo katika maeneo ambayo yanatuhakikishia usalama wa chakula nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa leo hii tunapowapa hatimiliki ya miaka 50 tusije tukafikiri kwamba tutakuwa sawa na Zimbabwe, Zimbabwe wao hawakuwa na hatimiliki, wao ni Wazungu tu walichukua yale mashamba kwa sababu walikuwa na utawala pale. Lakini sisi tunapowapa, tayari tunajifunga kisheria baada ya miaka 50 wanaweza waka-*renew* kwa hiyo, lile eneo linakuwa siyo letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sitegemei kwa mfano maeneo yale ya *The Big Four*, yanayolima mazao ya chakula mfano mahindi, Iringa, Ruvuma, Mbeya na Rukwa, kwa kweli kuruhusu kilimo cha mazao haya. Hata Mikoa ya Pwani na Morogoro pamoja na Kigoma, ni maeneo ambayo kusema kweli yanatuzalishia chakula, siyo maeneo ya kuingiza mazao kama hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haya mwekezaji wa Mbarali na Kapunga kulima mibono. Serikali inafuatilia sana mashamba yote ambayo tumeyabinafsisha kusudi waweze kulima mazao ya chakula ambayo ndiyo walioombea mashamba yale. Mwekezaji wa Mbarali pia tulimwandikia barua kuhusiana na suala hili, nasikia siku hizi halimi.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Pembejeo, taarifa za mikopo ya pembejeo inayotolewa Wilayani na Mikoani, iwasilishwe Bungeni. Hiyo tunakubaliana kabisa, taarifa hizo zitawasilishwa.

Mheshimiwa Spika, Mfuko uongezewe pesa ili utoe mikopo ya matrekta mingi zaidi. Nakubaliana kabisa na Waheshimiwa Wabunge, kila mwaka tunavyoona kwa kutegemea na bajeti, mfuko huu utaongezewa fedha.

Mheshimiwa Spika, vikundi vipewe mkopo wa mashine, vikundi hivyo ni vya Mtwara kule, vilipewa mashine ya kubangulia korosho. Hii tunakubaliana kabisa na Mheshimiwa Mbunge na tunashauri visajiliwe vikundi hivi na vipewe mkopo kupitia Halmashauri ya Wilaya husika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kwamba masharti ya Mfuko wa Pembejeo, ni magumu na muda wa kurejesha mkopo ni mfupi. Masharti ya mfuko huu ni nafuu sana kuliko taasisi yoyote ya fedha. Kwa mfano, muda wa kurudisha mikopo hii ni miaka mitano kwa trekta, miaka mitatu kwa *power tillers* na kwa pembejeo za kawaida, ni miaka miwili. Muda huo unatosha kabisa, wakati mabenki mengine ni miaka miwili, miwili. Muda wa kuanza kurudisha mikopo yaani kuna *grace period* mtu unapewa halafu unafanya kazi halafu baadaye unaanza kurudisha mkopo, kwa trekta ni miezi sita, kwa *power tillers* ni miezi sita na kwa pembejeo ni miezi mitatu na watu wana muda wa kuzalisha kabla hawajaanza kurudisha ule mkopo. Malipo ya awali ni laki tatu, yaani *evaluation fee* pamoja na asilimia moja na *documentation fee* ya gharama ya mkopo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu masharti ya mkopo, shamba lazima liwe ekari 50, hatimiliki iliyo na dhamana isiyohamishika. Maombi yapitishwe kwa *DED* na ankara kifani iwepo inayoonyesha mchanganuo wa mradi huo na vikundi kama *SACCOS* vinaweza kudhamiwa na Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, Wizara inachukua hatua gani za kuongeza matrekta? Kwanza, tunatoa mikopo ya matrekta na tunahimiza sekta ya binafsi kuingiza matrekta. Tunatafuta mikopo yenye masharti nafuu ya ili tuweze kuingiza matrekta 500 hadi 1,000 kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, matrekta ya *graduate* yanayotoka pale *SUA*, bado utafiti unaendelea na pindi utafiti utakapokamilika kwa kutumia *SUA, CARMATEC* na NYUMBU basi sekta ya binafsi itazalisha matrekta hayo.

Mheshimiwa Spika, miamba ya *phosphate* iliyopo Mpanda na Mbeya, itumike kujenga Kiwanda cha *Phosphate,* miamba hii aina *Carbon tight,* ni migumu sana kwa kweli, ni nadra sana kwa duniani kutumia miamba hii kwa ajili ya kutoa *Phosphate* ya

mbolea. Kwa hiyo, tutaendelea kutumia *Phosphate* ambayo gharama yake ni ndogo kuzalisha mbolea.

Mheshimiwa Spika, suala la wazee na watoto, linatoka kwa Mheshimiwa Diana Chilolo, wasio na uwezo, wasaidiwe mbolea kwa utaratibu wa vocha. Hii ni *idea* lakini kwa wakati huu kwa kweli hatukuandaa utaratibu huo na tutaendelea kuangalia kama utawezekana.

Mheshimiwa Spika, usajili wa wakulima wa kahawa, kusema kweli utaratibu huu ulichelewa kutokana na ukosefu wa fedha, lakini sasa hivi taratibu zimekamilika na wakulima wa kahawa kule Mbinga watasajiliwa vizuri na kwa sasa hivi tayari Wakaguzi wawili wameshateuliwa Wilayani Mbinga kwa ajili ya kukagua kahawa wakati wa ununuzi na Bodi itaendelea kusimamia madaraja ya kahawa.

Mheshimiwa Spika, tafsiri ya asilimia tano ya ushuru wa Halmashauri, ni ipi? Mheshimiwa Waziri Mkuu, ametoa ufafanuzi mzuri sana hapa asubuhi lakini nitazungumzia ile wanayotozwa kule Moshi. Ile wanayotozwa kule Moshi, ni vile vikundi ambavyo badala ya kupitia gulio kule Mbinga ama maeneo yanayolimwa kahawa, wanachukua kahawa ile moja kwa moja kutoka kwa wakulima, kwa hiyo hawatozwi ushuru kule. Kwa hiyo, ni lazima wanavyokwenda Moshi kwenye mnada waweze kutozwa ile asilimia tano. Itakuwa kubwa kwa sababu bei za kule ni kubwa lakini walikwepa gulio la kule Wilayani, ndiyo maana inabidi waingie kwenye utaratibu huo.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, watu wanauliza kwa nini tumbaku inalimwa wakati kila mwaka Serikali inasema tusivute sigara? Tumbaku inaingizia Watanzania kwa mfano, tumbaku inawaingizia wakulima shilingi bilioni 60. Tumbaku hii imeajiri Watanzania laki tano ambayo ni sawa na asilimia 1.3 ya Watanzania wote. Tumbaku hii inaingizia Taifa asilimia 17 ya mauzo yote ya fedha za kigeni kutokana na mazao makuu. Tumbaku inaingiza shilingi bilioni 75 kutokana na kodi. Tumbaku imekuwa inaziingizia Halmashauri zaidi ya shilingi bilioni 2.3 kama *District Cess.* Tumbaku italimwa na itaendelea kulimwa mpaka tupate zao mbadala kwa ajili ya kuondoa umaskini wa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Kilimo. Sasa nitamwita mtoa hoja, Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika. Anazo dakika zisizozidi 60, kwa kuwasilisha majibu ya hoja mbalimbali za Waheshimiwa Wabunge.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nitumie nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi na vile vile niwashukuru Wabunge wote kwa kweli, waliochangia kwa maandishi, waliosema kwa mdomo na ambao hawakusema kwa kutuunga mkono. Wote kabisa nawashukuru kwa sababu

hatukupata kwa kweli hoja ambazo zilionyesha kutotuunga mkono kabisa, hata wale waliosema hatuungi mkono baadaye walituandikia kuwa wanatuunga mkono. Nawashukuruni sana kwa michango yenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimshukuru Naibu Waziri kwa kutoa maelezo kwa baadhi ya hoja ambazo ziliwasilishwa na Waheshimiwa Wabunge. Ni dhahiri kwamba muda aliokuwa nao ni mfupi na kama angeweza kutumia muda mrefu kidogo angeweza kujibu hoja nyingi zaidi. Lakini vile vile niseme kwamba Wabunge ambao wamechangia hoja hii ni wengi. Hoja ambazo zimetolewa au kwa kauli au kwa maandishi ni nyingi sana. Tuna Wabunge 17 walizungumzia hoja hii kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu na wote nawashukuru lakini nataka kuwahakikishia kwamba hoja walizozungumzia kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, tumezichukua na tunazo. Nilikuwa napitia hii orodha, nikakuta baadhi yao tena wamesema katika kipindi cha hoja ya Wizara ya Waziri Mkuu. Kwa hiyo, hawa ni wadau wetu, tutaendelea kushauriana nao ili tuone mawazo yao yanavyoweza kusaidia sekta hii muhimu sana ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, vile vile Wabunge waliotuandikia, idadi yao ni 105 na Wabunge ambao wamesema kwa kauli ni 35. Kwa hiyo, kama ningeamua nijibu kila hoja iliyoandikwa na kila hoja iliyosemwa, kwa kweli muda ambao Mheshimiwa Spika umenipa, hauwezi kutosha. Kwa hiyo, nitajitahidi kuzungumzia masuala kwa jumla na kama kuna jambo ambalo nimeombwa niliseme *specifically* kwamba Waziri jibu, basi muda ukibaki nitajitahidi kadri ninavyoweza kujibu. Lakini kabla ya hapo, niwatambue Wabunge ambao wamechangia kwa maandishi kwa sababu nitakapokuwa najibu hoja itakuwa vigumu kuwarudia kuwataja tena.

Waliotuandikia ni Mheshimiwa *Engineer* Christopher K. Chiza, Mheshimiwa Profesa Philemon M. Sarungi, Mheshimiwa Dr. James A. Msekela, Mheshimiwa Aziza Ally, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa James P. Musalika, Mheshimiwa Susan A.J. Lyimo, Mheshimiwa George M. Lubeleje, Mheshimiwa Juma Njwayo, Mheshimiwa Kilontsi M. Mporogomyi, Mheshimiwa Mwadini A. Jecha, Mheshimiwa Lucas L. Selelii, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Pindi Chana, Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mheshimiwa Hemed Mohamed Hemed, Mheshimiwa Geofrey Zambi, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela na Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Ezekiel M. Maige, Mheshimiwa Sijapata F. Nkayamba, Mheshimiwa Juma H. Killimbah, Mheshimiwa Raynald A. Mrope, Mheshimiwa Azzan Zungu, Mheshimiwa Mossy Mussa, Mheshimiwa Profesa Raphael B. Mwalyosi, Mheshimiwa Kabuzi F. Rwilomba, Mheshimiwa Margareth A. Mkanga, Mheshimiwa Juma Said Omar, Mheshimiwa Aloyce B. Kimaro, Mheshimiwa Khadija S.A. Al-Qassmy, Mheshimiwa Capt. John Z. Chiligati, Mheshimiwa Dr. Charles O. Mlingwa, Mheshimiwa Dr. Luka J. Siyame, Mheshimiwa Paul P. Kimiti, Mheshimiwa *Engineer* Stella M. Manyanya, Mheshimiwa Jacob D. Shibiliti, Mheshimiwa Yussuf R. Makamba, Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko, Mheshimiwa P. Lwanji, Mheshimiwa Bernadeta K. Mushashu, Mheshimiwa George B. Simbachawene, Mheshimiwa Dr. Festus B. Limbu, Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mheshimiwa Fuya G. Kimbita, Mheshimiwa Ahmed M. Shabiby, Mheshimiwa Magdalena H. Sakaya, Mheshimiwa Shally J. Raymond,

Mheshimiwa Eustace O. Katagira, Mheshimiwa Mhonga S. Ruhwanya, Mheshimiwa Lediana M. Mng'ong'o, Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, Mheshimiwa Dr. Samson F. Mpanda, Mheshimiwa Dr. Guido G. Sigonda, Mheshimiwa Mchungaji Getrude Lwakatare na Mheshimiwa Stephen J. Galinoma. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Paschal C. Degera, Mheshimiwa Haji J. Sereweji, Mheshimiwa James D. Lembeli, Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir, Mheshimiwa Felix N. Kijiko, Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, Mheshimiwa Suleiman O. Kumchaya, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Dr. Harrison G. Mwakyembe, Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mheshimiwa Margareth S. Sitta, Mheshimiwa Mtutura A, Mtutura, Mheshimiwa Dr. Binilith S. Mahenge, Mheshimiwa Mohamed Ali Said, Mheshimiwa Mwanne I. Mchemba, Mheshimiwa Feteh Saad Mgeni, Mheshimiwa Siraju J. Kaboyonga, Mheshimiwa Abdul J. Marombwa, Mheshimiwa Dorah H. Mushi na Mheshimiwa Gaudence C. Kayombo. *(Makofi)*

Wengine Mheshimiwa Fred Mpendazoe, Mheshimiwa Dr. Maua Abeid Daftari na kwa Dr. Maua Daftari, nataka niongeze jambo moja tu kwamba wakati napongeza walioteuliwa wakati wa mabadiliko ya mwezi wa tano yeye alipelekwa katika Wizara mpya ya Mawasiliano na Sayansi. Kwa hiyo, nampongeza kama ambavyo nimepongeza wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Charles N. Keenja, Mheshimiwa Mariam S. Mfaki, Mheshimiwa Clemence B. Lyamba, Mheshimiwa Castor R. Ligallama, Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah, Mheshimiwa John M. Cheyo, Mheshimiwa Ruth B. Msafiri, Mheshimiwa Ludovick J. Mwananzila, Mheshimiwa Amour S. Arfi, Mheshimiwa Jackson M. Makwetta, Mheshimiwa Mariam R. Kasembe, Mheshimiwa Salum Khamis, Mheshimiwa Lucy T. Mayenga, Mheshimiwa Andrew J. Chenge, Mheshimiwa Manju S.O. Msambya, Mheshimiwa Hamza A. Mwenegoha, Mheshimiwa Yono S. Kevela, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, Mheshimiwa Profesa Idris A. Mtulia, Mheshimiwa Dr. Omari M. Nibuka, Mheshimiwa Mwanawetu S. Zarafi, Mheshimiwa Michael L. Laizer, Mheshimiwa Estherina J. Kilasi, Mheshimiwa Felister A. Bura, Mheshimiwa Joel N. Bendera na ndiyo wa 105.

Wabunge 35 ambao wamechangia kwa kaul ni Mheshimiwa Gaudence C. Kayombo, Mheshimiwa Richard S. Nyaulawa, Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mheshimiwa Yussuf R. Makamba, Mheshimiwa Bujiku P. Sakila, Mheshimiwa Ludovick J. Mwananzila, Mheshimiwa Lediana M. Mng'ong'o, Mheshimiwa Hasnain G. Dewji, Mheshimiwa Ibrahim Mohamed Sanya, Mheshimiwa Basil P. Mramba, Mheshimiwa William H. Shellukindo, Mheshimiwa Pindi H. Chana, Mheshimiwa Mgana I. Msindai, Mheshimiwa Rosemary K. Kirigini na Mheshimiwa Luhaga J. Mpina. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Said A. Arfi, Mheshimiwa Anthony M. Diallo, Mheshimiwa Kidawa Hamid Salehe, Mheshimiwa Mohamed S. Sinani, Mheshimiwa Anastazia J. Wambura, Mheshimiwa Elisa D. Mollel, Mheshimiwa Magdalena H. Sakaya, Mheshimiwa Charles N. Keenja, Mheshimiwa Godfrey W. Zambi, Mheshimiwa

Emmanuel J. Luhahula, Mheshimiwa Jackson M. Makwetta, Mheshimiwa Peter J. Serukamba, Mheshimiwa Mtutura A. Mtutura, Mheshimiwa Hamza A. Mwenegoha, Mheshimiwa Suleiman O. Kumchaya, Mheshimiwa Castor R. Ligallama, Mheshimiwa John M. Cheyo, Mheshimiwa James D. Lembeli, Mheshimiwa David M. David, Mbunge na Naibu Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hao ndio waliochangia, nawashukuru sana kwa michango yao.

Sasa ninapenda nitumie nafasi hii kuchangia, kutoa maelezo juu ya hoja ambazo zimezungumzwa na Wabunge wengi kwa pamoja. Moja ya hoja ni uwekezaji katika kilimo. Kwanza, nataka nikubali kabisa kwamba moja ya matatizo yanayokabili kilimo chetu, ni uwezekaji mdogo na hili siyo jambo la siri kwa sababu kwa miaka 15 iliyopita, wakati tunapita katika kipindi kinaitwa *structural adjustment programme*, hii sekta ya kilimo haikupata uwekezaji wa kutosha katika kipindi hicho. Haikupata uwekezaji wa kutosha siyo kwa sababu Serikali ilikuwa haitaki, lakini tulikuwa tunafanya kazi hii ya *adjustment* kwa kushirikiana na mashirika ya kimataifa. Kwa hiyo, mashirika haya yalikuwa yameweka mkazo zaidi katika sekta ambazo wao walikuwa wanasema ni sekta zinazoleta matokeo kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ukitazama hali ya uchumi wetu katika kipindi hicho, tulikuwa tunawekeza zaidi katika utalii, tumewekeza zaidi katika mawasiliano, tumewekeza zaidi katika sekta ambazo zilionekana zitaleta matokeo ya haraka na ni dhahiri kwa kweli kwamba kilimo si sekta ambayo unaweza ukawekeza leo ukapata matokeo kesho na kwa haraka. Kwa mfano kwa miaka ya 1990, bajeti ya Serikali iliyokuwa inaingia katika sekta ya kilimo ilikuwa kati ya asilimia 2 na asilimia 4. Kwa hiyo, kwa kweli ilikuwa hakuna namna kwamba unaweza ukasema kilimo hiki kinaweza kikatoa matokeo kwa haraka kutokana na *investment* kidogo kiasi hicho. Lakini vile vile uwekezaji katika kilimo haufanywi na Serikali peke yake. Uwekezaji katika kilimo unatakiwa uwekezwe vile vile na sekta binafsi. Sekta binafsi na yenyewe ilichelea sana kuwekeza katika eneo hili.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo lazima tulikubali kwamba ni udhaifu ni kwamba wakati tuna-*reform financial institutions* yaani sekta ya fedha, hicho *Kiswa-english* hicho sekta hiyo na yenyewe haikuelekeza fedha katika kilimo. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kusema ukweli sekta hii ya kilimo imepewa kipaumbele kidogo katika miaka hiyo, mabenki hayakuingiza pesa mle. Sekta binafsi haikuingiza pesa mle, ilibakia ni Serikali na Serikali ilikuwa inawekeza asilimia kidogo kwa sababu tulikuwa katika mfumo wa kubadilisha na kuleta mageuzi katika uchumi. Kwa hiyo, tunaposema sekta ya kilimo tena hapa nataka niwe namjibu Mheshimiwa Wambura kwa sababu aliniuliza siku moja swali la nyongeza hapa na Naibu Spika, akaniambia nijibu kwa ufupi. Kwa nini sekta ya kilimo haikui kwa haraka. Sasa nilitaka nitumie fursa hii kumwambia haikukua kwa haraka kwa sababu hatukuwekeza kwa

kiwango cha kuridhisha. Ndiyo maana sekta ya kilimo kwa kweli unaona asilimia kidogo, hilo moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile sekta hii inategemea mvua na hali ya hewa. Kwa hiyo, unauliza kwa nini inakuwa halafu inashuka? Ukishajua na kukubali kwamba hii sekta inategemea mvua, itakuwa mvua ikiwa mvua itakuwa nzuri na itashuka mvua ikikosekana, ni *logic* rahisi tu. Ndiyo maana unakuta mwaka mwingine inafika asilimia 4 mwaka mwingine inafika asilimia 5 mwaka mwingine tena imeshuka kwa sababu ya mazingira ya mabadiliko ya tabia ya nchi. Kwa hiyo, nataka nikubaliane na wale wote ambao wanasema tuwekeze katika kilimo zaidi, naungana nao mkono, nakubaliana nao kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hebu tutazame matokeo hayo, matokeo ambayo yametokea kutokana na upungufu wa uwekezaji katika kilimo, sekta zenye kuleta mapato kwa haraka zilizopewa kipaumbele zimekuwa. Zimetoa mchango zaidi katika uchumi wa Tanzania. Utalii umekua zaidi, madini yameongezeka zaidi uchimbaji wake na sekta ya mawasiliano imekua zaidi na michango ya sekta hizo katika uchumi wa Taifa umeongezeka. Lakini kwa sababu sekta ya kilimo haikupata uwekezaji mkubwa, katika hali hiyo ndiyo maana mchango wake katika Pato la Taifa umeendelea kushuka. Lakini hii ni *discrepancy* hiyo, ni ki-*Swanglish* kwamba ikiwa sekta hii ya kilimo mchango wake katika Pato la Taifa unashuka lakini inaendelea kuajiri sehemu kubwa ya watu, hapo kuna tatizo ambalo ni lazima tulirekebishe kwa kurekebisha uwekezaji katika kilimo. Lazima tuanze sasa kuelekeza rasilimali katika kilimo na ninaamini kwamba Serikali inakusudia kuongeza uwekezaji katika kilimo.

Mheshimiwa Spika, ziko hoja zilikuwa zimeulizwa mfano asilimia 10 ya bajeti, Bunge hili ndilo linaloweka vipaumbele. Wote tulikubaliana tuanze na elimu, tumewekeza katika elimu, wala hatuwezi kusema tumekosea. Kuwekeza katika elimu ni jambo zuri, uwekeza katika miundombinu ni jambo zuri kwa sababu hakuna kilimo ambacho kinawezekana kukua bila barabara. Kwa hiyo, mambo haya yana mahusiano, yanashabihiana sana. Kwa mfano, ukienda katika Mikoa ya magharibi, kama Tabora, Kigoma na Rukwa ambayo barabara siyo makini, yale maeneo yanafaa sana kwa kilimo lakini kuwekeza kule kwa ajili ya kutoa mazao ni jambo muhimu kabisa ama sivyo kwa kweli kilimo kile hakiwezi kukua katika maeneo hayo. Kwa hiyo, ndiyo maana tunakwenda kwa vipaumbele. Lakini ninaamini kabla ya mwaka 2010, tutakuwa tumefikia asilimia 10 ambayo imetamkwa katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimemwona Mheshimiwa Cheyo akitikisa kichwa na mimi namwomba aahirishe kutikisa kichwa mpaka mwaka 2010 na rafiki yangu Salum naye nataka nimuahidi kwamba ameleta hoja na maswali haya mapema mno, unatusuta kabla ya mwaka wa tano! Wewe subiri mwaka wa tano, halafu tutaelewana. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, sasa tunafanyaje maana hatuwezi kulalamika tu lakini siyo kwamba hatujaanza kuwekeza hasa kupitia Serikali. Kupitia Serikalini tumeanza ule mpango wa *ASDP* ambao Mheshimiwa Mbunge mmoja amesema unaonekana kwamba

bado haujaeleweka, pengine kweli haujaeleweka lakini tunapeleka fedha nyingi sana katika Wilaya. Kwa mfano, mwaka jana tumepeleka shilingi 58 bilioni katika Wilaya mbalimbali. Mwaka huu tunapeleka shilingi 58 bilioni nukta fulani kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu. Ukisoma jedwali lile la Ofisi ya Waziri Mkuu utaona zile fedha zinakwenda.

Mheshimiwa Spika, mimi maombi yangu kwa Waheshimiwa Wabunge wenzangu labda tujaribu kufuatilia vile vile kule kwenye majimbo yetu. Tuangalie hizi fedha zinazokwenda kule zinatumika kwa mambo yaliyokusudiwa? Tujaribu kwenda kule kwenye Majimbo yetu tuulize Halmashauri za Wilaya maana tunazipa fedha nyingi na kati ya fedha hizi nyingi, siyo kwa ajili ya utawala, hizi ni fedha kwa ajili ya uwekezaji katika miradi midogo midogo ya umwagiliaji maji katika mashamba darasa, katika kuimarisha huduma mbalimbali ambazo zinaweza zikamfikia mkulima moja kwa moja, ni fedha nyingi sana zinakwenda kule. Tujaribu kujihusisha kwa sababu kazi yetu moja ni kusimamia na hatusimamii hapa tunasimamia mpaka chini, kule kwenye Majimbo, twende tujihusishe kule tuone *ASDP* inavyoweza kusaidia.

Mheshimiwa Spika, Serikali mwaka huu tumeongeza ruzuku ya mbolea. Ni sehemu ya uwekezaji kupitia Serikali ili kujaribu kusaidia kilimo chetu kiweze kupiga hatua zaidi. Mpango wa ajira ya ugani ambao umeelezwa vizuri sana na Naibu Waziri, ni sehemu ya uwekezaji wa Serikali ili maarifa ya kilimo bora yaweze kuwafikia wakulima. Utafiti ambao tunaingiza fedha, vile vile ni sehemu ya uwekezaji kwa sababu matunda yake yanasaidia ongezeko la mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, jambo moja la kutia matumaini ni kwamba dunia ambayo zamani miaka 25 ilikuwa imepuuza kabisa kilimo, sasa imezinduka. Benki ya Dunia katika ripoti yao ya mwaka 2007, inasema *Agriculture for Development* yaani kilimo kwa ajili ya maendeleo. Benki ya Dunia sasa wamegundua, huwezi ukasaidia maendeleo hasa katika Afrika, Kusini mwa Jangwa la Sahara bila kukubali kuwekeza katika kilimo. Benki ya Dunia sasa inajua hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, juzi juzi hapa wakati Rais wetu anahudhuria mkutano wa *G8* huko Japan, viongozi wale matajiri duniani, Benki ya Dunia imemhakikishia Rais kwamba iko tayari kutuunga mkono katika kuwekeza katika kilimo. Kwa kweli Rais wetu amekwishakuiandikia Benki ya Dunia ili itusaidie kwa dharura kwa mwaka huu wa fedha au mwaka unaokuja ili tuanze kuingiza fedha katika kilimo kwa kutumia *grant* ya Benki ya Dunia na baadaye mikopo ya bei nafuu katika kilimo. Tumeiandikia kwa mambo yafuatayo:-

(a) Tumeiomba Benki ya Dunia itazame suala la mbolea kwa sababu bei zimepanda sana. Nchi maskini kwa kweli zinapata matatizo sana kuweza kutumia mbolea katika mazingira hayo; na

(b) Tumeiandikia Benki itazame uwezekano wa kuzalisha mbegu na kuongeza zaidi mbegu badala ya kuagiza mbegu kutoka nje, tuzalishe mbegu zetu wenyewe hapa

hapa. Kwa sababu vituo vyetu vya utafiti kila mwaka vinatoa mbegu, tatizo letu ni kuziongeza zile mbegu yaani *seed multiplication* ili ziweze kusaidia zaidi kilimo. Benki ya Dunia imeonyesha ya kwamba iko tayari kutusaidia katika eneo hili na tutashirikiana na nchi zingine rafiki zimeonyesha vile vile ziko tayari kutusaidia katika eneo hili licha ya michango yao wanayotoa kupitia *ASDP*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, katika mazingira haya ambayo dunia sasa imeelewa na dunia yote inazungumzia juu ya upungufu wa chakula na kupanda kwa bei, nadhani ni wakati muafaka sasa na sisi tuweke mkazo zaidi na msukumo zaidi katika kukuza sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, ziko hoja zimezungumziwa kuhusu chakula na wote waliozungumza ni kama wanakubaliana na Serikali kwamba chakula ni kitu muhimu sana. Hata rafiki yangu Mheshimiwa Salum, katika hotuba yake, amesema chakula ni sehemu ya usalama wa Taifa, nakubaliana naye. Lakini alijipinga kidogo lakini ni mambo ya kawaida, unajua mambo haya ukiambiwa wewe kazi yako ni kupinga, huwezi kuwa unasema mambo mema tu, mwishowe watakuuliza kwamba mbona umerudi kule kule tena. Kwa hiyo, wakati anasema chakula ni usalama wa Taifa tena anarudi anasema, kwa nini tunazuia kisiuzwe nje? Sasa nataka nijibu hilo kwamba kwa kweli hatuna sera ya kuuzuia kuuza nje lakini ni lazima tujikite katika kuhakikisha kwamba kabla hujauza nje, nchi hii ibaki na chakula cha kutosha kwa sababu ni sehemu ya usalama wa Taifa, nakubaliana naye kabisa. Sasa katika mazingira ya sasa, dunia haina chakula cha kutosha, bei zimepanda sana, Tanzania si nchi peke yake ambayo imezuia uuzaji nje, Vietnam inazalisha mpunga tani 39 milioni, inauza nje kila mwaka tani milioni 6, lakini imezuia, Thailand imezuia, India pia imezuia. Indonesia ilikuwa inaagiza mchele kutoka Vietnam, juzi nilikuwa nao Rome, Indonesia wanasema sasa hawawezi kuupata kwa sababu zile nchi walikuwa wanaagiza hawawezi kuupata. Kwa hiyo, kile kiwango ambacho walikuwa wanafidia kwa kuagiza sasa hakiwezekani.

Mheshimiwa Spika, ikiwa nchi kubwa na zenye kilimo kikubwa kama hicho, zimegundua kuna tatizo, sisi je tufanyeje, kwa sababu hali ndivyo ilivyo. Mwaka jana tumeruhusu wafanya biashara waingize tani laki tatu za mahindi kufidia upungufu wa mahindi hapa, tukawaambia na kodi tutawaondolea, wakaleta tani 8,000, maana yake bei zilionekana ziko juu kiasi kwamba wakileta hakinunuliki. Kwa hiyo, katika mazingira hayo ndiyo sababu inayofanya tuzuie chakula chetu kibaki hapa ili watu wetu wasije wakafa na njaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Makwetta, jana alitupa msemo mmoja akasema, *hungry men is a angry men.* Sasa sisi wote tunakuja humu kwa kupigiwa kura, sidhani kama tunataka kwenda kuomba kura kule kwa *angry voters?* Ni kazi ngumu sana kupata kura kwa *angry and hungry voters.* Kwa msingi huo, sisi kama viongozi wa Tanzania ambao tunalitakia heri Taifa letu ambalo hatutaki katika haya mazingira ya sasa ya dunia ambayo haina chakula, turuhusu chakula kitoke chote, tutarudi hapa kuja kuulizana tena sasa kimekwenda wapi?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa sababu kuongoza ni kuonesha njia na wakati mwingine ni kufanya maamuzi ambayo hayapendeki sana na baadhi ya watu, tukubali kuwa hiyo gharama yetu tuliyoomba ya kuongoza. Chakula chetu kilichopo hapa hakitatosha kama tukiruhusu kiuzwe nje kwa sababu mwaka 2006 kilikosekana na tunakumbuka mambo yalivyokuwa magumu, Mheshimiwa Lowassa ndiye alikuwa Waziri Mkuu, anakumbuka alitembea nchi yote hii anazungumza habari ya kugawa magunia, atakuwa shahidi kwamba kazi ya kugawa magunia ya njaa, ni *problem* kubwa kweli.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tuache kusema kama alivyosema rafiki yangu Mpina, lakini baadaye tuliongea nje, anasema tunawahujumu, Serikali inahujumu wananchi, aah bwana, Serikali ya *CCM* na *CCM* yenyewe kwa historia yake ni Chama cha watu masikini, hakiwezi kuhujumu wakulima hata siku moja, lazima niseme hii kabisa, haiwezekani. Lakini kuwahujumu ni pamoja na kuwaambia uzeni halafu mfe, hiyo ndiyo hujuma kali kuliko zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nasema tunafanya hili kwa nia njema kabisa. Kwa sababu tukiruhusu, Afisa mmoja wa nchi jirani, nitawaambia alichosema. Alikuja hapa kutaka chakula halafu akamnong'oneza Afisa wetu, lakini hawakuniambia niseme, akasema mkifungua mipaka, hatutakuja kuomba chakula maana kitakwenda tu. Sasa msiniulize ni wa wapi? Lakini alituambia kwa nia njema tu kwamba mkifungua mipaka, hawatakuja kwa sababu hiki kilichoko hapa chote kitakwenda. Lakini hiyo ni mkakati wa muda mfupi tu maana huwezi kuendelea kuzuia tu, hiyo nayo wala sio *solution* nzuri sana lakini katika mazingira ya muda mfupi huna namna.

Mheshimiwa Spika, mkakati wa kuzalisha chakula ndio jambo la msingi, sasa tumefanya nini? Tumeamua kwa kweli tuelekeze rasilimali zetu katika uzalishaji wa chakula kwa mwaka huu. Tumeamua Mikoa kama tisa hivi inayopata mvua nzuri, tuipe mbolea, tuipe mbegu za mahindi wazalishe chakula. Tunafanya uamuzi huu, sio kwamba wengine hawastahili, sisi ni nchi moja na mambo haya ya chakula yanatuhusu wote. Mwaka jana ulipotokea upungufu wa chakula kule Nzega na Shinyanga, mahindi ya *reserve* yalikwenda kule lakini yalikuwa yanatoka mikoa ya Nyanda za Juu Kusini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, chakula hiki ni cha nchi, kule ambako kinaota vizuri tuwape rasilimali walime chakula hiki tule wote. Ni jambo la wazi tu. Kwa hiyo, tumeamua kwamba tutapeleka kipaumbele Ruvuma, Rukwa, Mbeya, Iringa, Morogoro, Kilimanjaro, Arusha, Manyara, Kigoma, Wilaya ya Tarime na sasa tunaongeza Wilaya ya Sikonge katika Mkoa wa Tabora kwa sababu hali yake ya hewa inafanana na Wilaya ya Mpanda. Tunafanya maamuzi haya kama nchi kwa ajili ya manufaa ya nchi, lakini Mikoa inayobakia ambayo ni ya ukame tunaipa mbegu za mtama na uwele kwa ruzuku. Kwa kweli tunatilia mkazo maeneo hayo yaongeze uzalishaji wa mazao ya mtama. Baadhi ya mikoa hiyo ni Dodoma, Singida, Shinyanga, sehemu ya Tabora ukiondoa Sikonge, sehemu kubwa ya Mara, sehemu fulani ya Arusha, maeneo ya Upare, Nyanda za Chini Tambarare, haya maeneo yote tunataka yatilie mkazo mazao yanayostahimili ukame ili mradi tupate chakula. Wewe lima mtama, kama hutaki kula mtama utauza mtama

utanunua mahindi, lakini utakuwa umeshachangia na wewe katika kapu la chakula cha Taifa. Mimi nadhani hili ni jambo ambalo tunahitaji kulipa umuhimu mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, masoko ya chakula, maana ukiwaambia watu lima mahindi mengi zaidi, lima mtama, lazima uwaambie ziada watauza wapi? Kwa hiyo, nataka niwaambie kwamba kwanza tuna *NFRA* ambayo ilikuwa inaitwa ESJALA, sasa hivi imekwishakwenda Mikoani kwenda kununua mazao na kwa kweli nataka niliambie Bunge hili, bei ya soko la mahindi sasa ni kati ya Sh.190 na Sh.200, akiba ya Taifa tunanunua Sh.240 katika maeneo yote yanayolima mahindi na ndiyo tunaonesha njia. Kwa hiyo na wale wanunuzi wengine wanaotaka haya mahindi na wao wakanunue kwa Sh.240/-. Shabaha yetu ni kuwatia moyo wakulima lakini kwa mwaka unaokuja tunataka kufanya jitihada zaidi ya kuunda Bodi ya Mazao Mchanganyiko, ili pamoja na soko kununua lakini inapobidi Serikali iwe inaweza kutumia Bodi hii kuingilia kati soko na kupata chakula na kinachobaki tuuze nje.

Mheshimiwa Spika, vilevile tumeshazungumza na Shirika la Chakula Duniani wanaita *WFP*, wamekubali kwamba katika maeneo yanayozalisha chakula kwa wingi mwaka kesho watakuja. Wanaanza mwaka huu kujenga miundombinu, maghala na wataanza kununua chini ya mpango unaitwa *purchase for progress* kwamba unawapa wakulima soko. Kwa hiyo, unawatia moyo kufanya nini, kuzalisha zaidi. Kwa hiyo, watakuja na wamekuja wameonana na Rais wetu. Kufika mwezi wa 11 mwaka huu, watakuwa wako katika Mikoa inayozalisha mahindi kwa wingi ili kuweka utaratibu. Kwa hiyo, kule kusema kwa nini hatuuzi, tuzalishe tu tutauza, tutauza ndani na tutauza nje, lakini tuzalishe tuuze ziada, eeh, suala ni kuuza ziada. Kwa hiyo, *WFP* wenyewe kwanza ni soko la nje maana watanunua, watashauriana na Serikali wakati wanapohitaji, kuna maafa huko watapeleka na kingine kitatumika hapa katika kitu kinaitwa *school feeding,* ni chakula kitatumika hapa na kinaweza kwenda nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maswali mengine ambayo yameulizwa hapa ni mfuko na utaratibu wa kufikisha pembejeo hasa mbolea. Hili lilikuwa na kesi sana miaka ya nyuma, tumepata matatizo, tumeyaeleza vizuri sana matatizo hayo kwenye hotuba. Tumeeleza jinsi ambavyo tumeathirika kutokana na kupeleka na kutumia ruzuku ya makampuni. Yaani kampuni inapeleka mbolea, tunakubaliana nayo bei, halafu ndio inakuja sasa inadai ruzuku baada ya mbolea yake kuuzwa. Utaratibu huu haukuonekana kufanya kazi vizuri. Sasa tumeondokana na utaratibu huo, mwaka huu tunataka ile ruzuku, shilingi kama 27 bilioni hivi, tunaitoa kwa vocha lakini tunampa mkulima. Kwa mfano, tumezindua huo utaratibu kule Morogoro, yaani wewe kijiji chako kinakutambua kwamba wewe ni mkulima una ardhi, unalima aina ya mazao ambayo tunayawekea ruzuku, ambayo kwa mwaka huu zaidi yatakuwa ni mahindi na mpunga. Kijiji kikikukubali kwamba wewe unazo sifa hizo basi pale kwenye kijiji na kwa kweli sensa sasa inaendelea nchi nzima kujua hao wakulima wa namna hiyo ni wangapi ili tuweze kujua wapi tunapeleka kiasi gani cha ruzuku.

Mheshimiwa Spika, tumetengeneza vocha ambazo hazigushiki na zinajulikana sana zina *security* Benki ya *NMB* na wao wameshiriki kuzitengeneza. Huyu mkulima huyu ukimpa ile vocha anakwenda anapata saini zaMwenyekiti wa Kijiji chake, za

Bwana Shamba wake pale, Katibu wa Kijiji, zinakuwa saini kama nne hivi kuthibitisha kwamba huyu kweli amekubaliwa na hicho kijiji, anaenda kwa muuza mbolea. Tumefundisha watu tunawaita *Agro dealers* na tunaendelea kufundisha mpaka nchi yote ienee, lakini kwa sasa tumewafundisha katika Mikoa hiyo ambayo tunaanzia.

Mheshimiwa Spika, tukifika huko akimpa muuzaji mbolea ile vocha yake inampunguzia bei ya mbolea, yeye analipa kiasi kinachopungua halafu hiyo vocha itapelekwa kwenye benki na huyu muuzaji wa mbolea peke yake ndiye anayejulikana benki. Ukienda nayo wewe, benki ile haishughuliki na wewe hata kidogo, anayeenda nayo ni yule aliyeuza mbolea kuonesha kwamba mbolea imekwishafika na ndiye anayelipwa na benki kwa sababu fedha zile ni za Serikali lakini zinapita *NMB.* Hiyo itatuondolea huo mgogoro wa kusema kuna bei mbili, bei ya ruzuku na bei ya soko, zote zitakuwa ni bei ya soko tu lakini mwenye ruzuku anapunguziwa bei kwa kutumia vocha, huo ndio utaratibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nimesikia baadhi ya watu wanasema ooh, utaratibu huu ni nadharia. Lakini hakuna vitendo ambavyo huwa havianzi na nadharia. Sasa ukitaka kufanya lolote si unafikiri kwanza halafu ukishafikiri ndio unafanya, sasa unafanya tu kweli? Au unafanya kwa kufikiri, au unajifunza kwa watu wengine ambao walifikiri kabla yako. Sasa sisi tumefanya yote, tumefikiri halafu tumeenda Malawi pale tumejifunza kwa waliofikiri kabla yetu halafu na sisi tumeingia kwenye huo mpango. Sasa nadhani mtuunge mkono halafu tuone mambo yatakuwaje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yako maswali ambayo yameulizwa kuhusu mazao ya biashara. Mazao ya biashara yanahusu tumbaku, kahawa na chai. Kwanza, juu ya tumbaku, tunalitilia mkazo lakini tunalo tatizo ambalo tunataka kuliondoa mwaka huu. Nataka Mheshimiwa Nkumba, aliyesoma ile hotuba ya Kamati anisikilize vizuri.

**SPIKA:** Na Spika anasikiliza. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, naomba na yeye asikilize vizuri. Tatizo lililopo kwa wakulima wa tumbaku ni kwamba wale wanunuzi ndio wanapeleka pembejeo tena kwa mkataba. Lakini wanunuzi wale ni watu wajanja sana, wengi wao ni Wamarekani tu, anakuja na *book* kama hili anasema *we have come here now to negotiate, the deal is right here.* Msomi wa Kimarekani anazungumza na Wanyamwezi na Wangoni, lugha hawaelewani, wanasaini mkataba, hawajui *interest rate* ni kiasi gani, siku ya kudai anachukua hela zote za Mnyamwezi halafu anachukua za kwake anasema hizi zilizobaki ndio ninyi mtagawana. Kwa hiyo, aliyefanya uaminifu akaleta tumbaku yake kwenye Chama cha Ushirika, anakatwa yeye yule aliyetoroka, ndiye anayeenda. Kwa hiyo, mfumo wenyewe unatilia mkazo watu kutoroka vituo.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi wadau wa tumbaku wanajua nataka tuachanishe mfumo wa pembejeo na mfumo wa ununuzi. Nilitaka jambo hili liwezekane mwaka jana, nilishindwa maana makampuni haya yanasema yanawadai hawa, wana madeni. Sasa nataka kuwaahidi wakulima wa tumbaku na wao tutakaa na wanunuzi tuulizane

mnawadai shilingi ngapi? Eeh, mnawadai shilingi ngapi mpaka Wanyamwezi hawa na Wangoni wawe watumwa wenu, ngapi hizo? Bei ya utumwa huo ni shilingi ngapi? Ili tuwakomboe Wanyamwezi hawa, hawa Wanyamwezi ni wapiga kura wetu sisi, eeh. Kwa kweli nataka kuwaahidi, mazungumzo yale yatazaa matunda maana tutawakomboa. Tumefanya hivyo kwenye korosho, tutafanya hivyo kwenye tumbaku na wakulima hawa watakuwa huru kutokana na mifumo ambayo haiwezi kuwapa haki. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, hiyo ni tumbaku, sasa wanasema tutoe ruzuku. Mbolea hii yote ya mikataba inakwenda na makampuni hayo, ukitoa ruzuku unampa nani ruzuku hiyo? Tulijaribu, tulitoa ruzuku ya Sh.6,000/= mwaka mmoja zikafika Sh.600/=. Kwa hiyo, unatoa ruzuku kwa kweli kwa huyu anayepeleka mbolea sio kwa yule anayepokea. Kwa hiyo, kwanza tuondoe huu mnyororo, halafu ndio tuzungumze ruzuku ya tumbaku itakuwaje na hiyo *their days are numbered,* tutaondoa huo mgogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, liko suala la kahawa. Mimi sina ubishi na waliosema kahawa ina sababu nyingi za kushuka, wala sina ubishi kabisa. Mimi shabaha yangu na ya Serikali, ni kuona kahawa inaongezeka. Kwa hiyo, tunatoa ruzuku kwenye miche, ili wakulima wa kahawa waweze kupanda miche kwa wingi zaidi.

Mheshimiwa Mramba, namshukuru sana ametupa ushauri, yale aliyoyasema ya kung’oa na huyu anayeng’oa afanyeje, tutayazungumza na na yeye tutamkaribisha atusaidie kwa kutumia uzoefu wake ni nini hasa tufanye ili hao wenye miche ya zamani waondokane nayo waende kwenye miche mipya. Kwenye chai, tunafanya hivyo hivyo. Tunaelewa kwamba wakulima wa chai bado wana matatizo kidogo, chai inashuka kwa sababu pembejeo zimekwenda juu sana. Lakini kwa hali ya sasa na ya mwaka huu, tunawekeza katika uzalishaji wa chakula. Kwa hiyo, wenzetu wa chai ingawa na wao wanasema chai ni chakula, lakini nadhani chai ni kinywaji zaidi kuliko ilivyo chakula. Kwa sasa hivi nafikiri tuwekeze kwenye chakula halafu tutazungumza mambo ya kinywaji baadaye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, liko suala la pamba na imezungumzwa sana na ninataka niwaambie na mimi ni mdau wa pamba, maana na mimi natoka Bunda na sisi huko tunalima pamba tu. Hili jambo la pamba limeleta kasheshe. Mwaka jana, hali yetu ilikuwa nzuri sana. Pamba ilinunuliwa tena kwa mashindano na bei ya wastani ilikuwa Sh.500/=.

Mheshimiwa Spika, kuna Mheshimiwa mmoja alisema haungi mkono na kuuliza kwa nini mmeweka bei ya Sh.400/=? Mimi nataka kuwambieni, Serikali hatupangi bei ya mazao, tulikuwa tunapanga zamani, baadaye tulipoleta mageuzi, tukasema tuachie bei iwe ya soko, lakini Serikali inafanya kazi kama *referee* kwenye uwanja wa mpira, ndio mashindano yanakofanyika. Sasa ukiona *foul,* unapiga filimbi na una kadi nyekundu au njano, hiyo ndiyo kazi tunayofanya sisi. Ndio maana juzi tulipoona mambo hayaendi vizuri, tulipiga filimbi kupitia Bungeni hapa, jamani eee, mnaongea ninyi na wewe Mheshimiwa Cheyo, una ushahidi kwamba baada ya filimbi ile walianza kuongeza kidogo, ndiyo. Sasa hivi kuna wastani wa Sh.450/=, Sh.420/=, Sh.430/= lakini kama

tusingepiga ile filimbi wangeendelea na Sh.400/= hiyohiyo na bado tunawambia hatujaridhika, ongezeni bei kwa wakulima, hiyo ndiyo tunayowaambia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, labda tukubaliane kwamba tuanze kuutazama mfumo vile vile wa ununuzi wa zao la pamba kwa miaka inayokuja, hivi tutaendelea hivi hivi? Ni kweli tumeweka malengo ya kuzalisha marobota 1,500,000 na haya yanawezekana na hasa ule mfumo aliokuwa anauzungumzia Mheshimiwa Cheyo, ukiachwa ule wa kuchanganya mahindi na pamba.

Mheshimiwa Spika, nataka kumwambia rafiki yangu Mheshimiwa Cheyo, unajua hapo kuna mgogoro wa utaalamu tu. Kuna mdudu fulani anitwa *American bore,* anakula pamba na anazaliwa ndani ya mahindi, sasa ukichanganya mahindi na pamba unaanzisha kiwanda cha yule mdudu ndani ya shamba lako la pamba, huo ndio ukweli. Ndio maana huwa tunazuia kuchanganya mahindi na pamba. Wala sio amri isiyokuwa na maana, ni amri ya kisayansi tu. Ukisema ni shamba langu hata ikipungua lakini mdudu huyu anaweza kwenda kwenye shamba la jirani vilevile. Sasa ni lazima kuwa na sheria ambayo inalinda jambo hili.

Mheshimiwa Spika, lakini nataka niwaambie wakulima wa pamba, tunaelewa matatizo yao, tunajua bei wanayolipwa bado haitoshi, tunaomba wanunuzi watusikilize vizuri kwa sababu hatuna ushahidi wa bei kushuka katika soko la dunia. Kwa hiyo, wapeni wakulima bei nzuri kwa mazao yao. Kwa sababu wale wanaolipa bei ndogo, mwisho wa mwaka huu sio mwisho wa dunia, itabidi tuje tuzungumze kama wana sifa ya kununua mwakani. Tulifanya hivyo kwenye korosho mwaka wa kwanza tulipopata tabu mwaka wa pili tuliweka mfumo ulioondoa kabisa tatizo la korosho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, halafu nataka niwaambie wale wanunuzi hasa wenye *ginnery*, wakati sasa umefika wa kuanza kuwekeza kwenye viwanda vya nyuzi na nguo. Biashara ya *ginnery* ni bishara ya kizamani, kwani *ginnery* inafanya kazi gani, kutoa nyuzi tu? Unaweza ukawa na nyuzi pale lakini unazalisha nguo.

Mheshimiwa Cheyo, ni *expert* wa *technology* ya nguo, wewe ulisomea hiyo kazi, nenda ukawasaidie wale watu waelewe hiyo kazi. Tuanze kuwekeza kwenye nguo na kwenye nyuzi. Mimi nimekwenda Marekani juzi kwenye mkutano wa *AGOA Forum*, sisi hatuna cha kuuza. Tulikuwa na Mheshimiwa Waziri wa Biashara, tunao watu wanaitwa *gas pay* ambao wanataka kutusaidia kwenye nguo, tushirikiane na wale wawekezaji wa nguo sio lazima wawe wanatoka nje, hawa hawa walioko na *ginnery* hapa wanaweza kuwekeza na waanze kuwekeza. Tukibadili mfumo unaotenga *ginnery* na ununuzi, *ginnery* haitakuwa na faida sana. Maana itakuwa ni sawasawa na kiwanda cha mpunga kinachongojea wenye mpunga walete, watakuwa wanalipa *ginning fee* tu, kwa sababu tumeanza katika Mkoa wa Shinyanga, mfumo wa stakabadhi ghalani na ule ukifanikiwa, inawezekana ikawa ndio mfumo wa kununua zao la pamba hatua kwa hatua. Sasa wakati tunaelekea huko, ni lazima tuwape wenzetu wanaowekeza kwenye hili zao la pamba, kwenye *ginnery,* waanze kuingiza pesa zao katika utengenezaji wa nguo na wakifanya hivyo bei ya pamba itakuwa nzuri kwa sababu watakuwa wanauza nyuzi na nguo badala ya kuuza pamba ghafi, kuuza pamba ghafi ni mambo ya zamani sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uniruhusu nizungumze kidogo, niishukuru kwanza Kamati ya Kilimo, wametupa ushauri mzuri sana na kwa kweli wala mimi sitaki kuongeza kitu. Hii Kamati tunakutana nayo kila mara, kama kuna jambo lolote ambalo tunaweza kushauriana nayo na mengine, nimejibu kama lile la tumbaku, nadhani hapatakuwa na tatizo lolote, tutaweza tu kushirikiana nao na wataendelea kutupa mawazo wanayoona yanafaa.

Mheshimiwa Spika, lakini nitakuwa sikumtendea haki Waziri Kivuli, Msemaji wa Kambi ya Upinzani, kama sitasema kitu chochote juu ya yale aliyosema. Lakini unajua namheshimu sana Mheshimiwa Salum, halafu ni rafiki yangu, lakini nimemgundua jambo moja tu, anacheza na *statistics*, yaani takwimu, anajua sana kutumia takwimu. Ameenda kwenye kile Kitabu cha Hali ya Uchumi, akachukua mazao yaliyofeli na yale ambayo yamefanikiwa akayaacha, anacheza na takwimu. Sasa nataka kumwambia Mheshimiwa Salum, unajua wote tuliosoma takwimu, tunajua namna ya kucheza nazo sana lakini sina ugomvi wa ajabu sana maana ameniambia unajua bwana ndiyo kazi yetu sisi hapa eeh, lakini kazi yenu hii bwana wakati mwingine mambo yakiwa mazuri basi useme haya mazuri basi. Sasa kweli yote yawe mabaya? Eeh, itakuwa jambo gani hilo? Ufanye mambo mabaya tu? Nani amekuajiri kufanya mambo mabaya peke yake? Haiwezekani! *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, moja ya hoja aliyosema ni kwamba bajeti ya kilimo imeshuka, lakini ukweli ni takwimu tu, kwa kweli haitoshi lakini haikushuka. Kwa sababu mwaka jana tulipata shilingi 131 bilioni, mwaka huu tumeondoa fedha za umwagiliaji bilioni 14, tumeondoa za *DASIP* na *PADEP*, zilikuwa zinapita Wizara ya Kilimo, sasa zimeenda Halmashauri moja kwa moja. *DASIP* ni bilioni 16, halafu *PADEP* bilioni 5.6, ukizichanganya zote kama ingekuwa zimekuja kama mwaka jana bajeti ya kilimo ingekuwa bilioni 151.01. Kwa hiyo, haikushuka isipokuwa tunapeleka rasilimali hizi kwa wananchi wenyewe kule, kupitia Halmashauri za Wilaya.

Mheshimiwa Spika, suala la 10% nimelieleza, nataka Mheshimiwa Salum, uliahirishe mpaka mwaka 2010 maana utakuja kukosa hoja ya kuhoji jambo hili, maana kufika huko tutakuwa tuko kwenye 10%.

Mheshimiwa Spika, halafu vilevile alisema wakulima wadogo hatuwajali, sisi ndio wapiga kura wetu, ndio wanaotuleta huku, tunawajali kweli, ile mbaya.

Mheshimiwa Spika, katika kucheza na *statistics*, alichukua pareto, ambayo tuling'oa miche mwaka jana, lazima ilishuka tu, miche ya zamani tumeondoa sasa imeongezeka. Alichukua muhogo, muhogo uliugua ile inaitwa batobato kali, sehemu nyingi ya nchi waling'oa kama *solution.* Kwa hiyo, lazima ingeshuka tu. Lakini mazao ambayo hayakupata *disturbance* ulichukua ndizi, ndizi hizi bado kuna magonjwa, tunayafanyia utafiti hatujapata jibu. Kwa hiyo, ndizi zina matatizo, lakini zitashuka tu. Sasa ukiwa unachukua hizi uwe unachukua na zile ambazo zimeongezeka, huo ni ushauri tu wa bure. Halafu ukulima wa pamba si kweli kwamba tunazalisha kilo 250 kwa hekta, hapana ni kilo kati ya 500 mpaka 750 kwa hekta, hii 250 mpaka 300 ni kwa eka. Ndio

maana ni ushauri tu, tusingefika tani tulizofika mwaka mwaka huu kama ingekuwa uzalishaji ni chini kiasi hicho, lakini hatujaridhika, tunataka kwenda juu zaidi. Tutaweka mfumo wa kununua ambao utawahakikishia wakulima wa pamba kwamba waendelee kulima tu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, mfuko wa pembejeo hatudaiwi bilioni 10, tunadaiwa bilioni tano na tunadai na hao tunaowadai tunawajua na dhamana wanazo na wengine tumeanza kuwafikisha Mahakamani. Lakini siku hizi kuna hiki Kiswahili cha ufisadi, sasa labda tukitumie vizuri kwa sababu mimi nikipeleka hoja ya kutaka kukopa halafu biashara yangu ikaharibika, mimi sioni kama ni fisadi ni mufilisi tu. Eeh, nimefilisika tu kutokana na biashara yangu kuharibika. Sasa ukiniita fisadi, utaogopesha watu kwenda kukopa. Huu sio ufisadi, huku ni kukopa na kutengeneza biashara, ukishindwa, Marekani pale huwa wana Sheria yao inaitwa *Chapter 11*, mambo yako yakienda vibaya unaingia *Chapter 11*, hawakudai mpaka ujirekebishe muda wako wa *Chapter 11*, ukiisha ndio wanaanza kukudai. Sasa sisi hapa ukishindwa kulipa siku moja wanasema fisadi, eeeh inatisha, itakuwaje? Acha hiyo bwana! *(Makofi/kicheko)*

Mheshimiwa Spika, mawazo mengine ambayo ametoa wala sina matatizo nayo, nilitaka kujibu hayo machache tu.

Mheshimiwa Spika, ninapenda sasa kujibu baadhi ya mambo *specific* tu, ambayo Waheshimiwa Wabunge walisema Waziri ukijibu, utujibu. Mheshimiwa Gaudence Kayombo, ameshajibiwa mambo ya kahawa na Naibu Waziri.

Mheshimiwa Nsanzugwanko, anasema mradi wa *DASIP* unaendeshwa hovyohovyo, kizamani. Mimi nataka kumsaidia tu kwamba *DASIP* kama tunavyoiendesha sasa, fedha zote zinakwenda kupitia, ni sawasawa na *ASDP tu* na mfumo wake ni wa kuamuliwa mambo yote katika Halmashauri. Mgawo wa fedha ambao unatolewa, umegawanywa kwa kufuata wingi wa Wilaya na kila Wilaya imepewa fedha zile zile sawa sawa na Wilaya nyingine lakini ukienda Shinyanga wana Wilaya nyingi zaidi, ukienda Mwanza wanazo nyingi zaidi, ukienda Mara utakuta wana chache na Kigoma wana chache. Kwa hiyo, kila Wilaya inapewa fedha zinazolingana na Wilaya inayofuata.

Mheshimiwa Spika, isipokuwa ulichokuwa unasema pale Mheshimiwa Nsanzugwanko, ni kwamba maamuzi yanafanywa mwanzo. Sasa tumesema fedha ikienda Kigoma maamuzi yafanywe Kigoma hukohuko na wasimamie huko huko kama wanavyosimamia *ASDP*, ndiyo maana hata hizi za *DADPs* tumezipeleka moja kwa moja kwenye Wilaya.

Mheshimiwa Daniel N. Nsanzugwanko alikuwa anazungumza juu ya ile ramani kwamba haikuonyesha kama mnaweza kulima, katika lile jedwali namba tatu. Sasa nataka kusema lile jedwali ukilisoma pamoja na ile ramani, kuna ramani ambayo hatukuitoa maana ni kubwa sana na tungeifanya iwe ndogo isingesomeka. Lakini

Mheshimiwa Daniel N. Nsanzugwanko tunaweza tukakupa nakala moja ya ramani ambayo inaonysha *ecological zones* na mazao ambayo tunapendekeza, ipo imeandikwa vizuri tu na kahawa kule Kigoma inalimwa tena kuna eneo moja ambalo wanalima kahawa vizuri sana na sisi tunawapongeza na Chama chao cha Ushirika kinafanya kazi yake vizuri.

Mheshimiwa Spika, kuna Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, kwanza nataka kumpongeza sana Mheshimiwa Anne Kilango kwa kuwawakilisha vizuri sana wananchi wa Same na kwa jinsi anavyojihusisha na matatizo na maendeleo yao. Wanataka kujenga kiwanda na alitaka sisi tumpe shilingi milioni 500. Sasa ninataka kumwambia kwamba ningekuwa nazo kweli kwa huruma kabisa ningekupa ila tatizo ni kwamba hazipo. Kwa hiyo, huruma yangu hii haina maana sana. Lakini nataka kusema kwamba ule mradi ni mzuri tena mzuri sana kwa sababu makusudio yake ni kuongeza thamani. Kwa hiyo, ninapendekeza kwamba wale wanaojenga ule mradi watuletee andiko tu ili tushauriane na Wizara ya Viwanda, tuone namna tunavyoweza kukusaidia. Tena nataka kuwapongeza wananchi wa Same kwa kufikiria jambo hili kwa kweli hivi ndivyo tunataka mazao yote ya kilimo yaanze kuongezewa thamani ili tuachane na hii tabia ya kuuza tangawizi bonge badala ya kuuza ambayo imetengenezwa. Kwa hiyo, nakushukuru sana na kwa kweli tunakuunga mkono.

Mheshimiwa Bujiku Philip Sakila, alizungumzia suala la chakula na bei ya pamba. Nimeshazungumzia bei ya pamba, katika wale wanaozungumzia bei ya pamba, kwa kweli hakuna kitu ambacho natofautiana nao, wote naungana.

Mheshimiwa Spika, wengine wamesema kwamba benki inayowakopesha wananchi na yenyewe imejiingiza kutaka kulazimisha bei iwe chini. Sisi hatuna ugomvi na Benki na hatuna ushahidi bado juu ya jambo hili lakini tunataka benki ijue kwamba hatuwezi kukubaliana na jambo hili, benki haiwezi kupanga mazao ya wakulima. Mazao ya wakulima yaachwe yapangwe na soko, benki ina mteja wake, wasome *cash flow* ya mteja wao halafu wampe hela kulingana na *cash flow* yake halafu wamuachie yeye akatengeneze faida kule kwenye soko. Lakini benki ikisema lazima ulipe eeh! Benki tena? Benki haiwezi kupanga bei ya mazao, hiyo siyo sahihi. Tunaheshimu benki lakini hiyo siyo sahihi.

Mheshimiwa Spika, suala la Mheshimiwa Ludovick John Mwananzila, limejibiwa na Naibu Waziri, suala la Mheshimiwa Lediana Mafuru Mng'ong'o na lenyewe limejibiwa ila Naibu Waziri alifikiri ni la Diana Mkumbo Chilolo, lile la watu ambao hawana uwezo wa kununua mbolea, limeshajibiwa na kwamba hatuna utaratibu huo labda tuanze kuzungumza sasa namna tunavyoweza kusaidia lakini kwa sasa hatuna mfumo unaoweza kujibu swali hilo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Benki ya Kilimo, hili ni jambo ambalo tumekubali lakini tutajipa muda kwa sababu huwezi kuanzisha benki asubuhi ikaanza lakini Rais wetu amelitolea ufafanuzi kule Tanga amesema *TIB* itakuwa na dirisha la kilimo na rasilimali ya *TIB*, inakuzwa, halafu tutaanzia hapo. Baada ya hapo, tutakwenda hatua kwa hatua katika *process* ya kuanzisha Benki ya Kilimo lakini kimsingi tumeshakubali.

Mheshimiwa Spika, mradi wa *Japanese Food Counterpart* kwamba ulisitishwa hapa, fedha yake ndiyo shilingi 200 milioni, *maximum* ndiyo maana haikuongezeka.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *scheme* na mambo yote yanayohusu umwagiliaji maji, sikuyagusa siyo kwamba hayana uzito katika Wizara ya Kilimo, hapana! Tunashirikiana na Wizara ya Maji na mliona Waziri wa Maji, ananiaga, watu wake walikuwa hapa wakati mnajadili hoja zote zinazohusu umwagiliaji. Kwa hiyo, anatafuta majibu kwa hoja ambazo mmezisema kupitia Wizara ya Kilimo. Kwa hiyo, hilo nalo linashughulikiwa na Wizara ya Maji na Umwagiliaji ndiyo maana sikulizungumza.

Mheshimiwa Rosemary Kirigini, alizungumzia juu ya fedha za wakulima na yupo ndugu yangu fulani alisema kwamba yeye haungi mkono mpaka niseme kama tutalipa. Sasa ninamwomba Mheshimiwa James Lembeli, aunge mkono maana tumeanza kulipa na tulipa na hela tunazo tunaanza kuzi-*dispatch* na hii ni ahadi tulitoa hapa Bungeni mwaka jana na kwa kweli ingekuwa ni vigumu sana kuja mimi tena na ningetamani kama ningekuwa nimehamishwa ili nisije mimi bila kulipa zile hela maana mimi ni mwoga sana wa kusema mambo ambayo siwezi kufuatilia. Kwa hiyo, tunalipa na ninamuomba Mheshimiwa James Lembeli aunge mkono halafu tuendelee.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *Mara Cooperation Union,* nao walikuwa wanadai fedha, walishakufa lakini wakulima wao wanadai shilingi milioni 240, wakulima ambao walikopa pamba ni pamoja na wale wa Kahama na wale wa Wilaya ya Chunya kwa rafiki yangu pale Guido Gologolio Sigonda. Wale wa Chunya walikuja hapa, tukazungumza nao nikawahakikishia tunalipa na sasa nataka kurudia tena kwamba tunawalipa kati ya sasa na mwezi unaokuja, wanalipwa na tunaweka utaratibu.

Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, alizungumzia matrekta, tunashughulikia juu ya kutafuta uwezekano wa kupata mikopo rahisi ili tuingize matrekta na tuweke utaratibu ambao utawawezesha wakopaji kukopa.

Mheshimiwa Spika, rafiki yangu Castor Raphael Ligallama, alikuwa anazungumza kwamba watu wanaishi kwenye shamba. Lakini naona kama tatizo lenyewe walishalimaliza wenyewe maana wanasema walishakutana wakazungumza. Sasa Serikali haina mgogoro wowote kama wanabaki kijijini kule na wawekezaji hawana matatizo na sisi hatuna matatizo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu wakulima wa kahawa, nafikiri ni Mheshimiwa Ndugu yangu James D. Lembeli, kuhusu watu waliokopwa, nimeshajibu.

Mheshimiwa John Momose Cheyo, alikuwa anazungumza juu ya utaratibu wa pembejeo na alikuwa anashangilia kufutwa kwa ule mfumo wa zamani uliokuwa unaitwa *Pass Book* na mimi nilikuwa miongoni mwa wale ambao walikuwa hawautaki kwa hiyo na mimi nimeshiriki kuufuta.

Mheshimiwa Mpina, alisema siku nyingine tulitoka nje ya mkutano, mimi sijatoka naye lakini tulikubaliana kuukataa ule mfumo. Kwa hiyo, ule mfumo haupo ila tunataka mawazo, tuweke mfumo gani mbadala na lazima uwepo. Kwa mwaka huu, watu watanunua na tutaendelea kuweka ruzuku, bei tutashusha. Lakini tumesema dawa hii ipelekwe kwenye kijiji na kama kuna watu hawawezi kabisa kabisa kununua kwa *cash* wajiorodheshe kwenye kijiji, watafute udhamini wa kijiji chao, wakope lakini kijiji kihakikishe wanalipa ili tusirudishe chini uzalishaji wa pamba. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, sikujibu kila swali maana ni vigumu kweli lakini nimetoa ufafanuzi wa mambo makubwa. Mambo mengine ambayo hatutajibu na kama kuna mtu yeyote ambaye anadhani alistahili kujibiwa lakini muda haukutosha, tunaomba atukumbushe, tutampa maandishi kwa kirefu ili ajue hoja aliyoitaka ni hoja gani.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

(*Hoja Iliamuliwa na kuafikiwa*)

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

Fungu 43 - Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika

Kif. 1001 *Administration and General* …………… Sh.1,783,424,200/=

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mimi langu dogo tu. Wakati Mheshimiwa Waziri …

**WABUNGE FULANI:** Kifungu!

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Kifungu hichohicho, tuko wengi na ni utaratibu wa siku zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Waziri anajibu hoja yangu ambayo ameijibu vizuri tu kuhusu mradi wa *DASIP* nilikuwa nataka ufafanuzi wa kina kwa sababu mtindo wa kugawa rasilimali za mradi wa *DASIP*, unazingatia idadi ya Wilaya, ni kwa nini sasa asione ni muhimu mpango wa kugawa rasilimali hizo ukazingatia idadi ya watu kwa sababu Mikoa mingine ina Wilaya chache na ina watu wengi. Kwa hiyo, nilikuwa nafikiri kigezo hicho ni kigezo cha kizamani sana. Ningemwomba Mheshimiwa Waziri afikirie kwa sababu mradi wenyewe bado ni mpya na bado ni mbichi sana, wafikirie kwa heshima zote kugawa rasilimali hizi kwa kufuata idadi ya watu. Naomba ufafanuzi wa suala hili.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, huu mradi ulikwishafanyiwa maamuzi baina yetu na wafadhili wa huu mradi ni wa Benki ya Maendeleo ya Afrika na tulichokubaliana ni mgao wa rasilimali ufuate wingi wa Wilaya na kwa kweli ukienda hata na wingi wa watu bado utakuta tofauti haitakuwa kubwa. Kwa mfano, Mikoa inayohusika ni Mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Kagera, Kigoma na Mara. Bado ukifuata wingi wa watu inawezekana hata wa Shinyanga na wa Mwanza wale wakatunyang'anya wa Mara na Kigoma kwa sababu wako wengi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kilichofanyika ili kuleta usawa kabisa ni kwamba kila Wilaya ilipewa shilingi bilioni 1,450,000/= Kigoma ina Wilaya tatu na ilipewa bilioni 4,350,000/=, Kagera ina Wilaya saba ikapewa bilioni 10,150,000/=, Mara wana Wilaya nne wakapewa bilioni 7,250,000/=, Mwanza wana Wilaya sita ambazo zinashiriki ziko nyingine za mjini ambazo hazimo wanapata bilioni 8,700,000/= na Shinyanga wana Wilaya saba wanapata bilioni 10. Huo ndiyo mfumo wa kufuata Wilaya kwa sababu maendeleo yetu yanasimamiwa na Halmashauri za Wilaya. Sasa tukikaa tuanze kupiga mahesabu ya watu, mimi mimi siamini kama hesabu hizi zitabadilika sana. Kwa hiyo, nataka kumshauri Mheshimiwa Nsanzugwanko tukubaliane kwamba utekelezaji kwa kuwa umeanza na mfumo ni huu na tulikubaliana na *African Development Bank*, tukianza kufumua huu mradi, inawezekana tutauchelewesha. Kwa hiyo, tuendelee na kazi kama ilivyopangwa.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niulize swali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka maelezo tu kwa Mheshimiwa Waziri kwamba katika hotuba yake ameeleza kwamba mafunzo ya cheti yatarudi kwa ajili ya Maafisa Kilimo na hasa ngazi ya Kata na Vijiji. Nataka nijue kwanza, kwa nini walifuta mafunzo haya ya cheti? Hilo la kwanza.

Lakini la pili, hawa watakaopata mafunzo ya cheti, je, Serikali itawaajiri moja kwa moja au tena itabidi baada ya kumaliza mafunzo basi watafute kazi wao wenyewe?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli hii kada ilifutwa, ni katika hiyo niliyokuwa naeleza *structural adjustment programme*, tupunguze ukubwa wa Serikali basi katika kupunguza basi na kada hiyo ikaathirika.

Lakini kwa kweli tukizungumza juu ya kuwapa elimu wakulima na baada ya kujaribu kufanya mazoezi ya kupata watu wa Kidato cha Sita ili ndiyo wasome, tunanyang'anyana na Wizara nyingi sana. Kuna watu wa Elimu, wanawachukua, watu wa Afya wanawachukua na sisi tulipata kama 1000 lakini tulikuwa tunatafuta 3000. Tukiendelea kwa mtindo huo, tunaona hatutafika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu vilevile tulijiuliza hivi kweli mtu aliyesoma *Form Four,* tukimfundisha *certificate,* tukampeleka kwenye kijiji, hivi hawezi kusaidia

wale wakulima kweli? Anaweza! Kwa hiyo, tukasema kwa mfumo huo, turudishe na vyuo vyetu vya kilimo vyote vimeshapokea maombi mengi sana ya *Form Four*. Chuo kimoja cha Kidatu, kinashangaza maana walitangaza wameomba 6000 kwa hiyo inaonekana hawa *Form Four* ni wengi  na tunaweza kufikia lengo la kupeleka kila mtaalamu kila kijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile siyo kwamba *Form Six* hatuwachukui, hapana! Tunachukua *Form Four* na *Form Six* na hao *Form Four*. Mheshimiwa Lediana Mafuru Mng'ong'o, alikuwa anasema watakwendaje sasa wakati hakuna kupanda! *Form Four* anaweza akasoma *certificate* akaenda akasoma *Diploma* baadaye halafu akapanda akaenda Chuo Kikuu, kwa hiyo mfumo wa kupanda upo tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ndiyo maelezo.

**MHE. AZIZA S. ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii, kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa kuuona Mkoa wa Tabora ni Mkoa mmojawapo ambao unaweza ukasaidiwa na kuweza kuzalisha chakula kwa wingi zaidi.

Lakini naomba nimkumbushe Mheshimiwa Waziri kwamba hivi juzi tu Mheshimiwa Waziri alitoa tamko kuhusu Tabora, kwamba isitoe chakula kingi kupeleka Kenya na kutoa ruhusa katika zao la Karanga ziweze kupelekwa Kenya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimfahamishe Mheshimiwa Waziri kuwa hali ya hewa ya Tabora na Mpanda yote iko sawa na ndiyo maana anaona chakula kingi sana kinazalishwa Tabora na tunamshukuru kuiweka Wilaya ya Sikonge ikiwa ni mojawapo ya kupata pembejeo. Lakini naomba nimfahamishe kuwa Wilaya ya Sikonge, Urambo, Uyui na Tabora, hali ya hewa inafanana. Haoni umuhimu wa mbolea hiyo au pembejeo hizo kuziunganisha katika Wilaya hizo ambazo ni muhimu sana na zinazalisha chakula kwa wingi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, eti huoni kweli umuhimu wa kuiweka Urambo katika mpango huo? (*Kicheko*)

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, umuhimu nauona ila uwezo ndiyo haupo kwa sasa. Kwa hiyo, naomba jamaa wa Urambo na Uyui wasubiri ngoja kwanza tuanze na Sikonge ambayo iko karibu sana na Mpanda halafu Wilaya nyingine tutazitengenezea mkakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Tabora ina hali ya hewa zinazosigana sana kwa mfano ukichukua mahali kama Igunga, Nzega ukasema nayo ni Tabora kama Sikonge, kwa kweli nadhani hapa sio kweli. Kwa hiyo, tuanze na Sikonge kwa sababu huu siyo mwisho, tunaanza mahali halafu tunaendelea. Kabla ya uchaguzi tutafika huko.

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nami nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa picha waliyoionyesha kwa wakulima wa zao la pamba jinsi wanavyoonyesha kuwajali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, limekuwepo tatizo wakati wa hotuba ya Waziri Mkuu, nilielezea tatizo la watafiti wangu pale Ukiriguru wamekuwa na mradi ambao umechukua muda mrefu, miaka mingi kweli lakini jibu sijapata na pesa wanazo. Ninapenda Mheshimiwa Waziri anieleze tatizo hasa ni nini? Ili angalau tuweze kuwasaidia hawa watafiti wanafunzi wa Chuo cha Kilimo pala Ukiriguru, wananchi wangu wa Mwalo pamoja na Buganda pamoja na Nyanhorongo, hebu atueleze Mheshimiwa Waziri huu, mradi utakamilika lini?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naujua huo mradi anauzungumzia Mheshimiwa Shibiliti, tatizo ambalo limeuchelewesha ni tatizo la manunuzi kwa sababu ilibidi tufanye kwa kufuata Kanuni za wale wanaotusaidia kwenye ule mradi. Lakini nataka kumhakikishia Mheshimiwa Jacob Shibiliti kwamba tutauvalia njuga ili tuusimamie na tuhakikishe kwamba sasa unatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia upo mradi mwingine unaofafana na huo kule Mringano, Tanga ambao unatoa maji kutoka Jiji la Tanga kupeleka pale na wenyewe utakwenda katika mkumbo huo, tutausimamia kuona kwamba unatekelezwa.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Nina mambo mawili mafupi na ambayo yanahitaji ufafanuzi.

La kwanza ni matumizi ya vocha ambayo Mheshimiwa Waziri anasema tutaondoa mifumo ile miwili ya bei ya soko na ile ya ruzuku jambo ambalo ni jema na mimi nalifurahia sana lakini kule Mbozi kuna wakulima zaidi ya 100,000, sasa Waziri anihakikishie ni namna gani wakulima hawa watapata hizo vocha, utaratibu utakuwa namna gani ili kuondoa tena tatizo lile la kuanza kung'ang'ania hizi vocha kama wote watapata au namna gani mimi nadhani wangependa sana wasikie ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri.

Lakini jambo lingine nilisema kwamba Mfuko wa Taifa wa Pembejeo, unatusaidia sana kukopa zana za kilimo, madawa na kadhalika, lakini mfuko huu umekuwa Dar es Salaam na wakopaji ni wakulima wa kawaida wanatoka vijijini, mbali sana. Anaonaje ku-*decentralise* shughuli za Mfuko wa Pembejeo wa Taifa ili wananchi wengi waweze kufaidika huko waliko.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ule mfumo wa vocha, kama nilivyoeleza, kwa kweli unaanzia kwenye kijiji pale maana hapo ndiyo wakulima walipo, tumeshatoa maelekezo kwenye Mikoa yote ambayo mfumo huu utaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi nilipata fursa ya kuzungumza na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya tukiwa huko Morogoro, wakati tunazindua huu mpango. Tumekubaliana ifanywe sensa tena kwa haraka kati ya sasa kabla kilimo hakijaanza, vitabu vya vocha vimekwishachapwa, tunachotaka kujua Mbozi Kijiji gani tunawapa vocha watu wangapi, hiyo itatusaidia kufanya bajeti ili kujua fedha tuliyonayo kama inaweza ikakidhi na kama

haikidhi tunafanyaje kwa sababu tunajaribu kutafuta fedha nyingine. Huu mpango ni mkubwa ndiyo tumepeleka *on emergence basis* maombi *World Bank,* inawezekana *World Bank* waka-*respond* kwa sababu Rais wetu ametusaidia kupeleka barua yeye mwenyewe *in person*. Kwa hiyo, inawezekana, tukaongezewa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo basi, tukishajua kiwango gani cha watu, katika muda wa mwezi mmoja ujao, itatusaidia sana lakini tunataka huyu mwenye sifa ya kupewa atokane na kijiji, Halmashauri iseme sisi watu wetu ni hawa, idadi yao ndiyo wenye sifa kwa kufuata masharti tuliyopeleka halafu Mkutano Mkuu wa Kijiji ukubali hiyo orodha ili mtu mmoja asije tena akasema unajua tukisema vizuri na mimi nitaingizwa. Ni Mkutano Mkuu maana unaweza kuwa huna ardhi au wewe hulimi mahindi lakini na wewe unataka vocha kwa kweli hatuna fedha za kupeleka kwenye mazao mengine kwa sababu shabaha yetu ni hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nadhani Mheshimiwa Godfrey Zambi akitaka maelezo zaidi, tunaweza tukazungumza kwa sababu yeye yupo Mbozi anaweza kwenda kutusaidia zoezi hili ili liweze kufanikiwa vizuri zaidi lakini tunataka mkulima anayeandikishwa na vocha tuzipeleke kulekule kwa Katibu wa Kijiji ndiye anayeziandika na Mwenyekiti wake anaweka saini na Bwana Shamba na huyu anayepewa vocha mkulima naye anasaini. Kwa hiyo, kunakuwa na saini kama nne hivi. Hiyo ni 20,000 na 40,000 sasa watu wanne wote waweke saini kutaka kuiba 40,000 nadhani itakuwa ngumu kidogo. Lakini hakuna mfumo ambao ni 100% *perfect* maana umetengenezwa na binadamu lakini ngoja tuanze tuone sisi tunaamini kabisa kwamba mfumo huu unaweza ukatusaidia kuondoa hii habari ya kusema hii mbolea ya ruzuku na hii siyo lakini huu ndiyo utaratibu ambao tutaufuata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mfuko wa Pembejeo, tumesema kwenye hotuba yetu kwamba tunaandaa Muswada wa kuleta mabadiliko katika mwenendo wa huo mfuko. Wakati huo ukifika maana *issue* yenyewe ya ku-*decentralise* wala siyo tatizo, tatizo ni uwezo wenyewe wa mfuko, unaweka shilingi milioni tatu kwa mwaka, utafungua Ofisi ngapi? Ukifungua Ofisi nyingi sana zile hela zote zinaweza kutumika kwa utawala wa hizo Ofisi, ukakosa mkopo. Kwa hiyo, acha tubadili mfumo wa Sheria halafu tutazame uwezekano wa kutumia huo mfuko na kuwekeza kule zaidi halafu tunaweza tukafanya mabadiliko ambayo Mheshimiwa Godfrey Zambi anayapendekeza.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza, napenda kusema kwamba naunga mkono sasa rasmi hoja ya Waziri wa Kilimo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingawa ninazo hoja chache zilizobaki hazijatolewa ufafanuzi na Mheshimiwa Waziri, kwanza, kama nilivyozungumza mimi na katika kitabu chake cha hotuba amelizungumzia suala la kuiondosha *Pass Book* baada ya matatizo yake na malalamiko mengi ya wakulima lakini amebainisha wazi kuwa wakulima walipunjwa na kwa kuwa wakulima walipunjwa sasa je, kama Serikali yenyewe inajua kwamba wakulima wake walipunjwa inao mkakati gani wa kufanya tathmini ili kujua mapunjo hayo ni kiasi gani ili wananchi waweze kulipwa fidia na malalamiko ya wananchi wangu

wa Kata ya Rubiga, Itinje, Mwabusalu, Mwandoya, Lingeka, Mwabuma, Sakasaka na kwingineko nchini ili madai ya pamba yaweze kumalizwa?

La pili, nilitaka kujua ni kwa nini Serikali inapanga utaratibu wa msimu wa pamba mwezi wa sita tena mwishoni ni karibia tu na kusema kwamba ni Julai, lakini wakati huohuo pamba inaiva mwezi wa nne na katika takwimu inaonyesha kwamba katika miezi ya Aprili na Mei bei ya pamba huwa iko juu je, Serikali haioni kwamba utaratibu huu kama ulikuwa unatumika kule nyuma sasa umepitwa na wakati na irekebishe muda huo?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza hili la mapunjo, tulishaanza kulishughulikia siku nyingi na katika maeneo mengine kama Maswa, wakulima msimu uliopita walikuwa wanapewa dawa zaidi kuliko fedha iliyokuwa kwenye *pass book* ili kufidia zile za nyuma. Tulikwishatoa maelekezo kwa Bodi ya Pamba, kama tatizo hili bado ni kubwa sana katika eneo analotoka Mheshimiwa Mpina, tunaiagiza Bodi ya Pamba ishirikiane na uongozi wa Meatu ili tuone ni kiasi gani cha watu wamepunjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile liko tatizo wanasema kuna wengine waliongeza hela wakafoji sasa wasije wakasikia hii kauli halafu wakafoji zaidi. Kwa hiyo, tunawaambia wakifoji zaidi itakuwa ngumu kutekeleza hii kauli maana kuna kushtakiwa ukifoji na wewe vilevile kwa lugha ya Mheshimiwa Hamisi Ally, unaweza kuwa fisadi, kwa hiyo itabidi naye ashughulikiwe kama anafoji. Kwa hiyo, waende watu ambao kweli wana tatizo *genuine*, halafu Bodi ya Pamba tunaiagiza ifanye tathmini.

**MWENYEKITI:** Kuhusu msimu.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu msimu, tarehe za mwisho wa mwezi wa sita, maelezo yake siyo makubwa sana. Kwanza mwezi wa nne, kwa kweli katika Mikoa ile ya pamba huwa kuna mvua na uchukuzi wa pamba kutoka Vijijini unakuwa mgumu sana kwa sababu mawasiliano nayo ni *problem*. Hilo ni tatizo moja ambalo lipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile wengine wanapanda pamba, Desemba mwishoni, wengine Januari, inapofika mwezi wa Nne, huwa inaanza kutoa pamba lakini bado haijawa safi sana, wakianza kuinunua watachukua hata ile ambayo si safi sana wapeleke. Nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mpina kwamba kama mwezi wa Sita mwishoni inaonekana ni mbali sana tutajaribu kuangalia, kushauri na Bodi ya Pamba tuone tunaweza kuanzia wakati gani maana si tatizo kubwa sana la sera. Lakini wakati ule bei huwa ni kubwa kuliko mwezi wa Sita, labda nimwambie Mheshimiwa Mpina kwamba, wale wanaonunua pamba huwa wanauza pamba kabla hawajainunua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, bei ikiwa nzuri mwezi wa Nne wanauza, wanaita *forward sell*, wanafanya mikataba kwa bei iliyopo wakati ule. Hawa ni wajanja tu hata wanavyokataa kuongeza, wakati mwingine huwa tunawabana kwa sababu huwa tunawajua, huwa wanauza huo mwezi wa Nne bila kuwepo pamba. Kwa hiyo,

wakishasaini hiyo mikataba na bei nzuri hawana sababu ya kutomwongezea mkulima bei nzuri, lakini tutashauriana ili tuone jinsi ya kufanya.

**MHE. DR. BINILITH S. MAHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nachangia kwa maandishi pamoja na kuishukuru Serikali kwa kufufua zao la pareto, nilitoa mapendekezo kwamba, kwa kuwa mwekezaji wa sasa ambaye anamiliki Kiwanda cha Mafinga ndiye anayepanga bei za pareto kwa kuzingatia kiwango cha sumu kilichomo kwenye ua la pareto na kwa kuwa yeye ndiye mwenye maabara za kupima hiyo sumu suala ambalo limeonyesha maslahi ya wananchi au wakulima wa pareto wa Mikoa ya Iringa, Mbeya na Arusha kutozingatiwa ikilinganishwa na suala la wachimbaji wa madini ambao wakichimba wanakwenda ku-*test* kwenye maabara zao Ulaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nikatoa mapendekezo kwamba, ni vizuri Serikali ikajenga maabara yake kwa ajili ya ku-*test* hiyo sumu lakini nikaendelea kusema kwamba ni vizuri hii zao likawa *processed* kwa kikamilifu ili tukatoa mali ambayo inaweza kuuzwa ikiwa imekamilika. Naomba ufafanuzi, ahsante sana. (*Makofi*)

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wa ununuzi wa zao la pareto, ni *unique* kidogo kwa sababu mnunuzi ni mmoja, ni kiwanda kipo pala Mufindi, ndiye anayenunua, anaye-*process* na ndiye aliye na maabara. Sasa hoja ya Mheshimiwa Dr. Mahenge kwamba tutengeneze maabara yetu wenyewe, ni hoja nzuri lakini si kwamba utekelezaji wake unaweza kuwa wa mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa hivi, habari nilizonazo ni kwamba pamoja na kuwa hatuna uhakika kwamba wakulima wale wanalipwa kwa haki lakini bei ya pareto imeongezeka sana ukilinganisha na miaka ya nyuma nadhani inakaribi Sh. 900/=, kuliko ilivyokuwa Sh. 500/= na kadhalika na kwa kweli pamoja na kwamba huyu mtu wa kiwanda ni mtu binafsi lakini nadhani naye amechangia katika kufanya zao la pareto liongezeke maana lilikuwa limekufa hili zao, lilifika mahali pagumu sana. Kwa hiyo, niko tayari kukutana na wadau wa zao la pareto ili tuje tuzungumze tuone utaratibu gani unaweza kuwapa maslahi wananchi hata ikibidi hata kabla hatujaweka maabara, tunaweza kuwa na *association* ya wakulima wakawa wanawakilishwa katika kujua kama ile maabara kweli inapima sahihi na kile kiwango cha sumu kinacholipiwa kweli kipo sahihi, hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kuhusu kutengeneza kiwanda ambacho kitaweza ku-*process*, huyo huyo mwekezaji yupo tayari kuwekeza, kutengeneza mazao yanayotokana na pareto na kwa sababu hatuna njia nyingine nadhani Mheshimiwa Dr. Mahenge, tuko tayari kukutana na wadau tuzungumze, tuone tunaweza kufanya nini, lakini tunamkaribisha yule bwana awekeze ili badala ya kuuza pareto *semi processed*, tuwe tunauza pareto ambayo ni sumu yenyewe ambayo tayari imeshatengenezwa.

**MHE. DR. LUKA J. SIYAME:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa miaka kumi iliyopita, kilimo cha pamba kilipigwa marufuku Wilayani Chunya na maeneo yanayolizunguka Ziwa Rukwa Wilayani Mbozi kutokana na kuwepo kwa mdudu wa

pamba aitwa *Cotton Red Weevil* aliyekuwa anapatikana nchini Malawi lakini hadi leo kule Malawi bado wanalima pamba. Je, ni hatua gani zinachukuliwa kufufua kilimo cha pamba Wilayani Chunya ili kuweza kukifanya Kiwanda cha Pamba kifunguliwe pale Mbeya na wananchi wa Wilaya ile na Mbozi ambao sasa hivi wamejikita kwenye uvuvi wa samaki na kuliwa na mamba waanze kujipatia kipato kutokana na kilimo cha pamba? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Poleni sana. (*Kicheko*)

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba Mungu nisiulizwe swali hili leo kwa sababu swali hili lina *controversy* nyingi sana. Yapo mawazo ambayo si sahihi sana ya kufikiri wananchi wa maeneo hayo wanazuiwa kulima pamba kwa makusudi na wengine wanafikiri labda wenye pamba huko hawapendi kuwa na wenzao huko Kusini, hiyo si sahihi hata kidogo. Kwanza pamba yenyewe kulima ni tatizo kubwa sana, naijua ni *fatigue* na malipo yake ndiyo haya tuliyozungumza na Cheyo. Unalima, unapanda, unapalilia mara tatu, unapuliza dawa, unamaliza unauza, halafu unang'oa miti na unaanza tena, wala si kazi rahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa kweli kwa nia njema kabisa, tungewakaribisha watu wa Kusini nao walime, wapate tabu kama wanayoipata wale wanaolima lakini wataalam wanaofanya utafiti wamemaliza ule utafiti na taarifa za awali zinaonyesha kwamba yule mdudu sasa amechachamaa zaidi kule Kusini, yaani ameongezeka na kuna miti inaitwa pamba pori, maana yule mdudu anakuwa *hosted* na pamba pori na pamba yenyewe na sasa hivi yupo kwenye pamba pori.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wataalam wale wanasema ukilima kule pamba, anahama kutoka kwenye pamba pori anakwenda kwenye pamba halisi. Hili ni suala la kiuchumi kabisa, ni la kisayansi lakini vilevile ni la kiuchumi kwamba ili uweze kumdhibiti mdudu huyo lazima tufanye *costs* ili tuone mkulima huyu tukimruhusu kulima pamba na akawa anahitaji madawa ya kupambana naye kwa eka moja atatumia fedha kiasi gani na atapata ngapi? Tufanye *economic analysis*, hiyo haijafanyika, lakini utafiti ule wa awali wa kisayansi umemalizika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa tunafanya *economic analysis* halafu tushauri, kama ni busara kulima basi walime, kama inaonekana kiuchumi si busara twende kwa wenzetu tukawaambie hiki kitu hakiwezekani tutafute zao lingine. Maana hata pamba yenyewe huko inakolimwa ni tabu, kwa hiyo si jambo la kushangilia sana, natoka Bunda ambako kuna pamba ningeweza kupata korosho nikalima kule, ningewaambia wapiga kura wangu tulime korosho sasa, naona hii pamba kulima kwake ni tabu, lakini ngoja tumalize utafiti wenzetu wa Chunya na maeneo mengine, tutayatoa.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nimhakikishie Mheshimiwa Waziri mwenzangu kwamba, nilijaribu kumsaidia hapo kwa kumwonyesha upungufu, yale ambayo sikuyaonyesha, labda hafanyi vibaya sana, kwa hiyo asiwe na wasiwasi.

**MWENYEKITI:** Kwa lugha ya pamba kuna pamba pori na pamba halisi. Endelea Mheshimiwa.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza suala la takwimu. Nashukuru Mheshimiwa Waziri hapa amethibitisha kwa mazao ambayo nilieleza kwamba yameshuka kwa kutoa sababu kwa mfano pareto, kwamba iling'olewa miche yote na mhogo ulipata ugonjwa na ndizi vilevile. Lakini kinachoshangaza katika kitabu chake kwa mazao hayo hayo ambayo kaeleza sababu za kushuka, kasema yamepanda, kwa mfano pareto amesema imepanda, pia zao la sukari kasema limepanda wakati nilisema limeshuka. Sasa kwa bahati nzuri nilizungumza na baadhi ya Wenyeviti wa Bodi za Mazao hayo na wamethibitisha hivyo kwamba haya mazao yameshuka. Kwa hiyo, ningependa maelezo zaidi labda takwimu zake zina matatizo au vipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu deni la Mfuko wa Pembejeo. Mheshimiwa Waziri anafahamu kwamba Kamati yetu ilitembelea katika maeneo yale ya Mfuko wa Pembejeo na tulipata ripoti rasmi ya hali inavyoendelea kule na hizi takwimu ambazo nimezitoa ni za taarifa hii ya Mfuko wa pembejeo kwamba walikopesha Sh.18.5bn/= waka-*recover* asilimia arobaini ambayo ni Sh. 8.5bn/=, kwa hiyo zimebaki Sh. 10bn/=, hizi ndiyo nilikuwa nahoji, nani wahusika na hatua gani wamechukuliwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu…..

**MWENYEKITI:** Ni mawili tu ndiyo utaratibu.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Hayo mawili Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani zile takwimu za pareto Mheshimiwa Khamis alichukua za mwaka jana ambao ndiyo tulikuwa tumeng'oa halafu tukapanda upya, hizi nimeleta *current*, kwa hiyo, kwa namna yoyote zile haziwezi kukubaliana maana wewe unakwena na *base* ya tofauti na mimi nina mwaka mwingine na nadhani alikuwa anapenda kutafuta zilizoanguka sana ndiyo maana hakutaka kuona hizi zilizoongezeka lakini sisi tumekwenda na miaka miwili tofauti kabisa. Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mfuko wa Pembejeo, nimesema kwamba, baada ya kufanya utafiti, unajua hii *recovery* ya madeni kila mwaka tuna-*recover* zaidi. Kwa hiyo, tumeuliza ule Mfuko na tumepata ushahidi kwamba fedha ambayo bado inadaiwa ni Sh. 5bn/= na vilevile watu ambao wanadaiwa wanajulikana na wengine kesi zao ziko Mahakamani na wengine dhamana zao zitauzwa ili kurudisha zile fedha. Hiyo nimeeleza, kwa hiyo, hakuna kitu ambacho kinafichwa na katika suala la kudaiwa hakuna cha kigogo wala nani, wewe ukikopa unadaiwa, ni wewe uliyekopa, huwezi kusema

unajua mimi ni Spika, nimekopa kwa hiyo mimi ni kigogo. Hakuna cha kigogo, kama umekopa unalipa, usipolipa tunauza dhamana.

**MWENYEKITI:** Mara nyingi vigogo wapo Serikalini sisi wengine, basi… (*Kicheko*)

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba nichukue nafasi hii kwanza kumshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kutamka kwamba Serikali itaanza kufuatilia suala ambalo ni kero kubwa kwa wakulima wa tumbaku wa Wilaya ya Urambo na Mkoa wa Tabora kwa ujumla. Inasikitisha kuona kwamba Serikali inakuwa wapi mpaka makampuni kutoka nje yanakwenda kuingia mikataba ya ajabu na wakulima wetu, mikataba ambayo ni ya unyanyasaji, ukandamizaji kiasi hiki, kiasi kwamba inapelekea wakulima wetu kuendelea kuwa maskini bila kufaidika na kilimo chao, naomba Serikali iwe makini kwenye suala kama hili katika mazao mengine na wakulima wa mazao mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Waziri atuambie kwamba kwa kuwa wakulima wa tumbaku bado mikataba hii inaendelea kuwabana na hawataishia kuendelea kudaiwa kwa sababu kila siku wanapewa pembejeo na yale mazao wanayozalisha yanaendelea kulipiwa pembejeo badala ya kuendelea kuwalipa wao ili waendelee kunufaika, tunaomba kujua kwamba ni lini Serikali itavunja mikataba hii na makampuni haya ili wakulima hawa wawe huru na ikiwezekana watafute maajenti wengine watakaonunua tumbaku yao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine dogo, kwenye mchango wangu nilipenda kujua kuna uhusiano gani kati ya Wizara hii ya Kilimo pamoja na sekta ya Utalii hapa nchini. Ni kwa nini kwenye mahoteli ya kitalii vyakula karibu vyote vinatoka nje na wakati wakulima wetu hapa wanalima mbogamboga, matunda na nafaka? Naomba ufafanuzi. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kuhusu lile suala la tumbaku, utaratibu wa kuwa na *contract farming* upo duniani, tunachokataa sio *contract farming* yaani kilimo cha mkataba, tunachokataa ni mfumo ambao upo ndani ya mkataba wa wakulima wa tumbaku na hayo makampuni lakini kusema kwamba tuyaondoe makampuni hayo, tutafute wanunuzi wengine duniani humu tumbaku haina makampuni mengi yanayonunua, haya yaliyoko hapa yapo Malawi na kila mahali ambako tumbaku ipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Kenya kuna kitu kinaitwa *Alliance One* na Morogoro ipo, kuna nyingine inaitwa *TLTC*, iko kila mahali duniani na hapa ipo, ukiwafukuza hawa unaweza kuwa na tumbaku bila mnunuzi. Kwa hiyo, *issue* hapa ni kuweka mahusiano ya haki nasi na tunadhani namna moja ya kuweka mahusiano ya haki, ni kuondoa mfumo wa pembejeo kupitia kwao ili pembejeo zipitie benki na mikataba kwenda kwenye Vyama vya Ushirika vya wakulima wa tumbaku. Hilo ndilo tunafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tuliachaje wakaingia, walishaingia maana ndiyo wanaonunua tumbaku, sasa unawafanyaje? Unawaambia msiingie wakati wameshaingia,

wapo? Sasa tunarekebisha kile ambacho kipo, tulidhani wakiingia watafanya mambo vizuri na kwa sababu ndiyo wanunuzi wa tumbaku pekee duniani sijui tutawafanyaje, hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kwamba tutavunja lini mkataba, wala hatuvunji mkataba, tutarekebisha tu, kwa sababu mikataba ile si ya kudumu, ni ya msimu, kwa mfano, wakulima wa Chunya mwaka huu wamejitoa kwenye ule mkataba, kulikuwa na ubishi tumeuamua hapa, wamesema watakwenda kukopa katika Vyama vyao vya Ushirika, *CRDB* imewakopesha pembejeo kwa mara ya kwanza, kwa hiyo watu wa Chunya wamejikomboa, kwa hiyo, mwakani watakuwa huru kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale ambao hawajajikomboa ambao watakuwa bado, ni wakulima wa Mpanda au Kigoma. Ndiyo nimesema, tutakaa nao pamoja na wanunuzi tuulize hiyo bei ya kuwakomboa ni shilingi ngapi, tuone kama bei ni kubwa sana basi tutazungumza, kama ni ya kawaida tu basi tutawakomboa lakini mtupe muda tuone namna ya kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uhusiano wetu na Wizara ya Maliasili na Utalii, mgawano wetu wa kazi ni sisi kuzalisha, wao kununua ndiyo uhusiano wetu, lakini kuna soko ambalo ndilo linanunua mazao haya. Kwa hiyo, wale watu wa biashara wakichangamkia, wawe wananunua mazao yetu halafu wafanye mikataba na mahoteli, wao watauza na tumesaidia kuunda chama kabisa, Umoja wa Wakulima wa Mazao ya Bustani ambao wanaweza kukutana wakazungumza. Kwa hiyo, naunga mkono mawazo ya Mheshimiwa Sakaya kwamba lazima tufanye zaidi ili kuhakikisha kwamba mazao yetu yanayozalishwa hapa ndiyo yanatumika katika mahoteli yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mahoteli yale yana tabia ya kuagiza hata maji ya kunywa, Rais wetu alikwenda wakampa maji ya kigeni, akakataa kunywa kwa sababu maji yapo hapa Tanzania. Kwa hiyo, si mazao ya kilimo tu ni pamoja na bidhaa zingine zinazozalishwa hapa nchini. Kwa hiyo, nakubaliana naye kwamba nafikiri wakati sasa wakati umefika, lakini *supermarket* zetu zimeanza kupokea mazao ya kilimo, ukienda kwenye *supermarket* za Dar es Salaam utayakuta, yameanza kuingia, ni hatua lakini polepole tutafika.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza, nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa ustadi wake zaidi leo katika kujibu maswali, sijui amelala vizuri wapi lakini nampa hongera sana. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati ambapo nachangia, nimezungumza sana juu ya *issue* ya kuwapa wakulima habari za awali, *early warning*, kwa sababu mkulima kama anaweka fedha yake akitegemea mwaka kesho bei itakuwa Sh. 500/=, sio ameshatumia fedha yake na pia ametumia nyenzo nyingine mbalimbali halafu anaambiwa sasa bei imeteremka, huku si kutoa haki kwa wakulima na uwezo huu Serikali inao na pia kuwahamasisha hata wale wanunuzi na yeye ni *expert* kwa mambo haya, kwamba wauze

ile pamba yao mapema, Mheshimiwa Waziri, anajua maana amekulia humo humo. Kwa hiyo, naomba anieleze huu utaratibu ataanza lini? Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia sikatai kwamba kunapokuwa na njaa basi chakula kisitoke nje, nilichokuwa nasema kama basi hawatatoa chakula walicholima na wametumia fedha basi tunapotoa hiyo amri pia tuwe na *guarantee*, tuweze kuwaambia wakulima tutanunua sisi kwa sababu usipofanya hivyo ndiyo kusema wakulima watapoteza fedha na vitu kama hivyo!

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini zaidi unapokataza vitu vingine ambavyo ni nusu chakula kwa mfano ufuta, karanga, sijaona mtu amemwalika mwenzake kwa mlo wa karanga au ufuta. Sasa hii ni njia mojawapo pia ya kuwasaidia wakulima kuondokana na zao moja tu. Napenda Waziri atofautishe hilo na aseme wazi kabisa kwamba ufuta soko huria uza, karanga soko huria uza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufafanuzi kwa hayo.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa swali la kwanza kuhusu *early warning*, sidhani kama kweli tunaweza kumpa mkulima *early warning* kabla hajalima maana *issue* ya *early warning* ina-*make sense* kwake kabla hajalima na anaanza kulima mwezi Novemba, kwamba mwezi Novemba unaweza kufanya *prediction* ya soko itakuwaje mwezi wa tano mwaka unaokuja ni muda mrefu sana kwa *circulation* ya masoko hayo. Kwa hiyo, kwa kweli hiyo ni *problem* kidogo.

Lakini labda lile alilolisema Mheshimiwa Mpina la kwamba tuwahishe msimu, labda tulitazame hilo lakini mfumo tunaoutumia wa *early warning* ni kukutanisha wanunuzi na wakulima na Bodi ili kuona bei inayotuongoza iwe kiasi gani. Tumefanya hivyo mwaka huu lakini mwaka huu kumekuwa na matatizo kwa sababu wanunuzi hawa na benki wanasema tena nayo imo ndiyo maana mambo yamekuwa si mazuri lakini mwaka jana ulikuwa safi hatukupata matatizo. Kwa hiyo, kwa sababu tunajifunza kutokana na matatizo, ngoja tumalize mwaka huu tuone tunaweza kuchukua hatua gani za kurekebisha hali hii ili mambo yasiwe mabaya sana kwa wakulima wa zao la pamba. Nataka kutumia nafasi hii vilevile kuwaomba wakulima wa pamba wajue kwamba Serikali yao ipo pamoja na wao, hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, juu ya ufuta na karanga kwamba Mheshimiwa Cheyo amesema hajaona watu wanaalikana kula, hiyo ni kweli, kumwalika mtu kula karanga tu itakuwa ngumu kidogo lakini hatukuzuia karanga, ufuta wala choroko bali tumetumia mazao mengine ambayo yanaitwa ya chakula pamoja na maharage tumezuia kwa sababu ni chakula tena chakula kikubwa sana. Kwa hiyo, hayo ndiyo tuliyozuia na nia yetu ni njema nimeshaieleza lakini mazao ya *horticulture* tumeruhusu yaani mazao ya bustani. Mwanzoni Polisi walipoanza walikuwa wakali kweli, wakawa wanawakamata hata wale walio na nyanya, lakini tumeruhusu *horticulture*, choroko, karanga na mazao

yote ya mafuta kwa sababu vilevile pamoja na kula tunatakiwa kupata fedha ya kigeni na tuna-*promote* mazao yale ili tupate fedha ya nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Cheyo kwa kusema nimejibu kwa ufasaha na kwa upole. Unajua huwezi kupigana vita kama haipo, utakuwa mtu wa ajabu, wewe unapigana tu, unapigana vita wakati vita ipo ama sivyo utastukia unapigana mwenyewe. (*Kicheko/Makofi*)

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kwa ajili ya ile *early warning*, Mheshimiwa Waziri amefanya kazi kwenye pamba, ukiangalia hata kwa bei ya pamba kuna bei ya mwaka huu, bei ya mwaka kesho na hata bei ya miaka mitatu mbele. Labda nitaridhika akiniambia atarudi walifanyie kazi maana yake si kwamba halijafanyika linaweza kufanyika, nitaridhika akisema atarudi alifanyie kazi sina matatizo nalo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini juu ya ufuta wale basi wa Sirari na sehemu zingine kwenye mipaka, naomba Waziri atamke sasa kwamba waache kuwakamata watu wanaouza ufuta na karanga. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshasema hatuzuii, kwa hiyo hawawezi kukamatwa na kama wamekamatwa wataachiwa lakini wasiweke karanga halafu chini wakaweka mahindi, maana tuna *problem* hiyo, wasiweke juu karanga halafu chini mahindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pengine nitumie nafasi hii kueleza jambo moja ambalo limesemwa, lakini lilikuwa halijajibiwa vizuri, Rais wetu aliombwa na Serikali ya Kenya, walikuja *delegation* kabisa wakamfuata kule Mkinga, sasa alipokubali tuwauzie tani elfu nne, magazeti yakasema kuna *contradiction* kati ya kupiga marufuku na kuuza chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusema katika tabia za Waafrika, majirani kuombana chumvi, ni jambo la kawaida. Hivi kweli Rais wa Kenya ametuma *delegation* kwa Rais wetu, amwambie hakuna ondoka huko. Mambo hayaendi hivyo duniani. Kwa hiyo, Rais aliidhinisha na aliwaambia, maombi yenu mnayoomba hatuna uwezo wa kuwapa, lakini nitawapa *token* kwa ajili ya kuheshimu kanuni za ujirani mwema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii haipelekwi na mfanyabiashara, ni *SGR* tunaiuzia Serikali ya Kenya, ni *Government to Government*, yule aliyekuwa anangojea tenda hakuna tenda katika hili na tuko *serious* kwa sababu watu wetu lazima wale. Haiwezekani tukaruhusu watu wakafa kwani wakifa hapa tutakuwa *more responsible* kuliko lawama ya kusema haturuhusu, hilo moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lile la *early warning*, namwomba Mheshimiwa Cheyo tushirikiane atupe naye uzoefu wake, yeye anataka tufanyeje, maana zamani tulikuwa tunatangaza bei kabla hawajalima, Waziri wa Kilimo alikuwa anasema mwaka huu bei itakuwa *so much* lakini mfumo huo hauwezi kufanya kazi kwa sababu Serikali tulijitoa katika mfumo wa kupanga bei. Mfumo huo ulikuwa unawezekana wakati wa ukiritimba na hata unaposema *early warning* husemi kwa kweli Wizara ya Kilimo iseme, labda unasema Bodi ishauriane na wanunuzi mapema halafu watazame *trend* halafu waseme tunadhani hali inaweza kuwa hiyo

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ni hivyo, tunaweza kuzungumza, lakini kwenye pamba nimesema tunaanza ku-*study* juu ya mfumo wa stakabadhi ghalani ambao ukianza kutumika inawezekana na hii *problem* itaondoka kwa sababu hapa kuna *force* zinapingana, kuna wanunuzi binafsi wanataka faida kubwa na kuna wakulima wanalima kwa gharama lakini hawaonani. Kwa hiyo, lazima *referee* aingilie kati aone tunaweza kuweka mfumo gani ambao utawapa haki wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefanya hivyo kwenye korosho na wote, hata wale waliokuwa wanapinga sana kwenye korosho walikuja wakasema huu mfumo mzuri kwa sababu hatupeleki fedha vijijini kununua. Tukasema acheni kupeleka, acheni wanunue hawa wa Vyama vya Ushirika, halafu ninyi mje mnunue kutoka kwao, *it is working*. Kwa hiyo, nafikiri tuzungumze nami ni mdau wa pamba, kwa hiyo, asipate tabu sana.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuomba ufafanuzi katika masuala ambayo niliyaandika katika mchango wangu wa maandishi, nayo ni mawili.

La kwanza, ni kuhusu Benki ya Wakulima. Nimemsikiliza Mheshimiwa Waziri akizungumzia suala hili lakini inavyoelekea ni kwamba, tatizo ni mtaji na mtaji huu unakuwa tatizo kwa sababu Serikali inataka itoe kwenye fedha zinazotokana na kodi na kipato chetu cha kodi kina mambo mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilikuwa naomba kupata ufafanuzi, kwa nini Serikali isizitake Benki za Biashara katika faida zake ambazo zinapata zitenge fungu maalum kwa ajili ya kukopesha wakulima kwa muda mrefu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kuna suala la Hati Fungani za muda mrefu. Serikali ikitoa Hati Fungani za muda mrefu ikipata fedha hizo izipeleke kwenye Benki ya Wakulima. Naomba kupata ufafanuzi juu ya hayo mambo mawili. Lakini hili ni moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, katika mchango wangu wa maandishi, nilisema Wizara kwamba inatumia fedha nyingi sana kuagiza mbolea kutoka nje na leo hii katika maelezo yake Mheshimiwa Waziri, ametuambia kwamba hata *World Bank* itatupa fedha

kwa ajili ya hili la mbolea.  Lakini hizo fedha tunazitumia kuagiza mbolea wakati hapa nchini tuna malighafi za kutosha kuanzisha viwanda vya mbolea.  Kwa nini tuzitumie fedha hizo kuanzisha viwanda vya mbolea?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupata ufafanuzi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi, muda unaanza kukutupa mkono sasa.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa utanisaidia kweli! Hapa naomba muda unisaidie kweli kweli! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Siraju Kaboyanga ni mtaalam wa mambo ya *Banking*, na sasa anataka kuniingiza katika mgogoro kwa sababu haya mambo anayoniuliza ni mambo yanayosimamiwa na Wizara ya Fedha na kwa kweli mambo ya *banking* na mambo ya kuuza *bonds* ni mambo yanayosimamiwa na Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoweza kusema hapa ni kwamba tumekubaliana kimsingi kwamba itaanzishwa Benki kwa ajili ya kugharamia Sekta ya Kilimo. Itaanzishwa namna gani?  Nani ataingiza fedha mle? Hiyo itakuwa ni hoja itakayoamuliwa na Serikali kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nadhani Mheshimiwa Siraju Kaboyonga anachotaka kujua ni kama tunakubali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa juu ya *TIB*, Serikali imesema kupitia Waziri wa Fedha kwamba tunaingiza shilingi bilioni 50 na jana nilizungumza na Mheshimiwa Waziri wa Fedha, akanihakikishia kwamba ameanza kupata fedha za kuingiza zaidi ya shilingi bilioni 50 ndani ya *TIB.* Ameniambia, nilikuwa namtafuta anieleze, kabla sijaja kujibu hapa, kwa hiyo, nadhani tupo kwenye *right track* katika jambo hili.  Lakini tujipe muda kwa sababu kuanzisha Benki ni jambo ambalo linahitaji *study*, linahitaji vitu vingi. Lakini tutaanza na *TIB*, halafu baadaye tutaenda mbele zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juu ya malighafi, kwa nini tunanunua mbolea kutoka nje? Kwanza, Serikali hainunui mbolea kabisa. Mbolea inanunuliwa na makampuni, isipokuwa mwaka huu kwa sababu ya ufanisi Tanzania *Fertilizer Company* ndiyo tumeipa kazi kubwa zaidi ya kununua mbolea ya  Mijingu na kuisambaza.

Kwa hiyo, ukienda Kusini nyanda za juu utakuta malori ya *TFC* yanakwenda kule hivi sasa yanapeleka mbolea ili ikifika wakati wa kilimo iwepo kule kule wakati wanaanza kulima.  Hata *TFC* nayo ni Kampuni ila ipo *owned* na Serikali, lakini Serikali yenyewe *per say* haiagizi mbolea.  Sisi bajeti yetu tunakwenda kumsaidia mkulima ainunue mbolea iliyokwishaagizwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuwekeza juu ya viwanda, tunayo malighafi, tunayo Minjingu *phosphate* ambayo tunakaribisha watu ambao wanaweza kushirikiana na watu walioko pale kupanua. Tunayo gesi ambayo makampuni mengi sana yameonyesha *interest* ya kutaka kuja kutengeneza mbolea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda kwa taarifa yake Mheshimiwa Siraju Kaboyonga tarehe 31 Julai, 2008 na Kampuni ya Wana-Nigeria ambao wao wamesema wapo tayari kuanza hata kesho, wanakuja na mimi nimewakaribisha waje tuzungumze.

Kwa hiyo, yapo makampuni ambayo yapo tayari kuwekeza na sisi katika hili tunawapa nguvu. Yapo makampuni mengi yanafika kama 12 nasikia. Hakuna ukabila katika kuwekeza. *No tribalism in investment*. Yeyote anayekuja ilimradi aweze kuwekeza na masharti yetu anayakubali, tunazungumza naye. Sasa huwezi ukasema utazungumza na Wazungu ukatae Waafrika, hiyo siyo *fair*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninasema Serikali inalipa suala la kuwekeza katika mbolea umuhimu mkubwa. Kwa hiyo, tujipe muda. *(Makofi)*

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Mchango wangu upo katika upande wa korosho. Kwa hili nataka kumpongeza kwanza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo kwa utaratibu mzuri ulioanzishwa mwaka huu wa Stakabadhi Ghalani ambapo wakulima wa korosho wameupenda sana na wengi wamepata fedha za kutosha kutokana na utaratibu huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sasa kulikuwa na suala la *export levy*. Hii *export levy* kwa karibu miaka mitatu, Serikali ilikuwa inachukua fedha za wakulima wa korosho bila kuwarudishia. Sasa nataka leo wasikie wenyewe, Mheshimiwa Waziri anasema nini? Atawalipa lini ile asilimia 6.5 ambayo kwa kweli ilikuwa ilipwe kwa wakulima wa korosho kwa Halmashauri zao ili ziweze kuagizia mbolea na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, linalofanana na hilo ni kwamba: Je, Serikali kwa misingi tu ya utawala bora, kama imetumia fedha za wenyewe kwa kipindi hiki chote italipa riba au fidia kwa Halmashauri zilizokosa mabilioni ya fedha ambazo mpaka sasa hivi zipo Serikalini?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajibu kwa kifupi kwa sababu suala hili lilikwishazungumzwa hapa Bungeni wakati Mheshimiwa Waziri wa Fedha anawasilisha Bajeti ya Serikali na kwa kutumia *Hansard* ninajua Mheshimiwa Waziri wa Fedha alikwishajibu na akasema kwamba atawasiliana na Halmashauri zinazohusika juu ya hayo madai. Isipokuwa mwaka mmoja ambao fedha zake zimetumika kwa ajili ya kufidia ruzuku ya korosho kwa sababu zile fedha zilizokuwa zimetengwa na Serikali zilikuwa haziwezi kutosheleza na tusingefanya hivyo zao la korosho lingeshuka. Hata hivyo, zimefanya kazi ile ile ambayo ilikusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini masuala ya kulipana na madeni, nani anamdai nani, nafikiri niiachie Wizara ya Fedha ambayo ilikwishatoa kauli hapa Bungeni. Sasa kwamba walipe kwa riba, mimi sielewi Hazina huwa wana uhusiano gani na Halmashauri za Wilaya. Maana sidhani kama wanafanya biashara ambayo inazaa riba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nadhani Serikali kwa Serikali wanalipana bila kudaiana riba. Maana mimi sijawahi kusikia Halmashauri ikiidai riba Serikali wala Serikali Kuu ikiidai Halmashauri riba.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi ninashukuru kwa ufafanuzi aliotoa Mheshimiwa Waziri kuhusu zao la Tumbaku. Lakini ninakerwa na *issue* moja kwamba Manyoni tunalima sana na hasa maeneo ya Mgandu na mwaka huu wameuza tumbaku ya zaidi ya bilioni mbili. Sasa *Alliance One* na *TLTC* ni wanunuzi wa tumbaku katika eneo hilo. Sasa kwa kushirikiana na hizo Halmashauri za Tumbaku waliwa-*convince* wakulima kuuza kwa *rate* ya *dollar*, yaani *dollar* moja sawa na Sh. 1,250/=.

Sasa ulipofika wakati wa kuanzia kununua, wanapokata hizo pembejeo wanatumia *rate* hiyo ya Sh. 1,250/=, lakini wakati wa kununua mazao yaliyobaki kwa mkulima wanatumia Sh. 1,200/=. Sasa hiyo shilingi 50 inakwenda wapi na hapo ndipo kuna tatizo. Sasa hivi kuna wajumbe kutoka kijiji cha Makale ambao wametajwa katika orodha ya wageni leo wamekuja kuulizia suala hilo k wamba inaonekana wanadhulumiwa na wanapunjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ni kwamba toka mwaka juzi wananchi wa maeneo ambao wameambiwa walime mazao yanayostahimili ukame. Tulilalamika kuhusu kwelea kwelea na Mheshimiwa Waziri mwaka juzi alikuwa Waziri wa Kilimo, mwaka jana akabadilishwa akawa Waziri wa Wizara nyingine, lakini wakati ule alituahidi kwamba ndege ya shirika la *locust* ingekuwa *efficient* mwaka jana kutusaidia na mwaka huu, lakini wakati ule alipokuwa hayupo, tulipata shida sana kupata hiyo ndege. Kwa hali hiyo, tuligawana mazao na ndege hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukipanda mbegu unagawana na panya kwanza, kwale, ngurume, ngedere, kwelea kwelea, tembo, vizuizi, amri za Serikali, sasa mkulima atapata nini? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba ufafanuzi ni lini Serikali ndege yake yenyewe badala ya kusubiri hiyo ndege ya bure sijui kutoka nchi gani, maana ile ndege inatumiwa na nchi saba. Kweli ningeomba Mheshimiwa Waziri atupe ufafanuzi tuelewe ili tuweze kulima tupate mazao ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze na lile la tumbaku. Mheshimiwa John Lwanji alilileta hili suala ofisini jana na tulizungumza kidogo. Hili ni tatizo la mikataba ile niliyokuwa naiongea. *Tanzania Tobacco Council* ndiyo iliidhinisha mikataba ifanywe kwa *dollar*. Wakati ule

walikuwa wanadhani mkulima angefaidika kwa maana kwamba *dollar* ilikuwa na nguvu zaidi kuliko fedha ya Tanzania. Sasa wakakubaliana watumie *dollar*. Sasa kuna *advantage* na *disadvantage* katika mambo haya. Sasa shilingi ina nguvu zaidi kuliko dollar. Sasa wale wanawalipa kwa *dollar,* wanapomdai pembejeo wanamdai kwa *dollar,* lakini kwa *exchange rate* ya kuuza na hii wanawalipa kwa *exchange rate* ya kununua. Hapo ndipo tatizo linapotokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimewaambia Tanzania *Tobacco Council* ifute utaratibu wa kutumia *dollar* katika vikao vyao ili jambo hili lisije likatokea tena. Kwa sababu *currency* yetu sisi ni shilingi, kwa nini walifanya mkataba kwa *dollar*? Halafu *dollar* imeendelea kushuka ikilinganishwa na fedha nyingine za dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa nafikiri Mheshimiwa John Lwanji tutazungumza na wakulima wake kama tulivyowaahidi, lakini kwamba tutapata jibu la sasa hivi na wakati walisaini mkataba kwa *dollar* wakati ule ni ngumu sana. Lakini tutajaribu kuona jinsi tutakavyoweza kuwaambia. Mimi ninafikiri *solution* ya mbele ni kuondoa kabisa huo mkataba unaozingatia *dollar* badala ya shilingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kama kweli wakulima wamegawana kiasi hicho na ndege, kwa kweli mimi ninachoweza kuahidi hapa ni kwamba tutajitahidi kufanya hiyo kazi iwe inafanyika mapema na kwa ufanisi zaidi na kwamba niliahidi halafu nikatoka, hiyo siyo sababu, kwa sababu nilikuwa naahidi kwa niaba ya Serikali na Serikali ilikuwepo. Lakini kama imetokea bahati mbaya, ni bahati mbaya tu, basi haitokani na kutokuwepo mimi, maana mimi ninaweza nikafa na bado wale kwelea kwelea wakaendelea. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutashirikiana na Mheshimiwa John Lwanji ili kuona kwamba tunatoa huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu kuna lingine lililoulizwa kwamba tembo hawakuorodheshwa kama waharibifu. Tembo ni *problem* kweli. Sikuwaorodhesha kwa sababu mwenyewe yupo hapo, Mheshimiwa Waziri wa Maliasili. Lakini hata sisi kule Bunda tembo ni tatizo kubwa kweli. Sisi tumeorodhesha kama Wilaya ambayo itakuwa na njaa, moja ya sababu ni kwamba tembo wametoka kwenye *reserve* wamekula chakula chote cha wananchi pale. Kwa hiyo, tunafahamu matatizo haya, na mimi nataka kumwambia Mheshimiwa John Lwanji mimi na yeye wote tupo katika *boat* moja.

**MHE. MANJU S. MSAMBYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ametueleza mila na desturi za Waafrika za kuazimana chumvi. Mimi namkubalia, lakini Waafrika hatuishii kuazimana chumvi tu. Mtoto wa nyumba moja anaweza kwenda kula chakula hata nyumba ya pili, lakini asisemwe. Lakini mtoto huyo akienda kula nyumba ya pili halafu baba yake, chakula hiki akatengeneza pombe, ataimbwa nyimbo kijijini pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kusema ni hilo hilo la sisi kuwapa Kenya mahindi. Umekuja ujumbe mzito ukamfuata Mheshimiwa Rais wetu kule Tanga na

akashawishika akawapa sehemu tu ya kiasi walichoomba. Lakini wenzetu Kenya wakati wanakuja kuomba chakula huku chakula, wanaiuzia *WFP* mahindi; hivi Wizara ilishindwa na yenyewe kutafuta *tender* hiyo ambayo Kenya wameiuzia mahindi ikiwasaidia wakulima wetu sisi waweze na wenyewe kuuza kule ambako Kenya wameuza? Lakini Kenya wameuza halafu kiasi chao wao kile walichouza wanaziba pengo kwa kuja kununua mahindi Tanzania kwa bei ya chini kuliko ile ambayo wameuza kule *WFP*. Je, Wizara inasema nini kuhusu hilo? *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli hatuna ushahidi sana juu ya jambo hili. Tumesoma kwenye gazeti, sasa sio kila kitu kinachoandikwa kwenye magazeti unaweza ukasema ni kweli. Mimi ninachojua ni kwamba wenzetu wa Kenya wana matatizo makubwa ya chakula. Sababu zinazofanya wakafika hapo, tunazijua wote na sisi wenzetu kama nchi tumeshirikiana nao kuwaondoa katika balaa lililokuwa limewakumba, hilo tunalijua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama wameuza au hawakuuza, kwa kweli mimi kama Waziri wa Kilimo wa Tanzania, bila ushahidi siwezi nikasimama katika Bunge hili nikasema wameuza au hawakuuza. Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kwa nini sisi hatukutafuta *tender* hiyo ya *WFP*. Nimesema *WFP* wameamua watakuja hapa mwakani kununua mahindi kwa mfumo unaoitwa *purchase for progress.* Tumekubaliana, siyo hawa kwamba wanakuja kwa mwaka mmoja wanakuja kwa miaka yote na wanajenga maghala hapa nchini kwa ajili hiyo. Kwa hiyo, wataendesha mfumo ule wa stakabadhi ghalani kwamba unakusanya mahindi thamani yake ikipanda ndiyo wanayanunua. Mimi nadhani tumepata dili nzuri kuliko hiyo ya Kenya kama wanayo.

Kwa hiyo, nafikiri Mheshimiwa Msambya jirani yako akija kuomba chumvi halafu akaenda kuchunguza kama ameweka kwenye mboga na hilo nalo siyo utaratibu mzuri sana. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. CLEMENCE B. LYAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Katika mchango wangu wa maandishi nilikuwa nimeomba ufafanuzi kwa Mheshimiwa Waziri kama anafahamu kwamba baadhi ya wafanyabiashara wenye vibali vya kuagiza sukari kutoka nje ya nchi wanakiuka masharti ya vibali walivyopewa kwa kuagiza sukari tofauti na ile waliyoruhusiwa na madhara yake inaishia kupunguza bei ya sukari na pia inapunguza bei ya miwa ya wakulima wadogo kwa sababu wakulima wanalipwa kufuatana na bei ya soko, viwanda vinapouza sukari.

Sasa wafanyabiashara baadhi yao wanaoagiza sukari kutoka nje wanapaswa kuagizwa *refined* ambayo inapaswa kutumika kama *raw material* kwa bidhaa ambazo wanapaswa kutengenezwa. Lakini badala yake wanaingiza *plantation white sugar* ambayo ni *quality* inayofanana na sukari inayozalishwa nchini wanai-*dump*, waki-*dump* bei ya sukari inabidi iwe chini na ikiwa chini, uwiano wa bei ya miwa kwa wakulima nayo inakuwa ndogo *accordingly*. Nilimwomba Mheshimiwa Waziri afafanue: Je, anafahamu hilo na Serikali inachukua hatua gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nilikuwa nimeomba ushirikiano, Mheshimiwa Waziri athibitishe kama anaweza kukubali kwa vile wakulima wa miwa kwa miaka mingi walikuwa wanadaiwa *VAT* kwenye huduma za kukata miwa, kupakiwa miwa na kusomba miwa, jambo ambalo Mheshimiwa Waziri wa Fedha wakati alipokuwa anajumuisha hoja za Waheshimiwa Wabunge alikiri hilo na kuona kwamba kwa kweli kuna haja ya kurekebisha hali hiyo kwenye hii sheria ya *VAT*. Nilimwomba Mheshimiwa Waziri aeleze kama atakuwa tayari kushirikiana nami kumwomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha kuleta kabla ya mwisho wa mkutano wa Kumi na Mbili, *Bill of Supplement* kwa ajili ya *amendment* ya *schedule two* ya sheria ya *VAT* kwa sababu wakulima wamekuwa wanakatwa fedha hizo kwa miaka mitano iliyopita bila stahili hiyo. Ahsante.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la sukari nitajibu kwa ufupi sana kwa sababu na muda wenyewe una matatizo. Lakini suala la sukari kuna wazalishaji, wanazalisha sukari ambayo haitoshelezi mahitaji kwa wakati fulani. Kwa hiyo, kuna kipindi huwa inabidi kuagiza sukari kutoka nje ili kufidia pengo la uzalishaji wa ndani. Kuna Kamati nayo inafanya kazi chini ya Bodi ya Sukari ambayo inaitwa Kamati ya Ufundi ambayo hawa wazalishaji na baadhi ya wanunuzi nao wapo *CTI*. Kwa hiyo, wanaletwa wote kwa pamoja wanakubaliana kwa mwaka huu uzalishaji wa sukari ni kiasi gani na pengo ni kiasi gani. Kwa hiyo, Bodi ya Sukari ndiyo inatoa leseni kwa watakaokubaliwa kwenda kuiagiza ili kujaza pengo kati ya uzalishaji na mahitaji. Hiyo ndiyo hali halisi.

Sasa kama kuna watu wengine wanaingiza sukari inaitwa ya ku-*dump*, hiyo kwa kweli nadhani ni suala la *TRA* kwa sababu ukiingiza sukari bila kibali cha Bodi ya Sukari unatozwa kodi asilimia mia. Ukiingiza hapa sukari kwa kodi ya asilimia mia huwezi kuiuza maana bei yake itakuwa kubwa zaidi kuliko bei ya sukari inayozalishwa hapa nchini. Huo ndiyo msingi. Sasa suala la kama wanaagiza aina nyingine labda Mheshimiwa Lyamba najua tumeshughulikia jambo hili na wakati mwingine tumeshughulikia chini ya Ofisi ya Uongozi wa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nadhani limeshawekewa misingi kwamba kama huna leseni ya kuagiza sukari, huwezi kuagiza sukari. Hoja nyingine iliyokuwa inasema ni kwamba sukari inaingizwa halafu inaingizwa halafu inakwenda transit, wenzetu wa *TRA* wameweka utaratibu kama ni *transit* wanahakikisha ya kwamba umelipa kodi *in advance* ikishapata ruhusa ya kwamba imeingia kwenye nchi ya jirani kule ilikokuwa inakwenda unakuwa *refunded*. Hizo zote ni hatua za Serikali ambazo zimechukuliwa kuondoa suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini habari ya viwanda kusema wanalipa kidogo, kwa sababu hiyo na yenyewe nayo haina uhakika sana kwa sababu mimi nimewahi kuwauliza kama kuna *dumping* kubwa hivyo, mbona bei ya sukari haishuki? Kwa sababu mimi nafikiri tu-*liberalize* vile vile hata ile sukari inayozalishwa hapa ili wasambazaji wawe wengi ili kuwepo na *some element* ya *competition* ili na mlaji naye apate nafuu. Lakini Mheshimiwa Lyamba atashirikiana kuendelea kwa sababu tunaelewa matatizo ya

wakulima wadogo wa eneo hilo la Kilombero pamoja na kiwanda cha Mtibwa. Hilo kwanza. Juu ya *VAT* nadhani umeshalifikisha!

**SPIKA:** Samahani Mheshimiwa Waziri, sasa zimesalia dakika kumi kufikia muda wa kuahirisha Bunge. Nilikuwa na mawili, ningeweza kufupisha mjadala, jambo ambalo lingemfurahisha Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, lakini nimeamua nikae upande wa demokrasia. Kwa hiyo, natumia mamlaka yangu chini ya kanuni 104(1) kuongeza muda usiozidi dakika 30 baada ya saa 7.00. Mheshimiwa Waziri endelea. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hili la *VAT* Mheshimiwa Lyamba umeshalifikisha kwa Waziri anayehusika. Kwa hiyo, unachoniomba mimi ni kushirikiana na wewe tu kumshawishi anafika leo asubuhi, nitamwambia umeniambia, tena na nitaomba aliwekee maanani ili tuondoe mgogoro huo unaohusiana na wakulima. Kwa hiyo, hiyo haina matatizo makubwa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Spika anawatakia kheri katika hilo.

**MHE. DR. SAMSON F. MPANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza awali ya yote ninashukuru kwa kuwa Waziri ataleta mpango wa kuunda Bodi ya Mazao Mchanganyiko ambayo ni kilio changu cha muda mrefu sana na sasa kitakuja huenda mwaka huu. Lakini nina maswali mawili ya nyongeza ya kutaka kupata ufafanuzi. Kwanza, kuhusu suala la zao la ufuta, kwa kuwa Chama cha Mapinduzi kinasema kwamba ufuta tuuze kwenye Vyama vya Ushirika na sasa hivi wananchi wangu wamelima ufuta mwingi mno hasa kule Kipatimo, Chumo, yaani kila sehemu sasa hivi ufuta ni mwingi sana. Lakini fedha hakuna. Sasa sisi tutafanyaje katika kutatua tatizo hilo?

Suala la pili, kwa kuwa mimi simwogopi, naomba Mheshimiwa Waziri angekuja kule kwangu Kipatimo akaona machungwa yetu yanavyoharibika kwa kukosa soko, halafu angelitolea kauli maana sisi kunywa *juice* ambazo hazina mpango kusema kweli zinatuharibia afya zetu mpaka wengine hata macho hakuna. *(Makofi/Kicheko)*

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu zao la ufuta habari nilizonazo mimi ni kwamba uongozi wa Mkoa wa Lindi ndiyo waliamua baada ya mafanikio ya korosho ndiyo waliamua kwamba ufuta sasa ununuliwe na chama Kikuu cha Ushirika cha Ilulu.

Mimi sioni ubaya wowote kama wakulima wanapata maslahi kupitia mfumo ule. Lakini Serikali kwa ujumla hatujasema ni marufuku kwa wanunuzi wengine kununua kwa ufuta kwa sababu bado soko la mazao mengi hapa ni soko huria, lakini Chama cha Ushirika kikishindana na hawa wanunuzi na wakulima waka-*benefit* kwa kupata malipo zaidi. Mimi nadhani litakuwa jambo la muafaka. Kwa hiyo, hili tutazungumza na Mkuu wa Mkoa wa Lindi tuone hali ilivyo tuone kama kuna jambo lolote tunaweza kufanya ili kurekebisha hali hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juu ya machungwa kwamba tunakunywa *juice* mpaka macho yanapofuka, kwa kweli hili ni jambo ambalo tumelizungumza kwenye hotuba yetu, tunatilia mkazo uzalishaji wa *horticulture*, lakini vile vile tunawatia moyo wawekezaji wa ndani na nje wawekeze katika usindikaji wa mazao ya matunda. Mimi nadhani hiyo ndiyo tunachoweza kufanya, nadhani tutashirikiana na Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara katika kuendelea kuwavutia watu wanaowekeza kwenye matunda na mazao mengine ya bustani. Lakini kwa sasa hali ndivyo ilivyo na maendeleo sio kitu ambacho unafanya siku moja.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niombe ufafanuzi kwenye suala moja. Suala hili linahusu benki ya maendeleo ya kilimo. Napenda kupata uhakika ni nini tunatakiwa tufanye kwa sababu hoja hii ilikwishakubaliwa na Bunge lako Tukufu katika Mkutano wa Tisa tarehe 12 Novemba, 2007. Kwa hiyo, hatua inayofuata, nadhani ndiyo tunataka tuhakikishiwe kwamba itakuja mapema na kama kuna Muswada wa kuletwa kwa *certificate of agency* ni huu unaohusu Benki ya Maendeleo ya Kilimo.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani tumeshajibu hili suala. Tumelijibu kwa kusema hivi, kimsingi, Bunge hili linakubali na kimsingi Serikali inakubali. Kwa hiyo, hapa hakuna hoja ya kusigana. Tatizo lililobaki ni utekelezaji. Sasa, kwa sababu kuanzisha benki kupitisha Muswada ni suala moja na kuanzisha benki ni suala lingine, kuanzisha benki kunatakiwa *study* ya kutosha ili uweze kuona hiyo benki itatoa wapi mtaji, itafanya nini na kadhalika.

Kwa hiyo, hayo mambo nafikiri tungeachia sasa Serikali kwa maana ya Hazina na wadau wengine wote wanaohusika tushauriane tuone jinsi tunavyoweza kwenda. Lakini hatua ya awali ambayo imeshakubaliwa ni kwamba tunawekeza kwenye *TIB,* tunaweka dirisha la kilimo. Kwa hiyo, kilimo kitapata mkopo, kwa sababu ukichanganya viwanda na kilimo katika *TIB* hela zote zitakwenda kwenye viwanda. Kwa hiyo, lazima uweke fungu na uweke *strictly* kwamba hizi zinakwenda kwenye kilimo. Kwa namna hiyo, kilimo kitaanza kupata fedha kutoka kwenye ile Benki. Lakini wakati ule ule ndio tunaendelea sasa na hatua ya kuanzisha hiyo Benki. Lakini tukizungumza habari ya kuleta Muswada *under the certificate of urgency,* tunaweza tukaupitisha na Benki bado haijaanza. Maana maandalizi yatakuwa bado. Kwa hiyo, mimi nadhani tujipe muda kwa kuwa tunakubaliana wote kimsingi.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa maelezo ya Mheshimiwa Waziri, nilitaka tu kukumbusha kwamba Wizara ya Kilimo mwaka 1985 iliagiza utafiti ufanywe na ulisimamiwa na Marehemu Banker Nsekela. Kwa hiyo, utafiti ulishafanywa, lakini uliahirishwa kwa sababu tuliingia kwenye ubinafsishaji. Lakini sasa tumekumbuka kwamba ubinafsishaji umeleta matatizo, tunahitaji Benki. Kwa hiyo, utafiti upo na nina nakala ya huo utafiti.

**MWENYEKITI:** Nadhani hamshindani, ila utafiti wa mwaka 1985 hauwezi kusaidia kuunda Benki ya mwaka 2008. Kwa hiyo, yote hayo yachukuliwe yatusaidie kwenda mbele.

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri wakati anahitimisha hoja yake, lakini naomba ufafanuzi katika mambo yafuatayo:-

Kwanza sikusikia majibu yake kuhusu ushirika na kule Mbinga kuna ushirika wa *MBIFACU* ambao ulikuwa umefifia na kwa kweli tulikuwa tumekubaliana kimsingi uweze kufufuliwa na Serikali. Nilikuwa namwomba Mheshimiwa Waziri, zile juhudi alizozifanya mwaka jana kule Mtwara na Lindi angezifanya leo katika ushirika huu ingekuwa ni faraja kubwa kwa watu wa Mbinga.

Pili, kuhusu ushuru wa asilimia tano ambazo Halmashauri zinaruhusiwa kutoza kisheria, ni kwamba kuna watu binafsi ambao wanakwenda kununua vijijini na kule huu ushuru unatozwa. Lakini pia kuna Vyama vya Ushirika na vikundi ambavyo havitaki kuuza kwa mtu binafsi na Serikali inahimiza mambo haya. Sio kwamba wanakwepa kama Mheshimiwa Naibu Waziri alivyokuwa anajaribu kutoa sura. Hawa ni wale ambao wanatekeleza sera ya Serikali ili waweze kupata fedha wakauze kwenye soko lile la kule Moshi. Hawa sasa wanakwenda kukatwa huu ushuru wa asilimia tano kule na *TCB. TCB* wanakuwa *agent* wa Halmashauri wa kufanya hiyo kazi na wala si ushuru mwingine. Hasa athari yake ni kwamba hawa wanakatwa kabla ya gharama nyingine hazijakatwa.

Kwa mfano, wanakuwa wamesafirisha hiyo kahawa mpaka Makambako hizo zote ni gharama zao. Lakini yule anayelipa pale kijijini kwa mtu binafsi ambaye Serikali kwa kweli inajaribu kukatisha tamaa jambo hili ndio wanapata fedha nyingi zaidi kuliko hawa wanaushirika na wana vikundi ambao wanauza kupitia *action* ya ushirika. Tulikuwa tunaomba ufafanuzi wa Serikali kuhusu jambo hili ili hawa wanaushirika wasiadhibiwe kwa sababu ya kutaka kupata fedha zaidi kadri ya sera ya Serikali.

Lingine ambalo ningependa…

**MWENYEKITI:** Kwa mujibu wa kanuni ni mawili tu yametosha.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Nimezungumza na Mheshimiwa Gaudence Kayombo juu ya ushirika wa Mbinga na tulianza kuchukua hatua. Idara ya Ushirika imesimamia uchaguzi kule na viongozi wapya wameshapatikana na nilimuahidi tunapeleka wataalamu wa ushirika kule Mbinga. Tatizo lilikuwa bado ni la kibajeti bajeti. Sasa mradi ule muda ulioongezwa karibu unakwisha, tutapata fedha, kwa hiyo, tutapeleka wataalamu kule Mbinga na Msajili wa Ushirika yuko hapa anasikia apeleke wataalam upesi waende watazame jinsi watakavyoweza kusaidia Chama Kikuu cha Mbinga kiweze kufanya kazi. Tulishakubaliana naye juu ya hili.

Juu ya hili la kodi, nadhani vile vikundi na ushirika ndio wana-*complicate* hii kitu. Kwa sababu bei inayolipwa ile Sheria ya Kodi ya *Local Government* inataka walipe *maximum of 5%,* sasa bei ya kahawa pale kijijini inajulikana, hata hivyo vikundi vinanunua kutoka kwa wakulima.

Kwa hiyo, bei hiyo ndio iwe msingi wa wao kulipa kodi hata kabla hawajaanza safari ya kwenda Moshi. Walipe pale pale wakienda Moshi wanakwenda kutafuta faida yao tu, sio tena kuja kuzungumza habari ya kodi na kufuata. Hata kule kufuata Moshi kwa kweli wanaongeza gharama za Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga. Wao vikundi sio kwamba sisi Serikali tunataka wauze kwa vikundi. Kwa hiyo, tunawashawishi wakwepe kodi. Wao waende walipe kulingana na bei wanayonunulia kwa mkulima. Ile sheria inasema ni *X farm Gate*. *X farm Gate* ni pale unaponunua ndiyo bei unayolipia kodi na safari ya kwenda Moshi itapungua kwa wale watoza kodi wenyewe.

**MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti nashukuru sana. Naomba niulize ufafanuzi sehemu mbili. Kwanza Mheshimiwa Rais alivyotembelea Rufiji katika kijiji cha Mloka, Naibu Waziri wa Kilimo baada ya kuona ardhi ya Rufiji imejaa rutuba na magugu yake makubwa mipanje ile akaahidi kwamba Serikali sasa itaweka utaratibu wa vituo vya kukodisha matrekta kwa Wilaya ya Rufiji, tangu Desemba mpaka sasa haionekani hatua yoyote inayochukuliwa. Katika mchango wangu wa maandishi nimemwuliza Mheshimiwa Waziri *actual* na kumpa *warning* kwamba nitasimama kama sikupata maelezo ya kina, kwa bahati mbaya hata hakutaja hata jina kwamba huyu Bwana aliuliza habari ya matrekta kule Rufiji, hilo la kwanza naomba ufafanuzi.

La pili, juzi nimetoka kwenye vijiji vyangu kule Rufiji, bahati mbaya sana bei ya *sulphur* imepanda mno, wale ndugu zangu wameshindwa kwa haki kabisa, hawawezi kununua. Nilikuwa nimeandika katika mchango wangu wa maandishi kwamba, naomba Serikali iruhusu Vyama vya Msingi vya Ushirika viweze kukopesha hii *sulphur* kwa wakulima ambao wanayo mashamba ya korosho na yanatoa maua sasa na kwamba watalipa wakati wa mauzo. Nayo vile vile sikupata *reference* yoyote wakati Mheshimiwa Waziri anahitimisha. Naomba ufafanuzi. Ahsante sana.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, sikumtaja. Nilimtaja Professa kuwa amesema, lakini muda wa kusema kila mtu alisemaje ndio ulikuwa haupo. Hata Professa Sarungi naye alisema anataka pamba kule Rorya, nikamwambia sawa, lakini sikusema humu, sasa nasema maana hawa Maprofesa lazima kuwajibu. *(Makofi/Kicheko)*

Sasa, yule Profesa anazungumza juu ya matrekta, sisi sera iko wazi ya sekta binafsi kuanzisha vituo vya matrekta. Tunatoa mikopo na kwa kweli hivi karibuni tunaanza kuzungumzia juu ya uwezekano wa kuingiza trekta zaidi kwa kusaidia kutoa *guarantee* kwa sekta binafsi, Waziri wa Fedha alisema humu. Sasa tunataka kukubaliana tuanze kutoa *guarantee* ili matrekta yaingie na Jumanne ijayo mimi na Waziri wa Fedha tunazungumza juu ya kutekeleza kazi hiyo. Sasa tunachosema ni kwamba sekta binafsi ijizatiti ianzishe hivyo vituo, sisi tutaingiza matrekta wao wayakope. Kitu ambacho

tunashindwa ni kwamba Serikali iende Rufiji na kituo, hiyo kwa kweli kituo kitafilisika. Maana *experience* yetu ya kuendesha vitu hivyo inaonyesha kwamba Serikali sio Meneja mzuri wa vitu hivyo. Kwa hiyo, tunaambiwa vituo hivyo viendeshwe na *private sector*.

Mheshimiwa Mtulia, *private sector* ya Rufiji au hata ya Dar es Salaam kama kuna watu wa Dar es Salaam ambao wako tayari kwenda Rufiji waanzishe umuhimu wa kuanzisha kituo kama hicho halafu kupitia hayo matrekta tuliyoyataka kuyaingiza nchini wayakope. Namna nyingine ni kutumia sheria ile ya *lease* maana tumepitisha hapa Bungeni Sheria ya Kukodi, sio lazima wanunue au wakope. Wanaweza wakayakodi wakaanzisha kituo halafu wakawa wanayalimia na wanalipa kama tulivyopitisha sheria ile. Kwa hiyo, nadhani fursa zipo ila tu tuwahamasishe sekta binafsi kufanya hiyo kazi.

Juu ya bei ya *sulphur*, naijua iko juu sana kwa kweli. Lakini kwamba tunaweza kufanya kwanza *sulphur* hata kule Mtwara na Lindi ambao ndio wazalishaji wakubwa wa korosho *sulphur* ya unga bei imeshindikana kabisa ni ya juu kama ya mbolea. Kwa hiyo, tumewashauri watumie *sulphur* ya maji.

Kwa hiyo, kitu ambacho naweza nikamsaidia Mheshimiwa Prof. Mtulia ni kwamba tutaiagiza Bodi ya Korosho itafute uwezekano wa kuwapelekea *sulphur* ya maji. *Sulphur* ile ni ya maji na hii ni ya unga. Ya unga iko juu sana kwa bei, hii ya maji ni nafuu. Kuliko kusema tutumie *sulphur* ya unga kule Rufiji kwa mkopo bila ya kuweka taratibu zenyewe za kukopeshana, mimi nadhani tutumie *sulphur* ya maji. Mtwara sasa wameanza kuiona, Lindi tuli-*liberalize* sasa watu wengi zaidi wanatumia aina mbalimbali za dawa mbadala. Nadhani hii inaweza kusaidia, lakini *sulphur* hata tukiwakopesha wakulima wa Rufiji tutakuwa tunawa-*burden* kwa sababu ya ukali na ugumu wa bei ya *sulphur* ya unga.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Professa kumbe bado hukuridhika?

**MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniruhusu kusimama. Hoja yenyewe ni kwamba hiyo *private sector* haipo, inayotaka kufanya biashara ya matrekta. Serikali haiwezi kuacha hii kazi muhimu ya kunyanyua kilimo kwa *private sector*. Kwa hiyo, nilikuwa nadhani tusijivue koti letu hili la kulazimisha upanuaji wa kilimo, lazima Serikali isimamie, sio *private sector.* Ahsante. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *private sector* ni pamoja na Professa Mtulia. Kwa hiyo, Professa Mtulia akiungana na wananchi wengine walio na *interest* na maendeleo ya Rufiji na iwapo Prof. Mtulia mwenyewe aliwahi kuanzisha Chama cha Maendeleo ya Rufiji kikajenga sekondari, nazijua, mimi nilikuwa Mkuu wa Mkoa kule, kwa hiyo, sio kweli kwamba Rufiji haipo kabisa *private sector*. Mheshimiwa Prof. Mtulia uwaongoze wale watu walioanzisha kile Chama cha Maendeleo cha Rufiji, sasa waingie kwenye matrekta.

**MWENYEKITI:** Mtani wangu acha mambo ya kuogopa kukopa eeh! Tunaendelea.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nilitaka ufafanuzi kuhusu masuala niliyoyaandika nilipochangia kimaandishi kwamba katika Tarafa ya Enduimet kuna mwekezaji mmoja ambaye ameua mazao ya wananchi alipokuwa akipiga dawa katika shamba lake akatumia ndege kuua magugu kwenye shamba lake, sasa ndege ilipokuwa ikizunguka ikamwaga dawa ya kuua magugu katika mashamba ya wananchi ambao wao wamekwishaotesha mazao.

Kwa hiyo, mwaka juzi, 2006 wananchi wa Tarafa hii hawakupata mazao kabisa kwa ajili ya hiyo dawa. Wananchi wameleta malalamiko mpaka Ofisi ya Waziri Mkuu lakini mpaka sasa hawakulipwa fidia na wanalalamika na kwa bahati mbaya sana mwaka jana mvua haikunyesha katika ukanda huo wote, kwa hiyo, wana njaa kweli. Sasa nilitaka ufafanuzi kuhusu fidia na hali ya njaa iliyoko katika eneo hilo.

Jambo la pili, ni pembejeo. Tarafa hiyo ni wakulima sana. Nadhani *Breweries* wanafahamu kwa sababu wanachukua ngano katika maeneo hayo, lakini Serikali haijawahi kuwatambua kuwapa pembejeo ya madawa ya chochote; haijawahi kabisa kuelekeza pembejeo huko.

Sasa nataka ufafanuzi: Je, Serikali itawatambua wananchi na kuwapa madawa pamoja na fidia ya huyo mwekezaji? Kwa sababu yeye ameotesha mwaka huo na amepata na nadhani bado mpaka sasa wananchi wanalalamika. Hata juzi waliniambia niulize jambo hilo, wanataka walipwe fidia na huyo mwekezaji. Imekuwa ni kawaida wananchi wanapootesha yeye anazungusha ndege yake kuua magugu katika shamba lake na kuua mazao ya wananchi na Serikali inakaa kimya. Nataka kujua ili nipate maelezo ya kuwapelekea hao wananchi.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, maswali matatu yameulizwa?

**MWENYEKITI:** Nilipitiwa basi.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Nadhani.

**MWENYEKITI**: Jibu mawili.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Kwanza ameuliza ile la fidia halafu akasema tunasema nini juu ya njaa ya wale wananchi pale, hilo likawa la pili. Halafu pembejeo kwa wakulima hilo la tatu. Lakini kwa Mheshimiwa Michael Lekule Laizer nadhani mimi nitajibu yote tu uniruhusu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri sio matatu.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Hayo sio matatu?

**MWENYEKITI:** Ndege ndiyo iliyosababisha athari ya njaa. Kwa sababu ilinyunyiza na mazao yakaathirika, ndiyo maana nililichukua moja.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Hilo ni ya njaa mwaka 2006 na anazungumzia njaa ya mwaka 2008 yatakuwa mawili, lakini sio neno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, lile la kunyunyiza lilitokea na malalamiko yalifika na Mkuu wa Mkoa wa Arusha aliunda Tume ya kwenda kuchunguza ikishirikisha kituo chetu cha *TPRI* Arusha. Ripoti iliandikwa ikawasilishwa kwa Mkuu wa Mkoa. Taarifa tulizonazo ni kwamba watafiti wale walisema hawakuona kama athari ile imetokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunapata *problem* ya kupata *basis* ya kuwadai fidia kutoka kwa huyo mwekezaji. Lakini Mheshimiwa Michael Lekule Laizer kwa sababu wananchi wake bado hawajaridhika na hili jibu basi namkaribisha aje tuzungumze tuone ni namna gani tunaweza tukaendelea kuzungumza na wakulima hawa kwa sababu kazi yetu sisi ni kuwatia moyo na sio kuwakatisha tamaa, hilo la kwanza.

Lakini la pili, lilihusu njaa na pembejeo. Lile la njaa tunalishughulikia kama tunavyoshughulikia matatizo haya katika maeneo mengine. Mwezi *August* tutafanya utafiti wa maeneo yale ambayo yana upungufu wa chakula ili kuona ni kitu gani ambacho tunaweza tukafanya. Tunao mfumo wa kuweza kusaidia maeneo yaliyo na upungufu wa chakula.

Mwisho, suala la pembejeo, ikiwa wakulima wa eneo lile wanalima mahindi, pembejeo ambayo itakwenda Mkoani Arusha kwa ruzuku itatumika kwenye maeneo hayo vile vile. Kwa hiyo, hilo tunaweza kulijibu kwa namna hiyo.

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Laizer nadhani kwa kuzingatia muda na Mheshimiwa Waziri amekualika ofisini. Nadhani ebu tuwape nafasi wenzio. Narudi katikati, Mheshimiwa James Lembeli.

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nikichangia hoja hii jana kwa huzuni nilisema sitaunga mkono hoja kama Serikali haitatoa kauli ya uhakika na ya mwisho ya ahadi za kila mara za kuwalipa wakulima wa zao la pamba wa Kahama, Bukombe na Wilaya ya Uyui ambao wamekuwa wakikidai Chama Kikuu cha Ushirika cha *KACU* tangu mwaka 2004 na Serikali ilikuwa inaahidi kila mwaka kuwalipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kauli ameitoa Mheshimiwa Waziri nina hakika ni ya mwisho na ya uhakika na wakulima wa Kahama, basi wakae mkao wa kula wakisubiri kulipwa fedha zao mwaka huu. Sasa kwa heshima kabisa naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, ahsante.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi na mimi niulize machache kama ifuatavyo:-

Kwanza nampongeza Mheshimiwa Wasira kwa kazi nzuri aliyoifanya kwa hotuba yake na kujibu maswali, lakini basi, niombe tu anisaidie. Nilipokuwa nasoma kitabu chake nilitazama takwimu za mazao katika eneo la kahawa, huku mwisho mwaka 2006 tani zilikisiwa 51,000, mwaka 2007/2008 mwaka huu 41,000 na mwaka huu wa fedha ambao tunaujadili zinakisiwa tani 50,000, lakini hapa katikati kwenye kitabu hiki ameonyesha kwamba kuna miche bora zaidi ya milioni 4.9 ambayo imelimwa mwaka huu. Sasa hivi anakisia milioni 10 kwamba zitakwenda kwa wakulima.

Sasa kinachoshangaza, wakati kulikuwa hakuna utaalamu wowote tulipata tani 51,000 sasa wakati wa *improvement* ya kilimo inaonekana mazao yanashuka. Mimi suala hili kwa kweli sikulielewa, nimeshindwa kuliweka katika mahesabu likakaa vizuri. Nikahisi kwamba pengine hakuna mkakati mzuri au hakuna mahesabu mazuri yanayowekwa kuangalia takwimu na idadi ya uzalishaji.

Lakini kwenye hoja yangu niliyompelekea Mheshimiwa Waziri kwa maandishi, nilimwuliza hii miche mnategemea kuipanda kwa mtindo gani? Kwa sababu sasa hivi wakulima, mwingine anachukua 10, mwingine 100, mwingine 1,000 hali ambayo naona haiwezi kuboresha kilimo na uzalishaji wa kahawa kwa kipindi kirefu. Nilikuwa napendekeza kuwe na watu maalum binafsi badala ya hivi Vyama vya Ushirika anavyovitaka ambavyo vimefeli, havitaweza kuifanya kazi hii vizuri ili kuweza kuona kwamba ni akina nani ambao wanaweza kuchukua kwa wingi na maeneo gani ambayo hawa wataalamu wataweza kufuatilia ili zao hili liweze kuwa *improved.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, kuhusu hilo la kahawa kuna bei tofauti kwa haya mazao ya kahawa toka Mkoa hadi Mkoa. Kwa mfano, Mkoa wa Kagera humo humo nisiende hata nje kuna mahali ambapo kahawa yetu sisi inanunuliwa kwa bei…

**MWENYEKITI:** Muda sasa ni tatizo.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia. Kuna mahali ambapo kahawa yetu inanunuliwa kwa bei kidogo lakini wengine kahawa ile ile inanunuliwa kwa bei kubwa. Nilikuwa napenda hizi bei zifanane ndani ya Mkoa mmoja kwa kahawa ya aina ile ile kuliko ilivyo sasa hivi inavyofanyika. Nafikiri Mheshimiwa atakuwa amenielewa vizuri, ahsante.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa kanuni zetu, sasa hivi haiwezekani tena kuendelea na hiki ambacho nimejitahidi sana tukifanye. Kwa hiyo, tutaingia kwenye mafungu sasa.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1001 - *Administration and General* … Shs. 1,783,424,200/=
Kif. 1002 - *Finance and Accounts* … … Shs. 828,702,800/=
Kif. 1003 - *Policy and Planning* … … Shs. 1, 435,774,100/=

Kif. 1004 - *Agriculture Training Institutes* … Shs 1,161,330,500/=
Kif. 1005 - *Internal Audit Unit* … Shs. 100,000,000/=
Kif. 1006 - *Procurement Management Unit…* Shs. 340,000,000/=
Kif. 1007 - *Information, Education and Communication* … … Shs. 350,000,000/=
Kif. 1008 – *Legal Unit* … … … Shs. 200,000,000/=
Kif. 2001 – *Crop Development* … … Shs. 48,927,377,900/=
Kif. 2002 – *Directorate of Irrigation and Tech Serv.* … … Shs. 1,612,712,500/=
Kif. 2003 - *Agriculture Land Use Planning and Manage* ... … Shs. 400,000,000/=
Kif. 2004 - *Plant Breeder's Unit* … … Shs. 160,000,000/=
Kif. 3001 - *Research Development* … ... Shs. 14,142,914,200/=
Kif. 4001 - *Coooperative Development* … Shs. 5,292,876,700/=
Kif. 5001 - *National Food Security* … Shs. 16,969,105,100/=
Kif. 5002 - *Strategic Grain Reserve …* Shs. 0/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

Kif. 1001 - *Administration and General* ... Shs. 553,000,000/=
Kif. 1003 - *Policy and Planning* … … Shs. 5,129,100,000/=
Kif. 2001 - *Crop Development* … ... Shs. 7,204,623,400/=
Kif. 2002 - *Directorate of Irrigation and Tech Serv.* … ... Shs. 0/=
Kif. 2003 - *Agriculture Land Use Planning and Manage* … ... Shs. 75,000,000/=
Kif. 3001 - *Research Development* … ... Shs. 6,171,109,000/=
Kif. 4001 - *Coooperative Development* … ... Shs. 100,000,000/=
Kif. 5001 - *National Food Security* … … Shs. 800,000,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako Tukufu limekaa kama Kamati na kuipitia

Bajeti ya Wizara yangu Fungu 43 ya Mwaka 2008/2009 kifungu hadi kifungu na kuipitisha bila ya mabadiliko.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI**: Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika Kwa mwaka 2008/2009 yalipitishwa na Bunge)*

*(Saa 07.26 mchana Bunge lilifungwa mpaka Saa 11.00 jioni)*
*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2008/2009 – Wizara ya Maji na Umwagiliaji

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kupokea taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kilimo, Maji na Mifugo, naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako Tukufu likubali kujadili na kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa mwaka wa fedha 2008/2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kutumia fursa hii kuishukuru iliyokuwa Kamati ya Bunge ya Kilimo na Ardhi, chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Gideon Asimulike Cheyo, Mbunge wa Ileje, kwa maoni, ushauri na maelekezo iliyoyatoa kwa Wizara yangu. Pia, nachukua nafasi hii kuishukuru Kamati ya Bunge ya Kilimo, Maji na Mifugo chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Gideon Asimulike Cheyo (Mb) kwa ushauri, maoni na maelekezo yaliyotolewa na Kamati hiyo wakati nilipowasilisha Taarifa ya kazi zilizotekelezwa mwaka 2007/2008 na Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara yangu kwa mwaka 2008/2009. Maoni na mapendekezo hayo yameboresha kwa kiwango kikubwa maandalizi ya mpango na bajeti ya Wizara yangu kwa mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie fursa hii na kwa namna ya pekee kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuchaguliwa kuwa mwenyekiti wa Umoja wa Afrika na pia, kwa kuchaguliwa kuwa Kamishna wa Kamisheni ya Afrika iliyo chini ya Uongozi wa Waziri Mkuu wa Denmark. Natumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Mbunge wa Mpanda Mashariki kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais na kuthibitishwa kuwa Waziri Mkuu na Bunge lako Tukufu.

Pia, nitumie fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Celina Ompeshi Kombani na Aggrey Deaisile Joshua Mwanri kwa kuteuliwa kuwa Waziri na Naibu Waziri katika Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI. Vilevile, naomba nitumie fursa hii adimu, kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Rais kwa imani na heshima kubwa aliyonipa, kuniteua kuwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji. Nitajitahidi kwa kadri Mwenyezi Mungu atakavyonijalia kuilipa imani hiyo kwa kuwatumikia kwa uaminifu na uadilifu wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie fursa hii vilevile, kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wapya waliojiunga na Bunge lako Tukufu katika kipindi cha mwaka 2007/2008. Wabunge hawa ni Mheshimiwa Benedict Ngalama Ole-Nangoro Mbunge wa CCM Jimbo la Kiteto, Mheshimiwa Mchungaji Dkt. Getrude Rwakatare na Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma Wabunge wa Viti Maalum (CCM) na Mheshimiwa Al-Shaymaa John Kwegyr, Mbunge aliyeteuliwa na Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru na nawapongeza Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Waziri Mkuu na Mheshimiwa Mustafa Haidi Mkulo, Waziri wa Fedha na Uchumi. Hotuba zao zimetoa dira na mwelekeo wa bajeti, uchumi na utekelezaji wa kazi za Serikali kwa mwaka 2008/2009. Nawapongeza pia, Waheshimiwa Mawaziri wengine wote walionitangulia kuwasilisha hoja zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu ilipokea kwa masikitiko makubwa taarifa za vifo vya Waheshimiwa Wabunge wenzetu, Hayati Salome Joseph Mbatia - Mbunge wa Viti Maalum aliyeaga dunia kutokana na ajali ya gari wakati akitekeleza majukumu ya kitaifa na Hayati Benedict Losurutia - Mbunge wa Kiteto. Naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kutoa pole kwako wewe Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge lako Tukufu, familia za Marehemu, ndugu na wananchi wa Mkoa wa Kilimanjaro na Jimbo la Kiteto. Mwenyezi Mungu aziweke roho za Marehemu mahali pema Peponi. Amin.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Sekta ya Maji, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2005 inaelekeza Serikali kuendeleza utoaji wa huduma ya maji kwa lengo la kuboresha maisha ya wananchi na kuwapunguzia umasikini. Ilani inaelekeza kuwa, nanukuu:- "Kutokana na umuhimu wa maji, Serikali chini ya CCM katika kipindi cha 2005-2010 zitaendelea kutekeleza majukumu yaliyoainishwa katika Sera ya Taifa ya Maji ya mwaka 2002 na kusisitiza yafuatayo:-

(i) Kuwawezesha wananchi mijini na vijijini kupata maji safi, salama na ya kutosha kwa matumizi yao ya kawaida karibu na sehemu wanazoishi na kwa mahitaji ya kiuchumi. Lengo ni kuwafikishia huduma hiyo asilimia 90 ya wakazi wa mijini na asilimia 65 ya wakazi wa vijijini ifikapo mwaka 2010;

(ii) Kuhimiza utekelezaji wa ujenzi wa malambo na mabwawa mapya, ukarabati na kufufua malambo ya zamani ili maji mengi zaidi yaweze kupatikana kwa ajili ya matumizi ya wananchi na mifugo;

(iii) Kushirikisha kwa ukamilifu nguvu za wananchi katika hatua zake zote za kutoa huduma ya maji ikiwa ni pamoja na kupanga, kujenga, kuendesha na kumiliki miradi yenyewe kwa njia ya kueneza kamati za maji za vijiji sambamba na kuimarisha mifuko ya maji ambayo imeanzishwa na wananchi;

(iv) Kukamilisha miradi mikubwa ya maji ambayo ni pamoja na Mradi wa Maji toka Ziwa Victoria kwenda Wilaya za Shinyanga Mjini na Kahama, Mradi wa Maji wa Chalinze katika Mkoa wa Pwani na Mradi Kabambe wa Kufufua Mifumo ya Maji Safi na Maji Taka katika Jiji la Dar es Salaam;

(v) Kuhimiza, kuimarisha na kupanua teknolojia nyepesi na rahisi ya kukinga, kutunza na kutumia maji ya mvua; na

(vi) Kuandaa mazingira mazuri ya kisheria kuhusu rasilimali za maji na kubaini vyombo na muundo utakaomudu majukumu, mipango na menejimenti ya rasilimali ya maji nchini." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2005 yameweka bayana maeneo ya msisitizo katika kuendeleza kilimo cha Umwagiliaji kama ifuatavyo:-

(i) Maji yakingwe kwenye visima, malambo na mabwawa kwa matumizi ya watu, mifugo na umwagiliaji; na

(ii) Kipaumbele kiwe katika kuendeleza miradi midogo na ya kati, ikiwa ni pamoja na kuandaa mifumo ya uvunaji wa maji ya mvua na kuchimba mabwawa ili kuendeleza kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa mwaka 2008/2009 imepewa majukumu ya utekelezaji kulingana na Sera ya Maji ya mwaka 2002, Sera ya Kilimo na Mifugo ya mwaka 1997, Mkakati wa Maendeleo ya Sekta ya Maji na Mkakati wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo. Kutokana na hayo tumebaini dira na dhamira ya Wizara kuwa kama ifuatavyo:

Dira: Kuwa na mfumo endelevu wa kusimamia na kuendeleza rasilimali za maji utakaoleta manufaa ya kijamii na kiuchumi na kuimarisha Sekta ya Umwagiliaji kwa lengo la kuongeza uzalishaji, kuongeza pato la taifa, na hivyo kuchangia katika kupunguza umaskini; na

Dhamira: Kuhakikisha rasilimali za maji zinasimamiwa, zinaendelezwa na zinatumika kwa njia endelevu kwa kuwashirikisha wadau kwa kuzingatia mahitaji ya sekta mbalimbali kupitia uboreshaji wa miundombinu ya umwagiliaji, usambazaji majisafi na uondoaji wa majitaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inatekeleza majukumu yake kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji *(Water Sector Development Programme-WSDP)* na Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo *(Agricultural Sector Development Programme-ASDP).* Majukumu hayo yanazingatia ahadi zilizotolewa na Serikali, malengo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA), Malengo ya Milenia, na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025. Majukumu hayo ni pamoja na:-

(i) Kutayarisha na kusimamia utekelezaji wa sera, mikakati na programu za kuendeleza Sekta za Maji na Umwagiliaji;

(ii) Kutayarisha na kusimamia sheria mbalimbali za maji na umwagiliaji;

(iii) Kukusanya, kuhifadhi na kuchambua takwimu muhimu za Sekta za Maji na Umwagiliaji;

(iv) Kusimamia matumizi endelevu ya rasilimali za maji;

(v) Kusimamia na kuratibu utoaji wa huduma za maji kwa sekta mbalimbali za kiuchumi na kijamii;

(vi) Kutafuta, kuchunguza, kuhifadhi na kuendeleza vyanzo vya maji;

(vii) Kuendeleza teknolojia mbalimbali za utoaji huduma ya maji safi na usafi wa mazingira mijini na vijijini;

(viii) Kutoa mafunzo kwa wataalam wa maji na umwagiliaji katika ngazi na maeneo mbalimbali ya utekelezaji;

(ix) Kutoa miongozo kuhusu matumizi ya teknolojia sahihi za umwagiliaji;

(x) Kusimamia na kuwezesha ukarabati wa skimu za umwagiliaji za wakulima wadogo;

(xi) Kusimamia ujenzi wa miradi ya maji na umwagiliaji; na

(xii) Kuongeza matumizi ya maji ya chini ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera ya Maji na Sera ya Kilimo na Mifugo: Wizara yangu katika kutekeleza majukumu yake, inaongozwa na Sera ya Maji ya mwaka 2002 na Sera ya Kilimo na Mifugo ya Mwaka 1997. Sera ya Maji inatoa mwongozo unaolenga kuhakikisha kuwa rasilimali za maji nchini zinalindwa, zinahifadhiwa, na zinatumiwa kwa uwiano kwa kuzingatia mahitaji ya binadamu, mifugo, uvuvi, kilimo, umeme, viwanda na hifadhi ya mazingira. Wizara imeanza kazi ya kutafsiri sera hiyo katika lugha nyepesi ili jamii nzima iweze kuielewa vizuri na hivyo kushiriki kikamilifu katika kuitekeleza. Kazi hiyo itakamilika katika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Sekta ya Umwagiliaji, Wizara yangu, katika juhudi ya kuwa na dira ya utekelezaji sahihi wa maendeleo ya kilimo cha umwagiliaji, inaandaa sera ya umwagiliaji. Katika maandalizi ya sera hiyo, mikutano mitatu ya wadau imefanyika kwa lengo la kupata maoni yao. Maoni yaliyotolewa na wadau katika mikutano yameboresha rasimu ya sera. Katika kuandaa sera hiyo, tumetumia uzoefu tulioupata katika kutekeleza Mpango Kabambe wa Taifa wa Umwagiliaji (*National Irrigation Master Plan – NIMP*) ambao nao utafanyiwa mapitio ili uendane na hali ya sasa katika sekta.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila mwaka Wizara yangu hutathmini utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji kwa kushirikisha washirika wa maendeleo katika sekta, idara na mashirika ya serikali na taasisi zisizo za kiserikali. Hii ni kulingana na makubaliano kati ya Serikali na washirika wa maendeleo yaliyofikiwa wakati wa maandalizi ya Programu.

Tathmini ya mwaka 2007/2008 ilifanyika mwezi Oktoba 2007 ambapo Serikali iliwakilishwa na Wizara yangu, Wizara ya Fedha na Uchumi, na Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI). Tumekubaliana yafuatayo:-

(i) Kuharakisha mageuzi katika Sekta ya Maji na kuimarisha usimamizi na uratibu wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji;

(ii) Kuharakisha kupitisha Mkakati wa Sekta ya Maji na sheria mpya ya maji, na kuoanisha Mkakati wa Sekta ya Maji na Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji;

(iii) Kuandaa mfumo wa kufuatilia utekelezaji katika Sekta ya Maji;

(iv) Kuandaa mfumo utakaoiwezesha Serikali kuwekeza kwa uwiano katika Sekta ya Maji kwa lengo la kuendeleza huduma za maji vijijini na mijini, na usimamizi wa rasilimali za maji.

(v) Kuandaa taarifa ya mwenendo wa uwekezaji katika Sekta ya Maji;

(vi) Kuandaa utaratibu wa mawasiliano, ushawishi, uhamasishaji na ushiriki wa sekta binafsi na vyama vya kiraia katika kuendeleza Sekta ya Maji;

(vii) Kuanzisha na kuendeleza majadiliano kati ya Wizara inayosimamia Sekta ya Maji na Wizara inayosimamia Sekta ya Afya ili kubaini majukumu na uwajibikaji wa kila sekta katika kuendeleza kikamilifu sekta ndogo ya usafi wa mazingira; na

(viii) Kukamilisha na kuanza kutekeleza Mkakati dhidi ya maambukizi ya UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kongamano la Wataalam wa Maji: Tukio lingine muhimu ni Kongamano la Mwaka la Wataalam wa Maji. Kongamano hilo hukutanisha wataalam wa maji kutoka ndani na nje ya nchi. Wataalam hao hupata fursa ya kujadili masuala ya utekelezaji wa Sera ya Maji, kubadilishana uzoefu na kujifunza mambo mapya yanayojitokeza katika Sekta ya Maji hapa nchini na katika nchi nyingine.

Kwa mwaka 2007/2008, Kongamano hilo lilifanyika mjini Arusha mwezi Februari 2008. Maudhui ya Kongamano hilo yalikuwa ni Ufanisi katika Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji. Jumla ya mada 16 ziliwasilishwa na kujadiliwa. Kongamano lilitoa maazimio katika maeneo yafuatayo:-

(i) Kuimarisha usimamizi wa ubora wa maji;

(ii) Kuimarisha mipango shirikishi ya matumizi ya ardhi na mazingira;

(iii) Kuhimiza matumizi ya teknolojia ya uvunaji wa maji ya mvua;

(iv) Kuhimiza uanzishaji wa vyama vya watumiaji maji;

(v) Kuhimiza ushiriki wa wanawake katika utoaji wa maamuzi katika Sekta ya Maji; na

(vi) Kuanzisha benki ya takwimu za maji.

Maazimio hayo yatatusaidia katika kufanikisha jukumu la kuimarisha usimamizi wa rasilimali za maji na utekelezaji wa miradi ya maji nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila mwaka Wizara yangu huandaa Mkutano wa Mwaka wa Mamlaka za Majisafi na Majitaka Mijini, mkutano ambao huwakutanisha pamoja watendaji wakuu na wawakilishi wa Bodi za Mamlaka hizo. Madhumuni ya mkutano huo ni kuhamasisha utekelezaji wa Sera ya Maji na kutoa fursa ya kubadilishana uzoefu kuhusu masuala ya kiufundi, kifedha na kiuendeshaji.

Vilevile, Mamlaka hizo hufanyiwa tathmini ya utendaji kazi na utekelezaji wa maazimio ya mkutano uliopita. Matokeo ya tathmini hiyo yanaongeza ufanisi katika utoaji wa huduma za maji mijini. Mkutano wa kumi ulifanyika mjini Mtwara mwezi Februari 2008 ukiwa na maudhui ya Kukidhi Mahitaji ya Usimamizi wa Maji Mijini *(Realization of Water Demand Management in the Urban Water Supply Authorities)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkutano wa Mawaziri wa Maji wa Nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika *(SADC)* ulifanyika *Windhoek*, Namibia, mwezi Machi, 2008. Mkutano ulitathmini utekelezaji wa maamuzi mbalimbali ya mikutano iliyotangulia na kufikia maazimio yafuatayo:-

(i) Nchi 13 wanachama wa *SADC* ambazo bado hazijasaini Mkataba wa Makubaliano wa Baraza la Mawaziri wa Maji wa Afrika (*AMCOW*) zimehimizwa

kuharakisha ukamilishaji wa taratibu zinazohusika ili utekelezaji wake uanze. Hadi sasa ni Tanzania pekee ndiyo iliyosaini Mkataba huo;

(ii) Nchi za Tanzania, Zimbabwe na Malawi bado hazijaridhia mkataba wa makubaliano ya uanzishaji wa Kamisheni ya Bonde la Mto Zambezi (*Zambezi Watercourse Commission (ZAMCOM)).* Tumehimizwa kuongeza kasi katika mchakato wa kuridhia mkataba huo ili Kamisheni hiyo iweze kuanzishwa;

(iii) Nchi za *SADC* zimekubaliana kupanua wigo wa kutoa tuzo ya uandishi bora katika masuala ya majishirikishi *(SADC Water Media Award on Transboundary Water Resources)* kwa waandishi watakaoandika habari zenye mada bora ya maji *(Thematic focus on water).* Kutokana na hatua hiyo, Wizara inaangalia uwezekano wa kuwa na tuzo ambayo itakuwa inatolewa kwa waandishi bora watakaoandika habari za maji kwa utaratibu utakaopangwa;

(iv) Nchi za *SADC* zilihimizwa kujiandaa vyema ili kushiriki kikamilifu katika Mkutano wa Wakuu wa Nchi za Umoja wa Afrika uliofanyika mwezi Julai 2008 katika mji wa Sharm El-Sheikh, nchini Misri; na

(v) Nchi wanachama wa *SADC* zilihimizwa kujiandaa ili kukabiliana na changamoto katika Sekta ya Maji inayotokana na mabadiliko ya tabianchi ikiwa ni pamoja na kushiriki kikamilifu katika mazungumzo yanayoendelea ili Sekta ya Maji, pamoja na maeneo mengine, ifaidike na mfuko wa kuhimili mabadiliko hayo. Mfuko huo ulianzishwa mjini Bali, Indonesia kupitia Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu mabadiliko ya tabianchi (*United Nations Framework Convention on climate change).*

Mheshimiwa Naibu Spika, nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba katika mkutano huo wa Windhoek, Tanzania ilichaguliwa kwa kauli moja kuwa mwenyeji wa Mkutano wa Mawaziri wa Maji wa Jumuiya ya *SADC* utakaofanyika mwezi Novemba, 2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila mwaka, Wiki ya Maji huadhimishwa kuanzia tarehe 16 Machi na kilele chake kuwa tarehe 22 Machi ambayo ni Siku ya Maji Duniani.

Lengo la maadhimisho hayo ni kutoa nafasi kwa wadau wa Sekta ya Maji kujadiliana kuhusu Sera ya Maji, mikakati na mipango ya maendeleo na hufahamishwa kuhusu mafanikio na changamoto zinazoikabili Sekta ya Maji kwa njia ya mikutano, semina, warsha na maonyesho. Maadhimisho hayo hutoa fursa ya kuhamasisha wananchi kushiriki katika kupanga, kujenga, kusimamia na kuendesha miradi ya maji na kutunza mazingira na vyanzo vya maji. Maadhimisho ya wiki ya maji kwa mwaka huu yalifanyika kitaifa Jijini Dar es Salaam na kaulimbiu ilikuwa ni Fanikisha Usafi wa Mazingira.

Naomba nichukue nafasi hii kuwashukuru wananchi wengi waliojitokeza kuadhimisha siku ya maji duniani. Nawashukuru viongozi wote kuanzia ngazi ya kata hadi mkoa kwa kuratibu na kusimamia maadhimisho hayo. Kwa namna ya pekee

nawashukuru viongozi wa Mkoa wa Dar es Salaam, wakazi wake, taasisi na kampuni zilizoshiriki katika maonyesho ya huduma na bidhaa kwa wiki nzima ya tukio hilo. Baadhi ya Mawaziri wenzangu walishiriki katika matukio mbalimbali ya Wiki ya Maji, nawashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkutano wa Mwaka wa Maafisa wa Maji wa Mabonde: Baada ya Serikali kuanzisha Ofisi za Mabonde na kuunda Bodi za Mabonde yote tisa ya maji nchini, Wizara yangu iliandaa mkutano wa kwanza wa mwaka uliowakutanisha Maafisa wa Maji wa Mabonde tisa. Mabonde hayo ni ya Pangani, Wami/Ruvu, Rufiji, Ruvuma, Ziwa Nyasa, Ziwa Rukwa, Bonde la Kati, Ziwa Tanganyika na Ziwa Victoria. Mkutano huo ulifanyika mjini Bagamoyo mwezi Aprili 2008. Mkutano ulihudhuriwa pia na Washirika wa Maendeleo katika Sekta ya Maji, ikiwa ni pamoja na Benki ya Dunia, Shirika la Maendeleo la Kiufundi la Ujerumani *(GTZ*); Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Japan *(JICA*); Shirika la Kimataifa la Hifadhi ya Mazingira (*IUCN*); na Shirika la Dunia la Hifadhi ya Wanyamapori (*WWF*). Maudhui ya mkutano huo yalikuwa ni Kuweka Mfumo wa Usimamizi wa Rasilimali za Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkutano huo ulijadili taarifa za utekelezaji za Mabonde na mada mbalimbali ziliwasilishwa. Mada hizo zilihusu uzoefu wa Mabonde ya Pangani na Wami/Ruvu katika kutathmini mahitaji ya maji kwa ajili ya mazingira, na uzoefu wa usimamizi shirikishi wa rasilimali za maji kitaifa na kimataifa. Mkutano huo ulifikia makubaliano kuhusu mfumo unaofaa wa usimamizi wa rasilimali za maji hapa nchini. Mfumo huo ndio utakuwa msingi utakaoziwezesha Bodi za Maji za Mabonde kufuatilia na kutathmini utekelezaji na changamoto zinazojitokeza. Maazimio yaliyofikiwa katika mkutano huo yatakuwa chachu ya utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkutano wa Mawaziri wa Maji Nchi za Maziwa Makuu: Kikao cha 12 cha Baraza la Mawaziri wa Maji wa Nchi za Maziwa Makuu, katika Bonde la Mto Nile, kilifanyika mjini Bujumbura, Burundi mwezi Aprili 2008. Kikao hicho kilijadili masuala yanayohusu uendeshaji wa Programu Tanzu ya nchi hizo (*Nile Equatorial Lakes Subsidiary Action Program-NELSAP*). Kikao kilipitisha pendekezo la nchi wanachama kuchangia gharama za uendeshaji wa *Nile Basin Initiative* kwa lengo la kupunguza utegemezi wa nchi hizi kwa wafadhili. Masuala mengine yaliyojadiliwa yalihusu utekelezaji wa miradi chini ya *NELSAP* kuandaa mfumo endelevu wa kusimamia rasilimali za maji, na mkakati wa uwekezaji katika mabonde madogo ya mto Kagera na mto Mara. Kikao kiliazimia yafuatayo:-

(i) Kuharakisha utekelezaji wa mradi wa umeme wa maporomoko ya maji ya Rusumo utakaozihusisha nchi za Tanzania, Rwanda na Burundi;

(ii) Kuharakisha maandalizi ya mradi mpya wa kilimo *(Regional Agricultural Trade and Productivity Project),* ambao utazinufaisha nchi husika katika kilimo chenye tija na biashara ya mazao ya kilimo; na

(iii) Nchi wanachama kukamilisha mkakati wa utafutaji fedha za kugharamia miradi mipya *(NELSAP Scaling-up Strategy)* ambapo kwa upande wa Tanzania miradi mitano ya umwagiliaji, 24 ya maji safi na usafi wa mazingira na mmoja wa kusimamia rasilimali za maji, imependekezwa na kuwasilishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkutano wa Wadau wa Bonde la Mto Ruvuma: Mkutano wa wadau wa maji katika Bonde la Mto Ruvuma ulifanyika katika mji wa Bagamoyo mwezi Mei 2008. Wajumbe walioshiriki katika mkutano huo walitoka Tanzania na Msumbiji. Mkutano ulilenga katika kuongeza ufanisi wa kusimamia na kuendeleza rasilimali za majishirikishi, na kufafanua mipango ya maji iliyoibuliwa kwa kuzingatia misingi iliyoainishwa kwenye Itifaki ya Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika juu ya Majishirikishi *(SADC Protocol on Shared Watercourses).* Mkutano huo ni miongoni mwa jitihada zinazoendelea kuchukuliwa na nchi hizi mbili katika kutafuta mbinu za pamoja za kusimamia mazingira na mfumo wa ikolojia katika bonde hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkutano wa Wakuu wa Nchi za Umoja wa Afrika: Mkutano wa Wakuu wa Nchi za Umoja wa Afrika ulifanyika tarehe 30 Juni 2008 hadi tarehe 1 Julai 2008 katika mji wa Sharm El-Sheikh, nchini Misri. Maudhui ya Mkutano huo yalikuwa ni Kuharakisha Kufikia Malengo ya Milenia Kuhusu Maji na Usafi wa Mazingira Barani Afrika. Maudhui hayo yalishabihiana na kaulimbiu ya Wiki ya Maji Kimataifa kwa mwaka 2008 ambayo ni Fanikisha Usafi wa Mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mkutano huo Wakuu wa Nchi za Umoja wa Afrika walitoa azimio la Sharm El-Sheikh kuhusu kuharakisha kufikia malengo ya Milenia kwenye nyanja za maji na usafi wa mazingira barani Afrika katika maeneo yafuatayo :-

(i) kutekeleza maazimio ya mikutano iliyopita yanayohusu maji na usafi wa mazingira;

(ii) kurekebisha sera, sheria, mikakati na programu ili kuharakisha maendeleo ya maji na usafi wa mazingira barani Afrika;

(iii) kujenga uwezo wa serikali kuu, serikali za mitaa na sekta binafsi ili kufikia Malengo ya Milenia kuhusu maji na usafi wa mazingira barani Afrika;

(iv) Kuhimiza Benki ya Maendeleo ya Afrika, washirika wa maendeleo na mawaziri wa maji na fedha kukutana na kutayarisha sera ya uwekezaji katika sekta ya maji na usafi wa mazingira barani Afrika.

(v) Kutilia mkazo masuala ya uhakika wa upatikanaji wa maji kwa ajili ya kilimo ili kuwa na usalama wa chakula kama ilivyobainishwa katika maazimio ya kisekta na matokeo ya wiki ya kwanza ya maji ya Afrika;

(vi) Kujenga uwezo wa kitaasisi na kitaalam katika ngazi zote kwa ajili ya utekelezaji wa programu mbalimbali za maji na usafi wa mazingira katika kuimarisha mfumo wa mawasiliano, uratibu na usimamizi; na

(vii) Kuchukua hatua za kuimarisha uwezo wa nchi za Afrika katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na rasilimali za maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mikutano na Matukio Katika Sekta ya Umwagiliaji katika mwaka wa 2007/2008, katika Sekta ya Umwagiliaji kulikuwa na mikutano na matukio mbalimbali kama ifuatavyo:-

(i) Maadhimisho ya Siku ya Wakulima ya Nane Nane yalifanyika kitaifa katika mji wa Arusha na kikanda katika miji ya Morogoro, Mbeya na Dodoma;

(ii) Mikutano, iliyowashirikisha wadau wa sekta binafsi katika Sekta ya Umwagiliaji, ilifanyika mwezi Desemba, 2007 na Januari, 2008. Mada kuu ilihusu Nafasi iliyopo kwa sekta binafsi kushiriki katika utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo, hasa Umwagiliaji na fursa zilizopo kwa sekta hiyo kuwekeza katika kilimo cha umwagiliaji. Mikutano hiyo ilifanyika katika Kanda zote saba za umwagiliaji ambazo ni Morogoro, Mbeya, Kilimanjaro, Tabora, Mtwara, Mwanza na Manyara;

(iii) Mkutano wa Maafisa wa Kanda za Umwagiliaji nchini ulifanyika jijini Dar es Salaam mwezi Februari, 2008 ili kujadili utekelezaji wa majukumu ya sekta; na

(iv) Mikutano ya kitaifa ya kujadili rasimu ya sera ya taifa ya umwagiliaji ilifanyika katika miji ya Mwanza, Arusha na Iringa mwezi Mei, 2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu ina maji mengi yanayopatikana kwenye mito, maziwa, chini ya ardhi na maeneo oevu. Hata hivyo, baadhi ya maeneo ya nchi yetu hukumbwa na uhaba wa maji au mafuriko kutokana na mabadiliko ya tabianchi. Vilevile, maji yanayofaa kwa matumizi mbalimbali yanaendelea kupungua mwaka hadi mwaka kutokana na ongezeko la watu, uzalishaji mali katika sekta mbalimbali na uharibifu wa mazingira ya vyanzo vya maji. Katika mwaka 2007/2008, maeneo mengi nchini yalipata mvua za kutosha na kuwezesha kupatikana kwa maji ya kutosha kwa shughuli za uzalishaji wa umeme, kilimo cha umwagiliaji, na matumizi ya viwandani na majumbani.

Mheshimiwa Naibu Spika, idadi ya wananchi wanaopata huduma ya maji safi na salama vijijini imeongezeka kutoka asilimia 55.7 mwaka 2006/2007 hadi asilimia 57.1 mwaka 2007/2008 ikiwa ni ongezeko la asilimia 1.4. Jumla ya watu wanaopata majisafi vijijini wamefikia milioni 18.8 mwaka 2007/2008 kulinganisha na milioni 17.7 mwaka 2006/2007 sawa na ongezeko la watu milioni 1.1. Kwa upande wa mijini, idadi imeongezeka kutoka asilimia 78 mwaka 2006/2007, hadi kufikia asilimia 79.9 mwaka 2007/2008, ikiwa ni ongezeko la asilimia 1.9 katika miji mikuu 19 ya mikoa inayosimamiwa na Mamlaka za Maji Mijini. Mamlaka hizi zimeanzishwa chini ya Sheria

ya Maji ya mwaka 1998. Katika eneo linalohudumiwa na *DAWASA,* chini ya Sheria ya *DAWASA* ya mwaka 1997 linalojumuisha Jiji la Dar es Salaam na Miji ya Kibaha na Bagamoyo, hali ya upatikanaji wa huduma ya majisafi ni asilimia 68.

Watu wanaopata majisafi mijini wamefikia milioni 5.32 mwaka 2007 ikilinganishwa na milioni 4.97 mwaka 2006 ambapo wastani wa upatikanaji wa maji katika miji mikuu ya mikoa na Dar es Salaam umeendelea kuwa ni wastani wa saa 17 kwa siku. Mafanikio yaliyopatikana yametokana na ongezeko la uwekezaji baada ya kuanza utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji. Mvua za kutosha zilizonyesha katika maeneo mengi ya nchi ziliongeza upatikanaji wa maji katika vyanzo mbalimbali. Ushirikishwaji wa wananchi katika kutekeleza na kusimamia miradi ya maji na hifadhi ya vyanzo vya maji uliongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ina rasilimali nyingi ambazo zinaweza kutumiwa kuongeza uzalishaji katika kilimo. Rasilimali hizo ni pamoja na ardhi na maji. Mpango Kabambe wa Taifa wa Umwagiliaji Maji wa mwaka 2002 ulibaini kuwa nchi yetu ina eneo la hekta milioni 29.4 ambazo zinafaa kwa kilimo cha umwagiliaji. Kati ya hizo, hekta milioni 2.3 zina uwezekano mkubwa wa kuendelezwa *(high irrigation potential*), hekta milioni 4.8 zina uwezekano wa kati (*medium irrigation potential*) na hekta milioni 22.3 zina uwezekano wa chini wa kuendelezwa *(low irrigation potential).*

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo chetu kimekuwa kikitegemea mvua ambazo upatikanaji wake kwa ujumla umekuwa sio wa kuridhisha na mtawanyiko wake ukiwa hautabiriki. Kutokana na hali hiyo, ukame na mafuriko yamekuwa yakitokea mara kwa mara na kusababisha upatikanaji mdogo wa mazao ya kilimo na uharibifu mkubwa wa mali na miundombinu, ikiwemo ya umwagiliaji. Umuhimu wa kilimo cha umwagiliaji umekuwa ukionekana zaidi katika maeneo ambayo Serikali imeweka miundombinu ya umwagiliaji ambapo uzalishaji wa mazao umeongezeka na kuwa mara mbili hadi tatu zaidi ya ule unaotokana na kilimo cha kutegemea mvua.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2007/2008, eneo la umwagiliaji liliongezeka kwa kiasi cha hekta 15,300 na kufanya eneo lote lililoendelezwa kufikia hekta 289,245. Kati ya eneo hilo, hekta 249,245 ni mashamba ya wakulima wadogo na hekta 50,075 ni mashamba ya wakulima wakubwa wa mazao ya biashara ya chai, kahawa, miwa, maua, mbogamboga na mpunga. Aidha, Wizara yangu itaendelea kuhimiza uendelezaji wa miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba ya wakulima wadogo, wa kati na wakubwa ili kuongeza uzalishaji wa mazao, uhakika na usalama wa chakula na kupunguza umaskini. Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo imeweka kipaumbele cha ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji kwenye maeneo yenye uwezekano mkubwa wa kuendelezwa. Wizara yangu inafanya jitihada kuhakikisha kwamba yanakuwepo matumizi bora na endelevu ya rasilimali za maji kwa kilimo cha umwagiliaji bila ya kuathiri mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2007/2008, Wizara yangu iliendelea kutekeleza Programu Ndogo ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji katika Mabonde yote tisa. Chini ya Programu hiyo, Wizara ilipanga kutekeleza kazi kwenye maeneo makuu matatu kwa

madhumuni ya kuhakikisha kuwa rasilimali hizo zinatumika kwa uwiano kwa sekta zote na kwa njia endelevu. Maeneo hayo ni yafuatayo:-

(i) Kuimarisha Ofisi na Bodi za Mabonde kwa kuzijengea uwezo, ikiwa ni pamoja na kutoa mafunzo, kujenga na kukarabati majengo ya ofisi, kutoa vitendea kazi na kuboresha mifumo ya mawasiliano;

(ii) Kuandaa mipango shirikishi ya usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji katika mabonde *(Integrated Water Resources Management Plans*); na

(iii) Kuwezesha ujenzi wa miundombinu yenye kipaumbele ya menejimenti ya rasilimali za maji katika mabonde ya Pangani, Wami/Ruvu na Bonde la Kati.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/2008, Wizara yangu iliajiri wataalam wapya 18, ikijumuisha wahaidrolojia watatu, maafisa maendeleo ya jamii 11 na mafundi sanifu wa haidrolojia wanne. Vilevile, tathmini ya awali ya ujenzi wa ofisi mpya za mabonde na ukarabati wa ofisi zilizopo ilikamilika. Wizara iliandaa hadidu za rejea na nyaraka za mapendekezo ya zabuni ya kuwapata wataalam washauri watatu wa kusanifu na kuandaa michoro pamoja na kusimamia ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu ilitayarisha nyaraka za zabuni kwa ajili ya kununua magari, pikipiki, kompyuta, na vifaa vya ofisi kwa lengo la kuboresha mazingira ya kazi katika Ofisi za mabonde yote tisa. Wizara ilitayarisha nyaraka za zabuni kwa ajili ya kununua vifaa vya kupima kina cha maji na wingi wa maji kwenye mito, mabwawa na maziwa, kupima hali ya hewa, na ubora wa maji. Vifaa vingine ni vya kupimia mvua, maji chini ya ardhi, kupima ardhi na vifaa vya kuanzisha mtandao wa mawasiliano kwa njia ya kompyuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu itaajiri wataalam wapya 45, ikijumuisha wahaidrolojia 10, wahaidrojiolojia 10, maafisa maendeleo ya jamii watatu, wahandisi wa mazingira sita, mafundi sanifu wa haidrolojia sita, mafundi sanifu wa haidrojiolojia sita na maafisa ugavi wanne. Wizara itakarabati na kujenga ofisi za mabonde, na kununua vitendea kazi. Vitendea kazi hivyo ni; vifaa 1,160 vya kupimia maji, kompyuta 166, magari 27, pikipiki 35 na vifaa vya mawasiliano kwa njia ya kompyuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa 2007/2008, mafunzo ya muda mfupi na warsha zinazohusu utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji katika Ofisi za Mabonde yaliendeshwa kama ifuatavyo:-

(i) Kutathmini maji kwa ajili ya mazingira katika mabonde ya Pangani na Wami/Ruvu;

(ii) Utayarishaji wa taarifa za utekelezaji wa Programu;

(iii) Warsha ya wadau kuhusu menejimenti na matumizi endelevu ya rasilimali za maji za bonde dogo la Ngerengere na bwawa la Mindu mjini Morogoro; na

(iv) Mkutano wa Maafisa wa Maji wa Mabonde kuhusu utayarishaji wa viashiria vitakavyotumika katika kupima utekelezaji wa Programu uliofanyika mjini Morogoro mwezi Mei, 2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu itawezesha mafunzo ya muda mfupi na warsha za kuwajengea uwezo Maafisa wa Maji na Bodi za Maji za Mabonde. Mafunzo yalihusu usimamizi na uendelezaji shirikishi wa rasilimali za maji, masuala ya fedha, ugavi, usimamizi wa kandarasi, tathmini na ufuatiliaji wa utekelezaji wa Programu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu inaandaa mipango shirikishi ya usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji kwenye mabonde ili kukidhi mahitaji ya maji kwa sekta mbalimbali za kiuchumi na kijamii. Katika mwaka 2007/2008, Wizara ilianza kutayarisha mipango hiyo kwa kuanzia na bonde la Rufiji na bonde la Kati ambapo taratibu za kumpata mtaalam mwelekezi zimekamilika. Katika bonde la Rufiji, mpango huo unalenga katika kuboresha usimamizi ili kuongeza maji katika mto Ruaha Mkuu yaweze kutiririka mwaka mzima na kukidhi mahitaji ya maji ya kuzalisha umeme, umwagiliaji, na hifadhi ya mbuga ya wanyama ya Ruaha. Katika Bonde la Kati mpango huo utaboresha usimamizi wa rasilimali za maji ili kuongeza upatikanaji wa rasilimali hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu itamuajiri mtaalam mwelekezi wa kuandaa mipango shirikishi ya usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji katika bonde la Rufiji na Bonde la Kati. Wizara pia, itatathmini rasilimali za maji katika mabonde ya Pangani, Wami/Ruvu na Ziwa Victoria kwa ajili ya kuwezesha maandalizi ya mipango shirikishi ya usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji katika mabonde hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu hufuatilia mwenendo wa rasilimali za maji juu na chini ya ardhi kwa kutumia mtandao wa vituo vya kupimia wingi na ubora wa maji. Taarifa na takwimu zinazopatikana zinaiwezesha Serikali kuandaa mipango shirikishi ya usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji katika mabonde husika. Vilevile, huiwezesha kuchukua hatua za tahadhari dhidi ya majanga mbalimbali pamoja na kusanifu miradi ya maji. Hivi sasa mtandao huo una jumla ya vituo 362 vya kupimia wingi na ubora wa maji kwenye mito, maziwa na mabwawa, vituo 98 vya hali ya hewa, vituo 659 vya kupima kiasi cha mvua, na vituo 65 vya kufuatilia mwenendo wa rasilimali ya maji chini ya ardhi. Mtandao huo utaendelea kuboreshwa kwa kuwa haukidhi mahitaji ya ukusanyaji wa takwimu kutokana na matatizo mbalimbali ambayo ni pamoja na uharibifu wa vifaa katika vituo, unaosababishwa na binadamu, wanyama na mafuriko.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/2008, Wizara yangu, chini ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji ilikamilisha tathmini ya awali na kubaini

mahitaji ya kuboresha mtandao wa kufuatilia mwenendo wa rasilimali za maji. Katika mwaka 2008/2009 Wizara yangu itakarabati vituo 250 vya kupimia wingi na ubora wa maji, vituo 63 vya hali ya hewa na vituo 229 vya kupima kiasi cha mvua. Vituo vipya vitano vya kufuatilia mwenendo wa rasilimali za maji chini ya ardhi vitajengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera ya Maji ya mwaka 2002 inasisitiza ushiriki wa wananchi katika kusimamia na kuendeleza rasilimali za maji. Katika mwaka 2007/2008, chini ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji, Wizara yangu ilianza kuchukua hatua za kuimarisha ushirikishwaji wa wadau katika usimamizi endelevu wa rasilimali za maji kupitia vikundi na vyama vya watumia maji. Kwa mwaka 2008/2009, Wizara yangu itawezesha uanzishaji wa vikundi na vyama vipya vya watumia maji na kuimarisha vikundi vilivyopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu kupitia Ofisi za Mabonde, ilichunguza matoleo ya maji ili kubaini idadi yake. Hatua hiyo itaiwezesha Wizara yangu kudhibiti matumizi ya maji na makusanyo ya maduhuli yatokanayo na matumizi ya maji. Katika mwaka 2007/2008, jumla ya matoleo 15,021 yalitambuliwa. Kati ya hayo, matoleo 4,951, sawa na asilimia 33, yana hati za haki ya kutumia maji, na matoleo 10,070, sawa na asilimia 67, hayana hati. Kutokana na hali hiyo, Wizara inachukua hatua za kuwaelimisha wadau juu ya umuhimu wa kuwa na hati za haki za kutumia maji. Tunatoa hati za haki ya kutumia maji kwa lengo la kuhakikisha matumizi endelevu ya rasilimali hiyo. Jumla ya hati 245 zilitolewa ikilinganishwa na hati 184 zilizotolewa mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu itaendelea kubaini matoleo mengine zaidi na kuwahamasisha wadau juu ya umuhimu wa kuwa na hati za haki ya kutumia maji. Wizara itaendelea kutoa hati za haki ya kutumia maji katika mabonde yote tisa kwa lengo la kuongeza idadi ya matoleo yatakayokuwa na hati na hivyo kuhakikisha matumizi endelevu ya maji na kuboresha makusanyo ya maduhuli.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu husimamia rasilimali za majishirikishi kwa kushirikiana na nchi tunazochangia mabonde ya maji ili kuhakikisha kuwa rasilimali zilizopo zinaendelezwa na kutumika kwa njia endelevu na kwa manufaa ya nchi zetu. Mabonde yenye rasilimali hizo ni Pangani, Ruvuma, Bonde la Kati, Ziwa Victoria, Ziwa Nyasa na Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/2008, Serikali ilishauriana na nchi zilizomo katika bonde la Mto Nile na kukubaliana namna bora ya kukamilisha majadiliano ya Mkataba wa Ushirikiano. Majadiliano ya Mawaziri wa Maji wa nchi hizo yalikamilika mwezi Juni mwaka 2007. Sasa yapo kwenye ngazi ya Wakuu wa Nchi hizo ambao watatoa uamuzi kuhusu kifungu kimoja cha Rasimu ya Mkataba kilichobakia kinachohusu uhakika wa upatikanaji wa maji *(water security)* kwa nchi zote za Bonde la Mto Nile. Baadhi ya nchi hazitaki kuingiliwa katika matumizi ya sasa ya maji na haki zao juu ya matumizi hayo *(current uses and rights).* Msimamo wao unajikita katika mikataba ya mwaka 1929 na 1959 ambayo Serikali ya Uingereza iliingia nao kwa niaba ya makoloni yake. Jambo hilo limekataliwa na Tanzania na nchi nyingine za Bonde.

Hatukubaliani na mikataba hiyo ya zamani ambayo tuliikataa wakati nchi yetu ilipopata uhuru. Hatukubaliani pia, na tafsiri yoyote katika rasimu ya Mkataba wa Ushirikiano inayoturudisha nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2007/2008, Serikali iliendelea kutekeleza miradi ya pamoja na miradi midogo inayotekelezwa na nchi moja moja katika bonde hilo (*Shared Vision* na *Subsidiary Action*) chini ya *Nile Basin Initiative - NBI*. Miradi hiyo ni ifuatayo:-

(i) Usimamizi wa pamoja wa hifadhi ya mazingira;

(ii) Kutoa mafunzo;

(iii) Uzalishaji wa umeme;

(iv) Matumizi bora ya maji kwa ajili ya umwagiliaji;

(v) Mipango na usimamizi wa rasilimali za maji;

(vi) Maendeleo ya jamii;

(vii) Usimamizi wa rasilimali za maji katika mabonde madogo ya mto Kagera na Mara;

(viii) Kujenga mazingira ya kuaminiana;

(ix) Ushirikishaji wa wadau katika matumizi ya maji ya Bonde la *Mto Nile*; na

(x) Uratibu na ufuatiliaji wa miradi ya pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Serikali itaendelea kushauriana na nchi za Bonde la Mto Nile kwa lengo la kukamilisha majadiliano ya Mkataba wa Ushirikiano. Mkataba utawezesha kuundwa kwa Kamisheni ya Bonde hilo ambayo itasimamia matumizi endelevu ya rasilimali za maji. Vilevile, Serikali itaendelea kutekeleza miradi midogo na miradi ya pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2007/2008, nchi yetu, kwa kushirikiana na Kenya na Uganda, iliendelea na maandalizi ya awamu ya pili ya Mpango wa Hifadhi ya Mazingira ya Ziwa Victoria. Mpango huo unalenga kuboresha mazingira ya Ziwa na Bonde lake na hivyo kuimarisha na kuendeleza huduma ya maji, uvuvi, viwanda, usafiri wa majini, maliasili na kilimo. Mpango huo utatekelezwa kwa kipindi cha miaka sita kuanzia mwezi Oktoba, 2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/2008, Wizara yangu iliendelea na taratibu za kuridhia Mkataba wa kuanzisha Kamisheni ya Bonde la Mto Zambezi *(Zambezi Watercourse Commission-ZAMCOM).* Vilevile Wizara yangu iliendelea

kushiriki katika kutayarisha Mkakati wa Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Maji (*Strategy for Integrated Water Resources Management*) chini ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika *(SADC)*. Mkakati huo utakapokamilika ndio utakuwa msingi wa kupanga namna bora ya kuendeleza na kutumia kwa njia endelevu rasilimali za maji za Bonde la Mto Zambezi. Katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu itakamilisha taratibu za kuridhia Mkataba wa kuanzisha Kamisheni ya Bonde la Mto Zambezi na kuendelea kushiriki katika kukamilisha Mkakati wa Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Maji kwenye bonde hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2007/2008, Wizara yangu iliendelea na taratibu za kuridhia Mkataba wa kuanzisha Kamisheni ya Pamoja ya Maji kati ya Tanzania na Msumbiji. Hatua zilizotekelezwa, kulingana na Mkataba huo ni kama, ifuatavyo:-

(i) Kuunda Kamisheni ya Pamoja ya Maji kati ya Tanzania na Msumbiji;

(ii) Kuainisha na kujadili na wadau changamoto za matumizi na usimamizi endelevu wa rasilimali za maji katika Bonde hilo;

(iii) Kuajiri watendaji wakuu wa mradi wa usimamizi endelevu wa rasilimali za maji katika bonde hilo; na

(iv) Kuunda kamati ya usimamizi wa mradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu itakamilisha taratibu za kuridhia Mkataba wa kuanzisha Kamisheni ya Pamoja ya Maji kati ya Tanzania na Msumbiji. Wizara itaendelea kushiriki katika kubuni miradi ya pamoja itakayotekelezwa katika Bonde la Mto Ruvuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu ina wajibu wa kuhakikisha ubora na usafi wa maji kwa lengo la kulinda afya za wananchi. Katika kutimiza azma hiyo, mwaka 2007/2008, Wizara ilipanga kukagua na kuhakiki usafi na ubora wa maji katika vyanzo vya maji 1,500 hapa nchini kwa kutumia maabara zake 16, ambapo sampuli 3,000 zingekusanywa na kuchunguzwa. Vilevile, sampuli 250 za majitaka kutoka viwandani na mitambo ya kusafisha majitaka zilipangwa kukusanywa na kuchunguzwa kimaabara. Katika kipindi hicho kazi zilizotekelezwa ni zifuatazo:-

(i) Jumla ya sampuli 2,925 za maji zilikusanywa katika maeneo ya mijini na vijijini na kuchunguzwa viwango vya kemikali na uwepo wa vijidudu. Sampuli 2,691 sawa na asilimia 92 ya sampuli zote zilikuwa kwenye viwango vinavyokubalika;

(ii) Jumla ya sampuli 189 za majitaka kutoka viwandani na mitambo ya kusafisha majitaka, katika Majiji ya Dar es Salaam, Mwanza, na Tanga, Manispaa za Morogoro, Dodoma, Bukoba, Musoma, na Iringa zilichunguzwa. Matokeo yalionyesha kuwa sampuli 166 sawa na asilimia 88 zipo kwenye viwango vinavyokubalika kwa majitaka hayo kurudishwa kwenye mazingira;

(iii) Sampuli nane za madawa ya kusafisha maji aina ya shabu *(Aluminium sulphate)*, na sampuli 10 za madawa ya *Calcium hypochlorite*, ambayo hutumika kuua vijidudu katika maji, zilihakikiwa ubora wake. Matokeo yalionyesha kuwa madawa hayo yapo katika viwango vinavyokubalika;

(iv) Wizara ilishiriki katika zoezi la kimataifa la kupima uwezo na utendaji wa maabara (*Inter-Laboratory Comparison*), chini ya mpango wa *SADC Measurement Traceability* na Jumuiya ya Nchi za Afrika Mashariki. Lengo lilikuwa ni kupata ithibati (*accreditation*) kwa maabara zetu. Maabara Kuu ya Ubungo na Maabara ya maji ya Mwanza zilihusika kwa kuchunguza na kupima viashiria 19 *(parameters)*, vya sampuli za maji kutoka Namibia na Uganda. Matokeo ya tathmini yanaonyesha kuwa uwezo wa maabara zetu zilizoshiriki upo katika kiwango cha asilimia 75; na

(v) Kuandaa hadidu za rejea za kumpata mtaalam mwelekezi kwa ajili ya kuandaa Mkakati wa Usimamizi wa Ubora wa Maji na Udhibiti wa Uchafuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/2008, Wizara iliendelea kukusanya takwimu na sampuli za maji kwa kutumia mtandao wake wa utafiti wa Ziwa Victoria, ikiwa ni pamoja na kutoka kwenye Ziwa, mito, viwandani, angani, mijini na kwenye makazi yaliyo kando ya Ziwa Victoria. Sampuli zote zilichunguzwa katika maabara za maji za Mwanza, Musoma na Bukoba. Wizara yangu iliendelea kuhimiza uzalishaji bora katika viwanda 12 vilivyopo kando ya Ziwa Victoria ili kupunguza uchafuzi wa maji katika ziwa hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2008/2009, Wizara yangu itaendelea na uchunguzi wa usafi na ubora wa maji. Sampuli 3,500 zitakusanywa kutoka vyanzo mbalimbali nchini. Sampuli 300 za majitaka kutoka viwandani na mitambo ya kusafisha majitaka zitakusanywa na kuchunguzwa kimaabara. Kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji, Wizara yangu itaendelea na mpango wa kuziimarisha maabara za maji nchini kwa kuzikarabati na kuzipatia vitendea kazi. Wizara imepanga kuwa na mfumo wa kuratibu ubora wa maji kwa kuwa na vituo maalum (*Water Quality Monitoring Network*) ambavyo vitasaidia kufuatilia kwa karibu usafi na ubora wa maji katika vyanzo vya maji. Wizara yangu itahakiki usalama wa kutumia chumvi katika kuzalisha chlorine kwa ajili ya kuua vijidudu kwenye maji teknolojia ambayo hivi sasa inatumika katika mradi wa maji wa Chalinze.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2007/2008, chini ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji, Wizara yangu ilianza maandalizi ya ujenzi wa mabwawa na uchimbaji wa visima. Lengo ni kuongeza upatikanaji wa maji ili kukidhi mahitaji ya sekta mbalimbali za kiuchumi na kijamii. Hatua zilizochukuliwa ni kubaini maeneo yanayofaa kujenga miundombinu ya kuhifadhi maji ili kuwezesha maji kupatikana mwaka mzima kwa kuanzia na mabonde ya Wami/Ruvu, Rufiji na Pangani.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Bonde la Wami/Ruvu, Wizara imeandaa hadidu za rejea za kuwapata wataalam waelekezi wa kuchunguza kwa kina hali ya miamba na athari za kimazingira ili kuwezesha kusanifu miundombinu katika eneo litakakojengwa

bwawa la Kidunda. Katika Bonde la Rufiji, Mkutano wa wadau katika eneo litakapojengwa bwawa la Ndembera ulikubali ujenzi wa bwawa hilo. Bwawa litatumika kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji na kuwezesha upatikanaji wa maji katika Mto Ruaha kutiririka mwaka nzima.

Vilevile, Wizara iliendelea na kazi ya upimaji wa eneo la bwawa hilo na imeandaa hadidu za rejea za kumpata mtaalam mwelekezi. Wizara ilichunguza maeneo ya kuchimba visima virefu katika bonde la Usangu. Katika Bonde la Pangani, uchunguzi wa kubaini maeneo ya kuchimba visima virefu katika maeneo ya Kahe na Sanya ulianza kwa kuandaa hadidu za rejea ili kumpata Mkandarasi wa kuchimba visima. Hadidu za rejea za kumpata mtaalam mwelekezi wa kuandaa mbinu za kuudhibiti Mto Kikuletwa, unaohamahama kwenye maeneo ya karibu na chemchemi za Rundugai, ziliandaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kuajiri wataalam waelekezi wa kuchunguza hali ya miamba na athari za mazingira kuwezesha kusanifu miundombinu katika eneo litakakojengwa bwawa la Kidunda na kutayarisha nyaraka za zabuni Kazi hizo zitakamilika mwezi Mei 2009;

(ii) Kuweka mipaka eneo litakalotumika kwa ujenzi wa mradi huo, kazi ambayo itafanyika kati ya mwezi Septemba na Desemba 2008 ili kuwezesha tathmini ya makazi, mali na viumbe vitakavyolazimika kuhama ili kupisha ujenzi;

(iii) Kuajiri mtaalam mwelekezi wa kusanifu bwawa la Ndembera na kutayarisha nyaraka za zabuni;

(iv) Kuajiri wataalam waelekezi wa kuandaa mbinu za kuudhibiti Mto Kikuletwa; na

(v) Kuteua mkandarasi wa kuchimba visima katika bonde la Usangu na maeneo ya Kahe na Sanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, rasilimali ya maji chini ya ardhi ni chanzo muhimu cha kuwapatia wananchi huduma ya maji hasa vijijini na katika maeneo kame. Katika mwaka 2007/2008, Wizara yangu ilibaini maeneo 447 yanayofaa kuchimba visima vya maji. Maeneo hayo ni kama ifuatavyo: Bonde la Pangani 67, Wami/Ruvu mawili, Rufiji 62, Ruvuma 57, Ziwa Nyasa 13, Bonde la Kati 106, Ziwa Rukwa 51, Ziwa Tanganyika 35 na Ziwa Victoria 54. Katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu itaendelea kuchunguza maeneo mbalimbali, lengo likiwa ni kubaini maeneo yanayofaa kuchimba visima virefu kwenye wilaya zote nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/2008, Wizara yangu, kupitia Ofisi za Mabonde, iliendelea kuratibu uchimbaji wa visima vya maji hapa nchini unaotekelezwa na Wakala wa Uchimbaji Visima na Ujenzi wa Mabwawa na kampuni

binafsi. Lengo ni kuhakikisha kuwa taratibu zilizowekwa, chini ya Sheria ya Usimamizi wa Matumizi bora ya Maji, zinafuatwa ili kulinda rasilimali hii muhimu. Jumla ya visima 749 vilichimbwa na kusajiliwa. Kati ya hivyo 461vilichimbwa na Wakala wa Uchimbaji Visima na Ujenzi wa Mabwawa na vingine 288 vilichimbwa na kampuni binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/2008, Wizara yangu iliendelea kutatua migogoro mbalimbali iliyojitokeza katika kusimamia matumizi ya maji. Katika zoezi hilo Wizara ilibaini vyanzo vya migogoro ikiwa ni pamoja na vifuatavyo:-

(i) Uvamizi wa vyanzo vya maji kutokana na kupanua maeneo ya kilimo, ufugaji na ujenzi wa makazi;

(ii) Kuchepusha maji kinyume cha utaratibu kwa kubomoa miundombinu ya umwagiliaji;

(iii) Utupaji holela wa majitaka, taka ngumu na kemikali ikiwemo zebaki kwenye vyanzo vya maji, hali inayosababisha uchafuzi wa maji;

(iv) Baadhi ya watumiaji maji kutokuwa na hati za haki ya kutumia maji na ambao wana hati hizo kutolipia ada kulingana na sheria;

(v) Kutokuelewa vyema na kutozingatia sheria ya matumizi na utunzaji wa rasilimali za maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/2008, Wizara yangu ilipokea migogoro 27 ya maji ambapo 11 ni kutoka Bonde la Pangani, mitatu Bonde la Kati, mitano Bonde la Ziwa Rukwa, mitatu Bonde la Wami/Ruvu na mitano Bonde la Rufiji. Migogoro ilihusu wananchi kugombea maji ya umwagiliaji, matumizi ya nyumbani na uchimbaji wa madini. Hatua zilizochukuliwa na Wizara yangu ni pamoja na kutoa elimu kwa wananchi kuunda kamati za pamoja za kusuluhisha migogoro katika maeneo husika, kuhamasisha uundaji wa vyama vya watumia maji na pale inapobidi kutumia vyombo vya sheria katika kutatua migogoro ya maji. Hadi kufikia mwezi Juni 2008 migogoro tisa ilipatiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu itaendelea kutatua migogoro iliyopo na itakayojitokeza. Wizara itaendelea kuelimisha wananchi, kuhamasisha uundaji wa kamati za pamoja za usuluhishi katika maeneo husika, na uundaji wa vyama vya watumia maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia Bunge lako Tukufu natoa wito kwa wananchi kuzingatie utunzaji na matumizi bora ya rasilimali za maji kulingana na sheria, kanuni na taratibu zilizopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzia mwaka 2007/2008, Wizara yangu, kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI, Wizara ya Fedha na Uchumi, na Washirika wa Maendeleo, ilianza kutekeleza Programu Ndogo ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini. Utekelezaji wa Programu hiyo ulihusisha Halmashauri zote nchini,

ambapo fedha za kuandaa na kutekeleza miradi ya maji na kujenga uwezo zilipelekwa kwenye Halmashauri mwezi Juni 2006 chini ya utaratibu wa utoaji ruzuku ya maendeleo kwa Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu iliendelea kuratibu utendaji wa wahandisi 96 walioajiriwa na Wizara mwaka 2006 na kukabidhiwa Halmashauri na Sekretarieti za Mikoa ambazo hazikuwa na wahandisi wa maji. Kati ya wahandisi hao, 75 walipangwa katika Halmashauri ili kuziimarisha kwa ajili ya kuanza kutekeleza Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji katika ngazi ya wilaya. Wahandisi 17 walipangwa kwenye Sekretarieti za Mikoa ili kushauri Halmashauri kuhusu masuala mbalimbali ya maji na usafi wa mazingira chini ya Programu hiyo na wanne katika miradi ya maji ya kitaifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzia mwaka 2008/2009, Wizara yangu, kwa kushirikiana na TAMISEMI, itaendelea kuimarisha Sekretarieti za Mikoa kwa kuongeza wataalam wa maji hadi kufikia watatu kwa kila mkoa. Wataalam hao watashauri Halmashauri na kusimamia usanifu na utekelezaji wa miradi ya maji. Kulingana na programu ya kuboresha utendaji katika Serikali za Mitaa, Halmashauri zinaruhusiwa kuajiri wataalam kutoka sekta binafsi kwa ajili ya kusanifu miradi mbalimbali. Wizara kwa kutambua uwezo mdogo wa baadhi ya Halmashauri, itatumia wataalam wake na kutoka sekta binafsi ili kuzisaidia Halmashauri, pale ambapo itaonekana kuna upungufu.

Katika kutekeleza azma hii, Wizara yangu, kwa kushirikiana na Halmashauri za Mbozi, Rungwe na Lushoto itasanifu na kufikisha hatua ya kuandaa nyaraka za zabuni tayari kwa utekelezaji wa miradi ya *Lukululu Group, Iyula Group, Masoko Group* na *Mwakaleli Group* na miradi husika katika Wilaya ya Lushoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/2008, Wizara yangu iliendelea kutoa miongozo na ushauri wa kitaalam kwa Halmashauri kwa kushirikiana na Sekretarieti za Mikoa ili kuongeza kasi ya utekelezaji wa Programu. Wizara iliendesha mkutano na wataalam washauri wa maji wa Sekretarieti hizo uliojadili majukumu yao katika kusimamia utekelezaji. Wizara ilitoa mafunzo kwa watendaji wa Halmashauri zote juu ya taratibu za kuandaa taarifa za utekelezaji. Katika kuziimarisha Halmashauri hizo kutekeleza majukumu yao, Wizara imetangaza zabuni za kununua pikipiki. Katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu itaendelea kutoa miongozo mbalimbali na kutoa ushauri wa kiufundi pale inapohitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2006/2007, Wizara ilipeleka jumla ya Shilingi bilioni 19.3 kwa ajili ya kutekeleza miradi iliyo chini ya mipango ya wilaya iliyolenga kuleta matokeo ya haraka. Fedha hizo zilipelekwa kwenye akaunti za Halmashauri za Wilaya na Sekretarieti za Mikoa mwezi Juni 2007. Kati ya fedha hizo, Shilingi milioni 353.5 zilipelekwa Sekretarieti za Mikoa kwa ajili ya kusimamia utekelezaji wa miradi hiyo katika ngazi za Halmashauri. Shilingi bilioni 18.9 zilipelekwa kwenye Halmashauri zote.

Kati ya Halmashauri 121 zilizokuwepo, Halmashauri 84 zilikuwa zimetimiza masharti ya utoaji ruzuku ya maendeleo kwa Serikali za Mitaa. Halmashauri hizo zilipewa fedha kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miradi ya maji na kujijengea uwezo. Halmashauri 37 ambazo hazikuweza kutimiza masharti ya kupewa ruzuku, zilipewa fedha kwa ajili ya kujijengea uwezo tu. Halmashauri 23 zilipewa fedha kwa ajili ya kujenga ofisi mpya na 60 zilipewa fedha kwa ajili ya kukarabati ofisi. Fedha hizo zilitumika katika mwaka 2007/2008 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi yenye kuleta matokeo ya haraka (*quick wins*) na kuzijengea uwezo Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/2008, miradi 1,478 yenye kuleta matokeo ya haraka ilipangwa kutekelezwa. Hadi kufikia mwezi Machi 2008 miradi 969 ilikuwa imekamilika na miradi mingine 509 ilikuwa katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Halmashauri 34 zilikamilisha ukarabati wa ofisi na Halmashauri nane zilikamilisha ujenzi wa ofisi mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi Juni 2007 Wizara yangu, kupitia Hazina ilipeleka Shilingi bilioni 11.95 kwenye Halmashauri zote ili kuendelea na utekelezaji wa miradi inayotoa matokeo ya haraka na fedha kwa ajili ya kuzijengea uwezo. Kati ya Halmashauri 132 zilizopo, kwa mwaka 2007/2008, Halmashauri 120 zilizokuwa zimetimiza masharti ya kupewa ruzuku ya maendeleo zilipewa fedha kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miradi ya maji pamoja na kujenga uwezo. Halmashauri 12 hazikuweza kutimiza masharti, hivyo zilipewa fedha kwa ajili ya kujenga uwezo tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009 Serikali imekasimia jumla ya Shilingi bilioni 62.7 kwa ajili ya maendeleo ya maji katika ngazi za wilaya na mikoa. Sekretarieti za Mikoa zitapelekewa fedha kwa ajili ya kusimamia utekelezaji wa miradi ya maji katika ngazi za Halmashauri. Fedha za kujenga uwezo zitapelekwa kwenye Halmashauri zote na fedha za ruzuku ya maendeleo zitapelekwa kwa Halmashauri zilizofuzu tu. Halmashauri zote zitaendelea kutekeleza Programu Ndogo ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini kulingana na mipango ya Halmashauri zenyewe ya kujenga na kukarabati miradi ya maji ambayo haihitaji utaalam wa kiwango cha juu katika usanifu na ujenzi. Miradi hiyo ni ile inayotarajiwa kuleta matokeo ya haraka. Sambamba na zoezi hilo, Wizara yangu inaendelea na juhudi za kuzisaidia Halmashauri kuwaajiri wataalam washauri watakaofanya usanifu na kuandaa zabuni kwa ajili ya miradi ya maji katika vijiji 10 katika kila Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na juhudi za kuharakisha upatikanaji wa wataalam washauri, Halmashauri nyingi zimeshindwa kupata idadi inayotakiwa ya kampuni za kushindania zabuni kulingana na taratibu za Benki ya Dunia. Hata hivyo tarehe 8 Julai 2008 Benki ya Dunia ilikubali kulegeza masharti hayo kwa Halmashauri 82 hivyo kuashiria mwanzo wa kupatikana na kuajiriwa mapema wataalam washauri kwa kila Halmashauri na utekelezaji wa miradi 10 kwa kila Wilaya kuanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, zoezi la kuwapata na kuwaajiri wataalam kwa kila Halmashauri linatarajiwa kukamilika kabla ya mwezi Machi 2009. Wataalam hao pia, wataandaa nyaraka za zabuni na kusaidia Halmashauri kusimamia utekelezaji wa

Programu katika maeneo yao. Wizara itaendelea kuratibu utekelezaji wa miradi iliyoibuliwa na Halmashauri hizo, ikiwa ni pamoja na kutoa mafunzo, miongozo na ushauri. Wizara pia, itatafiti kuhusu maeneo ya kusaidia katika kuimarisha ushiriki wa sekta binafsi. Wizara itaendelea kutoa huduma na nyenzo za kazi kwa Halmashauri ili kuongeza tija katika utendaji. Kwa ajili hiyo, Wizara itanunua magari 111, pikipiki 252, seti za kompyuta 111 na vifaa vya kujenga mfumo wa mawasiliano kwa njia ya kompyuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2007/2008, Wizara yangu iliendelea kutekeleza miradi mingine ya maji vijijini ambayo ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini ulianza kutekelezwa mwaka 2003 baada ya Sera ya Maji ya mwaka 2002 kupitishwa. Mradi huo ulianza kutekelezwa katika Wilaya tatu za Rufiji, Kilosa na Mpwapwa, zikiwa ni wilaya za mfano, kwa kutumia mkopo nafuu kutoka Benki ya Dunia. Mradi ulihusu ukarabati na upanuzi wa miradi iliyopo na ujenzi wa miradi ya Maji ya mwaka 2002 kupitishwa. Mradi huo ulianza kutekelezwa katika wilaya tatu za Rufiji, Kilosa na Mpwapwa, zikiwa ni wilaya za mfano, kwa kutumia mkopo nafuu kutoka Benki ya Dunia. Mradi ulihusu ukarabati na upanuzi wa miradi iliyopo na ujenzi wa miradi mipya.

Kutokana na mafaniko yaliyopatikana, mwaka 2005 mradi ulipanuliwa hadi kufikia wilaya 14. Wilaya 11 zilizoongezeka ni Morogoro, Mvomero, Handeni, Kilindi, Kiteto, Igunga, Iramba, Singida Vijijini, Manyoni, Kongwa na Kondoa. Mwaka 2007/2008, jumla ya miradi midogo 44 vijijini na sehemu ya mji mdogo wa Kondoa ilikamilishwa. Jumla ya wananchi 347,495 wanapata huduma ya maji safi na salama. Mradi umemaliza muda wake mwezi Juni 2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa Mradi wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini ulikabiliwa na changamoto mbalimbali. Moja ya changamoto hizo ni kutopata maji kwenye baadhi ya visima virefu vilivyochimbwa na hivyo kulazimika kurudia utafiti na uchimbaji katika maeneo ya mbali na vijiji husika (kwa mfano wilaya za Kondoa, Kilindi na Handeni). Changamoto nyingine ni uwezo mdogo wa baadhi ya wakandarasi na wataalam waelekezi wa mradi. Katika maeneo ambayo hayakupata vyanzo vya maji, utekelezaji utaendelea chini ya Programu Ndogo ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini kuanzia mwaka wa 2008/2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2007/2008, Wizara yangu, kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Ujerumani *(KfW)*, iliendelea na utekelezaji wa mradi wa maji katika wilaya za Moshi Vijijini na Hai. Kwa upande wa Wilaya ya Hai, kazi zilizotekelezwa ni ujenzi wa chemchemi ya Kiarowi, upanuzi wa mradi katika kijiji cha Tito kwa urefu wa kilomita 12, ujenzi wa vituo 13 vya kuchota maji, na ujenzi wa matanki mawili ya kupunguza msukumo wa maji (*break pressure tanks*). Kazi nyingine ni ufungaji wa mita katika nyumba 2,500, ujenzi wa skimu ya Roslin kutoka chanzo cha mto Simba, kuunda upya Bodi ya maji ya Losaa KIA na kuunda na kusajili Bodi ya maji ya Lyamungo-Umbwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Wilaya ya Moshi Vijijini, kazi zilizotekelezwa ni kukamilisha ujenzi wa ofisi ya mhandisi wa maji wa wilaya na usanifu wa kina wa mradi, ununuzi wa magari saba, pikipiki 17 na malori matatu, ujenzi wa matanki 15 ya kuhifadhi maji, matanki matatu ya kupunguza msukumo wa maji na kuendeleza chanzo chamaji cha Monyo. Aidha, vijiji 29 vimehamasishwa kushiriki katika utekelezaji wa mradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka 2008/2009, utekelezaji wa mradi wa kusambaza maji na usafi wa mazingira katika wilaya ya Moshi Vijijini na mradi wa wilaya ya Hai utaendelea. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na uchimbaji wa mitaro na ufungaji wa mabomba, ujenzi wa matanki ya kuhifadhi maji na ya kupunguza msukumo wa maji, uchimbaji wa visima, na uhamasishaji na uundaji wa vyombo vya watumiaji maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/2008, Serikali, kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Afrika *(AfDB*), iliendelea kutekeleza Mradi wa Maji na Usafi wa Mazingira katika Wilaya za Monduli na Longido. Mradi huo unatekelezwa katika tarafa za Kisongo, Manyara na Makuyuni, katika Wilaya ya Monduli na tarafa za Kitumbaine na Longido, katika Wilaya ya Longido. Kazi zilizotekelezwa ni ujenzi wa mabwawa 22, uchimbaji wa visima virefu 31, ujenzi wa skimu 16 za maji zenye mtandao wenye urefu wa kilomita 184.2 na ujenzi wa matanki 34 ya kuhifadhi maji. Kati ya hizo, bwawa moja, visima 14 na skimu za maji mbili ziko katika wilaya ya Longido na mabwawa 21, visima 17 na skimu za maji 14 ziko katika wilaya ya Monduli. Katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu itakamilisha utekelezaji wa mradi huo kwa kujenga mabwawa mawili katika vijiji vya Ngoswaki na Orkesumet na ufungaji wa pampu katika visima saba, na kutafuta uwezekano wa kuongeza bwawa na visima katika Wilaya ya Longido.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/2008, Wizara yangu, kwa kushirikiana na Serikali ya Japani *(JICA)* imekamilisha awamu ya kwanza ya usanifu wa kina wa mradi wa maji katika mikoa ya Pwani na Dar es Salaam. Ujenzi wa mradi ulianza mwezi Mei, 2008 katika vijiji 10 ambavyo ni Kwamduma na Kibindu (Bagamoyo), Msimbu (Kisarawe), Minazi Mikinda na Kitomondo (Kibaha), Yaleyale Puna, Tundwi Songani, Mji Mwema-Salanga na Kibugumo (Temeke) na Matosa (Kinondoni). Mradi unahusisha pia ujenzi wa visima virefu vyenye pampu za mikono na pampu za umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Wizara itaendelea na ujenzi wa mradi katika vijiji 10 vifuatavyo:- Kwamduma na Kibindu (Bagamoyo), Msimbu (Kisarawe), Minazi Mikinda na Kitomondo (Kibaha), Yaleyale Puna, Tundwi Songani, Mji Mwema-Salanga na Kibugumo (Temeke) na Matosa (Kinondoni). Awamu ya pili ya usanifu wa kina wa miradi ya maji na ujezi itaanza katika vijiji vya Mwandege, Kipala, Kisemvule, Marogoro, Mfuru Mwambao, Njopeka na Vianzi (Mkuranga), Kitunda, Msongola na Pugu Station (Ilala) na Msimbu (Kisarawe).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa 2007/2008, Wizara yangu iliendelea kushirikiana na Serikali ya Japani (*JICA*) kutekeleza Mradi wa maji katika mikoa ya Mara na Mwanza. Kazi zilizotekelezwa ni kukamilisha usanifu wa awali wa miradi ya maji katika vijiji vya mikoa ya Mara na Mwanza. Vijiji hivyo ni Sogoso, Sotta, Isole, Busekeseke, Katoma Magulukenda, Nyancheche, Buswelu, Nyamiswi, Nyakasasa na Nyakahako (Sengerema), Mhulya na Hungumalwa (Kwimba), Kijereshi (Magu), Bugulala, Kasota, Kamena, Ndelema, Nyashishima, Bogogo, Ikina na Ibondo (Geita), Mcharo (Bunda), Sirorisimba, Ryamisanga, Kisamwene, Bugoji, Isaba na Saragana (Musoma), Nyankunguru, Kiwanja, Bisarwi, Kisumwa, Nyankonge, Masike, Bukama, Oliyo na Tatwe (Tarime), Busawe, Nyansurura na Kebancha (Serengeti), Busongo na Ngaya (Misungwi) na Manilembe na Bukonyo (Ukerewe). Katika mwaka 2008/2009 kazi zitakazotekelezwa ni usanifu wa kina wa miradi ya maji katika vijiji hivyo. Jumla ya Shilingi bilioni 1.8 zitatumika kwa kazi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa 2007/2008, Wizara yangu, kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Korea, ilikamilisha ujenzi wa matanki ya kuvunia maji ya mvua 11 katika shule za msingi tano na sekondari sita na kukarabati mradi wa maji katika kijiji cha Kilulu wilayani Bariadi. Visima vinane vilichimbwa katika wilaya ya Chamwino mkoani Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa 2007/2008, ujenzi na ukarabati wa mabwawa 11 ulifikia hatua mbalimbali za utekelezaji. Mabwawa saba ya Ugunga (Urambo), Kinyambwiga (Bunda), Moita na Ingamuriak (Monduli), Emboret (Simanjiro) Amasatwa (Kiteto) na Katoro (Geita) yamekamilika. Ujenzi wa bwawa la Mugumu (Serengeti) umefikia asilimia 90, bwawa la Nyambele (Bunda) asilimia 50, bwawa la Nyashitanda (Misungwi) asilimia 80 na ukarabati wa bwawa la New Sola (Maswa) uko katika hatua za mwisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka 2008/2009, Wizara yangu itajenga na kukarabati mabwawa 19 ya ukubwa wa kati. Ujenzi na ukarabati wa mabwawa manne ya Mugumu (Serengeti), Nyambele (Bunda), New Sola (Maswa) na Nyashitanda (Misungwi) utakamilishwa. Bwawa moja la Bulenya (Igunga) litakarabatiwa. Mabwawa 14 mapya yatajengwa katika maeneo ya Iguluba (Iringa Vijijini), Matwiga (Chunya), Sasajila (Chamwino), Masuguru (Bagamoyo), Habiya (Bariadi), Seke Ididi (Kishapu), Nyambori (Rorya), Mwanjoro (Meatu), Wegero (Musoma Vijijini), Ingodin (Longido), Mti Mmoja (Monduli), Salama Kati (Bunda), Kawa (Nkasi) na Loonderkes (Simanjiro). Pia, mabwawa manne ya Kanyisambo (Rorya), Kilolo (Kilolo), Kirurumo (Mwanga) na Mapogoro (Mbarali) yatafanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2007/2008, Wizara yangu kupitia Wakala wa Uchimbaji Visima na Ujenzi wa Mabwawa-*DDCA* ilifanikiwa kuchimba visima virefu 461 kati ya lengo la kuchimba visima 400, kama ilivyoainishwa kwenye Jedwali Na. 4. Kati ya visima hivyo, visima 392 vina uwezo wa kuzalisha maji mita za ujazo millioni 31 kwa mwaka. Vilevile, Wakala ulifanya upembuzi yakinifu wa mabwawa madogo matano na kukamilisha ujenzi wa tuta la bwawa kubwa la Mugumu, ambalo lina uwezo wa kuhifadhi maji mita za ujazo millioni 14. Wakala ulikamilisha ujenzi wa bwawa la

Kinyambwiga, wilayani Bunda na kukarabati bwawa la New Sola (Maswa) na Masuguru (Bagamoyo). Kazi za ujenzi wa bwawa la Nyashitanda wilayani Misungwi na bwawa la Nyambele katika wilaya ya Bunda zinaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/2008, Wizara iliendelea kuuongezea uwezo Wakala ili uweze kutoa huduma bora na kwa ufanisi zaidi. Mitambo sita ya kuchimba visima na mitambo sita ya ujenzi wa mabwawa ilikarabatiwa. Katika mwaka 2008/2009, Wizara, chini ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji, itaendelea kuimarisha Wakala kwa kununua mitambo minne mipya ya uchimbaji wa visima na mitambo miwili ya ujenzi wa mabwawa pamoja na vifaa vya kisasa vya uchunguzi wa maji chini ya ardhi na upimaji wa udongo. Wizara itatoa kipaumbele katika kuutumia Wakala katika miradi inayoisimamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/2008, Wizara yangu, kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Uchumi na Washirika wa Maendeleo, iliendelea kutekeleza Programu Ndogo ya Maendeleo ya Maji Mijini. Utekelezaji wa Programu hiyo, unahusisha Mamlaka za majisafi na majitaka katika miji mikuu ya mikoa, miji mikuu ya wilaya na miji mingine midogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma ya maji katika miji mikuu ya mikoa 19 inayohudumiwa na Mamlaka za maji zilizoundwa chini ya Sheria ya Maji Na. 8 ya mwaka 1998, ilifikia asilimia 79.9 mwaka 2007/2008 ikilinganishwa na asilimia 78 mwaka 2006/2007 sawa na ongezeko la asilimia 1.9. Mafanikio hayo yametokana na:-

(i) Kuboresha na kuongeza mitandao ya majisafi ambapo mitandao hiyo ilipanuliwa kwa urefu wa kilomita 228.2 kutoka kilomita 3,837.7 hadi kufikia kilomita 4,065.9 na ujenzi wa vioski vipya 41 kufikia jumla ya vioski 1,238;

(ii) Kuongezeka kwa idadi ya wateja waliounganishwa kwenye mtandao wa maji kutoka 199,106 mwaka 2006/2007 hadi wateja 203,962 mwaka 2007/2008, na kupunguza upotevu wa maji, kutoka wastani wa asilimia 39.7 mwaka 2006/2007, hadi asilimia 36.1 mwaka 2007/2008. Hii inatokana na ongezeko la ufungaji wa dira za maji, kutoka 162,611 hadi 169,252, katika kipindi hicho, sawa na asilimia 83 ya wateja wote;

(iii) Kuboresha huduma kutokana na ongezeko la makusanyo ya maduhuli, kutoka Shilingi bilioni 25.4 mwaka 2006/2007, hadi kufikia Shilingi bilioni 28, mwaka 2007/2008;

(iv) Kuandaa na kutoa ankara sahihi zaidi kwa wateja na kwa wakati kutokana na matumizi ya kompyuta;

(v) Kusambaza maji yenye ubora kutokana na kuimarisha mitambo ya kusafisha maji na kuwa na madawa ya kutosha ya kusafisha na kuua vijidudu kwenye maji; na

(vi) Mwezi Februari 2008 Mamlaka za maji za miji ya mikoa, ikiwa ni pamoja na Dar es salaam, zilikaguliwa hesabu zake za mwaka 2006/2007 (*Audited Accounts*)

kulingana na taratibu za kukagua hesabu hizo kila mwaka. Kati ya mamlaka 21 zilizokaguliwa, mamlaka 16 zilipata cheti safi, aina ya *Unqualified* ambapo Mamlaka tano za Mtwara, Singida, Babati, *DAWASA* na *DAWASCO* zilipata cheti chenye kasoro, aina ya *Qualified*.

Mheshimiwa Naibu Spika, upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama kwa wakazi wa eneo linalohudumiwa na *DAWASA*, chini ya Sheria ya *DAWASA* ya mwaka 2001, eneo ambalo linajumuisha Jiji la Dar es Salaam na Miji ya Kibaha na Bagamoyo, kwa sasa imefikia asilimia 68.

Kiwango hicho cha utoaji huduma katika eneo hilo kimepatikana baada ya zoezi la kuhakiki wateja wanaopata maji kutoka mitambo ya Ruvu Chini, Ruvu Juu, Mtoni pamoja na visima virefu 150 vya *DAWASA* na 100 vya sekta binafsi. Vilevile, uwezo wa kutoa huduma ulichangiwa kwa kuongeza ukusanyaji wa maduhuli ya *DAWASCO*, kutoka Shilingi bilioni 18.3 mwaka 2006/2007, hadi Shilingi bilioni 22 kwa mwaka 2007/2008. Uboreshaji wa kuandaa na kutoa ankara sahihi zaidi kwa wateja na kwa wakati umetokana na matumizi ya kompyuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana ya utoaji wa huduma za maji mijini kwa mamlaka za maji za miji ya mikoa na Dar es salaam, changamoto zilizojitokeza ni pamoja na huduma ya uondoaji wa majitaka kuendelea kubakia asilimia 17 mwaka 2007/2008 kama ilivyokuwa mwaka 2006/2007. Hali hii imesababishwa pamoja na mambo mengine na uchakavu wa miundombinu iliyopo na ongezeko kubwa la watu mijini, ongezeko ambalo haliendani na kiwango cha uwekezaji katika huduma hiyo.

Vilevile, mamlaka nyingine zimekwamishwa kutoa huduma bora kwa wateja wake kutokana na baadhi ya wateja na asasi za Serikali kutolipia huduma wanayopata kwa wakati. Mathalan, hadi kufikia mwezi Machi 2008, jumla ya Shilingi bilioni 29.5 zilikuwa ni malimbikizo ya madeni ya maji kwa wateja. Kati ya malimbikizo hayo ya madeni, Shilingi bilioni 28 ni wateja binafsi, na Shilingi bilioni 1.4 ni za asasi za Serikali. *DAWASCO* pekee wanadai Shilingi bilioni 23 toka kwa wateja binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kupitia Bunge lako Tukufu kutoa wito kwa wateja wa maji mijini kulipia huduma ya maji kwa wakati ili kuziwezesha mamlaka husika kutoa huduma bora na endelevu kulingana na Sera ya Maji ya 2002. Kwa upande wa idara na taasisi za Serikali, tutatafakari suala hili na kutafuta njia bora ya kuziwezesha kulipia madeni na ankara zao mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/2008, Wizara, kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji, iliendelea kuzijengea uwezo Mamlaka za Maji katika makao makuu ya mikoa na wilaya pamoja na miji midogo kwa kutoa mafunzo. Mafunzo hayo yalilenga kuziwezesha Mamlaka hizo kusimamia utekelezaji wa Programu pamoja na kuwawezesha wajumbe wa Bodi za Maji kuelewa wajibu wao katika kusimamia Mamlaka za Maji Mijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kutoa mafunzo, Wizara yangu, kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji, ilitekeleza yafuatayo:-

(i) Kuandaa hadidu za rejea na nyaraka za mapendekezo (*Request for Proposal*) za kuwapata wataalam waelekezi wa kusanifu na kutayarisha nyaraka za zabuni na kusimamia ujenzi na ukarabati wa ofisi za Mamlaka za Babati, Sumbawanga, Iringa, Kigoma, Bukoba, Lindi na Musoma;

(ii) Kutayarisha orodha na takwimu sahihi za kiufundi (*specifications),* na nyaraka za zabuni (*tender documents*), kwa ajili ya ununuzi wa magari 32, pikipiki 46 na kompyuta 42 za Mamlaka za Maji za Miji ya Bukoba, Babati, Lindi, Mtwara, Musoma, Iringa, Kigoma, Songea, Shinyanga, Singida na Sumbawanga;

(iii) Kutayarisha orodha na takwimu sahihi za kiufundi *(specifications)* na nyaraka za zabuni (*tender documents*), kwa ajili ya ununuzi wa kompyuta 47 na pikipiki 120 za Mamlaka za Maji za miji midogo. Magari 10 yatanunuliwa kwa ajili ya mamlaka za maji za miji mikuu ya Wilaya za Makete, Kilwa, Nachingwea, Mbozi, Misungwi, Mbinga, Urambo, Igunga, Handeni na Hanang;

(iv) Ununuzi wa vitendea kazi, ikiwa ni pamoja na vifaa vya kubaini uvujaji wa maji, dira za maji na vifaa vya kusafishia na kuzibulia mabomba ya majitaka kwa ajili ya mamlaka za maji za miji ya Bukoba, Kigoma, Babati, Lindi, Mtwara, Musoma, Sumbawanga, Songea, Mwanza, Shinyanga, Morogoro, Singida, Iringa, Dodoma na Tabora; na

(v) Utayarishaji wa hadidu za rejea kwa ajili ya kumpata mtaalamu mwelekezi wa kutengeneza mfumo wa taarifa za kimenejimenti kwa ajili ya mamlaka za Arusha, Dodoma, Mwanza, Mbeya, Tabora, Tanga, Moshi, Morogoro na Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu, kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji, itaendelea kuziimarisha Mamlaka za maji za miji mikuu ya Mikoa, miji ya Wilaya pamoja na skimu sita kubwa za maji, kwa kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kuanza ukarabati na ujenzi wa ofisi za mamlaka za maji za miji ya mikoa, kuzipatia vitendea kazi mamlaka za maji za miji mikuu ya Mikoa na miji midogo ya Wilaya;

(ii) Kuanzisha na kufunga mifumo ya taarifa za kimenejimenti na kufunga mitandao ya mawasiliano kwa njia ya kompyuta kwenye Mamlaka zilizopo kwenye Miji Mikuu ya Mikoa;

(iii) Kuziongezea uwezo skimu mikubwa za Maswa, *Handeni Trunk Main (HTM),* Makonde, Chalinze, Wanging'ombe na Mugango - Kiabakari kwa kuchangia gharama za uendeshaji;

(iv) Kuendelea na tathmini inayolenga kubaini njia ambazo zitachukuliwa kuiwezesha skimu kubwa za maji za *HTM* na Makonde kuweza kujiendesha na kuanza tathmini ya aina hiyo kwa skimu kubwa nne zilizobaki; na

(v) Kuendelea kutekeleza miradi ya maji inayoendelea katika miji ya Bariadi, Igunga, Kisarawe, Singida na Bunda.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu katika mwaka 2007/2008 ilituma Shilingi bilioni 16.5 kwa ajili ya kutekeleza miradi inayotoa matokeo ya haraka (*quickwins*) katika mamlaka za miji ya mikoa minane, miji ya wilaya na miji midogo 36 na kwenye skimu sita kubwa za maji za Maswa, Chalinze, Mugango Kiabakari, *HTM*, Wanging'ombe na Makonde, kama ilivyoainishwa kwenye Jedwali Na.6. Kazi zilizotekelezwa ni pamoja na kukarabati mifumo ya usambazaji maji, ununuzi wa dira na ufungaji wa mitambo ya kusukumia maji. Katika mwaka 2008/2009, miji midogo 36 itatekeleza miradi inayoleta matokeo ya haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu katika mwaka 2007/2008 iliendelea kuiongezea uwezo wa kujiendesha kwa kulipia umeme na madawa, miradi mikubwa ya Maswa, *HTM*, Makonde, Chalinze, Wanging'ombe na Mugango – Kiabakari. Hatua hiyo imechukuliwa kutokana na ukubwa wa skimu zenyewe kwa Halmashauri husika kutokuwa na uwezo wa kutosha, na uchakavu wa miundombinu. Wizara yangu katika mwaka 2007/2008, ilitoa jumla ya Shilingi bilioni mbili kwa ajili ya kulipia ankara za umeme na kugharamia uboreshaji wa miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu, kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Serikali ya Ufaransa *(AFD)* imekamilisha usanifu wa miradi ya maji na kutayarisha nyaraka za zabuni ili kuwapata makandarasi wa kujenga miradi ya maji katika miji tisa ya Ikwiriri, Kilosa, Mvomero, Kibiti, Mpwapwa, Kibaigwa, Gairo, Utete na Turiani. Miji hiyo ina jumla ya wakazi 283,565. Serikali imekubaliana na *AFD* kugharamia ujenzi wa miradi katika miji ya Mpwapwa na Utete kwa gharama ya *Euro* milioni 3.5. Ujenzi wa miradi ya maji katika miji saba iliyobaki utagharamiwa na Serikali kwa kushirikiana na washiriki wengine wa maendeleo, chini ya *WSDP*, na utekelezaji wake, ambao unakadiriwa kuwa *Euro* milioni 12, utaanza katika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu katika mwaka 2007/2008 iliandaa hadidu za rejea ili kumpata mhandisi mwelekezi kwa ajili ya kutoa ushauri wa jinsi ya kuunganisha uendeshaji wa mamlaka zaidi ya moja *(clustering)* kwa lengo la kupunguza gharama. Vilevile, kazi hiyo itajumuisha miradi ya majaribio na itakamilika mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/2008, Wizara yangu iliendelea kutafiti na kusanifu miradi ya majisafi na majitaka katika miji mikuu ya mikoa kwa lengo la kukidhi mahitaji ya huduma hizo kwa kipindi cha muda mfupi ambapo utekelezaji ulikuwa kama ifuatavyo:-

(i) Kukamilisha nyaraka za zabuni ya kuwapata makandarasi wa ujenzi wa kazi za dharura zinazohusu ukarabati na upanuzi wa miundombinu kwa ajili ya kuboresha mifumo ya utoaji huduma ya maji kwa miji ya Babati, Lindi, Mtwara, Sumbawanga, Masasi na Nachingwea; na

(ii) Kukamilisha nyaraka za zabuni ya kumpata mtaalam mwelekezi kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu, usanifu wa kina, utayarishaji wa nyaraka za zabuni na usimamizi wa kazi katika miji ya Arusha, Dodoma, Morogoro, Kigoma, Tanga, Songea, Babati, Lindi, Mtwara, Shinyanga,Tabora, Moshi, Mwanza, Musoma, Bukoba na Sumbawanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2008/2009, Wizara yangu itafanya upembuzi yakinifu, usanifu wa kina, utayarishaji wa zabuni na usimamizi wa kazi katika miji ya Arusha, Dodoma, Morogoro, Kigoma, Tanga, Songea, Babati, Lindi, Mtwara, Shinyanga, Tabora, Moshi, Mwanza, Musoma, Bukoba na Sumbawanga ikiwa ni pamoja na miji ya wilaya na miji midogo iliyo chini ya usimamizi wa Mamlaka za Maji za Miji ya Mikoa Hatua hizo zitaiwezesha Wizara kuanza ujenzi wa miradi ya maji katika mamlaka hizo. Wizara itaanza upembuzi yakinifu, usanifu wa kina na kutayarisha zabuni za usimamizi wa kazi katika Miji midogo 19. Kwa lengo la kuharakisha utekelezaji, Mamlaka za Maji za Miji Mikuu ya Mikoa zitasimamia na kuratibu utekelezaji katika Miji midogo iliyo katika Mikoa husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Miji ya Wilaya za Masasi na Nachingwea, mkoani Mtwara na Lindi, imekuwa na uhaba mkubwa wa vyanzo vya maji ili kukidhi mahitaji yao ya sasa ya maji yanayofikia mita za ujazo 12,600 kwa siku. Wizara yangu, kwa lengo la kutatua tatizo hilo, mwaka 2006/2007 ilikamilisha upembuzi yakinifu wa mradi wa maji kwa miji hiyo kwa kutumia chanzo cha chemichemi za Mbwinji. Mradi huo unalenga kukidhi mahitaji ya maji hadi mwaka 2025, yanayokadiriwa kufikia mita za ujazo 32,800 kwa siku. Mradi ulithaminishwa kuwa wa gharama za awali za shillingi billioni 34.5**.** Mradi huo pia, utanufaisha vijiji 23 vilivyopo kandokando ya bomba kuu litakalojengwa kutoka Mbwinji kwenda Masasi na Nachingwea.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** katika mwaka 2007/2008, Wizara yangu ilitayarisha nyaraka za zabuni za kumpata mtaalam mwelekezi wa kusimamia ujenzi wa mradi na mkandarasi. Katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu itabaini makandarasi wenye uwezo *(prequalification)* na kuwapatia nyaraka za zabuni ili kumpata anayefaa kuanza ujenzi. Napenda, kwa niaba ya Serikali, kuwathibitishia wananchi wa Masasi na Nachingwea kwamba mradi huu utatekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo tambarare ya Wilaya za Same na Mwanga, na Mji wa Orkesumet, katika Wilaya ya Simanjiro, yamekuwa yakikabiliwa na uhaba mkubwa wa maji kwa muda mrefu. Mwaka 2008/2009 Wizara yangu itaanza upembuzi yakinifu na usanifu wa miradi katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu, kwa lengo la kukidhi mahitaji ya huduma za maji mijini kwa kipindi cha muda wa kati na wa muda mrefu, iliendelea

kuandaa nyaraka za mapendekezo (*Request for Proposal*) ili kumpata mhandisi mwelekezi kwa ajili ya kufanya utafiti wa kuboresha huduma ya majisafi na majitaka kwa miji ya Lindi, Mtwara, Sumbawanga, Kigoma, Babati, Bukoba na Musoma, chini ya *ACP-EU Water facility*.

Mradi huu unalenga kuboresha huduma ya majisafi na majitaka kwa miji hiyo ili kukidhi malengo ya taifa ya huduma kwa wote ifikapo mwaka 2025. Katika mwaka 2008/2009 kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na kufanya usanifu wa kina, utayarishaji wa nyaraka za zabuni ya kuwapata makandarasi ambao wataanza ujenzi wa mradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/2008, Wizara yangu, kwa kushirikiana na Shirika la Ushirikiano wa Kiufundi la Ubelgiji (*Belgian Technical Cooperation- BTC* ), iliendelea kutekeleza mradi wa kuboresha upatikanaji wa maji na usafi wa mazingira kwa maeneo ya pembezoni mwa Jiji la Dar es Salaam. Mradi huo unalenga kuboresha huduma hizo katika maeneo ambayo hayana mtandao wa usambazaji maji Jijini, kwa gharama ya *Euro* milioni 7.85**,** ambapo upembuzi yakinifu umekamilika. Katika mwaka 2008/2009 usanifu wa mradi, pamoja na utayarishaji wa nyaraka za zabuni, utafanyika kwa ajili ya wilaya za Kinondoni, Temeke na Ilala.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/2008, Serikali, kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Marekani (*Millenium Challenge Corporation* - *MCC*) ilikamilisha uchambuzi wa miradi itakayogharamiwa na Shirika hilo. Miradi mitatu ambayo itagharimu Dola za Marekani milioni 66 ilipendekezwa. Miradi hiyo ni kama ifuatavyo:-

(i) Kutoa msaada wa kiufundi wa kudhibiti uvujaji wa maji na maji yasiyolipiwa kwa *DAWASCO* na mamlaka ya maji ya mji wa Morogoro;

(ii) Kupanua mtambo wa maji wa Ruvu Chini ili kuongeza uzalishaji wa maji kutoka uwezo wa sasa wa lita milioni 180 kwa siku hadi lita milioni 270; na

(iii) Kupanua na kukarabati miundombinu ya maji mjini Morogoro, ikiwa ni pamoja na chujio la maji la Mambogo na Mafiga. Chini ya mradi huo uzalishaji wa maji utaongezaka kutoka lita milioni 23 hadi lita milioni 33 kwa siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu imeandaa nyaraka za mapendekezo (*Request for Proposal*) ya kuwapata wahandisi waelekezi watakaosanifu miradi inayogharimiwa na *MCC*. Katika mwaka 2008/2009 wahandisi waelekezi wataajiriwa na kuanza kazi ya usanifu wa miradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/2008, Wizara yangu ilikamilisha usanifu wa awamu ya pili ya mradi wa maji wa Chalinze na kutayarisha nyaraka za zabuni za kuwapata makandarasi wa ujenzi. Katika mwaka 2008/2009 makandarasi wataajiriwa na kazi za kupanua mradi zitaanza, zikijumuisha ulazaji wa mabomba yenye urefu ya kilomita 401 kwenye vijiji 42**,** kujenga vituo viwili vya kusukuma maji, ujenzi wa chujio moja na matanki 37 ya kuhifadhia maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na Umoja wa Nchi za Ulaya *(EU)*, na Benki ya Maendeleo ya Ujerumani *(KfW)*, iliendelea kutekeleza miradi ya majisafi na majitaka katika miji ya Mbeya, Mwanza na Iringa, chini ya mpango wa kuboresha huduma za maji mijini *(Urban Regional Centers Program).* Katika kipindi cha mwaka 2007/2008 Wizara iliendelea kuboresha miundombinu ya majisafi na majitaka katika miji ya Mbeya, Mwanza, Iringa na Songea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mji wa Mbeya, Wizara ilikamilisha awamu ya kwanza ya ukarabati wa bomba kuu la maji la Majengo-Simike, kupanua vyanzo vya maji vya Mfwizimo-Nsoho, Nsoho-Majengo na Nzovwe. Mabomba ya kusambazia maji yenye urefu wa kilomita 44 yalitandazwa, pamoja na mabomba ya majitaka yenye urefu wa kilomita 1.5. Vilevile, ilikamilisha taratibu za kumpata mkandarasi wa kuanza awamu ya pili ya ujenzi wa mradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu itaanza utekelezaji wa awamu ya pili ya mradi huo kwa kupanua mtandao wa majisafi na majitaka katika maeneo ya Uyole, Iyunga na kujenga mabwawa ya majitaka eneo la Kalobe.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/2008, Wizara yangu ilikamilisha awamu ya kwanza ya mradi wa kuboresha huduma za maji katika mji wa Mwanza. Kazi zilizotekelezwa ni pamoja na upanuzi wa chanzo cha maji cha *Capri Point* katika Ziwa Victoria, kupanua mtambo wa kuchuja maji, ufungaji wa pampu, ujenzi wa matanki matano ya kuhifadhi maji, vioski 124 na ulazaji mtandao wa mabomba ya kusambaza majisafi wenye urefu wa kilomita 92 katika maeneo ya Ilemela, Nyakato, Pansiasi, Busweru, Igoma na Nyamanoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu itapitia upya nyaraka za zabuni ili kupata mkandarasi wa kuanza utekelezaji wa awamu ya pili. Awamu hiyo inayohusisha ukarabati na upanuzi wa miundombinu ya majitaka katika makazi yasiyo rasmi katika Jiji la Mwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nyaraka za kizabuni, ikiwa ni pamoja na tathmini, mahojiano na kuandaa mkataba wa kandarasi itakayohusu ukarabati na upanuzi wa mradi wa majisafi na majitaka katika mji wa Iringa zimekamilishwa. Katika mwaka 2008/2009, utekelezaji utahusisha kazi za upanuzi wa vyanzo vya maji vya Ndiuka na Kitwiru, upanuzi wa chujio, ujenzi wa matanki 11 ya kuhifadhi maji, ulazaji wa bomba kuu la urefu wa kilomita 19 na mabomba ya kusambaza maji yenye urefu wa kilomita 120.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2007/2008, Wizara yangu pia, iliendelea kutekeleza kazi za uimarishaji wa miundombinu ya majisafi na majitaka katika mji wa Songea. Kwa mwaka 2008/2009, Wizara yangu itaendelea na utekelezaji wa mradi huo, ikiwa ni pamoja na kuunganisha wateja kwenye mtandao wa majitaka na upanuzi wa mtandao wa majisafi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu, kwa kushirikiana na Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Afrika *(BADEA)* na Umoja wa Nchi zinazozalisha Mafuta kwa Wingi Duniani *(OPEC)*, ilikamilisha maandalizi kwa ajili ya ukarabati na upanuzi wa mradi wa majisafi katika Mji wa Singida. Kazi zilizotekelezwa ni pamoja na kupitia taarifa ya usanifu wa mradi na kuajiri mkandarasi atakayeanza ujenzi. Katika mwaka 2008/2009, ujenzi wa mradi huo utaanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/2008, Wizara yangu, kwa kushirikiana na Serikali ya Uswisi, kupitia shirika lake la *SECO*, ilifanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya kupanua na kukarabati mifumo ya majisafi ya manispaa ya Tabora. Utekelezaji ulihusisha pia, kubadilisha mtandao wa mabomba ya kusambaza maji kwenye makazi mapya ya manispaa ya Dodoma, ikiwa ni pamoja na kuanza kuweka mtandao mpya wa mabomba eneo la Chuo Kikuu cha Dodoma. Katika kipindi hicho, Wizara yangu kwa msaada wa Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China, iliendelea na juhudi za kupunguza uvujaji wa maji na kupanua mtandao wa maji katika manispaa ya Dodoma. China imetoa msaada wa mabomba yenye urefu wa kilomita 87 na viungio vyake, vyenye gharama ya Dola za Marekani 560,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2008/2009, Wizara yangu itaendelea na ukarabati na upanuzi wa miundombinu ya majisafi na majitaka katika Miji ya Dodoma na Tabora, ambapo kiasi cha shilingi milioni 400 zitatolewa na *SECO* na Serikali itatoa shilingi bilioni 1.5.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/2008, Wizara yangu kwa kushirikiana na Serikali ya Ufaransa, kupitia Shirika lake la Maendeleo la *AFD*, iliandaa nyaraka za mapendekezo (*Request for Proposal*) ya kumpata mtaalam mwelekezi. Mtaalam huyo atasanifu na kuandaa nyaraka za zabuni kwa ajili ya ujenzi wa mifumo ya majisafi katika miji ya Musoma na Bukoba. Kazi hizo zitakamilika mwaka 2008/2009, na ujenzi kuanza 2009/2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/2008, Wizara yangu iliendelea na ujenzi wa mradi wa kutoa Maji Ziwa Victoria kwenda miji ya Kahama, Shinyanga na Vijiji 54 vilivyo kando ya bomba kuu. Utekelezaji wa mradi huo ulikuwa kama ifuatavyo:-

(i) Ulazaji wa bomba kuu kutoka Solwa hadi Kahama na Shinyanga na mabomba ya usambazaji maji katika Miji ya Kahama na Shinyanga umekamilika;

(ii) Upanuzi wa kituo cha umeme cha Bulyanhulu na ujenzi wa njia ya umeme kutoka Bulyanhulu hadi kwenye mitambo ya Ihelele umekamilika;

(iii) Mitambo ya Ihelele ya kusafisha na kuua vijidudu kwenye maji imefanyiwa majaribio;

(iv) Kazi ya kujenga matanki na kulaza mabomba kwa ajili ya kuvipatia maji vijiji tisa katika Wilaya ya Misungwi, 10 Shinyanga Vijijini na 20 katika Wilaya ya Kahama imefikia asilimia 50; na

(v) Mamlaka ya kuendesha mradi wa maji wa Kahama Shinyanga, itakayojulikana kama *Kahama Shinyanga Water Supply Authority (KASHWASA)* imeanzishwa kisheria na taratibu za kuiendesha Mamlaka zinakamilishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi mzima kwa sasa unafanyiwa majaribio ya mwisho (*Final Testing*). Zoezi hili litachukua kipindi cha miezi miwili hadi Septemba 2008. Kazi ya uunganishaji wateja kwenye mtandao itachukua kipindi cha miezi mitatu zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kukamilika kwa ujenzi wa mradi wa majisafi wa Kahama-Shinyanga kwa kiwango kikubwa, katika mwaka 2008/2009 Wizara itakamilisha ujenzi wa matanki na kulaza mabomba kwa ajili ya vijiji vyote 54 (vijiji tisa katika Wilaya ya Misungwi, 10 Shinyanga Vijijini, 20 katika Wilaya ya Kahama na 15 wilaya ya Kwimba). Kazi ya kuunganisha wateja kwenye mfumo mpya wa usambazaji maji kwa miji ya Kahama na Shinyanga itaanza. Vilevile, mamlaka ya kusimamia uendeshaji wa mradi huo ya *Kahama Shinyanga Water Supply Authority (KASHWASA)*, itaanzishwa rasmi, na itaimarishwa ili iweze kutoa huduma endelevu. Mamlaka za maji za miji ya Kahama na Shinyanga na vijiji 54 watajengewa uwezo ili kusimamia uendeshaji wa mradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzia mwaka 2006, Wizara yangu, kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Makazi (*UN-HABITAT)* imeendelea kutekeleza mradi wa majisafi na usafi wa mazingira katika miji ya Bukoba, Bunda, Geita, Musoma, Sengerema, Muleba na katika mji mdogo wa Mtukula. Katika mwaka 2007/2008, awamu ya kwanza ya mradi ilitekelezwa katika miji ya Bukoba, Muleba na Mtukula ambapo ilihusisha ukarabati na upanuzi wa mitandao ya maji, ujenzi wa vioski, ununuzi wa dira za maji, uboreshaji wa vyanzo vya maji na kuboresha usafi wa mazingira. Awamu ya kwanza itagharimu Dola za Marekani milioni 4.9. Katika mwaka 2008/2009, utekelezaji wa mradi huo utaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia *DAWASA* inaendelea kutekeleza mradi wa uboreshaji wa miundombinu ya majisafi na majitaka Jijini Dar es Salaam (*Dar es Salaam Water Supply and Sanitation Project, DWSSP*). Mradi huo ulianza kutekelezwa mwaka 2003 na unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba 2009. Kazi zilizotekelezwa chini ya mradi huo kwa mwaka 2007/2008 ni zifuatazo:-

(i) Kuiongezea *DAWASCO* uwezo wa kujiendesha kwa kuipatia Shilingi bilioni mbili;

(ii) Kukarabati mitambo ya kusafishia maji Ruvu Juu, Ruvu Chini na Mtoni ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 85;

(iii) Kukarabati mabomba makuu yanayosafirisha maji kutoka matanki ya kuhifadhi maji ya Kimara na Chuo Kikuu umekamilika. Vilevile, tanki jipya lenye mita za ujazo 5,000 limejengwa eneo la Wazo na linatumika;

(iv) Kubadilisha mabomba ya kusambaza maji umbali wa kilomita 84 ili kurahisisha usambazaji wa maji;

(v) Kukarabati mtandao wa kusambazia maji ambapo mabomba ya urefu wa kilomita 316 yalilazwa na wateja 35,000 waliunganishiwa maji;

(vi) Kukarabati mfumo wa majitaka kwa kulaza mabomba mapya yenye urefu wa kilomita 66;

(vii) Kulaza bomba kuu la kumwaga majitaka baharini lenye urefu wa kilomita 1.04;

(viii) Kukarabati mabwawa ya majitaka katika maeneo ya Mabibo, Lugalo, Ukonga, Buguruni, Mikocheni, Vingunguti na Kurasini umefanyika na kufikia asilimia 85; na

(ix) Ujenzi wa miradi ya maji na usafi wa mazingira pembezoni mwa Jiji la Dar es Salaam umeendelea kutekelezwa ambapo miradi 16 kati ya 33 imekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu pia, katika kuboresha huduma za maji Jijini Dar es Salaam ilichimba visima virefu vitatu vya uchunguzi na vitatu vya uzalishaji huko Kimbiji na Mpera wilayani Mkuranga na Mpiji wilayani Bagamoyo. Visima vya Mpera na Kimbiji vimegundulika kuwa na maji mengi. Uchunguzi wa kina wa kutathmini wingi wa maji hayo na wakati huohuo kusanifu mfumo utakaofikisha maji kwa wakazi wa Dar es Salaam na Wilaya ya Mkuranga unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka wa jana, Wizara iliarifu Bunge lako Tukufu kuhusu mashauri mawili yaliyofunguliwa kwenye vyombo vya utatuzi wa migogoro ya kimataifa. Kampuni ya *City Water Services Ltd* ilifungua shauri la madai dhidi ya *DAWASA* na kampuni mama ya *City Water Service Ltd ya Biwater Gauff Tanzania Ltd (BGT)*, ilifungua shauri la madai dhidi ya Serikali kwa kuvunja isivyo halali mkataba wa kuendesha huduma za maji katika Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shauri hilo la *City Water Ltd* dhidi ya *DAWASA* lilikuwa chini ya chombo cha kusuluhisha migogoro ya mikataba ya kibiashara *UNCITRAL (United Nations Commission of International Trade Law*), wakati shauri la kampuni ya *BGT* dhidi ya Serikali limefunguliwa kwenye chombo cha usuluhishi wa migogoro ya vitega uchumi cha kimataifa (*International Centre for Settlement of Investments Disputes - ICSID).*

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 31 Desemba 2007, *UNCITRAL* ilitoa uamuzi wa shauri kati ya *DAWASA* na *City Water Services Ltd* dhidi ya *DAWASA* ambapo *DAWASA* ilishinda. Kutokana na uamuzi huo kampuni ya *City Water Service Ltd* imeamriwa kuilipa *DAWASA* Shilingi bilioni 7, pamoja na gharama za kuendesha kesi na riba. Taratibu za kufuatilia madai ya hukumu hiyo zinaendelea kupitia wakili aliyeteuliwa na Serikali kusimamia shauri hilo. Kuhusu shauri lililo chini ya *ICSID* usikilizaji wake umekamilika lakini uamuzi bado haujatolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji *(EWURA)* ambayo inasimamiwa na Wizara yangu, ilianzishwa chini ya Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania. Ilianza kazi mwezi Juni 2006. *EWURA* hudhibiti bei na hutoa leseni kwa watoa huduma katika Sekta za Maji na nishati baada ya waombaji kukamilisha masharti yanayolenga katika kuchochea ongezeko la tija. *EWURA* husimamia uwekezaji, ubora wa huduma na ushindani katika Sekta za Maji na Nishati. Katika mwaka 2007/2008, *EWURA* ilitekeleza yafuatayo :-

(i) Kujenga mifumo ya kitaasisi na kimenejimenti kwa kuajiri watumishi wenye sifa na kuwapa mafunzo ili kuwajengea uwezo; na

(ii) Kutoa elimu kwa wananchi kuhusu masuala mbalimbali katika sekta inazozisimamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, *EWURA* pia, iliendelea kutekeleza jukumu la kukagua miundombinu ya maji, umeme, gesi asilia na bidhaa za petroli kwa lengo la kuhakiki usalama, ubora wa huduma zitolewazo. Katika mwaka 2007/2008, *EWURA* ilikagua miundombinu ya Mamlaka za Maji Mijini, miradi mipya ya kuzalisha umeme na vituo vya mafuta. Mwaka 2008/2009, *EWURA* itaimarisha ukaguzi huo ili kulinda usalama wa watu na mali zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Sekta ya Maji, *EWURA* inadhibiti bei za huduma za maji kwa lengo la kulinda maslahi ya watumiaji na mamlaka zinazotoa huduma hizo. Katika mwaka 2007/2008, *EWURA* ilipokea na kuchambua maombi tisa ya kupandisha bei za maji kwa Mamlaka za Dodoma, Moshi, Musoma, Songea, Mwanza, Singida, Tanga, Mbeya na Iringa. Katika mwaka 2008/2009, *EWURA* itaendelea kupokea, kuchambua na kuyatolea maamuzi maombi yaliyowasilishwa na yatakayowasilishwa. Mamlaka zote za miji ya mikoa zina leseni ya muda na kwa sasa zinakamilisha taratibu za kupata leseni kamili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu, kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo, imeanza kutekeleza Programu ndogo ya Kuimarisha na Kuzijengea Uwezo Asasi za Sekta ya Maji ngazi ya Kitaifa, Mikoa na Wilaya. Katika mwaka 2007/2008, Wizara ilikamilisha maandalizi ya mipango na mikakati ya kuzijengea uwezo Taasisi zake na Sekretarieti za Mikoa katika kusimamia Programu kwa kutekeleza yafuatayo:-

(i) Kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa wataalam 300 wa Wizara na Sekretarieti za Mikoa yaliyolenga kuwajengea uwezo wa kutekeleza majukumu kulingana na mahitaji ya Programu;

(ii) Kuandaa taratibu za zabuni za kuwezesha ukarabati na upanuzi wa ofisi za Wizara;

(iii) Kuandaa taratibu za zabuni za kuwezesha ununuzi wa vitendea kazi kwa ajili ya matumizi ya Wizara na Sekretarieti za Mikoa;

(iv) Kuandaa taratibu za kuwezesha uboreshaji wa mfumo wa mawasiliano na upashanaji wa habari na kuimarisha Vitengo vipya vinavyosimamia na kuratibu mawasiliano;

(v) Kuainisha vipaumbele vitakavyotumika kuandaa mwongozo utakaosimamia uandaaji wa mipango ya kujenga uwezo katika ngazi zote za utekelezaji wa Programu; na

(vi) Kuwajengea uwezo Wakala wa Uchimbaji wa Visima na Ujenzi wa Mabwawa, *EWURA*, Chuo cha Maji, na Bohari ya Maji Kurasini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu itaendelea kukamilisha taratibu za ununuzi zitakazowezesha kuanza usanifu, ukarabati na upanuzi wa ofisi za Wizara. Magari 50 na seti za kompyuta 120 na vifaa vingine vitanunuliwa na kusambazwa kwa watekelezaji ngazi ya Wizara na Mikoa. Wizara itaandaa mwongozo wa mipango ya kujenga uwezo kwa kutumia vipaumbele vilivyoainishwa katika ngazi zote za utekelezaji wa Programu. Katika juhudi za kujenga uwezo, Wizara pia, itatekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kukamilisha na kuanza kutekeleza mpango wa mafunzo ya muda wa kati (miaka 3) wa Wizara. Jumla ya Watumishi 1,200 wa Wizara na taasisi zake, ikiwa ni pamoja na Wakala wa Uchimbaji wa Visima na Ujenzi wa Mabwawa, Chuo cha Maji na Bohari Kuu ya Maji na Maafisa wa Maji katika Sekretarieti za Mikoa watapatiwa mafunzo;

(ii) Kusambaza mwongozo wa kujenga uwezo kisekta na kuhamasisha wadau kuzingatia mwongozo huo katika kuandaa mipango yao; na

(iii) Kuimarisha ushiriki wa taasisi zisizo za kiserikali katika kusambaza, kuhamasisha na kufuatilia utekelezaji wa Mikakati ya Maendeleo ya Sekta za Maji na Umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu, kupitia Chuo cha Maji, ina jukumu la kujenga uwezo wa wataalam wa fani ya ufundi katika uendelezaji na usimamizi wa matumizi ya rasilimali za maji. Katika mwaka 2007/2008, Wizara yangu iliendelea kuboresha miundombinu na mazingira ya Chuo ili kukiwezesha kutoa mafunzo ya ufundi katika mfumo wa tuzo za kitaifa za elimu ya ufundi (*National Technical Award - NTA System).* Utekelezaji huo ulizingatia maelekezo na mapendekezo ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (*National Council for Technical Education - NACTE).*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua zilizochukuliwa katika kuboresha Chuo ni pamoja na kuandaa taratibu za awali za kununua vifaa na nyenzo muhimu na ukarabati wa Mabweni manne. Jumla ya wanafunzi 61 walisajiliwa katika mafunzo ya stashahada na wanafunzi 200 katika mafunzo ya ufundi stadi. Wizara, kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Serikali ya Ujerumani, kupitia Shirika la *GTZ*, imekamilisha mchakato wa kukiwezesha Chuo cha Maji kuwa Wakala. Mpango Mkakati wa Muda wa Kati wa Chuo cha Maji kama Wakala, unahusu, pamoja na mambomengine, yafuatayo:-

(i) Kutoa mafunzo yanayomwezesha mhitimu kuwa na ujuzi wa kutosha katika Sekta ya Maji;

(ii) Kutafiti na kutoa ushauri wa kitaalam katika kutatua matatizo ya Sekta ya Maji; na

(iii) Kuimarisha ufanisi katika uendeshaji na utawala wa Chuo ili kutoa huduma bora kwa wadau.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka 2008/2009, Wizara yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Washirika wa Maendeleo, kupitia *WSDP*, itaendelea kutekeleza mapendekezo yaliyoainishwa kwenye Mkakati wa Muda wa Kati (*Medium Term Strategic Plan*) na Mpango wa Uendeshaji wa Wakala wa Chuo cha Maji *(Business Plan)* ikiwa ni pamoja na kukamilisha yafuatayo:-

(i) Kubadili Jina la Chuo kutoka *Water Resources Institute (WRI)* na kuwa *Water Development and Management Institute (WDMI);*

(ii) Kuboresha mazingira ya Chuo, ikiwa ni pamoja na kukarabati na kujenga miundombinu na majengo mapya;

(iii) Kupandisha hadhi na viwango vya taaluma kwa kutoa wataalam wa fani ya ufundi sanifu na uhandisi katika uendelezaji na usimamizi wa rasilimali na matumizi ya maji pamoja na kuongeza idadi ya wanafunzi wapya wa stashahada kutoka 60 na kuwa 300 kwa mwaka;

(iv) Kuandaa mpango wa muda wa kati na muda mrefu wa maendeleo ya watumishi wa Wakala na kuanza utekelezaji wake ili kukidhi mabadiliko ya uendeshaji na utendaji;

(v) Kuboresha mifumo ya taarifa za kimenejimenti na teknolojia ya mawasiliano kwa njia ya kompyuta*;*

(vi) Kuimarisha utafiti na ushauri wa kitaalam katika nyanja mbalimbli za Sekta ya Maji; na

(vii) Kuboresha mitaala ya stashahada na kuandaa mitaala ya shahada katika fani ya maji na kuwasilisha *NACTE* kwa ajili ya ithibati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu pia inatekeleza Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo *(ASDP)*, inatekeleza Mkakati wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo *(Agricultural Sector Development Strategy – ASDS),* ambao umezingatia malengo ya MKUKUTA na malengo ya Milenia.

Katika utekelezaji wa *ASDP*, malengo makuu yaliyoainishwa ni pamoja na kuongeza tija mara mbili katika kilimo na mapato ya wakulima na kuwawezesha wakulima kupata mafunzo ya teknolojia za kisasa. Kilimo cha umwagiliaji kimeonekana kuwa na mchango mkubwa na katika kufikia azma hiyo. Sekta ya Umwagiliaji imepewa kipaumbele katika Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo. Sekta hiyo itachangia mabadiliko katika uzalishaji wa mazao ya kilimo na kuchangia kwa kiasi kikubwa kuongeza uhakika wa chakula na kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, maendeleo ya kilimo cha umwagiliaji yanatekelezwa kwa kiwango kikubwa katika ngazi ya Wilaya kupitia, Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya (*District Agricultural Development Plans – DADPs*), ambapo asilimia 75 ya mahitaji yote ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo ni kwa ajili ya kutekeleza kilimo cha umwagiliaji wilayani.

Katika Programu hiyo, pamoja na kutenga fedha kwa ajili ya Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya, zipo fedha za nyongeza ambazo miradi inayoanzishwa chini ya *DADPs* inaweza kupatiwa ili kuziba pengo la fedha kutoka Halmashauri kwa lengo la kukamilisha utekelezaji. Fedha hizo zinatoka kwenye Mfuko wa Kuendeleza Umwagiliaji katika ngazi ya Wilaya *(District Irrigation Development Fund – DIDF).* Fedha hizo hutolewa kama nyongeza kwa miradi iliyo chini ya *DADPs,* ambayo, mara nyingi, hupatiwa kiwango kidogo cha fedha za utekelezaji kutokana na ufinyu wa bajeti. Vilevile, upo Mfuko wa Kuendeleza Umwagiliaji Ngazi ya Taifa *(National Irrigation Development Fund – NIDF)* ambao unatumika kugharamia uendelezaji wa miundombinu ya umwagiliaji yenye gharama kubwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaalam unahitajika katika kutayarisha miradi ya umwagiliaji ili iwekwe kwenye Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya. Ofisi za Kanda za Umwagiliaji zinatoa utaalam huo kwa Halmashauri katika utayarishaji wa miradi, ikiwa ni pamoja na miongozo ya jinsi ya kuibua miradi hiyo. Kwa utaratibu huo, Sekta ya Umwagiliaji imeweza kuhamasisha na kuwapa uwezo wadau hao kuandaa na kutekeleza miradi ya umwagiliaji ambayo ni muhimu kwa kuzingatia hali ya mabadiliko ya upatikanaji wa mvua ambazo siyo za uhakika. Miundombinu ya umwagiliaji iliyoboreshwa imewezesha kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao kwa kiwango kikubwa na hivyo kuchangia katika kupunguza umaskini. Kuboreshwa kwa miundombinu ya umwagiliaji kumeongeza ufanisi katika matumizi ya maji na kuimarisha matumizi endelevu ya rasilimali na hifadhi ya mazingira katika skimu za umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hali hiyo, Sekta ya Umwagiliaji chini ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo, ina changamoto ya kuongeza uzalishaji wa mazao na matumizi ya teknolojia mbalimbali za umwagiliaji kwenye maeneo yenye

uhaba wa mvua. Sekta ya Umwagiliaji imepanga kujenga miundombinu ya umwagiliaji kwenye mikoa yenye uhakika wa maji ambayo ni Morogoro, Mbeya, Iringa, Rukwa na Ruvuma. Lengo la utekelezaji huo ni kuchangia katika kuifanya mikoa hiyo kuendelea kuwa wazalishaji wakubwa wa mazao ya chakula nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa maendeleo ya Sekta ya Umwagiliaji katika mwaka 2007/2008 ulilenga katika maeneo yafuatayo:-

(i) Upembuzi yakinifu na usanifu wa skimu za umwagiliaji;

(ii) Uendelezaji wa miundombinu ya umwagiliaji;

(iii) Ukamilishaji wa uendelezaji wa skimu za umwagiliaji kwa njia ya kuvuna maji ambazo zilianza kutekelezwa kabla ya *ASDP*;

(iv) Kutoa mchango wa kitaalam katika kuanzisha na kusimamia utekelezaji wa miradi ya kuendeleza umwagiliaji chini ya *DADPs;*

(v) Kuhamasisha na kuendeleza matumizi ya teknolojia za umwagiliaji zenye ufanisi wa juu katika matumizi ya maji;

(vi) Maandalizi ya Sera ya Taifa ya Umwagiliaji;

(vii) Mafunzo kwa watumishi na wakulima katika maeneo mbalimbali yanayohusu uendelezaji wa Sekta ya Umwagiliaji; na

(viii) Kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Wizara katika kuendeleza umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utekelezaji wa malengo ya Sekta ya Umwagiliaji, changamoto zilizopo ni pamoja na:-

(i) Miundombinu duni ya umwagiliaji;

(ii) Uhaba wa wataalam na vitendea kazi, hasa katika ngazi ya Halmashauri za Wilaya;

(iii) Udhaifu wa vyama vya umwagiliaji katika kusimamia utunzaji na uendeshaji wa miundombinu ya umwagiliaji; na

(iv) Uwekezaji mdogo katika Sekta ya Umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo ya kipaumbele katika kuendeleza umwagiliaji kwa mwaka 2008/2009 ni pamoja na:-

(i) Kukarabati skimu za umwagiliaji za wakulima wadogo na kuweka mazingira ya kuvutia uwekezaji katika kilimo cha umwagiliaji cha kibiashara kwa mashamba ya kati na makubwa;

(ii) Kuboresha miundombinu, hasa ile ambayo imeharibiwa na mafuriko;

(iii) Kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa maeneo yanayofaa kwa umwagiliaji;

(iv) Kutumia uzoefu wa kuendeleza miundombinu ya umwagiliaji kwa njia ya kuvuna maji ambao umepatikana katika maeneo mbalimbali na kuleta mafanikio, kama vile miradi ya kuvuna maji ya: Mradi Shirikishi wa Wakulima wa Mara (*Mara Farmers Initiative Project-MARAFIP)* na Programu Shirikishi ya Kuendeleza Umwagiliaji (*Participatory Irrigation Development Programme -PIDP);*

(v) Kuhakikisha matumizi ya teknolojia mbalimbali za umwagiliaji zenye tija na ufanisi katika matumizi ya maji;

(vi) Kujenga mabwawa ya kuhifadhi maji kwa matumizi ya umwagiliaji, mifugo na binadamu;

(vii) Kuhamasisha matumizi ya maji ardhini kwa umwagiliaji na matumizi mengine;

(viii) Kuangalia maeneo ya utafiti wa matumizi bora ya maji bila kusahau hifadhi ya mazingira;

(ix) Maandalizi ya Mkakati wa Umwagiliaji pamoja na Sheria ya Umwagiliaji;

(x) Mafunzo kwa watumishi na wakulima katika maeneo mbalimbali yanayohusu uendelezaji, uendeshaji na utunzaji wa miundombinu ya umwagiliaji; na

(xi) Kusimamia kwa ujumla utekelezaji wa majukumu ya Wizara katika kuendeleza umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/2008, Wizara yangu ilipanga kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa skimu za umwagiliaji zenye jumla ya eneo la hekta 125,579. Kati ya eneo hilo, skimu 116**,** zenye eneo la hekta 85,179, sawa na asilimia 68 ya eneo lililopangwa, zilitekelezwa.

Utekelezaji huu ulifanyika katika Kanda zote saba za Umwagiliaji ambapo idadi ya skimu ni kama ifuatavyo:- Tabora 13, Mwanza 10, Manyara 30, Mbeya 19, Morogoro 38, Kilimanjaro tatu na Mtwara tatu**.** Usanifu huo ulihusisha mabwawa 10 ambayo ujenzi wake utaanza mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu itaendelea kutayarisha na kuendeleza skimu za umwagiliaji kwa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu ili ziweze kutafutiwa fedha za utekelezaji. Skimu za umwagiliaji 68 zenye ukubwa wa eneo la hekta 200,000 zitatekelezwa (Jedwali Na. 9 na 10).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo, Wizara yangu ilipanga kuendeleza skimu za umwagiliaji zenye jumla ya eneo la hekta 20,515 kwa kujenga miundombinu ya umwagiliaji. Jumla ya hekta 15,300 zimeendelezwa kwa kujengewa miundombinu. Hii ni sawa na asilimia 74.6 ya lengo lililokusudiwa (Jedwali Na. 11). Ujenzi wa mabwawa ya Mangisa (Mbulu) na Iyuhwa (Mpwapwa) na ukarabati wa mabwawa ya Ikoa (Dodoma) na Isikizya (Uyui) umekamilika. Vilevile, ujenzi wa mabwawa ya Ulyanyama (Sikonge) na Kisangwa (Bunda) umeanza na utaendelea katika mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu itakarabati na kuendeleza jumla ya skimu za umwagiliaji 25 zenye eneo la hekta 16,406. Eneo hilo litajumuisha skimu za umwagiliaji zilizoibuliwa na wananchi na kupewa fedha kupitia Mipango ya Wilaya ya Maendeleo ya Kilimo na zile zilizopewa fedha kutoka Mpango wa Pamoja wa Msaada wa Chakula kati ya Tanzania na Japan (*Tanzania/Japan Food Aid Counterpart Fund - FACF*) kama ilivyoainishwa kwenye (Jedwali Na. 12). Mabwawa 10 yenye maji ya kutosha kumwagilia hekta 3,650 yatajengwa na baadhi kukarabatiwa katika kanda 4 za Umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika,  katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu itaendelea kushirikiana na Halmashauri za Wilaya katika kuendeleza teknolojia zinazotumia maji kwa ufanisi zaidi katika maeneo yaliyo pembezoni mwa Ziwa Victoria na Ziwa Nyasa. Utekelezaji huo utaenda sambamba na uhamasishaji katika kutumia pampu zinazoendeshwa kwa miguu, upepo, mionzi ya jua na mafuta ya dizeli kwa ajili ya kusukuma maji ya umwagiliaji na matumizi mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/2008, Wizara yangu kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la Maendeleo ya Kilimo (*International Fund for Agricultural Development – IFAD*), Serikali ya Ireland na Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (*World Food Program - WFP*), ilikamilisha utekelezaji wa Programu Shirikishi ya Kuendeleza Umwagiliaji *(Participatory Irrigation Development Programme - PIDP*).

Programu hiyo ambayo ilianza 2000/2001 inatekelezwa katika Mikoa yenye ukame zaidi ambayo ni Dodoma, Singida, Manyara, Mwanza, Tabora na Shinyanga. Katika kipindi cha utekelezaji, maeneo yenye jumla ya hekta 15,307, yaliyohusisha skimu 46 yaliendelezwa. Idadi ya skimu zilizoendelezwa katika wilaya ni Babati tatu, Dodoma saba, Igunga tatu, Iramba mbili, Kwimba nne, Manyoni sita, Maswa moja, Mbulu nne, Mpwapwa moja, Misungwi tatu, Nzega sita na Shinyanga sita. Katika kukamilisha awamu ya mwisho ya Programu hiyo, kwa mwaka 2007/2008, eneo la hekta 1,346 liliendelezwa, lililohusisha skimu sita katika wilaya za Igunga moja, Kwimba moja**,** Mbulu moja, Misungwi mbili na Mpwapwa moja**.**

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu itaendelea kuhamasisha matumizi ya teknolojia mbalimbali za umwagiliaji, ikiwa ni pamoja na kuvuna maji ya mvua.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/2008, Wizara yangu iliendelea kusimamia utekelezaji wa miradi ya umwagiliaji iliyoibuliwa na wakulima na kupitia taratibu ambazo ziliwezesha Halmashauri za Wilaya kuandaa Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya inayojumuisha umwagiliaji. Wataalam wa Kanda za Umwagiliaji wameendelea kutoa ushauri wa kitaalam katika usimamizi wa utekelezaji wa miradi kwa watendaji wa wilaya, ikiwa ni pamoja na utayarishaji wa miradi itakayoingizwa kwenye *DADPs.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ushauri wa kitaalam uliotolewa na Kanda za Umwagiliaji kwa Halmashauri, skimu za umwagiliaji 91 zilifuzu kupata fedha kupitia *DADPs.* Kati ya hizo, skimu 44 zilipata fedha za nyongeza kutoka katika Mfuko wa Kuendeleza Umwagiliaji ngazi ya Wilaya (*DIDF*).

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2008/2009, kwa kutumia wataalam waliopo katika Kanda za Umwagiliaji, Wizara yangu itaendelea kutoa utaalam kwa Halmashauri katika kuandaa na kusimamia utekelezaji wa miradi ya umwagiliaji chini ya *DADPs*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/2008, Wizara yangu iliendelea na uhamasishaji na uendelezaji wa matumizi ya teknolojia ya umwagiliaji kwa njia ya matone (*drip irrigation*). Teknolojia hiyo ina ufanisi mkubwa katika matumizi ya maji.

Utekelezaji ulifanyika kupitia Mradi wa Kuendeleza Wakulima wadogo unaofadhiliwa kwa pamoja kati ya Serikali, Shirika la Chakula Duniani na Serikali ya Japan. Utekelezaji ulifanyika kwa kuwafundisha wakulima namna ya kuvifunga vifaa vya umwagiliaji na kuwagawia vifaa hivyo ambavyo ni pamoja na seti za vifaa vya umwagiliaji wa matone 310, pampu za miguu 220 na pampu za kutumia mafuta 200. Vifaa hivyo vimegawiwa katika wilaya 22 katika Mikoa ya Kanda ya Ziwa. Mikoa hiyo na idadi ya wilaya zake ni: Kagera sita, Mara nne, Shinyanga saba na Mwanza tano**.**

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, maeneo yatakayoendelezwa kwa matumizi ya vifaa hivyo kwa kila mkoa katika ukanda wa Ziwa ni: Kagera hekta 300, Mara hekta 250, Shinyanga hekta 320 na Mwanza hekta 280. Matumizi ya teknolojia hizo pamoja na utumiaji wa maji chini ya ardhi utaenezwa katika maeneo mbalimbali kwa kuzingatia uibuaji wa miradi ya wakulima wenyewe chini ya uongozi wa wataalam.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu katika mwaka 2007/2008, iliendelea na utayarishaji wa Rasimu ya Sera ya Taifa ya Umwagiliaji. Kazi hii itaendelea kukamilishwa katika mwaka 2008/2009. Wizara pia, itaanza kuandaa mkakati wa umwagiliaji na rasimu ya sheria ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na utekelezaji katika maeneo hayo muhimu, katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu itaandaa mafunzo kwa wakulima 300 katika fani

za matumizi bora ya rasilimali ya maji, uendeshaji na utunzaji wa miundombinu ya umwagiliaji. Wataalam 50 katika ngazi mbalimbali watapewa mafunzo katika fani za matumizi bora ya rasilimali ya maji, upembuzi yakinifu na usanifu wa skimu za umwagiliaji. Fani nyingine ni usimamizi wa ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji, utafiti kuhusu teknolojia na masuala mbalimbali ya umwagiliaji. Wizara yangu itaimarisha usimamizi wa utekelezaji wa shughuli zote za umwagiliaji kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na uhaba wa wataalam wa fani ya umwagiliaji katika ngazi ya Halmashauri, Wizara yangu, kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika, itasaidia kujenga uwezo wa Chuo cha Umwagiliaji cha Igurusi katika Wilaya ya Mbarali ili kiweze kutoa mafundi sanifu wa kutosha na wenye sifa zinazostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera ya Maji ilipitishwa mwaka 2002. Mkakati wa Maendeleo ya Sekta ya Maji ulipitishwa rasmi mwezi Machi 2008. Sheria zilizopo, ambazo ni za zamani, hazikidhi mahitaji ya sasa kuhusu usimamizi na uendelezaji wa Sekta ya Maji. Wizara, kwa kushirikiana na wadau wengine, imeandaa rasimu ya sheria ya usimamizi na udhibiti wa rasilimali za maji na sheria ya huduma za maji na usafi wa mazingira. Ni nia ya Serikali kukamilisha matayarisho kwa sheria hizo ili zianze kutumika mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu ina wajibu wa kulinda vyanzo vya maji dhidi ya uchafuzi na kuhakikisha maji yanabakia na ubora wake ili kukidhi mahitaji mbalimbali. Katika mwaka 2007/2008, Wizara yangu, kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira, iliendelea kutekeleza Mkakati wa Kuhifadhi Mazingira ya Ardhi na Vyanzo vya Maji. Kazi zilizotekelezwa ni kutambua vyanzo vya maji 10,423, ambapo, kati ya hivyo, vyanzo 175 vimewekewa mipaka. Katika kuhakikisha utupaji wa majitaka katika mazingara unazingatia viwango vya ubora, Wizara yangu ilikagua miundombinu ya majitaka katika viwanda 20**,** miundombinu ya majitaka ya manispaa za Dodoma, Arusha na Morogoro na katika Jiji la Dar es Salaam, na miundombinu ya majitaka ya hoteli 11 za kitalii katika mbuga za wanyama za Tarangire, Manyara na Ngorongoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2008/2009, Wizara yangu, kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais na Halmashauri za Wilaya, itaendelea kubaini vyanzo vya maji na kuviwekea mipaka na kudhibiti matumizi holela ya maji katika kilimo cha umwagiliaji. Wizara itaendelea kuboresha mifereji ya kilimo cha umwagiliaji ili kutunza mazingira. Vilevile Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira, itaanza kutekeleza Mkakati wa Hatua za Haraka za Kuhifadhi Mazingira ya Bahari, Ukanda wa Pwani, Maziwa, Mito na Mabwawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu, kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji na Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo ilifanya tathmini ya awali ya athari ya mazingira katika miradi 139 ya maji. Kati ya miradi hiyo mradi mmoja ulibainika kuhitaji tathmini ya kina. Mwaka 2008/2009, Wizara yangu, kwa kushirikiana

na Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira, itawajengea uwezo wataalam na waratibu wa mazingira wa Sekta ya Maji na Sekta ya Umwagiliaji. Wizara itaendelea kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira na Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira *(NEMC)*, katika masuala ya ubora wa maji. Wizara itashirikiana pia na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii katika maandalizi ya sera ya usafi wa mazingira. Wizara itaimarisha kitengo cha usimamizi wa mazingira katika Sekta ya Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu iliendelea kuimarisha utaratibu wa kupashana habari, kutoa elimu na kuboresha mawasiliano baina ya Wizara, wadau wa Sekta za Maji na Umwagiliaji na wananchi. Katika mwaka 2007/2008, kazi zifuatazo zilitekelezwa:-

(i) Kuandaa taarifa za kiutendaji na kisera kuhusu Sekta za Maji na Umwagiliaji kwa ajili ya kuelimisha umma kwa kupitia vipeperushi, tovuti, radio, magazeti na televisheni;

(ii) Kuteua Afisa ambaye ni msemaji kwa niaba ya Wizara ambaye anahusika na utoaji wa taarifa za kiutendaji na kisera kwa vyombo vya habari na kuelimisha umma katika masuala hayo; na

(iii) Kushiriki katika maandalizi ya mbio za Mwenge wa Uhuru ambapo moja kati ya kaulimbiu za mwaka 2008 ni Tutunze mazingira ya vyanzo vya maji na tutumie maji tuliyonayo vizuri kwa maendeleo yetu na uhai wa vizazi vijavyo**.** Kaulimbiu hiyo itahamasisha wananchi kutunza vyanzo vya maji katika maeneo yao na kushiriki katika utekelezaji wa *WSDP*.

Katika mwaka 2008/2009, chini ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji, Wizara itaendelea kuimarisha kitengo hicho kwa kukiongezea rasilimali watu na vifaa ili kiweze kutekeleza kazi zake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu imedhamiria kuboresha mfumo wake wa utendaji na utoaji wa huduma kwa kutumia teknolojia ya habari na mawasiliano (*Information and Communication Technology)*. Kwa mwaka 2007/2008, Wizara ilikamilisha taratibu za kumpata mtaalam mwelekezi wa kuandaa Mkakati wa Matumizi ya Teknolojia ya Mfumo wa Taarifa za Kimenejimenti (*Management Information System Strategy*) ili kuongeza matumizi endelevu ya teknolojia hiyo. Wizara iliendelea kuboresha mfumo wa mawasiliano ya ndani na nje kwa kupitia mtandao wa kompyuta, intaneti, simu, na tovuti ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, kazi zifuatazo zitatekelezwa:-

(i) Kuandaa Mpango Mkakati wa Mfumo wa Taarifa za Kimenejimenti,

(ii) Kuanzisha mfumo wa kisekta wa taarifa za kimenejimenti na benki ya takwimu ili kuwezesha upatikanaji na utoaji wa taarifa na takwimu mbalimbali zilizo sahihi kuhusu rasilimali za maji na utoaji wa huduma za maji na umwagiliaji;

(iii) Kuunganisha mfumo huo na benki za takwimu za Ofisi za Mabonde, Halmashauri, Ofisi za Mikoa, Mamlaka za Maji na Kanda za Umwagiliaji;

(iv) Kutoa mafunzo ya teknolojia ya habari na mawasiliano kwa watumishi wa Sekta za Maji na Umwagiliaji katika ngazi zote; na

(v) Kuanza utekelezaji wa Serikali Mtandao (*e-Government*) kupitia Mpango wa Uboreshaji wa Utumishi wa Umma, Awamu ya Pili (*Public Service Reform Program Phase II*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu inatambua umuhimu wa masuala ya jinsia katika kutekeleza malengo ya MKUKUTA na Sera ya Maji ya mwaka 2002. Katika mwaka 2007/2008, Wizara yangu iliendelea kutoa mafunzo ya masuala ya kijinsia kwa wataalam na wadau wa Sekta za Maji na Umwagiliaji. Lengo likiwa ni kuwajengea uwezo wa kuelewa, kubaini na kuainisha masuala ya kijinsia katika kutekeleza mipango ya maendeleo na uendeshaji. Jumla ya Watumishi 98 walipatiwa mafunzo ya muda mfupi kuhusu masuala ya jinsia kwa lengo la kuwawezesha wataalam na watendaji kuzingatia mahusiano ya kijamii na matokeo yake katika sera, mikakati na uendeshaji wa kisekta.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanawake ndio wahusika wakuu katika Sekta ya Maji, ikiwa ni pamoja na utunzaji wa vyanzo vya maji na mazingira yake. Hata hivyo, ushiriki wao katika kupanga na kusimamia sera na mipango ya sekta hauna uwiano unaotakiwa. Idadi ya wajumbe wanawake, hasa kwenye Bodi za Maji za Miji midogo ya Wilaya na vyombo vya watumiaji maji, ni chini ya asilimia 30**.** Katika mwaka 2007/2008, kulikuwa na ongezeko la ushiriki wa wanawake katika maamuzi kwenye mamlaka za Maji za Miji Mikuu ya Mikoa kutoka asilimia 19 ya kipindi cha 2004-2007 hadi kufikia asilimia 34 kwa kipindi cha 2007-2010 sawa na ongezeko la asilimia 15**.** Ili kukabiliana na changamoto hiyo, Wizara imewawezesha wanawake wataalam wa Sekta za Maji na Umwagiliaji kujiendeleza kitaaluma, kuunda chombo chao na kuwapa uzoefu ili washike nafasi muhimu za uongozi katika Sekta.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu itaendelea kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Mkakati wa Kuendeleza Sekta za Maji na Umwagiliaji ikiwa ni utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia ya mwaka 2000. Lengo ni kuhakikisha kuwa sera, mifumo ya uendeshaji na usimamizi wa sekta hizi unazingatia dhana ya usawa wa jinsia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/2008, Wizara yangu iliendelea na utekelezaji wa awamu ya pili ya Mkakati wa Kitaifa wa Kupambana na Rushwa. Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Kitengo cha Utawala Bora pamoja na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa iliendelea kuwaelimisha watumishi umuhimu wa kushiriki katika mapambano dhidi ya rushwa kupitia makala, vipeperushi na miongozo mbalimbali. Watumishi 200 wamepatiwa mafunzo kuhusu rushwa na utawala bora kupitia utaratibu huo. Kamati ya Ukaguzi ya Wizara na Bodi ya Usimamizi wa Manunuzi zimeimarishwa ili kuboresha utoaji wa huduma. Mpango wa utekelezaji wa kusimamia masuala ya Rushwa na Maadili umekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu itaendelea kuimarisha mapambano dhidi ya rushwa katika Sekta za Maji na Umwagiliaji. Watumishi 400 kutoka katika idara, taasisi na asasi mbalimbali watapatiwa mafunzo kuhusu utawala bora. Wizara itaandaa mifumo ya ufuatiliaji ili kuziba mianya ya Rushwa, kuhamasisha watumishi na wadau kushiriki katika mapambano dhidi ya Rushwa, na kujenga utamaduni wa uadilifu na uwajibikaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mapambano dhidi ya *UKIMWI* limeendelea kupewa kipaumbele na limekuwa ni moja ya ajenda muhimu katika mipango ya sekta. Katika mwaka 2007/2008, Wizara yangu na taasisi zake iliendelea na utekelezaji wa mkakati wa mapambano dhidi ya *UKIMWI***.** Jumla ya Watumishi 550 walipatiwa mafunzo ya namna ya kujikinga na maambukizi na kuhamasishwa kupima afya zao kwa hiari. Hadi Juni 2008, watumishi watatu walioathirika walijitokeza na walianza kupatiwa huduma, kwa kuzingatia Waraka wa Utumishi wa Umma Na. 2 wa mwaka 2006.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka 2008/2009 Wizara yangu itaendelea kusimamia na kuratibu utekelezaji wa maeneo muhimu yaliyoainishwa katika Mkakati wa Maendeleo ya Sekta ya Maji na Mkakati wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo. Masuala muhimu ya utekelezaji ni pamoja na kuendesha kampeni za kuhamasisha watumishi kujiepusha na maambukizi ya UKIMWI pamoja na kushawishi upimaji wa hiari na kujitokeza kupata huduma kwa watakaogunduliwa wameambukizwa Virusi vya UKIMWI. Wizara inatarajia kuendesha uchambuzi wa hali ya UKIMWI ili kupata takwimu za awali (*Baseline data*) katika kupanga mipango na ufuatiliaji wa hali ya UKIMWI katika Sekta za Maji na Umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu ina jumla ya watumishi 1,947. Watumishi 1,765 ni wa Sekta ya Maji na Watumishi 259 ni wa Sekta ya Umwagiliaji. Mwaka 2007/2008, Wizara yangu iliajiri watumishi 52 na kuridhia Mikataba ya Ajira kwa mwaka mmoja na wahandisi ambao mamlaka zao za ajira hazikuweza kukamilisha taratibu za kuwapatia ajira za kudumu, ikiwa ni pamoja na kupata ikama za wataalam hao. Mikataba ya Wahandisi imeridhiwa kwa lengo la kuzijengea uwezo Halmashauri na Sekretarieti za Mikoa katika kutekeleza Programu ya Maendeleo ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka 2008/2009 Wizara yangu itaendelea kuboresha mazingira ya kazi kwa watumishi na wataalam wa Sekta ya Maji na Sekta ya Umwagiliaji kwa lengo la kuongeza ufanisi, ikiwa ni pamoja na kuboresha miundombinu na mifumo ya uendeshaji na usimamizi wa mipango ya kisekta. Wizara yangu inatarajia kuajiri jumla ya watumishi 75 wa kada mbalimbali na kuwapandisha vyeo watumishi 840 wenye sifa kwa kuzingatia Sera ya Menejimenti na Ajira, Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003 na marekekebisho yake ya mwaka 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu, kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Washirika wetu wa maendeleo, kupitia awamu ya pili ya Programu ya Kuboresha Utumishi wa Umma, itatekeleza yafuatayo:-

(i) Kupitia Mkataba wa Huduma kwa Mteja ili kubaini matatizo yaliyoathiri utekelezaji na kuweka viwango vinavyotekelezeka ikiwa ni pamoja na kujumuisha Sekta ya Umwagiliaji;

(ii) Kutekeleza Mfumo wa Usimamizi wa Utendaji kazi kwa Matokeo *(OPRAS);* na

(iii) Kuboresha mifumo ya uwekaji kumbukumbu za usimamizi na uendeshaji wa majukumu ya Wizara; na

(iv) Kuongeza matumizi ya teknolojia ya habari katika ukusanyaji, uhifadhi na utunzaji kumbukumbu za Watumishi na Masijala.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda sasa kuchukua fursa hii kuwashukuru wale wote waliochangia kwa namna moja au nyingine katika kuiwezesha Wizara yangu kufanikisha majukumu yake. Nakiri kuwa mafanikio yaliyopatikana katika mwaka 2007/2008 ni jitihada za pamoja, ushirikiano na misaada ya kifedha na kitaalam kutoka kwa Washirika wa Maendeleo, ikiwa ni pamoja na nchi wahisani, mashirika ya misaada, taasisi zisizo za kiserikali, mashirika ya kidini na taasisi za kifedha.

Napenda kuzishukuru Serikali za Ujerumani, Japani, Ufaransa, Jamhuri ya Watu wa China, Uholanzi, Denmark, Uswisi, Ireland, Ubelgiji, Uingereza, Korea ya Kusini, Sweden, Norway, Indonesia na Marekani. Vilevile, napenda kutoa shukrani kwa taasisi za fedha za kimataifa za Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika na Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Afrika, Benki ya Uwekezaji ya Umoja wa Ulaya, Umoja wa Nchi zinazouza Mafuta Duniani, Benki ya Maendeleo ya Ujerumani *(KfW)***,** Shirila la Maendeleo la Kiufundi la Ujerumani *(GTZ),* Umoja wa Ulaya, Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa *(UNDP)*, Shirika la Makazi Duniani *(UN Habitat)*, Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto *(UNICEF)*, Shirika la Chakula la Umoja wa Mataifa *(FAO)*, Shirika la Maendeleo la Kilimo *(IFAD),* Shirika la Mpango wa Chakula Duniani *(WFP)* na Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki *(IAEA)*, kwa misaada na michango yao ya utaalam katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu na malengo ya Wizara yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nayashukuru pia, Mashirika ya kidini ya *World Islamic League*, Shirika la *Al Munadhanat Al Dawa Al Islamia*, Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania, Kanisa la Kilutheri la Ujerumani na Kanisa Katoliki Tanzania, pamoja na Taasisi za *WaterAid*, Shirika la Kimataifa la Kuhifadhi Uasili *(IUCN), World Wide Fund for Nature (WWF*) na wale wote ambao kwa njia moja au nyingine wameendelea kuzisaidia Sekta za Maji na Umwagiliaji katika kutekeleza majukumu tuliyopewa. Naomba, kwa dhati kabisa, kupitia kwako Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuwashukuru wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba, pia, nitumie fursa hii kutoa shukurani za pekee kwa wananchi wote na wadau wengine ambao sikuweza kuwataja mmoja mmoja kwa kushirikiana na Wizara yangu katika kutekeleza Sera ya Maji na Sera ya Kilimo. Pia, shukurani za pekee ziwaendee Waheshimiwa Wabunge wote kutokana na michango yao

wanayotoa ndani na nje ya Bunge hili inayolenga kuboresha Sekta za Maji na Umwagiliaji nchini. Wizara yangu itaendelea kushirikiana nao kwa lengo la kuboresha hali ya maisha ya wananchi na uchumi wa Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa mnyimi wa fadhila nisipotoa shukrani za dhati kwa wananchi wa Jimbo la Rungwe Mashariki kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa na kunivumilia pale ninaposhindwa kuwa nao kutokana na majukumu mengine ya Kitaifa yanayonikabili. Imani yao kwangu ni kubwa. Nami nitaendelea kuwatumikia kwa juhudi na bidii kwa kadri Mwenyezi Mungu atakavyonijalia. Vilevile, niwashukuru kwa niaba ya Naibu Waziri Wangu, Mheshimiwa Christopher Kajoro Chiza kwa wananchi wa Jimbo la Buyungu kwa ushirikiano wanaompatia katika kutekeleza majukumu ya jimbo lake na yale ya Kitaifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, lakini siyo kwa umuhimu**,** naomba kutoa shukurani zangu za dhati kwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji**,** Mheshimiwa Christopher Kajoro Chiza, Mbunge wa Jimbo la Buyungu kwa msaada na ushirikiano wake.

Aidha, napenda pia, nitoe shukrani zangu kwa Katibu Mkuu wa Wizara yangu, Bwana Patrick Rutabanzibwa, Naibu Katibu Mkuu, Bwana Christopher Sayi, Wakuu wa Idara, Viongozi wa Mashirika na Taasisi chini ya Wizara yangu pamoja na wataalam na watumishi wote kwa kujituma katika kusimamia utekelezaji wa majukumu tuliyopewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili Wizara yangu iweze kutekeleza majukumu na malengo yaliyoelezwa katika hotuba hii, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako tukufu liidhinishe jumla ya Sh.156,243,079,700/= kwa ajili ya matumizi ya Wizara yangu kwa mwaka 2008/2009. Kati ya fedha hizo, Matumizi ya Kawaida ni Sh. 16,288,212,000/= ambapo Sh. 6,722,686,000/= ni Mishahara ya Watumishi (*PE*) na Sh. 9,565,526,000/= ni fedha za Matumizi Mengine (*OC*). Bajeti ya Maendeleo ni Sh. 139,954,867,700/=, ambapo kati ya hizo Shilingi 46,463,379,000 ni fedha za ndani na Sh.93,491,488,700/= ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tena nitoe shukrani zangu za dhati kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Hotuba hii pia, inapatikana katika Tovuti ya Wizara yangu kwa anwani: *www.maji.go.tz*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maji ni Uhai. Naomba kutoa Hoja. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono, sasa nitamwita msemaji wa Kamati iliyohusika na Wizara hii, Mheshimiwa Hilda Ngoye.

**MHE. HILDA NGOYE K.N. Y. MHE. GIDEON A. CHEYO-MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO NA ARDHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa kanuni ya 99 (7) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu

utekelezaji wa Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008 na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji ilikutana Dar es salaam tarehe 2 Juni, 2008. Katika Kikao hicho Kamati ilipata maelezo ya kina kutoka kwa Wizara kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2008/2009 ambayo yamezingatia Dira ya Taifa ya 2025, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005, Mpango wa Kukuza na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA), Mwelekeo na Majukumu ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji na Utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati kwa Wizara Kwa Mwaka 2007/2008 katika mwaka wa fedha wa 2007/2008, Kamati ilitoa maoni na ushauri katika maeneo mbalimbali yanayohusu Sekta ya Maji na Umwagiliaji. Nafurahi kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa kiasi kikubwa imeyafanyia kazi maeneo mengi. Hata hivyo, utekelezaji wa baadhi ya maeneo bado unaendelea. Katika maeneo ambayo juhudi zaidi zinahitajika, Kamati imeshauri na kutoa maelekezo ipasavyo. Baadhi ya maeneo hayo ni kama ifuatavyo:-

(i) Kuhusu Mradi wa Maji kutoka Ziwa Victoria kwenda miji ya Kahama na Shinyanga, Wizara imeendelea kulipa deni la Mkandarasi kiasi cha Shilingi bilioni 36.7 kati ya bilioni 51.9 ilizokuwa inadaiwa kwa mwaka 2007/2008. Jitihada za Wizara kwa hivi sasa ni kukamilisha mradi huo kama ulivyosanifiwa. Hii ni pamoja na kuvipatia huduma ya maji vijiji 54 karibu na linakopita bomba kuu kuelekea miji ya Kahama na Shinyanga. Maombi ya kuviingiza vijiji vingine kwenye mradi huo vilivyopo nje ya kilomita tano yatajumuishwa kwenye Halmashauri za Wilaya husika.

(ii) Wizara, kupitia *DAWASA*, inaendelea kutekeleza Mradi wa uboreshaji wa miundombinu ya Majisafi na Majitaka katika Jiji la Dar es Salaam *(DWSSP).* Mpaka sasa pampu nane mpya zimefungwa katika vituo vya Ruvu Juu na Ruvu Chini kwa lengo la kuboresha huduma za Maji katika Wilaya za Kinondoni na Ilala. Aidha, imebainika kuwa kuna maji mengi chini ya ardhi katika maeneo ya Kigamboni. Visima virefu vitatu vimechimbwa maeneo ya Kimbiji Mpera na Mpiji ili kusambaza maji katika Wilaya ya Temeke. Vilevile Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Marekani *(Millenium Challenge Corporation)* itagharamia upanuzi wa chanzo cha Ruvu chini na kuweka mitambo ya kusukuma maji.

(iii) Mafunzo ya namna ya kutathmini maji kwa ajili ya mazingira kwa Maafisa wa Mabonde yalifanyika. Aidha, chini ya *WSDP*, Wizara hatua kwa hatua itaboresha Ofisi hizo za Mabonde, kwa kuzipatia Ofisi hizo nyenzo za kufanyia kazi pamoja na wataalamu.

(iv) Wizara, kwa kushirikiana na Serikali za Mitaa na Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira, imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kudhibiti utupaji ovyo wa majitaka kutoka viwandani na kwenye makazi ya watu mijini. Hatua hizo ni pamoja na: kupanua miundombinu ya uondoaji majitaka ili kukidhi ongezeko la mahitaji ya huduma

hiyo. Chini ya mradi wa *Dar es Salaam Water Supply and Sewerage Project,* (*DWSSP*) ukarabati wa mabomba makuu ya majitaka jijini Dar es salaam na bomba kuu la kumwaga majitaka baharini umekamilika.

(v) Kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, Wizara ya Fedha na Uchumi na Washirika wa Maendeleo, Wizara imeanza maandalizi ya Programu ndogo ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini utakaohusisha vijiji kumi kila Wilaya kuanzia 2007/2008. Utekelezaji wa programu unahusu Halmashauri zote za Wilaya, Miji na Manispaa.

(vi) Katika kukabiliana na tatizo la maji katika maeneo kame nchini, Wizara imeendelea kutoa ushauri wa kitaalamu, miongozo na kutafuta fedha kutoka vyanzo mbalimbali ili kuziwezesha Halmashauri kutekeleza mipango ya maji. Halmashauri ndizo zenye jukumu la kujenga na kuendesha miradi ya maji ikiwa ni pamoja na ujenzi wa mabwawa.

(vii) Kupitia Programu ndogo ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini Wizara imeendelea kuhamasisha Taasisi mbalimbali kuvuna maji ya mvua. Miundombinu ya kuvuna maji hayo itajengwa kwenye taasisi za umma ikiwa ni pamoja na shule za msingi, masoko na vituo vya afya kwa mwaka wa fedha 2008/2009. Aidha, Wizara itaimarisha Wakala ya Uchimbaji wa Visima kwa kuongeza vifaa vya kuchimbia visima na ujenzi wa mabwawa kupitia Programu ya Mendeleo ya Sekta ya Maji.

(viii) Kutokana na Upungufu wa Wataalam wa maji nchini, hususan katika Halmashauri za Wilaya, Wizara inaendelea kukiboresha Chuo cha Maji cha Rwegarulila. Itakiongezea uwezo wa kufanya maamuzi na kusimamia uendeshaji wa kutoa mafunzo na ushauri wa kitaalam. Hivi karibuni Chuo kitakamilisha utaratibu wa kuwa Wakala wa Serikali.

Aidha, mkakati umeandaliwa wa kukiwezesha chuo kuhudumia wanafunzi wengi zaidi. Utafanyika pia ukarabati wa majengo, ujenzi wa majengo mapya, ununuzi wa samani na zana za kufundishia na kujifunzia. Vilevile idadi ya watumishi itaongezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Mwaka 2007/2008, Wizara ilitengewa Sh. 13,427,915,000/= kwa matumizi ya kawaida na Sh. 224,990,752,600/= kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utekelezaji wa mpango wa bajeti ya 2007/2008 Wizara ilipata mafanikio yafuatayo:-

(i) Vyanzo vya maji 175 katika mabonde tisa ya maji vilitambuliwa na kuwekewa mipaka kwa lengo la kuvihifadhi ili viwe endelevu.

(ii) Wizara iliendelea na ujenzi na ukarabati wa mabwawa 10 ya ukubwa wa kati ya Amaswata (Kiteto), Emboret (Simanjiro), Ingamuriak (Monduli), Moita (Monduli), Igunga (Urambo), Kinyambwiga (Bunda), New-sola (Maswa), Katoro

(Geita), Nyambele (Bunda), Nyashitanda (Misungwi) na kumalizia ujenzi wa Bwawa la Mugumu Wilayani Serengeti.

(iii) Usambazaji wa huduma ya maji safi na salama uliongezeka kutoka mita za ujazo milioni 99.99 mwaka 2006 hadi kufikia mita za ujazo milioni 100.2 mwaka 2007. Ongezeko hili limewezesha upatikanaji wa maji Mijini kufikia asilimia 73 na asilimia 55.7 kwa vijijini.

(iv) Kiwango cha ukusanyaji maduhuli kiliongezeka kutoka shilingi bilioni 22.56 mwaka 2006 hadi kufikia bilioni 25.39 mwaka 2007, ikiwa ni ongezeko la asilimia 15 la malengo yaliyowekwa.

(v) Matayarisho ya Rasimu ya Sera ya Taifa ya Umwagiliaji yalifikia hatua za mwisho.

(vi) Wizara iliendeleza hekta 15,300 za umwagiliaji ikiwa ni sawa na asilimia 74.5 ya lengo la hekta 20,515 zilizopangwa. Kazi zilizofanyika ni ujenzi wa mifereji na banio.

(vii) Kwa kupitia kanda za umwagiliaji, Wizara imefanya upembuzi yakinifu na usanifu wa skimu 100 katika kanda saba za umwagiliaji. Aidha, mafunzo kwa watumishi kuhusu teknolojia sahihi za kuendeleza kilimo cha umwagiliaji, usimamizi na uendeshaji wa skimu za umwagiliaji pamoja na matumizi bora ya maji yalitolewa.

(viii) Wizara, iliendelea kuhamasisha matumizi ya teknolojia za Umwagiliaji kupitia utekelezaji wa mradi wa kuendeleza wakulima wadogo, mradi huu unafadhiliwa kwa pamoja na Serikali ya Tanzania, Shirika la Chakula Duniani na Serikali ya Japan.Chini ya mpango huo vifaa mbalimbali kwa Wilaya 22 za Mikoa ya Kagera, Mara, Shinyanga na Mwanza viligawiwa.

(ix) Katika kuzijengea Halmashauri za wilaya uwezo, Wizara imewezesha kuibuliwa miradi 178 kutoka katika Halmashauri mbalimbali. Utekelezaji ulihusisha miradi iliyoendelezwa kwa fedha kutoka Serikali Kuu, Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya (*DADPs*), Mfuko wa pamoja wa Serikali za Tanzania na *Japan - Food Aid Counterpart Fund* na Mradi Shirikishi wa Kuendeleza Kilimo *(PADEP).*

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto katika utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2007/2007, pamoja na mafanikio yaliyopatikana mwaka 2007/2008, kulikuwepo na changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa Bajeti ya mwaka wa 2007/2008. Changamoto hizo ni pamoja na :-

(i) Ongezeko la uharibifu wa mazingira katika vyanzo vya maji linalotokana na kuongezeka kwa shughuli mbalimbali za kijamii na kiuchumi. Hali hii inaathiri upatikanaji wa maji kwa wingi na ubora unaotakiwa.

(ii) Ongezeko kubwa la gharama za uendeshaji wa miradi ya maji kutokana na kupanda kwa gharama za umeme na mafuta kumesababisha kupanda kwa bei ya maji na kuwa mzigo kwa wananchi. Vilevile kuongezeka gharama hizo za maji kumeathiri Kilimo cha Umwagiliaji.

(iii) Uwezo mdogo wa makandarasi binafsi katika ujenzi wa miradi ya maji na umwagiliaji hali inayoathiri ukamilishaji wa miradi kwa wakati.

(iv) Kiwango cha fedha kinachotengwa kwa ajili ya Sekta ya Umwagiliaji chini ya Programu ya Kuendeleza Sekta ya Maendeleo ya Kilimo (*ASDP*) hakitoshelezi malengo ya utekelezaji.

(v) Kutoshiriki kikamilifu kwa sekta binafsi katika kutambua, kuwekeza na kutoa huduma katika kilimo cha umwagiliaji.

(vi) Wataalamu katika ngazi ya Halmashauri za Wilaya na Miji kuwa na uwezo mdogo wa kuibua miradi na kufuata taratibu za manunuzi na masharti ya washirika wa maendeleo kwa ufanisi.

(vii) Uchelewaji wa Fedha za Washirika wa maendeleo kwa mfano Benki ya Dunia, umeathiri ukamilishwaji wa miradi mingi ya Maendeleo katika Sekta ya Maji.

(viii) Tatizo la upotevu wa maji kwenye mfumo wa usambazaji maji ni kubwa na linahitaji mkakati wa kipekee ili kukabiliana nalo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Malengo ya Bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2008/2009. Katika mwaka wa fedha 2008/2009, Wizara imelenga kutekeleza kazi mbalimbali, baadhi ni kama zifuatazo:-

(i) Kuhakikisha kwamba rasilimali za maji zinaendelezwa na kusimamiwa kwa njia endelevu kwa kuwashirikisha wadau wote.

(ii) Kukiwezesha kilimo cha umwagiliaji kilicho shirikishi kwa kuongeza uzalishaji endelevu na tija ili kuhakikisha usalama wa chakula, uhakika wa kupunguza umaskini na maendeleo ya kiuchumi ya Taifa.

(iii) Kutoa huduma ya majisafi Mijini ili kukidhi makundi yote ya kijamii.

(iv) Kuongeza huduma ya uondoaji majitaka kutoka asilimia 17 hadi 30 ifikapo 2009/2010.

(v) Kuongeza idadi ya wananchi wanaopata huduma ya maji safi na salama vijijini kutoka asilimia 53 mwaka 2003/2004 hadi asilimia 65 ifikapo 2009/2010.

(vi) Kuendeleza skimu za umwagiliaji hekta 20,515 kwa kuziwekea miundombinu ya umwagiliaji ifikapo 2009/2010 na kufanya upembuzi yakinifu na usanifu kwa eneo la skimu lipatalo hekta 125,579 ifikapo 2009/2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kueleza utekelezaji wa maoni ya Kamati na changamoto zilizoikabili Wizara katika utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka 2007/2008 na Malengo ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009, naomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009 kama ifuatavyo:-

(i) Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na tishio la upungufu wa chakula nchini na duniani, haja ipo ya kutoa kipaumbele katika ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji maji kwa ajili ya kilimo ili kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula. Kamati inashauri Wizara ya Maji na Umwagiliaji ishirikiane na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kutekeleza azma hii. *(Makofi)*

(ii) Kutokana na mahitaji makubwa ya maji mijini na vijijini, pamoja na umuhimu wa Kilimo cha Umwagiliaji maji mashambani, ipo haja kwa Serikali kutenga fedha za ndani za kutosha ili kupunguza utegemezi wa nje hatua kwa hatua. *(Makofi)*

(iii) Ofisi za Mabonde ni muhimu katika kuchangia kukua kwa Sekta hii ya Maji na Umwagiliaji kama zitaimarishwa na zitawezeshwa. Kamati inashauri Ofisi za Mabonde zipewe fedha za kutosha na kwa wakati muafaka.

(iv) Bwawa la Kidunda linahitaji kupewa kipaumbele kwani litakuwa ni chanzo kizuri cha maji kwa Mkoa wa Dar es salaam. Kamati inashauri Wizara ijitahidi kuhakikisha kuwa inakamilisha taratibu zote za ujenzi ili mradi huu uweze kuwapatia maji ya uhakika zaidi wakazi wa Jiji la Dar es salaam na maeneo jirani. Wakati huohuo, Kamati inashauri Serikali iendeleze juhudi za uchimbaji mabwawa katika sehemu mbalimbali nchini ili kukidhi mahitaji ya upatikanaji wa maji hasa katika maeneo yenye ukame. *(Makofi)*

(v) Pamoja na jitihada zote zinazoendelea hivi sasa kuboresha huduma za maji katika Jiji la Dar es Salaam, bado matatizo yapo. Kamati inashauri Serikali iendelee kuiwezesha Wizara na Taasisi zake kuendeleza na kukamilisha miradi yote ya maji kwa Jiji la Dar es Salaam. *DAWASA* na *DAWASCO* waendelee kuboresha huduma zao ili kuondoa upungufu wa maji na malalamiko yanayojitokeza mara kwa mara. Aidha, watumiaji wa maji waepukane na vitendo vya kuihujumu *DAWASCO* kwa kujiunganishia maji bila kufuata utaratibu na kutolipa Ankara zao. *(Makofi)*

(vi) Mradi wa maji Chalinze ni mkubwa lakini watumiaji wachache, Wizara ifanye jitihada za kuwahamasisha wananchi kutumia maji ya mradi huo kwani ni maji safi na salama. Aidha, watumiaji wakiwa wengi, itawezekana kwa mradi huo kujiendesha hatua kwa hatua. *(Makofi)*

(vi) Uhaba wa wataalam katika Halmashauri za Miji na Wilaya nalo ni tatizo katika utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kamati inashauri Wizara ijitahidi kuzisaidia Halmashauri za Wilaya ili ziweze kuajiri wataalam wengi na wenye ujuzi ili waweze kusimamia Sekta ya Maji na Umwagiliaji vizuri katika kila sehemu ya nchi.

(vii) Kamati inaipongeza Serikali kwa kukamilisha mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria kwenda miji ya Kahama na Shinyanga. Aidha, Kamati inashauri Wizara na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika maeneo ya mradi washirikiane kuhakikisha watumiaji maji wa vijiji vyote vya mradi wanapatiwa elimu ya utumiaji maji. Hii itasaidia kuulinda mradi huo usihujumiwe, kwa kuanzisha umoja wa watumiaji maji kwa lengo la kusimamia kazi hiyo vizuri. *(Makofi)*

(viii) Kamati inashauri serikali kutumia uzoefu wa kazi kubwa iliyofanyika ya kutekeleza mradi wa maji Shinyanga – Kahama kwa fedha ya ndani katika kutekeleza miradi mingine kama huo katika maeneo mengine nchini. Kukamilika kwa mradi wa maji Shinyanga – Kahama isiwe sababu ya kupunguza tengeo la fedha kwa Wizara ya Maji na Umwagiliaji.

(ix) Kutokana na kuongezeka kwa uchafuzi wa vyanzo vya Maji nchini unaotokana na utupaji holela wa majitaka kutoka viwandani na kwenye makazi ya watu, Kamati inashauri Serikali kuchukua hatua madhubuti ili kukabiliana na tatizo hili ikiwemo kuelimisha wananchi juu ya utunzaji wa vyanzo vya maji na kuongeza usimamizi na udhibiti wa Majitaka kutoka Viwandani. *(Makofi)*

(x) Ucheleweshaji wa utekelezaji wa Mradi wa Taifa wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini umeleta usumbufu kwa wananchi. Kasi ya utekelezaji imekuwa ndogo kutokana na maandalizi kuchelewa. Masharti ya Benki ya Dunia, kutoeleweka sawasawa au kubadilika badilika na uwezo mdogo wa wataalam wetu umechangia sana kuchelewa utekelezaji. Kamati inaishauri Serikali kuwa makini zaidi katika miradi ya washirika wa maendeleo na kuwataarifu wananchi baada ya kukamilisha maandalizi yote kwa uhakika. Hii itaepusha usumbufu kwa wananchi na Serikali yenyewe. *(Makofi)*

(xi) Kamati inashauri mchakato wa kutunga sheria mpya ya usimamizi na udhibiti wa rasilimali za maji na utoaji huduma za maji na usafi wa mazingira uharakishwe ili kuondoa mgongano uliopo wa kusimamia rasilimali za maji.

(xii) Elimu kuhusu uvunaji wa maji ya mvua iendelee kutolewa ili kuhifadhi maji ambayo yanaweza kutumiwa kipindi cha ukame.

(xiii) Kamati inaipongeza Wizara kwa kuendelea kutoa elimu na mafunzo kuhusu maambukizi ya virusi vya ukimwi kwa watumishi na mbinu mbalimbali za kujikinga na ugonjwa huo. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuongeza jitihada na kutoa huduma mbalimbali za kuwapatia watumishi walioambukizwa ugonjwa wa Ukimwi ili kupunguza kiwango cha maambukizo ya ugonjwa huo ifikapo Mwaka 2009/2010. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Maombi ya Fedha kwa Mwaka 2008/2009. Makadirio ya Mwaka wa Fedha 2008/2009 ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji, yameandaliwa kwa kuzingatia Dira ya Taifa 2025, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA).

Baada ya uchambuzi wa kina, Kamati inakubaliana na Makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji ya jumla ya shilingi 156,243,079,700/=. Kati ya fedha hizo, Shilingi 16,288,212,000/= ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Shilingi 140,954,079,700/= ni kwa ajili ya shughuli za maendeleo. Shilingi 46,463,379,000 ni fedha za ndani na shilingi 93,491,488,700 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kwa namna ambavyo wamekuwa wakitoa ushirikiano mzuri katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati. Wajumbe wa Kamati wamekuwa bega kwa bega katika kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa kutoa maoni na ushauri ambao Wizara imekuwa ikifanyia kazi. Napenda kuwatambua Wajumbe wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Gideon A. Cheyo - Mwenyekiti, Mheshimiwa Kidawa H. Saleh - M/Mwenyekiti, Mheshimiwa Kheri K. Ameir, Mheshimiwa Teddy L. Kasella – Bantu, Mheshimiwa Charles N. Keenja, Mheshimiwa Salim H. Khamis, Mheshimiwa Castor R. Ligallama, Mheshimiwa Joyce N. Machimu, Mheshimiwa Fred T. Mpendazoe, Mheshimiwa Benson M. Mpesya, Mheshimiwa Said J. Nkumba, Mheshimiwa Juma S. Omary, Mheshimiwa Shally J. Raymond, Mheshimiwa Mwanakhamis K. Said, Mheshimiwa Salum K. Salum, Mheshimiwa Abdulkarim E. Shah, Mheshimiwa Kaika S. Telele na MheshimiwaCynthia Hilda Ngoye.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji, napenda kutumia fursa hii kumpongeza Waziri wa Maji na Umwagiliaji Mheshimiwa Prof. Mark J. Mwandosya (Mb), Naibu Waziri Mheshimiwa Eng. Christopher K. Chiza (Mb), Katibu Mkuu wa Wizara Ndugu Patrick Rutabanzibwa pamoja na wataalam wote wa Wizara kwa juhudi wanazoendeleza kuzifanya katika kuboresha utendaji kazi wa Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii na Ofisi ya Bunge hasa Kaimu Katibu wa Bunge Dkt. Thomas D. Kashililah na Makatibu wake wasaidizi wa Kamati hii Ndg. Frank K. Mbumi na Pamela E. Pallangyo kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kuratibu shughuli zote za Kamati. Pia nawashukuru wafanyakazi wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuihudumia Kamati ipasavyo katika hatua zote za Maandalizi ya taarifa hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru sana wanawake wa Mkoa wa Mbeya na wananchi wote kwa ujumla kwa ushirikiano wao mkubwa sana wanaonipa katika kutekeleza kazi yangu ya Ubunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, kwa niaba ya Kamati naunga mkono hoja hii na naomba vile vile kuwasilisha. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA – MSEMAJI WA UPINZANI WIZARA KILIMO, ARDHI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia fursa hii kwa mujibu wa Kanuni za Bunge kifungu cha 99 (7) toleo la 2007 kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani, kuhusiana na Bajeti ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kuwepo hapa leo kujadili mambo muhimu kwa maslahi ya umma wa Watanzania na kwa mema yote ambayo amekuwa akitujalia. Ni matumaini yangu kwamba majadiliano yetu yataweka mbele maslahi ya Umma wa watanzania na Mungu atusaidie.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kwa nafasi ya kipekee kabisa kukishukuru chama changu cha CHADEMA kwa kuendelea kuniunga mkono katika kazi walizonikabidhi katika kipindi cha 2005-2010. Nawaahidi kuwa kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu nitajitahidi kutimiza majukumu yangu kwa masilahi ya Taifa langu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia natoa shukurani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed (MB) Kiongozi wa Upinzani Bungeni na Naibu wake Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa (MB) kwa kutoa muongozo sahihi kwa Kambi kwa mujibu wa kanuni za Bunge. Pia napenda kumshukuru naibu waziri wangu kivuli Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga kwa ushirikiano wake wakati wote wa kuandaa hotuba hii na hata kuniwezesha leo hii Kuwepo hapa na kuzungumza kwa niaba ya Kambi ya Upinzani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa lakini si kwa umuhimu napenda kukushukuru wewe binafsi Mheshimiwa Naibu Spika pamoja na Spika, wako kwa kuliendesha Bunge hili kwa umahiri mkubwa bila kuwasahau Wenyeviti wote watatu. *(Makofi*

Mheshimiwa Spika, wakati sekta ya maji ni eneo huria kwa vyombo vya aina yote vyenye moyo wa kuipenda sekta hiyo, Serikali kwa kupitia wizara yenye dhamana ya maji ina wajibu na kazi kuu zifuatazo:-

- Kuendeleza, kukagua na kukuza sera ya maji safi na maji taka;
- Kuhimiza, kushirikisha, kusimamia na kuratibu huduma za maji safi na maji taka kwa ajili ya watu wote kwa kutilia maanani masuala ya jinsia; na
- Kuwaendeleza wataalam wenye uwezo mkubwa kushughulikia sekta hiyo.

Hivyo basi, mchango wa Kambi ya Upinzani, utajikita zaidi kwenye kazi na majukumu haya ya Serikali na kuainisha kama Serikali imeweza kuyatekeleza na pia tutajikita kwenye changamoto zilizopo ili kuweza kuiboresha sekta hii ya maji na kuweza

kuboresha maisha ya watanzania wetu kwa vitendo na sio kwa nadharia. Kambi ya Upinzani, inaamini kuwa maji yana uhusiano wa karibu na afya, elimu, kilimo, ardhi, uwekezaji na mazingira.

Pia maji yanaweza kutumiwa kama aina fulani ya ushawishi katika medani za kimataifa (Mto Nile) aidha, maji kama raslimali ya utajirisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta hii ni muhimu sana katika kunyanyua uchumi wa nchi na ndio maana hata katika Sera ya Taifa ya Maji waliliona hili nakuahidi kuitumia sekta hii katika kunyanyua uchumi na kuondoa umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, upatikanaji wa maji salama ni muhimu katika kupigana na umaskini na matatizo ya afya. Watu maskini ambao wengi wao huishi vijijini wana nafasi finyu ya kupata maji safi kwa ajili ya matumizi ya nyumbani na kwa ajili ya mazao na matumizi ya afya. Faida za uchumi zinaweza kupatikana siyo kwa njia ya moja kwa moja tu bali kwa kuwa na afya bora na kuokoa muda unaotumika kuhangaika na kazi za kuchosha za kubeba maji kwa umbali mrefu hasa hili linawakera sana akina mama. Takwimu zinaonyesha kuwa magonjwa yanayoambukizwa kwa njia ya maji hupatikana zaidi katika sehemu ambapo watu wanatumia maji yaliyoambukizwa au hawana maji ya kutosha kwa matumizi yao ya kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, idadi ya magonjwa hayo ni zaidi ya nusu ya magonjwa yanayowaathiri watu na kwamba asilimia themanini ya magonjwa yanayowashambulia Watanzania wanaoishi vijijini. Serikali ni lazima ilenge katika upatikanaji wa maji vijijini tena yaliyo safi na salama. Usimamizi wa maji ni lazima uwashirikishe wadau wote kwa ajili ya kufanikisha upatikanaji wa maji wa kutegemewa, unaofaa na maji hayo yanatumika ipasavyo, yanalindwa na kuhifadhiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi na mahitaji makubwa kuliko yote ya maji ni ya nyumbani. Kutokana na shughuli za kiuchumi na za kuhudumia jamii ambazo, kwa njia moja au nyingine zote zinatumia maji, upatikanaji na usambazaji wa maji umekuwa ni mzigo mkubwa kwa wananchi wa Taifa hili. Kwa muda mrefu mchango wa sekta ya maji kwa pato la Taifa *(GDP)* limebaki kuwa asilimia 0.2 ambacho ni kiwango kidogo sana ikitilia maanani umuhimu wa sekta hii katika uchumi kwa kulinganisha na sekta nyingine, kwa mfano sekta ya kilimo ambayo kwa mwaka 1999 ilichangia asilimia 48.9 ya pato la Taifa.

Lakini maji kwa vyovyote vile, ni muhimu zaidi katika kukuza maendeleo ya uchumi wa Tanzania kwa sababu sekta hiyo inaunganisha sekta nyingine zote kwa mfano, hata kilimo ambayo ni sekta kubwa kuliko zote, hakiwezi kufua dafu bila maji. Kwa bahati nzuri maji nchini Tanzania ni sekta ambayo ina uwezo wa kukua ikilinganishwa na sekta nyinginezo. Mwaka 1999 maji yalichangia kwenye Pato la Taifa ongezeko la asilimia 3.0. Ukilinganisha na mchango wa shughuli za usambazaji maji katika pato la Taifa kwa mwaka 2007 ambao ulikuwa ni asilimia 0.4 kama ilivyokuwa miaka minne mfululizo. Kambi ya Upinzani inataka kujua ni kwa nini sekta hii imekuwa ikichangia kiasi hicho hicho kwa miaka minne mfululizo wakati matumizi ya maji yamekuwa yakiongezeka kila mwaka ?

Mheshimiwa Naibu Spika, Maji ni rasilimali muhimu katika vipengele vyote vya maendeleo ya jamii, maendeleo ya sekta tofauti kama vile viwanda, ufugaji, umwagiliaji, uzalishaji wa umeme, usafiri, utalii, madini unategemea sana sekta hii ya maji. Vile vile sekta hii ni muhimu katika maisha ya mwanadamu, bila ya kuwepo rasilimali hii hakuna uhai kwa binadamu, wanyama, ndege na mimea.

Mheshimiwa Naibu Spika, ingawa zaidi ya asilimia 70 ya dunia imechukuliwa na maji, lakini asilimia 2.5 tu ndio maji safi na katika asilimia hizo (2.5%) asilimia 70 imeganda katika barafu ya Antartika, Aktik na *Greenland* na asilimia zilizobakia ndizo zinazopatikana juu ya ardhi na chini ya ardhi. Katika asilimia hizi 30 kiasi cha theluthi moja ndio zinazopatikana kwenye maziwa, mito, mabwawa na maji yaliyoko chini ya ardhi ambayo yanahitaji gharama, sayansi na teknolojia ya hali ya juu katika upatikanaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maji ni rasilimali muhimu lakini kwa upande mwingine ni rasilimali adimu duniani hii ni kutokana na kuongezeka kwa idadi ya watu kumepelekea kuongezeka kwa mahitaji ya rasilimali hii. Baadhi ya nchi zimekumbwa na tatizo la uhaba wa maji, na wataalamu wa mambo ya maji wametabiri kwamba miaka michache ijayo kutatokea vita ya tatu ya dunia itakayosababishwa na upungufu wa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii karibu ya watu bilioni 1.1 katika nchi zinazoendelea wana matatizo ya upungufu wa maji na watu karibu bilioni 2.6 wanatumia maji ambayo si salama na hii imechangia vifo vya watoto zaidi ya milioni 1.8 kila mwaka kutokana na maradhi yanayoletwa na maji *(water born diseases).* Karibu ya nusu ya watu wa nchi zinazoendelea wana matatizo ya afya yanayosababishwa na aidha ukosefu au kunywa maji ambayo sio safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya maji inakumbana na changamoto kubwa sana hivi sasa ulimwenguni kote kutokana na tatizo la uchafuzi wa hali ya hewa na mazingira kwa ujumla wake, kwani ongezeko la joto ulimwenguni limesababisha vyanzo vingi vya maji ama kukauka kabisa ama kupungua. Mazingira yamekuwa ni changamoto kubwa sana kwa ajili ya ustawi na ukuaji wa sekta ya maji ulimwenguni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na tatizo hili la maji watabiri wanaeleza kwamba $^{2}/_{3}$ ya watu wanaoishi duniani watakumbwa na tatizo la maji ifikapo mwaka 2025 na migogoro zaidi inayohusiana na maji itaibuka duniani kote kati ya nchi na nchi, jamii na jamii na hata baina ya wakulima na wafugaji, wanyama na binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, huku dunia ikihangaika na tatizo la maji Tanzania ni nchi pekee iliyobahatika kuwa na vianzio vya maji vya kutosheleza vikiwemo mito tisa mikubwa kama vile Mto Rufiji, Mto Pangani, Mto Ruvu na Mto Ruvuma. Pia tuna vyanzo vingine kama Bahari ya Hindi, Ziwa Victoria ambalo ni kubwa kwa Afrika, Ziwa Tanganyika ambalo lina kina kirefu zaidi ya maziwa yote ya Afrika, Ziwa Nyasa, Ziwa Rukwa, Ziwa Eyasi na kadhalika na chemchem na maji ya kutosheleza yaliopo chini ya ardhi na hali ya hewa nzuri inayoleta mvua za mara kwa mara karibu sehemu zote za nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, licha ya rasililmali zote hizo tulizonazo, lakini bado sekta hii ya maji haijaleta tija na maendeleo yanayotegemewa na wananchi walio wengi kwani kama sekta hii bado haijaendelezwa vya kutosha na kama tungekuwa na mkakati mzuri na kuitumia vizuri rasilimali hii, basi leo nchi yetu tungekuwa tumepiga hatua kubwa kiuchumi na maendeleo kwa ujumla na kamwe tusingekuwa nchi ya tatu kwa umaskini duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitembelea tovuti ya Wizara ya Maji ambayo ni www.maji.go.tz utaona ya kuwa tovuti hiyo imeandaliwa kwa lugha ya Kiingereza. Kambi ya Upinzani inahoji tovuti hii ni kwa masilahi ya nani? Inamnufaisha nani? Hii ni kwa kuwa Watanzania ambao wanahitaji sana huduma za maji na taarifa mbalimbali kuhusiana na sekta ya maji hawajui hicho Kiingereza kilichoandikwa humo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inamtaka Waziri awaeleze Watanzania, ni kwanini ameamua kuandika masuala muhimu kama hayo kwa lugha ambayo Watanzania walio wengi hawaijui? Hivyo basi, tunaitaka Wizara itafsiri na kuandika taarifa zake kwa Kiswahili ili Watanzania ambao ndio wadau wakubwa wa maji waweze kupata taarifa hizi muhimu na kwa lugha ambayo wanaielewa kwa ufasaha zaidi (Kiswahili).

Mheshimiwa Naibu Spika, Maji yaliyoko chini ya ardhi ni chanzo kikubwa cha maji katika maeneo mengi ya Tanzania na ni njia nyingine ya nyongeza ya kuaminika ya kupata maji katika maeneo ya kati na kaskazini ya nchi ambayo yanakabiliwa na ukame katika mikoa ya Dodoma, Singida, Shinyanga, Tabora, Mwanza, Mara, Arusha, Pwani na kusini mwa Kilimanjaro.

Vyanzo vya maji yaliyo juu ya ardhi yanatokana na maziwa, mito, chemichemi na mabwawa ya asili au yaliyotengenezwa na binadamu. Asilimia 50 ya maji yaliyo juu ya ardhi yanapatikana kwenye mito ambayo humwaga maji yake moja kwa moja katika Bahari ya Hindi. Mito hiyo ni ya Pangani, Wami, Mkondoa, Ruvu, Rufiji, Ruaha, Mbwemkulu, Lukuledi na Ruvuma. Asilimia 50 ya maji ya juu iliyobaki imegawanywa katika maji ambayo hutiririka na kuishia katika mabonde bila kufika baharini. Maji hayo yanaishia Ziwa Rukwa, Bonde la Bubu, Ziwa Eyasi na Ziwa Manyara. Maji ya mito mingine hutiririka katika Ziwa Victoria (mito Meri, Maru na Kagera), Mto Malagarasi humwaga maji yake katika Ziwa Tanganyika na mto Songwe na Ruhuhu inatiririka kuelekea kusini na kumwaga maji katika mfumo wa Ziwa Nyasa – Zambezi.

Kambi ya Upinzani inasikitishwa na hali ya Serikali kutokuwa makini katika kuwa na mpango mkakati unaoeleweka wa kutumia vizuri vyanzio hivi vya maji kwa maendeleo ya Watanzania kwa maana ya matumizi yao ya nyumbani na hata kwa maendeleo ya kiuchumi wa nchi yetu. Kambi inamtaka Waziri wakati wa kuhitimisha atoe maelezo ya kina kuhusu mpango mkakati huo. Au ni mpaka hali hiyo ya mgogoro mkubwa wa upungufu wa maji utukumbe ndipo tuanze kuzinduka na kuwa na mipango ya Zimamoto? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Maendeleo ya sekta ya maji nchini yanaongozwa na sera ya sekta ya maji.  Sera inayotumika ni ile iliyotolewa mwaka 1991, pamoja na ahadi nyingi za mara kwa mara ndani ya Bunge hili kuwa Sera mpya inaandaliwa.

Hata  hivyo, hata bila Sera hiyo kuwa tayari, hivi karibuni serikali imeanzisha marekebisho ya mpango ambao utahusisha sekta zote za jamii, uchumi na siasa ikiwemo na ya maji.  Hivyo sekta ya maji imeongezewa nguvu kwa mpango unaoendelea kwa kurekebisha sekta hiyo ambayo inategemewa kuimarisha sera ya maji katika usimamizi na utendaji kwa kuzingatia yafuatayo:-

- Maji hustahili kufikiriwa kuwa ni hitaji la msingi;
- Kufanikisha mpango wa upatikanaji wa maji safi na salama na ya uhakika katika maeneo ya vijijini na mijini;
- Kuhakikisha kuwa maji safi na salama yanapatikana katika umbali usiozidi mita 400 kutoka sehemu wanazoishi watu; na
- Shughuli za kuendeleza na usambazaji wa maji ziongozwe na soko huru ambapo wote wanaohusika, kama vile jamii, sekta binafsi vyama visivyo vya kiserikali viwe vya hapa nchini au nje ya nchi viweze kuwekeza katika sekta hii ili kusaidia juhudi za serikali katika kuendeleza na upatikanaji wa huduma za maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi sasa, maji mengi yanayotumika ni kwa ajili ya matumizi ya nyumbani.  Ingawa asilimia 80 ya watu wanaishi vijijini na asilimia 20 tu wanaishi mijini, maji mengi zaidi hutumika vijijini.  Hata hivyo, licha ya umuhimu mkubwa wa maji ambao haujionyeshi, vyanzo vingi vya maji bado ni duni na kwamba idadi kubwa ya watu wanatumia maji kutoka vyanzo hivyo.  Hadi kufikia mwaka 1999, asilimia 45 ya watu waishio vijijini na asilimia 68 ya watu wanaoishi mijini walikuwa na uwezo wa kupata maji safi na salama.  Wakati takwimu hizo zinaonyesha wastani tu wa kitaifa lakini hali halisi inatofautiana sana kati ya sehemu na sehemu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu huduma ya maji machafu, maeneo mengi ya mijini huendelea kuathirika na huduma duni inayotolewa.  Kwa mujibu wa taarifa zilizopo ni asilimia saba tu ya wakazi wa mijini ambao huduma zao za maji machafu zimeunganishwa kwenye huduma ya mifereji ya maji taka ambayo hupatikana kwenye miji michache tu na kwamba mifereji hiyo ilijengwa miaka mingi iliyopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii ni ya hatari na ndio maana kila kukicha utasikia milipuko ya magonjwa ya kuhara na kipindupindu mijini zaidi hata ya vijijini na hii inatokana na ukosefu wa mfumo dhabiti wa maji taka mijini na hivyo kusababisha magonjwa ya mlipuko kila mara. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuweka mkakati wa kuhakikisha kuwa mfumo wa maji taka unaimarishwa mijini ili kuhakikisha kuwa wananchi wetu hawakumbwi na magonjwa ya kula uchafu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la maji limekuwa ni tatizo sugu hapa nchini mwetu. Pamoja na ilani ya CCM kwa kipindi cha 2005-2010 kusisitiza kuwa, nanukuu (ukurasa wa 82) “kuwawezesha wananchi mijini na vijijini kupata maji safi, salama na ya kutosha kwa matumizi yao ya kawaida karibu na sehemu wanazoishi na kwa mahitaji ya

kiuchumi. Lengo ni kuwafikishia huduma hiyo asilimia 90 ya wakazi wa mijini na asilimia 65 ya wakazi wa vijijini ifikapo mwaka 2010".

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na msisitizo huo kwenye Ilani Kambi ya Upinzani haioni kama Serikali inatilia mkazo wowote kuhakikisha kuwa wananchi wanapata maji safi na salama. Tunasema hivi kutokana na ukweli kuwa Bajeti ya mwaka huu wa 2008/2009 Wizara ya Maji imetengewa fedha pungufu kuliko ilivyokuwa Bajeti ya mwaka jana. Mwaka huu Wizara ya Maji imetengewa kiasi cha shilingi bilioni 230.6 ukilinganisha na shilingi bilioni 309.1 kwa mwaka 2007/2008 na hapa kimeongezeka kitengo cha umwagiliaji ambacho mwaka jana kilikuwa chini ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika. Huku Wizarani kwenye malengo yake ikisema kuwa ni kuongeza idadi ya wananchi wanaopata huduma ya maji safi na salama kutoka 53% mwaka 2003 hadi 65% ifikapo mwaka 2010/2011. Kambi ya Upinzani inajiuliza, Serikali inafanya kazi nje ya ilani ama ni ilani haitekelezeki? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwendo huu wa kupunguza Bajeti ya Wizara ya Maji huku kila kukicha yakitolewa matamko kuwa ilani ya CCM itatekelezwa ni kuupotosha umma kwani ilipaswa fedha za Wizara hii ziongezwe ili kuweza kuwafanya wananchi waweze kupata maji safi na salama. Haiwezekani kitendo cha kukamilika kwa ujenzi wa mradi mmoja wa kutoa maji ziwa Victoria uifanye Serikali kupunguza Bajeti kwa shilingi bilioni 79 kwa mujibu wa hotuba ya waziri wa fedha wakati akiwasilisha hotuba yake ya Bajeti alisema, nanukuu: "Bajeti ya Maji – inaonekana kushuka ikilinganishwa na mwaka huu wa 2007/2008. Sababu kuu ni kwamba ujenzi wa mradi mkubwa wa maji Shinyanga na Kahama, umekamilika. Aidha, mradi wa maji wa Monduli umepata fedha pungufu za wahisani mwaka ujao, kulinganisha na mwaka wa 2007/2008".

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaona kuwa ilani ya uchaguzi ya CCM haitaweza kutekelezwa kwani kasi ya uchimbaji wa visima hapa nchini imepungua kwa mwaka 2007, pamoja na ukweli kuwa Bajeti ya Wizara ilikuwa kubwa kuliko kipindi cha mwaka huu wa 2008/2009. Kwa mfano Mkoa wa Arusha kwa mwaka 2006 vilichimbwa visima 16 ila mwaka 2007 vikachimbwa visima nane, Dar es Salaam 2006 visima 200, huku mwaka 2007 visima 141, Lindi 2006 visima 33 mwaka 2007 visima saba, Morogoro 2006 visima 16, mwaka 2007 visima 6, Mtwara 2006 visima 44 huku mwaka 2007 visima 23. Kama mwendo wenyewe wa kuchimba visima ndio huu hatuoni kamwe kama malengo ya ilani ya CCM pamoja na malengo ya MKUKUTA yataweza kufikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inataka kuikumbusha tena Serikali ahadi zake ilizotoa kwa wananchi kupitia Ilani ya CCM pia kupitia ahadi zilizotolewa na aliyekuwa mgombea Urais wa CCM Mheshimiwa Jakaya Kikwete kama ifuatavyo:-

- Mkoa wa Dodoma aliahidi kuwa utapatikana ufumbuzi wa tatizo la maji wilaya za Kondoa, Kongwa, Mpwapwa na Dodoma Mjini;
- Mkoa wa Kagera aliahidi kuwa tatizo la upatikanaji maji katika miji inayozunguka Ziwa Victoria litakuwa limetatuliwa;
- Mkoa wa Kilimanjaro aliahidi kuwa ataongeza kiwango cha upatikanaji maji safi na salama katika Wilaya za Same na Mwanga;
- Mkoa wa Lindi, waliahidiwa kuwa tatizo la maji safi na salama litashughulikiwa;

- Mkoa wa Manyara, waliahidiwa kuwa tatizo la maji katika miji ya kiteto litatuliwa;
- Mkoa wa Mara waliahidiwa kuwa tatizo la maji safi na salama katika mji wa musoma na miji ya makao makuu ya wilaya;
- Mkoa wa Mtwara waliahidiwa kuwa tatizo la maji hasa Masasi, Tandahimba na Newala yanatatuliwa kwa kuwapatia miradi mikubwa ya maji kama ule wa *Makonde Water Supply;*
- Mkoa wa Tabora waliahidiwa kupatiwa huduma nzuri za maji safi na salama mijini na vijijini; na
- Mkoa wa Tanga waliahidiwa kuwa tatizo la maji kwenye miji ya Mango na Kabuku na Wilaya ya Lindi yatamalizwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani imelazimika kuzikumbusha ahadi hizi ili Serikali iweze kuchukua hatua kwani hatuoni kama inawezekana kutekeleza ahadi zote hizi wakati Bajeti ya Wizara ya Maji kwa dhahiri inapungua kama tulivyoainisha hapo juu na pia tangu zilipotolewa ahadi zote hizi mpaka sasa ni karibia miaka mitatu imekwisha. Kambi ya Upinzani inahoji:- Je, ahadi hizi zitatekelezwa na kama jibu ni ndiyo Waziri anaweza kuliambia Bunge hili mkakati wa makusudi wa kutekeleza ahadi hizo? Wananchi wanahitaji kufahamishwa mkakati unaoeleweka ili waendelee kuwa na matumaini? Rejea kitabu kilichotolewa na Ofisi ya Waziri Mkuu kinachoonyesha ahadi za Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwepo na tatizo la upatikanaji Maji hususan Mkoa wa Dar es Salaam kwani maeneo mengi hayapati maji ya kutosheleza maeneo yote ya jiji. Kambi ya Upinzani inataka kupata majibu kutoka Serikalini ni lini tatizo hili litatatuliwa? Kwani kadiri siku zinavyoongezeka maeneo mengi ya jiji badala ya kupata maji utakuta hata kule ambako maji yalikuwa yanapatikana hayapatikani tena, kwa mfano Changanyikeni ambako hakuna maji japo kipindi cha nyuma kulikuwa kunapatikana maji na pia maeneo mengi ya jiji na hili linawafanya wananchi kununua maji kwa kiasi cha Sh. 300/= mpaka Sh. 400/= kwa ndoo ya lita 20, huku ni kuwaumiza wananchi na kuwaongezea mzigo wa gharama za maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo kubwa sana la wananchi na haswa wanaoishi mijini kutokuletewa Ankara zao za maji kwa wakati na hili linawafanya wananchi kukumbana na matatizo na hasa ya kukatiwa maji pasipokuwa na sababu za msingi, mfano, katika Mkoa wa Kigoma, miaka ya 2001-2002 baadhi ya maeneo hasa eneo la Mwanga Majengo maji yalikatika kwa mwaka mzima na miezi minne bila hata siku moja maji kutoka, wakati tunalo Ziwa Tanganyika. Sababu nyingi hutolewa na Serikali ikiwemo uchakavu wa mitambo ya kusukuma maji na mabomba. Akijibu swali katika kikao hiki cha bajeti Mheshimiwa Naibu Waziri alisema, Kigoma imetengewa Shilingi milioni 227 za mabomba na milioni 69 kwa ajili ya mashine ya kusukuma maji.

Katika taarifa ya habari imesikika Mkurugenzi wa KUWASA naye akieleza tatizo la maji ni ukosefu wa vitu hivyo hivyo. Je, Serikali haitoi taarifa inapotoa pesa Mikoani? Kwa nini asieleze jinsi utekelezaji utakavyokuwa kuliko kuendelea kulalamika? Kambi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri alieleze Bunge na wananchi kwa ujumla wake ni lini tatizo hili la kukatika maji litamalizwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mradi wa mita za maji, pamoja na Serikali kutumia fedha nyingi kuwekeza kwenye mradi huu bado kwa maeneo ya Dar es Salaam na maeneo mengine ya nchi ambayo kuna mita hizi wananchi wengi wanaendelea kupelekewa Ankara kwa kutumia vigezo vya kukadiria *(estimations).* Kuna nini hapa? Kwa nini mamlaka za maji hazitumii mita hizi kwa ajili ya kuwapelekea wateja wao Ankara zao za maji kwa jinsi walivyoyatumia?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kutokana na uanzishwaji wa Bodi za maji za Wilaya hapa nchini kwa mujibu wa sheria ya *"Water Utilization[Control and Regulation] Act Cap 331 and Water Works Act, Cap 272.* ilipelekea kuanzishwa kwa bodi mbalimbali za maji kwenye Wilaya na miji mbalimbali hapa nchini.

Kambi ya Upinzani imeshangazwa sana na bodi hizi kulipana pesa nyingi sana pindi wanapokaa vikao vya bodi hizi. Kwa mfano, Bodi ya Maji ya Wilaya ya Moshi *(MUWASA)* kila wanapokaa kikao cha siku moja wanalipana kiasi cha Sh. 400,000/= . Hizi ni fedha nyingi sana kwa kikao kimoja tena ambacho kinahusisha Wajumbe kutoka eneo hilo hilo, yaani ndani ya Wilaya husika.

Kambi ya Upinzani haikubaliani na kiasi kikubwa namna hii kuwa ni posho za kikao kimoja cha Bodi ya Maji. Tunataka maelezo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, ni nani ama ni kipengele kipi cha sheria ambacho kinapitisha kiwango cha posho hizi? Je, kama fedha nyingi kiasi hiki zitatumika kwa ajili ya posho tutaweza kuwapelekea wananchi wetu maji? Sambamba na hilo, ni juzi kulikuwa na taarifa iliyolalamikia posho ya shilingi milioni moja wanayojilipa Wajumbe wa Bodi ya *TANAPA.* Hii ni hatari kwa maendeleo ya nchi changa kama Tanzania. Serikali inatoa kauli gani kwa viwango hivi vya posho katika Bodi mbalimbali na ni chombo gani kinaratibu au kidhibiti viwango hivi?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaona kuwa na Bodi za Maji ambazo kila wanapokaa wanalipana kiasi kikubwa kama hiki ni ufujaji wa fedha za wananchi na ni kuwaongezea wananchi mzigo wa kulipia gharama za maji ili kuwanufaisha Wajumbe wa bodi hizo.

Hivyo basi tunapendekeza kuwa ni lazima pawepo na sheria ama kanuni ambayo itaangalia jinsi ya kuwapa Wajumbe wa Bodi hizi posho za vikao na kuweka viwango maalum nchi nzima, kwani Sh. 400,000/= kwa siku kama wanavyofanya wanabodi wa Bodi ya Maji Moshi ni kuwaumiza wananchi. Kama kiwango cha chini cha mshahara ni Sh. 100,000/= kwa mwezi, kuna usawa gani kumlipa mtu posho ya Sh. 400,000/= kwa siku kama posho ambayo haikatwi kodi kiasi ambacho ni sawa na mshahara wa mfanyakazi wa kima cha chini wa Serikali kwa miezi minne?

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na posho hizi kubwa, zinasababisha kuwepo kwa ufisadi kama ilivyotokea huko Moshi ambapo Mhasibu wa Mamlaka ya Maji ya Moshi *(MUWASA)* anakabiliwa na tuhuma za wizi wa fedha kwa ajili ya posho za vikao, baada ya kugundulika ufisadi huo ambao ulifanyika kati ya tarehe 13 September, 2007, pale Mhasibu alipochukua fedha za posho na kuwalipa Wajumbe hewa

watatu ambao ni Prof. Suleman Chambo, Ndeshukurwa Sumari na Dr.Luciana Maruma ambao hawakuhudhuria kikao cha tarehe 13 september, 2007, lakini bado wakalipwa au kuonyeshwa kuwa walilipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo kubwa la MKUKUTA ni kuhakikisha kuwa ifikapo mwaka 2009/2010 zaidi ya asilimia 65 ya Watanzania waishio vijijini wanapata maji safi na salama ndani ya dakika thelathini kutoka makazi yao. Hii maana yake ni kwamba akina mama 65 kati ya mia waweze kutumia dakika thelathini tu kupata maji ifikapo mwaka 2010. Wakati huo huo, katika maisha halisi kuna pengo la ongezeko katika upatikanaji wa maji safi na salama kati ya matajiri na masikini na kati ya watu waishio maeneo ya vijijini na mijini pengo hili lililochochewa na sera za ubinafsishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, huu ni wakati wa kufanya kazi na kwa kweli tusilale mpaka malengo ya MKUKUTA katika Sekta ya Maji yafikiwe. Tujipime kila mwaka tumefikia wapi na Mheshimiwa Waziri wa Maji kila mwezi wa Juni au Julai atoe taarifa Bungeni kufanikiwa au kutofanikiwa katika kufikia malengo ya MKUKUTA kwa sekta yake ya maji katika mwaka uliokwisha. Hakuna Kulala mpaka kieleweke! Kueleweka ni wananchi wote kupata maji safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, mamlaka za usimamizi za mabonde ya maji, ni vyombo muhimu sana na ndio sababu zikaundwa kwa sheria ya Bunge. Raslimali hii ya mabonde kwa nchi yetu ni utajirisho toka kwa Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Naibu Spika, duniani kote miundombinu huwa ni jukumu la Serikali. Hivyo basi, Tanzania kwa kuwa tayari kuna mamlaka za mabonde, jukumu la kutengeneza miundombinu ya umwagiliaji lilitakiwa kuwa ni jukumu lake la msingi, ukiachiliaji kuangalia na kuendeleza vyanzo vya maji vya mabonde husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mamlaka za mabonde ya maji ni taasisi zenye uwezo kisheria na kiutendaji. Hivyo basi, Kambi ya Upinzani haioni sababu kwa mamlaka hizo kwa kipindi chote kukaa bila ya kufanya kazi badala yake kutegemea ruzuku kutoka Serikali kuu na au kukusanya ushuru kutoka kwa watumia maji badala ya kubuni mbinu ya kukuza upatikanaji wa maji. Hili ni jambo ambalo linadhalilisha bodi na kuzifanya bodi hizo kukosa ubunifu wa mikakati ya maendeleo katika mabonde yao. Kwa hali ilivyo sasa hivi, Bodi hizi hazina manufaa kwa wananchi licha ya kukusanya fedha za kuendeshea ofisi zao tu! Kama ziko Waziri alitolee ufafanuzi Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaamini kabisa kuwa mabenki yetu hapa nchini yanaweza kukopesha fedha za kujenga miundombinu ya umwagiliaji kwa kushirikiana na mamlaka za undelezaji wa mabonde. Hili linawezekana kabisa kwani pindi miundombinu itakapokuwepo wawekezaji katika kilimo ni dhahiri watapatikana, kumbuka kuwa siku zote watu wanafuata fursa na sio kinyume chake. Hivyo miundombinu hii inaweza kuwa inakodishwa kwa wakulima kwa kiwango muafaka kulingana na gharama za uwekezaji na uendeshaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inauliza na hili nalo ni la kutafuta wahisani? Hii ni dhahiri kuwa nchi yetu inakosa watendaji wabunifu ambao kwa mtindo huu raslimali zetu zitaendelea kutotumika au kutumika kwa manufaa ya wachache. Hivyo basi, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuondoa watendaji wasio wabunifu na kuwapa nafasi wale wenye kuona fursa na kuzitumia ipasavyo kwa maendeleo ya Watanzania wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiwango cha fedha kinachotolewa katika kuendeleza *component* ya umwagiliaji ya *ASDP* hakitoshelezi kwa ajili ya utekelezaji, hivyo basi, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kutafuta vyanzo vipya vya fedha ili kuweza kutekeleza miradi hiyo na haswa kipindi hiki ambacho dunia inakabiliwa na tishio la ukosefu wa chakula. Ni lazima tuchukue hatua mapema ili kuweza kuepukana na balaa hili ambalo linaweza kujitokeza na kuiathiri dunia pamoja na wananchi wetu. Inawezekana kuzalisha kwa wingi chakula cha kutosha kwa kutumia vizuri sekta ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa bwawa la Manchira Mugumu Wilaya ya Serengeti, umeistua sana Kambi ya Upinzani. Bwawa hili lilibuniwa mwaka 1977 takribani miaka 30 iliyopita na kutengewa fedha takriban kila mwaka. Bado mradi huu haujakamilika, wananchi wanavijiji wa Rwamchanga, Morotonga, Kebosongo, Kisungura, Rung'abure, na Nyamoko wameyasubiri haya maji kwa miaka 30 bila mafanikio. Kambi ya Upinzani inamtaka waziri awaeleze wananchi hawa kuwa bwawa hili litakamilika lini, na wategemee kupata maji lini . Hizi lugha za upembuzi yakinifu kila siku zinapoteza umaana wake kama wananchi hawa wameelezwa lugha hizo kwa zaidi ya miaka 30 iliyopita. Serikali itueleze ni lini mradi utakamilika na atueleze ni kiasi gani kinatumika toka 1977 mpaka leo?

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwenye ujenzi wa bwawa hili wananchi wametuletea malalamiko yao kuwa kwenye ulipaji wa fidia, wapo ambao walilipwa ile hali hawakustahili kulipwa na wale waliokuwa wanastahili kulipwa hawakulipwa na wale wachache waliolipwa wamelipwa fidia ndogo. Kambi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri alieleze Bunge lako Tukufu ni hatua gani zimechukuliwa mpaka sasa juu ya fidia za wananchi hawa ambao wamesubiri kwa zaidi ya miaka 30 bila bwawa kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna taarifa kuwa Serikali ilitoa shilingi milioni 70 mwaka 1977 kwa ajili ya ujenzi wa bwawa hili, pamoja na nyumba, huku taarifa za Wizara zilizowasilishwa mbele ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali walipotembelea ujenzi wa bwawa hilo tarehe 4 Juni, 2008 zilionyesha kuwa fedha hizo zilitumika kwa ajili ya ujenzi wa ofisi na nyumba za wafanyakazi. Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inaonyesha kuwa hakuweza kutoa maoni ya ukaguzi kwani hakuweza kupata viambatanisho vya miaka ya nyuma yaani miaka ya 1982, 1983, 1989 mpaka 1990.

Kambi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri atoe majibu kwa Bunge hili kuwa ni kitu gani kilifanya viambatanisho hivyo visiweze kupatikana kwa ajili ya

ukaguzi? Pia tunamtaka Mheshimiwa Waziri alieleze Bunge kuwa ni hatua gani zimechukuliwa na Wizara dhidi ya wale wote ambao wamehusika na upotevu wa viambatanisho hivyo, kwani bila kuwachukulia hatua utakuwa ni mchezo ambao utakuwa unafanywa kila wakati huku wananchi wakiendelea kusubiri Maji kwa miaka 30 bila kuyapata na huku fedha zao zikipotea bila wahusika kuchukuliwa hatua za kinidhamu na ama kuwajibishwa kwa mujibu wa sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, nashukuru sana kwa kunisikiliza na naomba kuwasilisha. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Mbunge. Sasa tulio nao hapa ni wengi. Lakini tukizingatia kwamba Wizara hii muda wake ulishachukuliwa na Wizara ile ya Kilimo. Kwa hiyo, idadi yetu ya wachangiaji itapungua sana. Hapa nina wachangiaji kama 40 na ngapi sijui. Kwa hiyo, naanza na wale ambao hawajachangia kabisa, ni Mheshimiwa Job Ndugai, Wabunge ambao wamechangia mara moja kwa muda tulionao hapa tunaweza kupata watu sita tu. Atakuwa Dr. Wilbrod Slaa, Mheshimiwa Kusila, Mheshimiwa Zabein Mhita, Mheshimwia Paschal Degera. Tuishie tutaona tunavyokwenda.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kwanza ili na mimi nichangie katika somo lililo mbele yetu kuhusiana na hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji - Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya.

Nianze kwa niaba ya wananchi wa Kongwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuteuliwa kwake kwa nafasi hiyo kwa vile toka apate nafasi hiyo sijasimama kuzungumza. Naomba azipokee salamu za watu wa Kongwa na sisi tunaahidi kabisa tutampa kila aina ya ushirikiano, tunamwalika kwa vile Kongwa ni karibu, akipata nafasi wakati wa Bunge hili, basi atutembelee tukazungumze huko huko Kongwa.

Pia tungependa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu aliyepita, Mheshimiwa Edward Lowassa kwa kazi nzuri ambayo alikuwa amefanya hasa kwa mashule ya sekondari ambako sisi Kongwa tulikuwa na sekondari tatu, lakini leo kwa msukumo mkubwa sana wa sekondari kutoka Serikalini tuna sekondari 25. Huwezi ukaamini. Tuna sekondari tatu ambazo tumekuwa tukizijenga mwaka jana hazikupata watoto. Zinakaa mwaka mzima zikisubiri watoto mwakani. Ni hatua ambayo katika mazingira ya kawaida tusingeweza kuifikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mwandosya kwa uwasilishaji mzuri wa hotuba yake, hotuba hii ni nzuri, inajieleza yenyewe, imeandaliwa kitaalam, inasomeka vizuri. Takwimu zimekaa sawa sawa. Nampongeza sana Profesa kwa maandalizi haya mazuri sana ya hotuba hii. Lakini pia ningependa kumpongeza Profesa kwa ziara ambayo aliifanya wiki iliyopita katika Wilaya ya Kongwa na kupitia maeneo mbalimbali kujionea mwenyewe hali halisi ya huduma za maji katika Wilaya ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukifanya ziara katika Wilaya ya Kongwa ukaenda kijiji chochote kile, ukawaambia wananchi wakuambie tatizo moja tu walilonalo, siyo mawili, wakuambie moja tu tatizo lao ni nini? Watakuambia ni maji. Ni kweli kuna tatizo kubwa sana la maji. Kama ilivyo kule Kongwa naamini kwa Mkoa wa Dodoma ni hivyo hivyo, mahali pengi tatizo kubwa kabisa ni maji. Nchi nzima kwa kweli maji ni tatizo, hata miji kama ya Mwanza ambayo iko pembeni kabisa ya ziwa, lakini maji ni tatizo. *(Makofi)*

Kigoma, pembeni ya ziwa maji ni tatizo. Kwa hiyo, katika vipaumbele vya matatizo vya huduma za jamii, huduma za wananchi, huduma za kiuchumi. Kwa kweli maji ina *rank number* moja. Ni tatizo kubwa ni shida kubwa inayokumba wananchi maji ya kutumia majumbani, maji ya mifugo, maji ya umwagiliaji, maji, maji, maji, maji. Ni tatizo kubwa sana. Kwa hiyo, matarajio yetu ni kwamba bajeti ya Serikali kiuwiano ingeipa uzito sana Bajeti ya Wizara ya Maji. Lakini ukweli ni kwamba bajeti ya mwaka huu imepungua kutokana na kupata maelezo ya ule mradi wa Shinyanga kuwa umekwisha. Sasa sijui hawa watani zangu baada ya wao kupata maji kwa hiyo sisi wengine ndiyo basi. *(Makofi/Kicheko)*

Mimi nafikiri kwa mwakani Serikali ingeliangalia jambo hili ili ile bajeti iliyokuwa inakwenda Shinyanga irudi na iongezeke lakini sasa ile bajeti igawanywe nchi nzima kila Wilaya, angalau kila Wilaya ikipata vijiji 6, 8, 10, 15 litakuwa ni jambo ambalo litatusogeza sana katika kupunguza shida kubwa sana ya maji ambayo iko nchi nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo hili la maji hasa katika Halmashauri za Wilaya, liko tatizo kubwa sana la kukosekana kwa wataalam. Wataalam wa sekta ya maji. Mahali pengi ni mafundi mchundo na watu wa aina hiyo. Tunahitaji wataalamu, nimeona hapa Chuo cha Rwegalulila kitaongezwa kidogo, afadhali, toka wanafunzi 60 sasa kitachukua 300 na kitu, angalau, lakini bado inahitajika hata zaidi ya hao. Hatuna wataalamu katika sekta ya maji, hili jambo litazamwe kipekee kabisa lirekebishwe haraka sana kwa sababu maji yanahitaji miundombinu ya gharama kubwa na ya teknolojia ya kisasa. Kwa hiyo, lazima tu-*train* watu wetu katika utaalamu huu wa masuala ya maji.

Sisi Kongwa kati ya mwaka 2202/2003 tulipata mradi ule wa maji vijijini uliokuwa unafadhiliwa na Benki ya Dunia, vijiji 10. Uekelezaji wa mradi huu kwa kweli umekuwa wa *disaster* kubwa kwa Kongwa. Katika vijiji vya Leganga, Chamae, Pandambili, Kiteto, Hembahemba, Manungu, Mautya, kati ya vile 10, vijiji karibu saba kama sio nane bado toka hiyo 2002/2003 mpaka leo 2008 miaka mitano baadaye hakuna hata tone la maji ambalo limetoka.

Kilichokuwa kinaendelea ni *consultancies* ni maandishi kushoto kulia, unashangaa mradi wa kijiji unafadhiliwa na Benki ya Dunia, mradi wa kijiji mfadhili Bendki ya Dunia, miaka mitano maji hayajatoka, kweli! Ukisomewa *figure* ya fedha ambazo zimelengwa kwa mradi huo, kubwa kabisa. Lakini kinachoendelea hakieleweki ni aibu kubwa sana. Wataalamu wanaofanya *Geology*, wanaoangalia hivi wapi kuna maji ili pachimbwe kisima, wanatoa mapendekezo ya ajabu kabisa. Kwenye kijiji kimoja

watachimba mara nne mara tano wanakosa maji, kwa nini? Upungufu mkubwa sana wa utaalamu na wate hao wanalipwa fedha zao, maji yapatikane yasipatikane yeye analipwa, upungufu mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ma-*consultant* wengi ni watu wa huko huko maji. Wengine walikuwa wanafanya kazi huko, wamestaafu, wengine walikuwa Makatibu Wakuu, walikuwa nani, ndio wamekomba kazi zote hizi. Mtu mmoja anafanya kazi Wilaya nne, Wilaya tano, matokeo yake anashindwa kumudu kazi zile. Akilipwa Kongwa, anakwenda kufanyia kazi Kondoa ambako amebanwa zaidi, akilipwa Kondoa anakwenda kufanyia kazi Rufiji ambako amebanwa zaidi. Matokeo yake Kondoa hakuwi bora, Rufiji kule kumesimama, Kongwa ndio kabisa, sasa Wizara iratibu mambo haya, mkandarasi mmoja kupewa miradi minne mitano ni kujihujumu sisi wenyewe. Hili jambo litazamwe sana, tujifunze kutokana na mapungufu makubwa sana yaliyofanyika katika mradi huu wa maji vijijini unaofadhiliwa na Benki ya Dunia, inasikitisha kabisa. Kongwa pekeyake ilikuwa imetengewa kwa miaka hii karibu shilingi bilioni tatu au zaidi, bilioni tatu au zaidi. Nini kiko pale sasa hivi?

Kule Kongwa, upembuzi yakinifu, usanifu, sijui nini, *consultancy*, uelimishaji, wewe unaelimisha nini? Wagogo, hawana maji hawa nduguzangu, unaelimisha kitu gani? Sisi tunataka maji na wananchi wamechangia 2002/2003, kijiji kimoja milioni tano kijiji kimoja milioni sita. Wameuza mbuzi wao wameuza ng'ombe wao 2002/2003, leo 2008 maelezo hakuna. Hivi mimi Mbunge wa Kongwa ninapitia wapi nirudi hapa? Ninawaambia kitu gani wananchi hawa? Sasa mnatuweka mahali pagumu sana lakini ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri, amejionea mwenyewe hali halisi, lakini nashukuru tutachukua hatua za kurekebisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mji mdogo wa Kongwa, imepewa kampuni ya wachina inaitwa *Henein International.* Katika baadhi ya hizi kampuni za wachina, Wizara tuwe makini baadhi yake si nzuri hata kidogo, Kongwa shida ya maji ni kubwa zaidi leo baada ya mradi huo kukamilika kuliko ilivyokuwa kabla ya hawa watu kuja, ni kubwa zaidi. Wametuharibia mfumo kabisa, shida ya watu ni kubwa zaidi, tunakaa hapa tunasema ufisadi, ufisadi, huu ndio ufisadi sasa. Wananchi hawana maji kampuni za kigeni kama hizo, Kongwa pale wamevuruga, kesho Mpanda au wapi watapewa hawa. Tuwaweke katika daftari zile kampuni za ajabu ajabu tusiwajaribishe katika maji. Eneo la maji sio la kujaribisha kampuni, apewe mtu ambaye tuna uhakika kabisa anaweza, wananchi watapata maji, inatia matumaini kwa utaratibu huo.

Awamu ya pili ya mradi huu wa maji vijijini Benki ya Dunia, tunategemea vijiji vyetu vya Njoge, mradi wa Ngumbi, kuteremka mpaka Vihingo na maeneo mengine yataangaliwa kipekee. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri, amezungumzia pale ukurasa wa 74 wa hotuba yake kuhusiana na mradi wa mji mdogo wa Kibaigwa ambapo pamoja na miji midogo mingine tisa ilikuwa ipate ufadhili kutoka shirika la maendeleo la Serikali ya Ufaransa, *AFD,* lakini tumeambiwa kwamba miji miwili ndio imepata mmoja Mpwapwa, jirani zangu na mwingine Utete. Hii mingine saba tumekosa, lakini Mheshimiwa Waziri ametuhakikishia kwamba mradi wa *WSDP* utaangalia kipekee miji hii iliyobaki.

Ningependa tu kumshauri Mheshimiwa Waziri na Wizara kwa ujumla kwamba Kibaigwa ni mji mdogo unaokua kwa haraka sana. Ni miji ambao kama usipotazama inakuwa kama Mererani, kwa hiyo, katika uteuzi ni vizuri tukaangalia miji ya aina hii tukaipa kipaumbele ikapata miundombinu ya maji. Vinginevyo pale ni hatari, kipindupindu, magonjwa ya kuhara damu, kuhara na mengine. Ni mahali ambapo ni hatari sana, magonjwa kama haya yanaweza yakasababisha madhara kwa watu wengi sana kwa sababu wahamiaji ni wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile kuna Mji wa Gairo ambao ni jirani pale na Kibaigwa. Mji ule wa Gairo una shida ya maji kwa miaka mingi sana, ni jirani zetu sisi tunafahamu. Gairo debe la maji 700/=, 800/= ni kitu cha kawaida. Pana shida kubwa sana ya maji na Serikali ilishaahidi kwamba itajitahidi sana kutatua tatizo la maji Gairo. Tungeomba sana miradi hii isiahirishike tena huko *WSDP* kwa sababu bahati nzuri usanifu ulishafanywa, ramani zipo, kila kitu kipo, kwa hiyo, twende kwenye utekelezaji moja kwa moja kama alivyosema Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye sekta ya umwagiliaji na sisi Kongwa tuna maeneo mazuri sana kwa ajili ya umwagiliaji. Tunashukuru kuna fedha tumepata kiasi, lakini bado ni ndogo sana kwa ajili ya kutengeneza miundombinu ya umwagiliaji. Viko vijiji vya Kiteto, kijiji cha Moreti, kijiji cha Majawanga, kule Tubugwe, kule Mseta, Chamkoroma, Mang'weta, Banyibanyi, tunaweza kabisa tukawa na umwagiliaji mzuri. Lakini kama ilivyo kwenye maji, sekata ya umwagiliaji vilevile wataalamu kwenye Wilaya hawapo. Kwa mfano, Wilaya yangu ya Kongwa hatuna hata mmoja. Tumejitahidi kutangaza mara kadhaa tupate mtaalamu, ni wachache sana watu hawa.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, ningeshauri kama ulivyosema mwanzo kwamba wataalamu wa sekta ya maji kwa ujumla tu-*train* wengi wa kutosha, lakini vilevile sekta ya umwagiliaji tuitazame kipekee kabisa. Toka enzi tume-*train* akina *Engineer* Chiza, sijui hapa katikati tume-*train* kiasi gani wataalamu wa masuala ya umwagiliaji! Kwa hiyo hili nalo tulitazame kama tulivyokuwa tunaongea leo asubuhi kuhusu kuboresha kilimo, kwamba, kama hatutakuwa na wataalamu wa uhakika wa umwagiliaji itakuwa ni jambo la ajabu sana kama tutaimarisha kilimo chetu.  Lakini mwisho, mitambo ya kuchimba visima vya maji hii ya *drilling* hii, iko michache sana nchini. Hivi kwanini kwa makusudi kabisa, tusiwe na mitambo ya Serikali mine au mitano angalau kila Mkoa ili kazi hii ya kuchimba visima iweze kwenda vizuri? Wale ambao tunawapa wachimbe visima wanapata matatizo ya kupata zile mashine za kufanya hiyo *drilling. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii. *(Makofi)*

**MHE. DR. WILBROAD P. SLAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yao yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze tu kwa kusema kwamba kwa bahati mbaya nimezunguka nchi hii, hotuba ya Waziri, mimi sitasema ni nzuri kwa sababu maneno

huwa hayazai matunda. Mimi ningepongeza matunda badala ya maneno. Unaponiambia kwamba umechimba visima 700, unaponiambia umebaini maeneo ya visima 447 kwa watu 40,000,000 mimi siwezi kukwambia hii hotuba ni nzuri na yenye takwimu.

Nashukuru kwamba wamefanya kazi, lakini maji amesema ni uhai na kama maji ni uhai na kama hotuba ya Msemaji wa Upinzani ilivyosema, sekta zote katika nchi hii zinategemea maji. Usipoweka mkakati maalum kwa ajili ya maji nchi hii tutaendelea na maneno na hatutafika mahali. Nimefika karibu kona zote nadhani kama kuna wilaya sijafika katika nchi hii ni kama tano. Maji ni matatizo, wananchi kila siku wanatembea kilometa na kilometa, badala ya kutumia muda wao kwa ajili ya kuzalisha shughuli za uchumi wanahangaika, akina mama badala ya kutunza familia zao na watoto, wanapoteza muda mwingi sana kwenye maji. Kama hatutakuja na mkakati tukaendelea kujisifu kwamba kuna kitu tunafanya, kwa kweli tutakuwa hatujiambii ukweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri, anikubalie leo haya mambo mnayoyaita *capacity building* tuyafute. Mimi sioni sababu ya kutumia *capacity building* bilioni saba, halafu watu hawana maji, wewe unajenga *capacity*, ya nini? Unajenga *capacity* bilioni tano, tena tunachukua kutoka kwa Benki ya Dunia na ninavyofahamu, Benki ya Dunia tunalipa. Hivi tunakopa tunakwenda kufanya semina, *capacity building* ni semina, tunakwenda kufanya semina bilioni saba hizi, tano hizi ninazoona za kwanza zingeweza kuchimba visima vingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule Karatu mlitususia, hamkuja kufungua mradi wetu hata mmoja. Ninatumia neno kususia kwa sababu nimealika nimechoka, hakuna hata mradi mmoja na katika vijiji vyangu 45, leo nina vijiji 35 vina maji. Mradi mmoja wa Kata, tulitumia Serikali, tukaletewa *estimate* ya bilioni moja, sisi tumeuchimba na kutengeneza huo mradi wa kilomita zaidi ya 19 na kilomita za *pipe* zaidi ya 50 na kitu, tumetengeneza kwa chini ya 400,000,000, milioni 400, lakini Serikali walituletea bilioni moja.

Mimi ninaomba, tuna matatizo makubwa na ninajua kabisa kwamba haya mambo mengi ya gharama kubwa ni kwa sababu tuna taratibu za kiserikali, hizi taratibu za Serikali hazisaidii wananchi. Tunaomba twende kwa wananchi, tunaomba wananchi wakae chini, wawezeshwe waruhusiwe na wao wenyewe waamue wanataka kutekeleza hii miradi namna gani. Serikali iwe na macho, Serikali isiweke mikono yake katika hii miradi, inawezekana tukiamua kufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukipita kwenye kitabu chote cha maendeleo, *development and management of water resources*, yaani kukuza ile bilioni 12, sijui ndani yake kuna nini, kwa sababu vitabu havionyeshi ni kazi gani inafanyika. Ukienda kwenye karibu kitabu chote hapa, mabilioni yote yaliyowekwa bilioni saba, *expansion of rural water supply*. Bilioni saba hii mimi ukinikabidhi Mheshimiwa Waziri, nitafanya maajabu katika maji kwa sababu ninajua inawezekana na ukiondoa zile semina ukiondoa zile safari, kwa mfano, nimeangalia tu magari yanayonunuliwa, sisi hatuhitaji magari hata kwa miguu tutatembea, lakini tupate maji. Haya magari kama yanakwenda kutembea huko na hayazai matunda, yanafanya *survey* munayoita, kila wakati ni *survey*, mimi

nadhani haya magari hayatusaidii. Wananchi wanataka maji, hawataki kuona magari yanayozunguka hayazalishi lita moja ya maji mwisho wa siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu niondoke huko kwanza kwenye Taifa nirudi kwangu, maana sijazungumza juu ya Karatu, siku nyingi sana. Nilisema kwamba Waziri, Wizara yake ilinisusia kwa sababu hawakuja kuzindua hata mradi mmoja. Sasa kwa kuwa hamkuja, naomba niwapongeze watu wangu walionisaidia mpaka vijiji 30 vimepata maji. Naomba kupongeza sana Jimbo Katoliki la Mbulu, naomba kupongeza Kanisa la *KKKT* Jimbo la Karatu na Dayosisi ya Kaskazini. *CARITAS Tanzania* pamoja na *Missereor* ambao wametusaidia miradi mingi sana. *CARITAS Australia* wametusaidia miradi mingi sana. Hivi karibuni, jana mimi sikuwepo hapa nilikwenda kupokea wageni tunapata wenzetu kutoka *Angel Mission* kutoka Marekani na wenzetu wengine ambao wamekuja kutoka *God TV* wote wametusaidia na juzi tu tumechimba visima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, inawezekana tumechimba visima na kwa bei ndogo tu nje tofauti na *quotation* tulizokuwa tunapewa na watu ambao ni *commercial.* Tunaweza kutumia vyombo vilivyopo vya kujitolea na taasisi yetu ya Serikali ikijiweka vizuri na hata Idara yetu ya *drilling* ikajiweka vizuri isiende *commercial* tunaweza tukachimba visima vingi. Serikali ni lazima ikubali kutoa *subside* kwa sababu hapa hata ile Idara ya kitengo cha *drilling* tukifanya *commercial* maji hatutayapata hata siku moja. Ni jukumu la Serikali itoe ruzuku tuwezeshwe kwenda kwenye maeneo na visima vichimbwe. Maji ni ya shida, naomba nikiri kwamba maji ni matatizo, tumekwenda eneo la Gidemulanda kule kwangu, tumechimba visima vine. Kati ya hivyo tumepata kimoja tu na kwa mita 200, mita 200 kwa wale wasioelewa ni usawa viwanja viwili vya mpira, urefu wake lakini kwenda chini. Kwa hiyo, ni kweli hatuna maji katika sehemu nyingi za nchi ni matatizo kupatikana lakini tukitaka yale kidogo tunaweza tukayapata.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Chiza, ametekelaza wajibu wake. Ni kweli hata nikipiga kelele ya kulaumu Serikali sio kwamba hawakufanya kitu kabisa, Mheshimiwa Chiza, amefika kule kwangu mara nyingi sana na matunda ya kazi yake nimeyaona. Mheshimiwa Chiza, nakushukuru sana, matunda ya Bonde la Eyasi nimeyaona. Una mradi kwa ajili ya Qanded, Barazani, Malekchand, Dunbechand, Laghangareri, Endamaghang, haya yamekwishafanyiwa kazi.

Nakushukuru sana kwa kazi hiyo, naishukuru Serikali kwa maana Mheshimiwa Chiza amekuja kwa niaba ya Serikali. Lakini nitaomba mniambie, Mji wa Karatu mmeuweka chini ya Babati. Babati na Karatu ni kilometa zaidi ya 300 kwa mzunguko. Hivi ni kwanini Karatu tunawekwa chini ya Mji Babati badala angalau kuwekwa chini ya Makao ya Mkoa ambayo yako Arusha? Nitaomba jibu wakati Waziri anahitimisha hoja yake.

Vilevile namshukuru Mheshimiwa Chiza, kwamba kule Mang'ola hekta 1,660 za vitunguu ambazo alizisimamia zimefanyiwa kazi, kwa hiyo, nawashukuru sana kwa kazi iliyofanyika naishukuru vilevile Wizara kwa miradi ya *quick win* ambayo tumepata na leo nimesoma kwenye gazeti wametangaza kwa miradi ya *World Bank* wale *consultants* sisi Karatu tuko kwenye Wilaya 82, nawashukuru kwa hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nataka kusema hivi, hao wanachaguliwa, wakishachaguliwa kinafuata nini? Hivi wakishachaguliwa sisi tumekunywa maji? Hivi wakienda wakafanya *survey* yao, tutakuwa tumekunywa maji? Kama tumechukua miaka 10 na majina yote niliyoyaona ni watu wa nje ya nchi, kampuni za Tanzania katika sita kama niliziona ni mbili tu. Naomba hii *World Bank* kama Serikali imeshindwa kuisimamia waleteni kwa Wabunge, kama wanaahidi miradi, Wabunge tukae nao tugombane nao. Kwa sababu haiwezekani unaahidi mradi kwa miaka 10 halafu hautekelezwi, bei inazidi kubadilika, wakati wa mwisho unaweza kuja kuambiwa kwamba hata mradi wenyewe haupo.

Masharti ya aina hii ni masharti ya gani? Bunge lako lilinituma kwenye *ACPU*, tuligombana miaka mingi kwenye miradi ya *ECF*, nakumbuka kwamba tulikubaliana tukaweza kurekebisha masharti ya vyombo vya kimataifa hata ya *World Bank* tunaweza tukakaa tukarekebisha, tunahitaji ku-*simplify* hizo *processes* ziweze kutuletea maendeleo. *World Bank* ni chombo cha Serikali na ni Serikali zote za Umoja wa Mataifa, hatuna sababu ya sisi kupiga magoti wakati masharti hayo hayatufai sisi. Naomba tuwe wakali na tunapokuwa wakali ni haki yetu kwa sababu na sisi ni wanachama kule. Hatuwezi kuwekewa masharti ambayo hayatunufaishi kwa namna yoyote ile.

Nimalizie tu kwa kusema kwamba vijiji 10 nimeviona, lakini vijiji 10 ambavyo vinapangwa kwa kila Wilaya kama kila Kijiji kitakuwa kimetekelezewa tutakuwa tumepiga hatua. Lakini kwa kiwango gani kwamba sasa tuna uhakika angalau katika miaka miwili ijayo? Mimi ningependa Waziri atuambie, ni hatua gani sasa amefika katika majadiliano na *World Bank* hawa aliotangaza leo, tena aka-*time* vizuri akawatangaza siku bajeti yake inasomwa. Ametangaza kwa sababu bajeti inasomwa au ni kwa sababu sasa kweli tuna matumaini ya kupata?

Ningependa jibu la uhakika katika hili kwa sababu *timing* yake imenistua, nchi nzima imetangazwa wameteuliwa, lakini siku zote hatukuona. Juzi alitupa taarifa hapa, namshukuru kwa taarifa zake ni mtu muwazi sana, anapenda kushirikisha, kama ni hivyo namshukuru, lakini kama nikutupa matumaini tu halafu tukae miaka mitano tena kwa kweli. Mimi sina imani na mradi wa namna hii. Vijiji 10 kwa kila Wilaya katika nchi hii, *impact* yake ni kubwa sana. Kwa hiyo, tunamuunga mkono kwa hilo, nahitaji msaada, atuambie tusaidiane katika kusukuma ili tuweze kufikia mahali pazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, nawashukuru vilevile kwa miradi ya *quick win* ambayo Karatu sisi imetusaidia. Bahati mbaya mradi wetu mmoja umeshindikana kukamilika kwa sababu ulihitaji *TANESCO* watuunganishie na Serikali iko hapa, nafikiri Waziri wa Nishati atusaidie kwa sababu kumbe unaweza kupata mradi mmoja, lakini kwa kuwa miradi hii inategemeana ikasimama kwa sababu huwezi kupata *transformer, transformer* hazipo, lakini kiwanda cha kutengeneza *transformer* kiko Arusha. Sasa tatizo ni nini? Mimi nafikiri Serikali itatusaidia kujibu, hili sio la Waziri wa Maji, nadhani watusaidie katika hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, nawashukuru wananchi wa Karatu ambao wameelewa kwamba maji yanalipiwa na sio kuchangiwa. Naomba kwa hilo

nilirudie kwamba maji yanalipiwa na sio kuchangiwa ndio maana katika Bodi zetu saba, Bodi ya *KAVIWASU* ni Bodi pekee ambayo imeimarika kwa sababu wananchi wa vijiji sita vya Karatu wanalipa maji na wana-*recover* gharama zote na wanapata faida, wanajua miaka 20 ijayo wanaweza waka-*replace* mabomba hayo bila kurudi kwa mfadhili. Hiki kitu tukikitaka kinawezekana, sasa bahati mbaya mradi huo unapigwa vita na bahati mbaya Serikali kila wakati inakwenda kule, kuna barua nyingi Mheshimwia Waziri anajua kwenye faili lake aangalie, jinsi *KAVIWASU* ambayo imefanikiwa inavyopigwa vita *including* na Serikali. Lakini Bodi sita nyingine ambazo hazijakwenda mbali hazisaidiwi hata kwa *capacity building,* hata kwa kuwapatia angalau hela kidogo na hao ndio ambao hawajapata maji ya uhakika katika sehemu kubwa.

Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri, achukue wakati wake na aniambie wakati wa *winding- up* kama atakubali kuja Karatu, angalau kuhamasisha watu wa Karatu kuwapa moyo kwa jinsi walivyochangia fedha katika miradi yao mbalimbali. Basi wanahitaji waione Serikali yao iko karibu, wafadhili wanaotuchangia wanataka kuona kama Serikali nayo iko karibu, lakini Serikali inapopita pembeni kila wakati, angalau hata shukrani haionekani kwa wale wafadhili, angalau barua moja tulipata huko nyuma, lakini baadaye wakakaa mbali, sijaelewa ni nini? Nitapenda Mheshimiwa Waziri anihakikishie kama atakuwa tayari kuja kuzindua angalau mradi mmoja ili tujue Serikali iko pamoja na sisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

**MHE. WILLIAM J. KUSILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii ya mwisho kwa siku ya leo, lakini hata hivyo ni nafasi ya tatu tu katika kuchangia bajeti ya Wizara hii na mimi katika miaka yangu yote 18 nikiwa Mbunge katika Bunge hili nafikiri ndio mara ya kwanza napata nafasi ya kipaumbele kama leo. Kwa hiyo, nashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, kwa hoja iliyoandaliwa vizuri sana, hoja yenye hekima na hoja yenye ufafanuzi inayoeleweka vizuri sana. Nampongeza yeye na timu yake yote kwa hoja hii nzuri sana. Lakini naomba nitumie nafasi hii vilevile kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa mwanzo mzuri sana katika kuiongoza Wizara hii.

Nasema wameanza vizuri kwa sababu katika muda mfupi sana tangu wameteuliwa kuiongoza Wizara hii kwa kweli wameshatembelea maeneo mengi sana ili kujionea matatizo yanayovikabili vyanzo vyetu vya maji na miradi mbalimbali ya umwagiliaji katika nchi hii. Nami binafsi na kwa niaba ya wananchi wa Bahi, naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwamba mara tu walipoteuliwa alitenga muda wake na kuembelea *scheme* zetu mbili za umwagiliaji ile ya Mtitaa na ya Bahi na kujionea matatizo ambayo yanazikabili *scheme* hizi. Nasema huu ni mwanzo mzuri sana kwa sababu kwa kuona, basi unaona matatizo wewe mwenyewe na unasikia kutoka kwa watu wanaohusika na kwa hiyo, unakuwa katika nafasi nzuri sana hata ya

kuyashughulikia matatizo hayo. Kwa hiyo, namtakia kila la heri, aendelee na msimamo huo katika kuiongoza Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Dodoma. Mkoa wa Dodoma ni Mkoa wa ukame, Mkoa wenye mvua za mtawanyiko, zinazonyesha kwa muda mfupi sana na mvua zisizoaminika. Kwa sababu ya hali hiyo ya hewa, ndio maana Mkoa wa Dodoma unakabiliwa na tatizo la upungufu wa chakula na hata majanga ya njaa ya mara kwa mara na ambayo yanaendelea kujirudia mara kwa mara. Lakini Mkoa wa Dodoma hatuna tatizo la ardhi na tena ardhi yetu ni nzuri sana, ardhi yetu ina madini mengi yanayofaa sana kwa kilimo cha mazao mbalimbali na kwa kweli sisi hata tatizo la mbolea kwetu sio tatizo ambalo ni kubwa sana. Katika maeneo mengi ya Mkoa wa Dodoma unaweza kulima tu mazao mbalimbali na yanastawi bila matumizi ya mbolea. Ingawaje kwa kuongeza uzalishaji basi bado tunawashauri wakulima wetu watumie mbolea tena mbolea ile ya samadi ambayo ndiyo asili.

Tatizo la Mkoa wa Dodoma ni hili la maji, lakini sio kwamba Mkoa huu haupati maji kabisa katika muda huo ambao tunapata hizo mvua za muda mfupi, hizo mvua za mtawanyiko na kadhalika tunapoteza maji mengi sana. Kutoka enzi za ukoloni ilikwishatambulika kwamba ili kuukwamua Mkoa huu na kuuwezesha nao uweze kuchangia katika uchumi wa Taifa hili, jawabu kwa kweli ni malambo na mabwawa makubwa na ya kati, hilo ndio ukombozi wa Mkoa huu. Maji ambayo tunayapoteza wakati wa msimu wa mvua ni mengi sana ambayo mnaweza mkayahifadhi ili yaweze kutumika kwa shughuli za kilimo na shughuli za ufugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama inavyoeleweka, hakuna ufanisi katika kilimo na kwa kweli tu hakuna kilimo bila maji. Wala huwezi kuwa na ufanisi katika ufugaji na kwa kweli hata haiwezekani bila maji. Sasa ili na sisi tuweze kutoa mchango wetu tuweze kuchangia katika uchumi wa Taifa hili na kuweza kujilisha sisi wenyewe ni vyema suala hili la malambo na mabwawa katika Mkoa wa Dodoma likatiliwa mkazo. Naishukuru sana Serikali, kwamba kwa mara ya kwanza kabisa nafikiri inaanza kujielekeza katika kulitatua tatizo hili. Mimi nashukuru kwamba katika Wilaya yetu ya Bahi katika mwaka wa fedha uliopita tulitengewa fedha za kutosha kwa ajili ya miradi ya umwagiliaji.

Wilaya ya Bahi, ipo katika ukanda wa Bonde la Ufa na ni ukanda ambao unafaa sana katika kilimo cha mpunga ili mradi tu kama maji ya kutosha yatapatikana na sisi tumetengewa fedha za kutosha kwa ajili ya miradi ya umwagiliaji, hiyo nashukuru sana. Lakini mimi tatizo langu katika hii miradi ya umwagiliaji ambayo inajengwa katika maeneo mbalimbali katika Mkoa wetu huu wa ukame ni kwamba miradi hiyo inategemea mito ya msimu ambayo mito hii nayo inategemea mvua hizi hizi ndogo. Kwa hiyo, mvua hizi zikikatika na mito hii inakatika na kwa hiyo mazao hata katika hizo *scheme* za umwagiliaji yanakauka sawa sawa kabisa na mazao ambayo hayako katika miradi ya umwagiliaji.

Sasa mimi sijui, sio mtaalamu sana wa suala hilo la umwagiliaji, lakini nilitazamia kwamba mradi wa umwagiliaji kama kweli utakuwa na sifa za neno lenyewe la umwagiliaji, basi imuwezeshe mkulima kumwagilia mazao yake pale mvua zinapokuwa

hazipatikani. Sasa miradi yote ambayo tunajengewa, kwa kweli haina sifa hiyo, inategemea maji ya mvua na mito ya msimu. Mito inategemea maji ya mvua, mvua zikikatika mito inakauka na kila kitu kinakatika na mazao yanakauka kama kawaida.

Kwa hiyo, mimi ningeliomba sana suala hili liangaliwe upya, kama hii miradi ya umwagiliaji ambayo tunajengewa katika Mikoa yetu hii ya ukame kama Dodoma kama itakuwa ni ya manufaa kwa wakulima, basi suala la mabwawa au malambo ya kuhifadhi maji kwa matumizi ya umwagiliaji mvua zinapokatika lazima lipewe kipaumbele kabisa ili iwe na maana. Tuna maeneo mengi sana ambayo yanafaa kwa ujenzi wa mabwawa na malambo na udongo wetu unahifadhi sana maji. Bila ya shaka mifano inaonekana humu kando ya barabara ambayo walichimba wakandarasi wa barabara tu, lakini haya maeneo waliyochimba kwa ajili ya ujenzi wa barabara mengine yamekuwa ni mabwawa ya kudumu, maji hayakauki. Kwahiyo, kuna maeneo mengi ya namna hiyo ambayo tukijengea mabwawa yatatusaidia sana kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaamini kabisa, katika kugawana huyo sungura mdogo ambaye tunamzungumza kila mara ni lazima tutazame vipaumbele vya kila Mkoa. Kwa hizo *big four* ambazo wenzetu hawana tatizo la mvua, tatizo lao ni mbolea, basi tuhakikishe kwamba tunawasaidia kukwamua tatizo hilo ili waweze kuzalisha kwa kadiri inavyowezekana.

Kwa hiyo, wao suala la mbolea ni lazima tuwawezeshe, mbolea ipatikane wazalishe, inapokuja kwenye suala la maji, basi tuangalie ile Mikoa yenye ukame. Tuhakikishe kwamba tunawatatulia hilo tatizo la ukame ili nao waweze kuzalisha kwa kadiri inavyowezekana. Lakini kama huyo sungura mdogo, basi tutasema kama ni sikio tugawane wote sawa, kama ni mguu, tugawane wote sawa, basi wote hatutatosheka.

Kwa hiyo, lazima tuweke vipaumbele sahihi katika kila eneo, katika Mkoa wa Dodoma sisi tunachoomba ni kutuwezesha kututatulia hili tatizo la maji na nina hakika kabisa kwamba tunaweza kuzalisha sawasawa na Mikoa mingine hii ya *big four* na Mikoa mingine ambayo inazalisha mazao ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutazalisha mahindi ya kutosha, tutazalisha mpunga wa kutosha katika mabonde yetu mengi ya *Rift Valley* huko na kadhalika, tutazalisha mtama na kwa mboga tena ndio penyewe. Tutazalisha nyanya za kutosha vitunguu vya kutosha na mboga nyingine kama mchicha na kadhalika na nina hakika Waheshimiwa Wabunge na wengine mmeona. Pale ambapo pana maji uzalishaji wake unakuwa ni mzuri sana, ninaomba sana Serikali iangalie sana suala la malambo na mabwawa katika Mkoa huu. Tangu tumepata uhuru nadhani hakuna mabwawa ambayo yamechimbwa au kujengwa katika Mkoa huu, licha ya ilani yetu ya uchaguzi ya *CCM* ambayo inahimiza uchimbaji na ukarabati wa mabwawa ambayo yameharibika, sura ya 67(b) lakini kwa kweli hatua za dhati kabisa katika kutekeleza azma hiyo ambayo imo katika ilani yetu ya uchaguzi katika Mkoa huu nafikiri bado ni ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu nakua nimekuta mabwawa hayo hayo ambayo mpaka leo yapo. Lipo bwawa la Nondwa, lipo lililokuwa limekufa, namshukuru Mheshimiwa Waziri, amesema sasa linakarabatiwa au limekwishakarabatiwa. Lipo

lingine ambalo limekufa la Mlowa, bado halijakarabatiwa, lilpo lile la Hombolo, haya ndio mabwawa ambayo tumeyakuta na mpaka leo yapo. Kama hayakujengwa wakati wa ukoloni, basi yalijengwa katika mipango ya ukoloni wakati huo kwamba walikuwa wamepanga mabwawa yajengwe wakati huo. Lakini sisi tangu tumeanza, kwa kweli tumeliacha lengo hilo kabisa na hatujafanya chochote na kwa hiyo, Mkoa huu badala ya kuendelea katika suala la kilimo na hata katika ufugaji unaweza kukuta tunapiga *mark time* sana kwa sababu suala la maji, malambo na mabwawa halijapewa uzito unaostahili. Mimi nasisitiza na kuomba Serikali, iliangalie suala hili kwa makini. Katika Mkoa huu tatizo letu sio kwamba hatuwezi kuzalisha kama nilivyosema na wala sio kwamba hakuna ardhi.

Ardhi ipo ya kutosha kabisa yenye rutuba, tatizo ni maji. Kuna mradi wa bwawa la Farkwa ambao unategemewa, ulibuniwa enzi hizo za ukoloni, michoro na takwimu zote zipo, lakini tukautelekeza. Lakini mradi huu ulitegemewa uwe ndio chanzo cha kuaminika cha maji ya mji huu wa Dodoma, kwa sababu hiki chanzo cha sasa tunachokitumia kinaweza kikafikia mwisho, kinatumia maji ya chini na yanaweza yakafika mahali yakakauka, lakini maji ya uhakika yalitegemewa yatoke kwenye bwawa hilo la Farkwa. Vilevile bwawa hili lilitegemewa liwe ni chanzo cha kilimo cha umwagiliaji katika eneo kubwa sana, kuanzia hiyo sehemu ya Farkwa mpaka Bahi mpaka Manyoni. Kwa hiyo, karibu Bonde lote la Ufa lingetumia maji ya mto Farkwa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sio hivyo tu, bwawa hili lilitegemewa vilevile lingekuwa ni chanzo cha umeme kwenye gridi ya Taifa. Bwawa hili lingeweza kuzalisha karibu *megawatt* 20 na kuziingiza katika gridi ya Taifa. Sasa huu mradi ulibuiniwa miaka mingi iliyopita, gharama yake haikuwa kubwa kiasi hicho wakati huo, lakini utekelezaji wake ukaachwa tu na hatulizungumzii tena. Sasa mimi naomba Serikali, tena irudi ikatazame uwezekano wa kujenga hilo bwawa haraka kwa kadiri inavyowezekana litasaidia sana. Bwawa hili linaweza kusaidia umwagiliaji katika sehemu kubwa sana ya Mkoa huu na kuwezesha mazao mengi tu, mboga na mazao mengine katika ukanda wote wa Bonde la Ufa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka nizungumzie hilo tu na ninaomba niishie hapo kwa kusisitiza sana kwamba na sisi tunahitaji maji kwa ajili ya kilimo, maji kwa ajili ya ufugaji ili na sisi tuweze kuzalisha kwa kadiri tunavyoweza na mifugo yetu vilevile iweze kunufaika kama sehemu nyingine za nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niishie hapo kwa kuunga mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda uliobaki ni mdogo sana kwa mtu mwingine kuweza kuchangia. Kama nilivyosema, bahati mbaya sana Wizara hii kesho tunaweza kupata watu 11 tu, kwa hiyo na idadi yetu ni kubwa lakini 11 tu ndio wataweza kuchangia. Kwa hiyo, wengi wenu mtakosa nafasi.

Baada ya kusema hivyo, ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, naomba kwa niaba ya familia yangu, nipende kutoa shukrani za pekee sana kwa msaada na faraja kubwa sana mliyotupa familia yetu baada ya kumpoteza mtoto wetu hapa Dodoma siku ya Jumamosi na ambaye alizikwa Jumapili kule Kongwa. Waheshimiwa Wabunge wengi mlikuja hapa Dodoma na hata kule Kongwa, familia yetu ilifarijika sana. Hapa Kongwa, mtoto mwenyewe alikuwa kama anajitegemea, kwa hiyo, ilikuwa kama ni ugenini lakini nyie mlikuwepo kama ndugu zake na majirani waliohusika. Naomba nishukuru sana kwa hilo kwa niaba ya familia, ahsanteni sana.

Baada ya kusema hivyo, Waheshimiwa Wabunge, tunaahirisha shughuli za leo mpaka kesho saa 03:00 Asubuhi.

*(Saa 01.36 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Ijumaa,*
*Tarehe 25 Julai, 2008 Saa Tatu Asubuhi)*